

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 2 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani :-

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Miundombinu kwa mwaka Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka 2008/2009.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU):**

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 142

**Utaratibu wa Makabidhiano kwa  
Waheshimiwa Wabunge**

**MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa Wabunge wanawakilisha kwa muda wa miaka mitano na kwa kuwa katika kipindi hicho huwa wamepata nyaraka pamoja na mwendelezo wa shughuli mbalimbali katika maeneo yao:-

- (a)Je, Wabunge wanapoacha uwakilishi hufanya makabidhiano na Mbunge mpya?
- (b)Kama utaratibu huo haupo, je, Serikali haioni kuwa wananchi wananyimwa mwendelezo wa mambo yanayokuwa yanafuatiliwa?
- (c)Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha utaratibu uliopo katika kuachiana madaraka kama ilivyo kwenye mihimili mingine ya dola?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA  
BUNGE alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer Stella Martin Manyanya*, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wabunge ni wawakilishi halali wa wananchi kwa mujibu wa Katiba na kwamba uwakilishi wao ni kwa kipindi cha miaka mitano ambapo baada ya kipindi hicho kwisha, uchaguzi Mkuu hutakiwa kufanyika kuchagua wawakilishi wapya wa wananchi kwa njia ya kupigiwa kura. Aidha, kwa mujibu wa mfumo uliopo sasa hakuna utaratibu wa makabidhiano baina ya Mbunge aliyemaliza muda wake na yule anayeingia kuanza muhula mpya wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge ni wawakilishi wa wananchi kwenye Majimbo wanayotoka na kwa kuwa masuala yote yanayohusu utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwenye Majimbo hufanyika kuitia vikao halali vya Madiwani kwenye ngazi ya Halmashauri ambapo Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe, Serikali haioni kuwa wananchi wananyimwa fursa ya mwendelezo wa mambo yanayokuwa yanafuatiliwa na Mbunge husika Jimboni kwake, ukiacha utekelezaji wa ahadi binafsi ambazo Mheshimiwa Mbunge alikuwa amewaahidi wananchi wa Jimbo husika wakati wa kampeni za uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyaraka muhimu zinazohusu mambo yaliyojadiliwa katika kipindi kilichopita, taasisi ya Bunge inayo maktaba na *Website* yenye kumbukumbu za kutosha kuweza kukidhi haja pale inapohitajika.

Aidha, nyaraka kuhusu mipango ya maendeleo kwenye Halmashauri ambapo Mbunge anawakilisha Jimbo nazo huweza kupatikana kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Maendeleo kwenye Halmashauri husika kwani mtendaji huyo hushiriki au kuwakilishwa kwenye vikao vyote vya Baraza la Madiwani na huwajibika pia kutunza taarifa zote muhimu zinazohusu maazimio na maamuzi mbalimbali yanayofanyika kupitia vikao hivyo vya Halamashauri. Kwa sasa Serikali haina mpango wa kubadili utaratibu uliopo isipokuwa msisitizo utaendelea kuwekwa katika kuhakikisha kwamba angalau katika kila Jimbo inajengwa Ofisi ya Mbunge kama ilivyokwishaahidi na Serikali.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini naomba niseme kwa kuwa nature ya Wabunge kazi zetu huwa zingine tunazifanya kwa kufuatilia wenyewe tunavyoona zinatafaa lakini Mbunge anapomaliza kazi yake huwa haweki kumbukumbu ana kazi gani, amefuatilia wapi na imeishia wapi.

Sasa je, Serikali haioni kwamba ni vema kuweka utaratibu wa Mbunge kuacha kumbukumbu katika ofisi yake anapomaliza Ubunge wake kazi alizozifanya na alizoachia kuzifuatilia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa mfumo wetu kwa sasa hakuna utaratibu wa makabidhiano lakini hii haina maana kwamba pale inapowezekana inakatazwa na sheria.

Kwa hiyo, pale ambapo inawezekana makabidhiano yanaweza kufanyika. Hata hivyo, bado tunasisitiza kwamba nyaraka zote muhimu za maendeleo ya Jimbo zitapatikana kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri husika. Yale masuala ya binafsi ya Mbunge kama ahadi ambazo zinatekelezwa au nyaraka zake huhifadhiwa na msaidizi wa Mbunge husika, basi utaratibu wa kawaida wa mawasiliano kati ya mtu na mtu yanaweza kutumika kupata nyaraka au kumbukumbu zinazohitajika.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa katika utekelezaji wa kazi zao Wabunge wanapofanya kazi na Halmashauri wanakuwa wajumbe lakini wala hakuna utaratibu wa kuwataka wakabidhi nyaraka au mchakato wa kazi zao kwa Mkurugenzi na kwa kuwa uchaguzi unapomalizika Ofisi za Wabunge zipo tofauti na Ofisi za Wakurugenzi ni kwa nini Serikali isiandae utaratibu kamili wa kisheria kwamba yaliyoko katika ofisi ya Mbunge

ambayo ni tofauti na Ofisi ya Mkurugenzi yakabidhiwe kwa utaratibu maalum unaokuwa endelevu kwa Mbunge anayefuata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, lakini nashangaa mmeburuzana kwenye uchaguzi unamkabidhi nini!! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu hali halisi inavyokuwa mara baada ya uchaguzi na wewe ni shahidi.

Sasa utaratibu uliopo sasa pale ambapo kuna ofisi nyaraka kama vile *Hansard* za Bunge kama Wabunge wanaweza kuzihamisha kutoka Dodoma kwenda Wilayani huwa zinakuwa kwenye Ofisi za Mbunge, lakini zile ahadi ambazo ni za Mbunge binafsi bado ni majukumu ya Mbunge na msaidizi wake kuyatekeleza.

Lakini ifahamike pia, la msingi ni kwamba, yale masuala muhimu ya maendeleo ya Jimbo, masuala ya msingi huwa nyaraka zake zinahifadhiwa kwenye Halmashauri husika.

Na. 143

#### **Sheria Zinazotawala Uanzishaji CDA**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa *CDA* ilianzishwa mwaka 1973 kwa Sheria Ndogo (G.N. No. 230 of 1973) kwa lengo la kuharakisha ujenzi wa uhaniaji wa Makao Makuu Dodoma na kwa kuwa Manispaa ya Dodoma imeundwa Kikatiba na Sheria Mama za Serikali za Mitaa zinazoipa mamlaka mbalimbali pamoja na yale yanayohusu usimamiaji wa ardhi na maendeleo yake:-

(a)Je, kati ya Sheria Mama na Sheria Ndogo ni ipi yenye uzito na kauli ya mwisho Kikatiba na Kisheria?

(b)Je, Serikali haioni kwamba kwa kuinyang'anya Halmashauri haki ya kusimamia ardhi yake kwa kutumia Sheria Ndogo ni kuwanyima wananchi uhuru wa kusimamia mambo yao?

(c)Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya Ibara ya 125 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kwamba itatunga sheria ya Uhamishaji Makao Makuu ya Serikali kuja Dodoma ili kuondoa mkanganyiko wa madaraka uliopo kati ya *CDA* na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA  
BUNGE alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya *CDA* lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uzito wa sheria tunaweza kuzipanga sheria zetu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sehemu nne muhimu:-

(i)Katiba ambayo ndiyo Sheria Mama.

(ii)Sheria za kawaida zinazojadiliwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

(iii)Sheria ndogo ndogo (*By laws or Regulations, Orders* na kadhalika ambazo sio lazima kupitishwa na Bunge.

(iv)Tangazo la Serikali (*Government Notice*) ambalo hutolewa na Rais au Waziri kwa mamlaka aliopewa na sheria fulani.

(b)Kiutendaji mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma katika nafasi zao tofauti huwa ni vyombo vilivyowekwa maalum ili kuwasilisha maslahi tofauti. *CDA* ni chombo kilichowekwa maalum kuwakilisha Serikali katika kutekeleza Program ya Ustawishaji Makao Makuu wakati Halmashauri ya Manispaa ni chombo cha utawala cha Dodoma Mjini. Serikali haijainyang'anya utawala wa Dodoma bali ni vile tu tunatumia sheria ndogo za *CDA*. Sheria ndogo hizo ni halali na kwa mujibu wa sheria hizo ndogo hasa ile ya mwaka 1987 ardhi yote ya Dodoma ilitolewa kwa *CDA* kwa hati miliki ya muda mrefu ya miaka 99 ambayo Namba yake ni 4585 iliyofanywa na *CDA* huwa kwa kawaida inaishirikisha Manispaa kama ambavyo mifano mingi inaonyesha, mifano michache ni kama ifuatavyo:-

(i) *Special Planning Committee* inashirikisha wajumbe wanne kutoka Manispaa.

(ii) Kamati ya Udhibiti wa Uendelezaji na kutoa vibali vyta ujenzi. (*Building Control Committee*) ina wajumbe watatu kutoka Manispaa.

(iii) Kamati ya Ugawaji Viwanja /Ardhi (*Plot Allocation Committee*) ina wajumbe watano kutoka Manispaa akiwemo Mstahiki Meya na Madiwani wawili.

(iv) Kamati ya Kutoa Majina ya Mitaa (*Street Naming Committee*) ya maeneo ya Dodoma yenye Sekretarieti yake Manispaa ina wajumbe wanne kutoka *CDA*.

(v) Mkurugenzi Mkuu wa *CDA* ni mjambe mwalikwa wa *Full Council* ya Halmashauri ya Manispaa.

(vi) Mkurugenzi wa Manispaa ni Mjumbe wa Bodi ya *CDA* na kama nilivyosema Mbunge pia ni Mjumbe wa Bodi ya *CDA*.

(vii) Kamati ya Mipango Miji ya Manispaa ya Dodoma ina Mjumbe kutoka *CDA*.

(viii) Timu ya usanifu na ufuatiliaji uendelezaji wa Kituo Kikuu cha Mabasi na Egesho la Malori inajumuisha wajumbe kutoka *CDA* na Manispaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na mifano hii ni dhahiri kuwa *CDA* na Halmashauri ya Manispaa zinafanya kazi pamoja katika suala zima la kusimamia ardhi ya Manispaa ya Dodoma.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ambayo yanatutia moyo sisi watu wa Dodoma na nadhani hata umma wote wa Tanzania kwamba hatimaye Serikali imeanza kulivalia njuga suala la Makao Makuu ya Serikali kuhamia Dodoma. Hata hivyo nina swali dogo la nyongeza.

Je, Serikali ipo tayari kutuhakikishia kwamba huo mchakato wa kutunga sheria ya kuitambua Dodoma kama Makao Makuu utakamilika katika kipindi cha mwaka mmoja ujao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sio tu kwamba tunatarajia kwa muda wa mwaka mmoja kutunga sheria ya kusimamia uhamishaji wa Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma lakini pia tunafanya tathmini ya program hii ya Makao Makuu Dodoma.

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza baada ya majibu mazuri ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa kuwa tatizo kubwa matatizo makubwa ya *CDA* ni mawili. La kwanza ni ukosefu wa wataalam amba walikuwepo mwanzo na baadaye wakatoka mmoja mmoja

Kwa hiyo hilo ni tatizo la kwanza. Tatizo la pili, ni fedha hata ukiangalia kwenye bajeti yetu ya mwaka hadi mwaka utaona jinsi *CDA* bajeti yake ilivyokuwa ikiteremka.

Je, Waziri anaweza kulihakikishia Bunge hili na watu wa Dodoma na Watanzania kwa jumla kwamba hayo matatizo mawili ya wataalam na la fedha ili *CDA* iweze kufanya kazi iliyopewa kikamilifu? (*Makofî*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli matatizo yote mawili yanafanana na yanaunganika, rasilimali watu na rasilimali fedha.

Tulipoanza kukosa fedha za kuhudumia Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu kwa hiyo wale watumishi wetu mahiri katika maeneo mengi walihama na hii ni kwa sababu ya hali halisi ya uchumi wa nchi wakati huo kati ya mwaka 1985 na mwaka jana, CDA haikuweza kupewa za kutosha hasa za maendeleo lakini pia wakati huo huo kwa sababu ya tatizo la rasilimali watu hata zile fedha kidogo walizokuwa nazo hazikuwa zinatumika vizuri.

Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mzee Malecela na Watanzania wote kuwa sasa tunaanza kujiweka sawa kuanzia mwaka uliopita wa fedha na mwaka huu tumeanza kuitengeta fedha za maendeleo na nadhani sasa program ya uhamiaji wa kuja Makao Makuu Dodoma utarejea katika hali yake kama ilivyotarajiwaa.

Na. 144

### **Mapendekezo ya Tume ya Haki za Binadamu**

#### **MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika utendaji wake imekuwa ikitoa mapendekezo kadhaa kwa taasisi husika kwa ajili ya utekelezaji na kwa kuwa kuna dalili kuwa mapendekezo hayo huwa hayatekelezwi:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni mapendekezo gani yaliyotolewa na Tume baada ya uchunguzi wa vifo vya mahabusu na wafungwa vilivyotokea Novemba, 2002 katika Kituo cha Polisi Rujewa?

(b) Je, ni hatua gani za utekelezaji zimeshachukuliwa hadi sasa na kama bado hazijachukuliwa ni kwa nini?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imekuwa inatekeleza mapendekezo yanayotolewa na Taasisi zake ikiwemo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Aidha, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba baada ya vifo nya mahabusu na wafungwa viliwyotokea Novemba, 2002 katika Kituo cha Polisi Rujewa, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya aliunda Tume kuchunguza tukio hilo na sio Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Baada ya uchunguzi Tume hiyo ilitoa mapendekezo mengi ambayo siwezi kuyanukuu yote lakini baadhi yake ni kama yafuatayo:-

(i) Vyombo nya dola vielekeze kupeleka kesi nyepesi zinazoweza kumalizika nje ya Mahakama kwenye vyombo nya Usuluhishi na Mabaraza ya Kata pia Polisi na Mahakama wasiweke vikwazo kwenye dhamana.

(ii) Serikali iongeze idadi ya Mahakimu na Mahakama za Mwanza, Wilaya, Mkoa na Majaji wa Mahakama Kuu.

(iii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ipeleke magari imara ya kubeba wafungwa /mahabusu kutoka Magereza kwenda Mahakamani.

(iv) Watendaji wote watimize majukumu na wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapendekezo ya Tume, Serikali yenye we imekuwa ikichukua hatua endelevu za kuboresha suala zima la kupunguza msongamano katika Magereza yote ya Tanzania. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(1) Kuendelea kuimarisha mpango wa huduma kwa jamii.

(2) Kuendelea kuimarisha mpango wa *Parole* ambapo hautawahu wafungwa wa vifungo nya maisha ambao wamefanya makosa ya ujambazi, ubakaji na makosa ya madawa ya kulevya.

(3) Serikali imetunga sheria ili kuhamisha jukumu la kuendesha mashtaka kutoka katika vyombo ya upelelezi kwenda kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

(4) Kuongeza idadi ya Majaji na Mahakimu ili kuharakisha usikilizaji wa kesi sambamba na Jeshi la Polisi kuharakisha upelelezi.

(5) Kukabidhi jukumu la kuwasafirisha mahabusu kwa Jeshi la Magereza kwa kuanzia na Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla yale yote yaliyopendekezwa na Tume hiyo ya Mbarari ni changamoto kwa Serikali yetu na tunaendelea kuyafanya kazi kadri uwemo wa Serikali utakavyoruhusu. Aidha, kwa upande wa Wilaya ya Rujewa tayari Serikali imeshajenga Gereza ambalo linaweza kutunza jumla ya mahabusu 200 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuheshimu sheria za nchi na haki za binadamu mara baada ya tukio hilo Serikali iliyafikisha Mahakamani Askari wote watano waliohusika na tukio hilo. Shauri hilo lilisikilizwa katika Mahakama Kuu ya Kanda ya Mbeya na mnamo tarehe 14 Desemba, 2007 ambao ni mwaka jana tu, askari mmoja alipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha miaka sita na wakati huo wakati kesi ilikuwa inasikilizwa Askari wawili walifariki na Askari wengine wawili waliachiwa huru.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imekiri kuongeza mabweni kwa ajili ya wafungwa na mahabusu na kwa kuwa mabweni hayo huwa ni mafupi kwenda juu na pia huwa hayana madirisha ya kuingiza hewa ya kutosha. Je, Serikali sasa iko tayari kujenga mabweni mrefu kwenda juu na kuongeza madirisha ili kuweza kupitisha hewa ya kutosha? Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amesema kwamba watendaji wote wanatakiwa watimize majukumu na wajibu wao kwa ajili ya sheria iliyopendekezwa na Tume hiyo. (*Makofi*)

Je, kwa wale watendaji watakaokiuka majukumu hayo na sheria hiyo Serikali itawachukulia hatua kali za kinidhamu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabweni, nitakiri kwamba mabweni mengi ambayo tumekuwa nayo hapa nchini yamekuwa ni yale yaliyojengwa muda mrefu kwa hiyo hayakuwa katika hali na standard ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge, lakini yale ambayo yanajengwa kwa sasa hivi ama kwa nyakati za sasa yamekuwa ni tofauti na yamekuwa yakizingatia mambo mbalimbali hasa kuhusu afya za wafungwa na kuhusu mambo ambayo yanaweza kuwasaidia katika kupata hewa kama alivyosema na hilo linazingatiwa na ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuhusu hilo. Swali la pili la kuhusu watendaji, hapana shaka, sheria iko palepale wale ambao watakiuka utaratibu na sheria ambazo zimewekwa, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itachukua hatua dhidi kali dhidi yao kwa kushindwa kutimiza wajibu wao au kutotimiza wajibu wa sheria inavyoagiza.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali wakati tukio hili limetokea mwaka 2002 ilitoa tamko rasmi nami nimekuwa nikiuliza hili swali la mahabusu waliokufa Wilaya ya Mbarali takriban sasa miaka sita na majibu ambayo nimekuwa nikipata ni ya matumaini, Serikali itafanya, Serikali itafanya, lakini mwanzoni walisema Serikali inasubiri kesi iishe na kwa sababu sasa kesi imekwisha.

Je, Serikali sasa haioni ni busara aidha kwa kutoa kauli ndani ya Bunge ili wananchi wa Mbarali walioathirika wajue Serikali inawapa matumaini gani? Kwa sababu iliahidi kwamba itatoa angalau kifuta machozi na ahadi hii ilitolewa na Waziri Mkuu wa nchi ya Tanzania. Sasa angalau itoe kauli kwamba lile tukio lililotokea lilikuwa ni tatizo kubwa na ni aibu kwa Serikali na kwa watumishi wa Serikali. Naomba Serikali itoe kauli ili wananchi wajue matumaini yao ni nini. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba majibu yawe mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hili suala ameliuliza mara kadhaa yeze mwenyewe binafsi na leo tumeshuhudia hili suala ambalo limeulizwa leo asubuhi. Napenda kusema kwamba Serikali ilikuwa inangoja hatma ya suala hili Mahakamani na hiyo kwa kweli imefanyika. Kuhusu tamko la Serikali nitasema kwa kuwa tamko liliwishawekwa bayana kama aliviyotajwa Waziri Mkuu aliyejita, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itakwenda kwa mujibu wa tamko hilo na kuhakikisha kwamba inatimiza yale ambayo Waziri Mkuu aliyatamka.

Na. 145

### **Fidia kwa Wananchi waliobomoa Nyumba zao**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2004 Serikali iliamua nyumba zilizowekewa alama ya X zibomolewe kuruhusu upanuzi wa barabara huko Kigoma Vijijini; na kwa kuwa, baadhi ya wananchi walitekeleza agizo hilo na kubomoa nyumba zao, na kwamba, nyumba ambazo hazikubomelewa mwaka 2007 ziliwekewa alama ‘L’ kwa ajili ya kupewa malipo pasipo kwanza kuwalipa wale waliokwisha bomoa nyumba zao:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwalipa hao wananchi walikwisha bomoa nyumba zao kwa sababu wanajulikana idadi yao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili, Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria Na. 167 ya mwaka 1967 ya Hifadhi ya Barabara; Serikali ilitoa maelekezo mwaka 2004 ya kuweka alama za ‘X’ nchi nzima kwenye mali za kudumu yakiwemo majengo katika hifadhi ya barabara. Utekelezaji wa zoezi hili ulihusisha pia maeneo yaliyopo kwenye barabara ya Kigoma-Ilunde ambako baadhi ya wananchi walioguswa na zoezi hilo waliamua mara moja kutekeleza kwa kubomoa majengo yao yaliyokuwa yameainishwa kuwemo kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelekezo hayo ya kuweka alama za ‘X’ nchi nzima Serikali baadaye ilitoa ufanuzi wa kuwa wananchi waliowekewa alama za ‘X’ kwenye majengo yao waendelee kubaki mpaka wakati wa kuijenga barabara husika utakapowadia. Ni kutokana na hali hiyo, mwaka 2007 wakati barabara ya Kigoma-Ilunde yenye urefu wa kilometra 136 ilipofanyiwa usanifu kwa ajili ya kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami; Serikali ililazimika kuweka alama nyingine

mpya zenyenye kuainisha baadhi ya maeneo mapya yaliyopitiwa na ujenzi wa barabara na hivyo wahusika kustahili kulipwa fidia.

Kwa hiyo, wanaostahili kulipwa fidia ni wale tu ambao mwelekeo mpya wa barabara umewafuata. Lakini kwa wale wananchi walioamua kubomoa nyumba zao kufuatia tahadhari waliyopewa ya kuondoka katika eneo la hifadhi ya barabara hawastahili fidia yoyote kwa vile walifanya hivyo kwa kutekeleza matakwa ya sheria.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa Naibu Waziri aliyejekwepo siku za nyuma alifuatwa na ujumbe kutoka Kata ya Kalindi Kigoma Vijijiini wakifuatana na Mbunge wa Kigoma Kusini, aliwaeleza kuwa hizo nyumba zilizowekewa alama ‘X’ zitatazamwa upya. Sasa huo mtazamo utakuwa lini?

(b)Katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri mwaka 2007 katika swali langu la msingi alijibu kuwa wale waliowekewa alama ya ‘X’ hicho ni kiashirio tosha kabisa ilitakiwa waanzishe kubomoa nyumba zao wakati wowote, na ni lini Serikali ilitoa agizo kuwa wakati huo upanuzi umesimamishwa mpaka hapo Serikali itakapoamua tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba waniambie tarehe ngapi na mwezi gani na mwaka gani? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ujumbe huo ultumwa ukaja kumwona Waziri au Naibu Waziri kufuutilia jambo hilo. Lakini kama majibu yalikuwa cha muhimu ni kutazama upya nadhani ni katika msingi ule lule wa maelezo hayo niliyoyaeleza hapa ya kwamba baada ya kuwekwa hizo alama za ‘X’ nchi nzima.

Lakini baadaye Serikali ilitoa maelezo ya ufanuzi kwamba kuwekwa kwa alama za ‘X’ haina maana basi waweze kuondoka mara moja, basi waendelea kubaki pale mpaka hapo usanifu yakinifu wa barabara husika utakapokuwa unafanyika ndipo waweze kuwa wanaondoka. Lakini wakati huo baadhi ya watu raia wema walikuwa wamekwishatekeleza agizo hilo, na kwa hiyo wale waliokuwa wamekwishatekeleza agizo hilo sisi tunawapongeza tu kwamba waliitikia sheria hii kwa nia njema.

Lakini vilevile, kama alivyokuwa amesema Mheshimiwa Mbunge kwamba wale waliowekewa alama za ‘X’ wanasubiri mpaka barabara zitakapokuwa zimepatiwa fedha za kuweza kutengenezwa ndipo hapo sasa wanaweza wakataarifiwa kwamba aidha, wapo kwenye Hifadhi hiyo ya barabara au sivyo. Kama hivyo ilivyojitekeza katika barabara hiyo ambayo sasa hivi inaendelea kujengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri muda wangu ni mdogo. Kwa hiyo, unaweza kusema kidogo.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitachukua muda mfupi sana kutoa maelezo ya ziada kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Sijapata Nkayamba ambaye ameuliza kwamba ni lini Serikali imetoa tangazo hilo kuwajulisha watu kwamba wanaweza kuendelea kukaa wakati miradi hiyo inaasisiwa. Ilivyokuwa kuwa Wizara ya Ujenzi ilitoa taarifa rasmi kwamba Vyombo vya Habari na nakala yake ninayo hapa tarehe 20 Mei, 2004 na kibwagizo kinachohusiana na kauli hiyo kinasema kwamba:

“Hata hivyo, kwa kuzingatia ubinadamu wa Serikali yetu; na kwa kuwa zoezi hili halilengi kuwakomoa wananchi katika maeneo ambako hakuna miradi inayokusudiwa kutekelezwa katika siku za karibuni, nyumba na mali za wahusika hazitabomolewa kwa sasa hadi hapo eneo hilo litakapohitajika yaani baada ya fedha za kutekeleza miradi ya barabara husika kupatikana.” Hilo ni tangazo la Serikali ambalo lilitolewa kweney Vyombo vya Habari. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 146

### **Barabara ya Kagoma – Lusahunga**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imesitisha ujenzi wa barabara ya Kagoma- Lusahunga iliyokuwa inajengwa kwa kiwango cha lami:-

- (a) Je, ni lini Serikali inakusudia kuendelea kujenga barabara hiyo?
- (b) Je, wale watanzania waliokuwa wakifanya kazi za vibarua mbalimbali kama vile ulinzi n.k, ambao wameachwa bila kulipwa madai yao sasa watalipwaje, na ni nani atakayewalipa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Kagoma – Lusahunga yenye urefu wa kilometra 154 ni sehemu ya mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mutukula –Lusahunga yenye urefu wa kilometra 292. Ujenzi wa barabara ya Mutukula –Lusahunga unafanyika kwa awamu. Awamu ya kwanza ilikuwa ni sehemu ya Mutukula – Muhutwe na awamu ya pili ilikuwa ni sehemu ya Muhutwe – Kagoma ambao ujenzi wake ulikamilika mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi wa awamu ya tatu ya sehemu ya Kagoma – Lusahunga ulitiwa saini tarehe 13 Machi, 2006 kati ya Wakala wa Barabara (*TANROADS*) na Kampuni ya ukandarasi ya *China State Construction Engineering Corporation* ya China, na kazi ya ujenzi ikaanza mwezi Aprili, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya Mkandarasi katika ujenzi wa barabara hiyo ilikuwa ndogo, na mara kadhaa alionya na kutakiwa ajirekebishe ili ujenzi uweze kukamilika katika muda uliopangwa. Pamoja na maonyo na ushauri aliopewa maendeleo ya ujenzi yaliendelee kusuasua kiasi kwamba hadi kufikia Desemba 2007, utekelezaji ulikuwa chini ya asilimia 15 wakati muda uliotumika ulikuwa ni zaidi ya asilimia 50. Hali hii haikuleta matumaini ya kukamilika kwa mradi huu na ilipofika mwezi Februari, 2008 Serikali ilichukua hatua ya kumuachisha kazi Mkandarasi huyo na kumuondoa katika eneo la mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kumpata Mkandarasi mwengine kwa ajili ya kuendelea na ujenzi umeanza ambapo utayarishaji wa nyaraka za zabuni umeanza na uko katika hatua za mwisho. Mara baada ya ukamilishaji wa nyaraka hizo, zabuni zitaitishwa na inatarajiwu Mkandarasi mwengine atapatikana ifikapo mwezi Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malipo ya vibarua, Wakala wa Barabara Mkoa wa Kagera amefuatilia suala hilo, kwa kuwataka wale wote waliokuwa wameajiriwa na Mkandarasi huyo wawasilishe vielelezo vyta ajira zao ikiwa ni pamoja na Mikataba ili Serikali iweze kutoa msukumo wa malipo toka kwa Mkandarasi. Jitihada hizo hazijatoa mafanikio kutokana na kukosekana kwa vielelezo muhimu vinavyothitibitisha kuajiriwa kwa wafanyakazi hao na Mkandarasi huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa vielelezo hivyo kumefanya iwe vigumu kwa Serikali kufuutilia malalamiko yao ya kutolipwa kiinua mgongo na mafao mengine. Hata hivyo, Serikali bado iko tayari kuendelea kusaidia tatizo hilo pindi vielelezo hivyo vitakapopatikana.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

La kwanza, barabara inayotoka Kagoma kwenda Lusahunga ni barabara inayopita katika eneo lenye mawe magumu na linalotunza maji kwa wingi na kuna umbali mrefu kutoka Kagoma kwenda mpaka Lusahunga ni kilomita 154.

Je, Serikali ikiyazingatia hayo kipindi inapotarajia kuleta hivo mkandarasi mwengine itahakikisha kwamba imeigawa vipande vipande hiyo barabara ili iweze kutengenezeka kwa haraka na kumalizika?

La pili, kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba imeshindwa kupata takwimu halisi zenyе vielelezo vya wale wafanyakazi ambaо walikuwa ni vibarua; na kwa kuwa Serikali imekwishatoa utaratibu kwamba katika ajira zote zinazofanyika katika miradi ya nchini, vibarua na hao wafanyakazi wenye utaalam wa kitanzania lazima watoke Tanzania.

Je, ni kwa nini Serikali inapokuwa inasaini mikataba hiyo haitoi nafasi ya kuanzisha utaratibu wa kuweka taratibu za wafanyakazi ili kuweza kujulikana kwamba nani kibarua na nani mtaalam na takwimu zao zikawa zinajulikana pale kuondokana na utaratibu uliopo sasa hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo swalı la kwanza, mimi sijasema kwamba Serikali imeshindwa isipokuwa Serikali imekuwa ikihimiza vielelezo hivyo vipatikane kwa maana ya kwamba wale waajiriwa kwa sababu ilikuwa kati ya mwajiriwa na mwajiri yaani mkandarasi, waweze kuvipata hivyo vielelezo ili Serikali iweke msukumo. Kwa hiyo, bado ninasisitiza tu kwamba kama kuna uwezekano wowote na mtu yejote anaweza kuwasaidia hao ili vielelezo hivyo vipatikane Serikali iweze kuwasaidia waweze kupata malipo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili swalı la pili, la kuweka maelekezo kwenye mikataba ili wafanyakazi waweze kupatikana ambaо ni wazalendo, nadhani ndivyo ilivyofanyika kwa sababu vinginevyo hao watumishi wasingeweza wakapatikana kama kungekuwa hakuna mwanya wa kuwaajiri hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lililokosekana hapo ni yale tu mapatano kati ya waajiriwa na mwajiri kutokuweka kumbukumbu wakati walipokuwa wanaajiriwa.

Na. 147

### **Miradi ya Kupeleka Umeme Wilayani Kisarawe**

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO** aliuliza:-

Kwa kuwa, maeneo mengi ya Wilaya ya Kisarawe yamekosa umeme kwa muda mrefu na hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya Wilaya hiyo; na kwa kuwa, mwaka 2005 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaahidi wananchi wa maeneo ya Mzenga, Maneromango na Masaki kuwa wataunganishiwa umeme haraka; na kwamba, pamoja na Mbunge wa Kisarawe kuikumbusha Serikali mara kwa mara kuhusu tatizo hilo bado Serikali haijaonyesha nia ya kutekeleza mradi huo:-

(a)Je, Serikali imepuuza maelekezo hayo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati huo?

(b)Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la umeme kwenye maeneo hayo?

(c) Je, kwa nini hadi leo Serikali haijajibu barua ya Mbunge wa Kisarawe ya tarehe 11 Februari, 2006 juu ya suala hilo?

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Said Janguo, Mbunge wa Kisarawe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijapuuza ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ya kuwapatia umeme wananchi wa maeneo ya Mzenga, Manerumango na Masaki. Ahadi hiyo ilizingatia vigezo mbalimbali kama mahitaji ya umeme kwenye mashule, vituo vya afya na mahitaji mengine yanayochangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya wakazi wa Wilaya hiyo. Utekelezaji wake umewekwa kwenye mpango wa utekelezaji wa miradi ya umeme nchini ambao unategemea upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kufikisha umeme maeneo mbalimbali nchini yakiwemo maeneo aliyyotataja Mheshimiwa Mbunge kwa lengo la kuwakwamua wananchi utoka katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu uliofanywa ulionyesha kuwa ili kupeleka kwenye maeneo aliyyotataja Mheshimiwa Mbunge inabidi kuongeza nguvu za umeme kutoka KV 11 kwa sasa kwa kujenga njia mpya ya umeme wa KV 33.

Vilevile inabidi kufanya ujenzi wa kilomita 20 za njia ndogo ndogo za kusambaza umeme kwenye vijihi alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, ufungaji wa transfoma nane katika vijihi hivyo na uejnzi wa *service line*. Mradi huo kwa ujumla wake unategemewa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 5.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia Serikali imetenga shilingi milioni 750 kupitia Mfuko wa Umeme Vijijini -REA ili kuhakikisha mradi unaanza kutekelezwa. Fedha hizi zitajumuisha gharama za upimaji wa kina na uagizaji wa baadhi ya vifaa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara yangu ilipokea barua ya Mheshimiwa Mbunge wa tarehe 11 Februari, 2006 iliyohusu mahitaji ya umeme katika vijihi vya Wilaya ya Kisarawe, na kuijibu tarehe 11/06/2008. Hata hivyo, ninaomba kukiri na ninamtaka radhi Mheshimiwa Mbunge kwa kuchelewa kujibu barua hiyo kwa wakati.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ambayo kidogo yanaridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo ya nyongeza.

La kwanza, barua yangu ilikuwa imeandikwa tarehe 11 Februari, 2006, lakini Wizara imejibu tarehe 11 Juni, 2008 miaka miwili na miezi minne. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna uzembe katika Wizara yake?

La pili, shilingi milioni 750 licha ya kwamba ni ndogo kati ya mradi ambaoukadiria kuwa bilioni 5.4, lakini fedha hizo zinategemewa kutoka katika Uhisan wa Sweden. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kuwathibitishia watu wa Kisarawe kwamba kati ya fedha hizo milioni 750 zilizopangwa yupo tayari kuongeza fedha ili kusudi kuweza kufanya upimaji wa kina na uagizaji wa vifaa vyote badala ya baadhi ya vifaa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Swali la kwanza amekwishakubali kwamba kuna uzembe. Sasa ajibu swali la pili. Si ndiyo maana ameomba radhi, maana yake kuna uzembe.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mradi huo unafanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2006 gharama za mradi wote ziliwa kama shilingi bilioni 2.5. Kwa sasa hivi kwa sababu ya kupanda kwa gharama za vifaa na kadhalika imefikia karibu bilioni 5. Sasa mradi wote wa Vijijini kupitia huo Mfuko wa REA umetenga kama bilioni 20 na miradi ni mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli kama tukitenga bilioni 5 tu kwa ajili ya mradi wa Kisarawe miradi mingine itakosa, na kwa sababu mradi huo wa Kisarawe utekelezaji wake ni wa muda mrefu. Wizara yangu imeona ni vizuri kwanza itenye hizo milioni 750 ambazo zitawezesha hatua za awali kufanyika kwa ufanisi. Halafu hapo baadaye kadri Mfuko wa REA unavyozidi kujazwa fedha kutokana na vyanzo mbalimbali vya Serikali tutazingatia utekelezaji wa hatua zinazofuata za mradi huo wa Kisarawe.

Na. 148

#### **Uhitaji wa Umeme - Ujiji Kigoma**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Kigoma - Ujiji uko kwenye giza kwa muda mrefu sasa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliondoa tatizo hilo kwenye kipindi kifupi kijacho cha mpango wa dharura?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Ujiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba tatizo la umeme wa Kigoma Ujiji ni tatizo la muda mrefu na limechangiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na miundombinu na mitambo chakavu na kwa maana hiyo uwekezaji katika maeneo hayo umekuwa duni. Mji wa Kigoma kuna jenerata 9 lakini zinazofanya kazi ni 6.

Jenereta hizo sita zinapofanya kazi zote zina uwezo wa kuzalisha umeme kati ya MW 2.8 na 3.0 Septemba, 2007 jenereta 4 kati ya hizo ziliharibika, zikabaki 2. Jenereta hizo 2 zilizoendelea kufanya kazi zikawa zinazalisha chini ya MW 1. Mahitaji ya umeme Kigoma Ujiji ni MW 5, hivyo ni dhahiri kulikuwa na uhaba mkubwa wa umeme uliosababisha kutoa huduma hizo kwa mgao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyojibiwa kwenye swali na. 128 liloulizwa na Mheshimiwa Mbunge Serukamba wakati wa Mkutano wa tisa kikao cha tisa cha tarehe 9 Novembra, 2007, Serikali imefanya jitihada za kuhakikisha tatizo la umeme katika Mji wa Kigoma Ujiji linatafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Kwa madhumuni ya udharura, ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali ilichukua hatua za kuzifanya ukarabati mkubwa jenereta zilizoharibika kwa kutumia spea zilizoagizwa kutoka nje ya nchi. Ukarabati ulikamilika Januari, 2008 wa jenereta nne, ambazo pamoja na zile mbili zinazalisha umeme wa MW 2.8 - 3.0.

Kwa hivyo basi, hadi sasa jenereta zinazofanya kazi ni sita na umeme unaozalishwa ni huo wa kukadiria MW 3.0. Ukiinganisha na mahitaji ya jumla ya MW 5, uzalishaji huo bado ni mdogo, lakini hukidhi mahitaji wakati ambao siyo wa mahitaji makubwa (*peak periods*). Wakati wa matumizi makubwa bado inalazimu kuwepo mgao. Kuna mpango wa kukarabati jenereta zingine mbili ambazo hazijafanyiwa matengenezo zenye uwezo wa kuzalisha MW 1.1 kwa pamoja. TANESCO katika bajeti yake ya ndani ya mwaka 2008 imetenga shilingi bilioni moja za ukarabati wa jenereta hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa muda mfupi ili kuondokana na tatizo ni kununua jenereta mpya ambapo Serikali imeshatenga kiasi cha *Euro* 8,130,600 sawa na shilingi 13,82,020,000/= kwa sasa kwa ajili ya kutekeleza mpango wa dharura unaolenga kuimarisha upatikanaji wa umeme Kigoma Ujiji. Wizara ya Fedha na Uchumi kuititia barua ya tarehe 16 Mei, 2008 ambayo Katibu Mkuu wa Wizara hiyo alimwandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, ilithibitisha kuwa inakubaliana na pendekexo la kutumia Akaunti ya Msamaha wa Madeni wa IMF (*MDRI*) kugharamia ununuzi wa mitambo mipy ya kuzalisha umeme katika Mji wa Kigoma Ujiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari TANESCO wako kwenye maandalizi ya kutangaza zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mitambo mitano yenye uwezo wa kuzalisha

jumla ya MW 6. Bodi ya Zabuni ilikaa tarehe 27/6/2008 ambapo pamoja na mambo mengine ilipitisha zabuni hiyo ili itangazwe. Ufungaji wa Mitambo hiyo unatarajiwu kukamilika mwishoni mwa mwaka 2009.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri ambayo yamekuwa yanajirudia kila nikiuliza swali hili, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipouliza swali hili Novemba, 9 mwaka jana nilijibiwa hapa ndani kwamba inapofika mwisho wa mwaka huu zitakuwa jenerata mbili zimefungwa, lakini leo sasa jibu linasema jenerata hizo zitakuwa zimefungwa 2009. Nilitaka kuuliza swali moja katika hili.

- (a)Je, sasa nichukue ipi jibu lile la Novemba ama jibu la leo? (*Makofi*)
- (b) Swali langu la msingi ni udharura lakini nikiangalia majibu ya Naibu Waziri sioni hapa kama kuna dharura. Sasa nataka kujua sasa Jambo la Kigoma limefanywa lisiwe dharura? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali ya shemeji yangu Mheshimiwa Peter Serukamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninayo *Hansard* ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini wakati akijibu swali hilo naomba kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa upungufu wa umeme wa Kigoma Serikali ina mpango wa kununua mtambo mpya wenye uwezo wa kuzalisha kiasi cha kilo watt 2000 ifikapo Desemba 2009. Makubaliano kati ya Shirika la *TANESCO* na Kampuni Agro Belgium *Cooperation* yameshakamilika na sasa kinachosubiriwa ni kuwekewa saini mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini bado kwa majibu haya mkakati ilikuwa ni kufikisha umeme huo Desemba 2009. Tumefanya tathimini mpya na tumekubaliana kwamba mahitaji ya Kigoma kwa kuangalia mahitaji ya sasa na mahitaji yanayokuja ukilinganisha pia mikakati mingine ya kitaifa inayofanywa kufungua *central corridor* lazima kutahitaji umeme mkubwa zaidi na hivyo ni vizuri kufanya maandalizi ya umeme mkubwa zaidi kuliko hizo *megawatt* mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mitambo inayonunuliwa inategemea kuzalisha *megawatt* 6 za nyongeza na hivyo umeme utakaokadiruwa kuwepo Kigoma baada ya kufunga mitambo hiyo ni mega watt 9. Tayari bodi ya *TANESCO* imefanya zabuni wiki iliyopita na sisi tunaendelea kulifuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu kwa pamoja na jibu la pili huo ni udharura naamini unakidhi kwa sababu miradi ya umeme siyo ya kukaa siku wiki moja au wiki mbili ni miradi ambayo utekelezaji wake ni miradi ya muda mrefu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Jamani muda hautoshi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakushukuru na nakuomba radhi kwa sababu ulishaamua tuendelee na safari. Nilikuwa nataka kuongezea majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu maswali ya nyongeza aliyouliza Mheshimiwa Peter Serukamba. Mimi nilijibu siku ile na ni kweli kama alivyo sema Mheshimiwa Naibu Waziri, tuliahidi kwenye swalii liloulizwa namba 128 kwenye Kikao cha 9 kwamba ufungaji wa mitambo ya kuzalisha *megawatt* 2 kwa maana ya *kilowatt* 2000 ungekamilika mwaka 2009 kwa hiyo, bado tuko kwenye kila ambacho tulikiahidi.

Lakini jingine ni la usikivu wa Serikali hii. Siku hiyo ya swalii alilouliza Mheshimiwa Peter Serukamba aliuliza akatupa changamoto kama Wizara kwamba mahitaji ya umeme yalikuwa yanazidi megawatt mbili ambazo sisi tulikuwa na mpango wa kuagiza huo mtambo. Kwa hiyo, baada ya hayo tukafikiria upya na ndiyo maana tumekuja sasa na suala la kuongeza mitambo yenye *Megawatt* 6 kufanya *megawatt* 9 lakini ukamilishaji unabaki pale pale mwishoni mwa Desemba mwaka 2009. Ahsante (*Makofii*)

Na. 149

#### **Mafunzo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilianzisha chuo kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, lakini mafunzo hayo yaliyolengwa kufanywa sanjari na yale ya ‘*diploma*’ yameachwa; na kwa kuwa, kuna upungufu wa zaidi ya Mahakimu 400 nchini na madhumuni ya chuo hicho cha Lushoto ilikuwa ni pamoja na kuziba pengo hilo la Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo:-

- (a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha malengo hayo yasifanikiwe?
- (b) Je, Serikali iko tayari kulambia Bunge hili mikakati yake ili tupate Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo?
- (c) Je, Serikali inaweza kutoa maelezo kwa nini imesitisha utaratibu huo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI- (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA  
NA SHERIA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Serikali ilianzisha Chuo cha Mahakama Lushoto kwa madhumuni ya kutoa mafunzo kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ilil kuziba pengo kubwa la upungufu wa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo. Hata hivyo, lengo hili limeshindwa kufanikiwa kwa sababu siyo wahitimu wote wanaomaliza mafunzo wanaoajiriwa kama Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuptia Mahakama ina mikakati ya kutatua tatizo la upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kwa kuajiri wahitimu wa Stashahada ya Sheria kutoka Chuo cha Lushoto hasa amba wanajisomesha wenyewe na wale wanaomaliza katika vyuo vingine. Pia Serikali ina makakti wa kuongeza uadhamini wa wanafunzi amba wakimaliza masomo yao wataajiriwa na Mahakama moja kwa moja tofauti na ilivyo sasa amba wahitimu wengi hawako chini ya udhamini wa Serikali na hivyo hawalazimishwi kuajiriwa na Mahakama. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali haijasitisha utaratibu huo bali inajitahidi sana kuuboresha ili kufikia malengo yanayotarajiwa.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa majibu yake. Itakuwa inashangaza kuona kwamba Serikali imeweka mikakati ya makusudi kwa kufungua Chuo cha Lushoto ili kupunguza uhaba wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo nchini. Sasa inapokuwa kwamba chuo hicho kimefunguliwa kwa ajili hiyo na mikakati ikawa haitimizi lengo kidogo ina matatizo.

(a)Je, sasa hivi mmeweka taratibu zipi kuhakikisha kwamba upungufu wa mahakimu unakuwa unakamilisha kwa maana ya *crash program*?

(b)Je, zile mahakama za Mwanzo zilizokuwepo katika Wilaya ya Pangani kama vile kata ya Mkwaja na Madanga ambazo majengo yake yanaharibika kwa kukosa mahakimu mtatufanya utaratibu gani tupate mahakimu hao ili kuziba pengo hilo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA  
NA SHERIA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya Mohamed Abdallah, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi hamna wazo lolote la kufanya crash program kwa ajili ya kupata Mahakimu wa Mwanzo, ila utaratibu ulioko sasa hivi utaendelea wa kuendelea kupata wale wanaokamilisha mafunzo yao ya stashada ya sheria katika Chuo cha Lushoto na kuhakikisha kwamba wale wote tunawaajiri ikiwezekana kuwa Mahakimu wa Mwanzo.

La pili, nakubaliana naye kwamba kuna matatizo ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo kwenye Wilaya yake ya Pangani. Ninavyofahamu ziko Mahakama za Mwanzo kama 7 hivi lakini ni mahakama ya Mwanzo Mjini ndiyo ina mahakimu wawili ambapo mmoja naye pia amekwenda mafunzo. Tunamhakikishia kwamba katika mwaka huu wa fedha tunatarajia kuajiri Mahakimu wengi tu na jimbo lake la Pangani litapewa kipaumbele. (*Makofi*)

Na. 150

**Marekebisho ya Sheria Mbalimbali**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa sababu mojawapo ya msongamano magerezani unaotokana na baadhi ya sheria zilizopitwa na wakati kuendelea kutumika:-

- (a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kurekebisha sheria, kwa mfano zile zinazoweka adhabu ya kima cha chini ya miaka mitano kwa makosa ya aina zote kama vile za kuku, sungura, bata na ng'ombe?
- (b) Kwa kuwa, kwenye nchi nyingine tafsiri ya ukomo wa kifungo cha maisha imetajwa bayana kama vile miaka 20, 30, n.k. Je, ni nini tafsiri ya ukomo wa kifungo cha maisha kwa mujibu wa sheria zetu?
- (c) Je, ni lini Serikali itarekebisha sheria ya Parole ili iwe na wigo mpana zaidi kwenye kusaidia kupunguza tatizo la msongamano Magerezani?

**MWENASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Shabani Kwaangw' Mbunge wa Babati Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna msongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza mengi hapa nchini. msongomano huo unasababishwa na sababu nyingi ikiwemo uwepo wa sheria zililopitwa na wakati. Hata hivyo Serikali kuititia Tume ya kurekebisha Sheria imekuwa ikifanya kazi ya kubaini mapungufu katika Sheria mbalimbali hapa nchini, hili limekuwa jukumu la kudumu la Tume na pale inapobainika mapungufu katika Sheria yoyote Tume hupeleka mapendekezo ya malalamiko ya Sheria hizo ili zifanyiwe mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungo cha maisha kama kinavyoonekana katika baadhi ya makosa yaliyoainishwa katika baadhi ya makosa yaliyoainishwa katika Sheria za nchi haina tafsiri nyingine yoyote zaidi ya ile kifungo cha maisha. Kama mtu anaitiwa hatiani na mahakama kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifungo cha maisha basi mtu huyo akipewa adhabu hiyo atatumikia kifungo cha maisha yake gerezani. Aidha kwa sasa Serikali haina dhamira ya kurekebisha sheria ya Parole kwani sheria hii imefanyiwa marekebisho na hivyo kufanya wigo wa parole kupaniliwa. Serikali inaamini wigo uliowekwa na Sheria hiyo kwa sasa una kidhi haja na hivyo hakuto kuwepo mahitaji ya kufanya marekebisheso.

**MHE. OMAR S. KWAANGW'**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa Serikali imesema kwamba haina dhamira ya kurekebisha Sheria hii ya Parole kwa sasa kwa kuwa wigo wake unatosha ili tupime vizuri. Je, Serikali ipo tayari kutupa takwimu kabla pengine Mheshimiwa Waziri hajasoma Bajeti yake itakayoonyesha kwamba Sheria hii ya Parole imeweza kupunguza msongamano kwenye magereza mbalimbali nchini?

**MWENASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba Serikali ipo tayari itatoa takwimu kuhusiana na suala hilo la Parole kama ilivyoweza kupunguza msongamano wa mahabusu kule rumande hivi sasa.

Na. 151

#### **Idadi ya Watoto wa Mitaani**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Kwa kuwa Idadi ya watoto wa mitaani inazidi kuongezeka siku hadi siku, na kwa kuwa hali haionyeshi picha nzuri kwa Taifa letu.

(a)Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha hali hiyo kwa miaka ya hivi karibuni?

(b)Je, ni tabia gani ya jumla walizonazo watoto hao?

(c)Je, watoto hao ni wangapi kwa ujumla na Serikali ina mipango gani mahususi ya kuondokana na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** aliibuso:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a). (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za misngi zinazosababisha idadi ya watoto wa mitaaani kuongezeka miaka ya hivi karibuni ni pamoja na umaskini, mifarakano ya kifamilia, wazazi kutowajibika katika malezi ya watoto wao, ulaghai unaofanywa na watu wasio waaminifu wanaowatoa watoto vijijini kuja kuwafanyisha kazi zao mijini za biashara na nyingine zisizo halali kama vile biashara ya ngono na kuuza madawa ya kulevyta. Watoto wengine huenda mitaani kutokana na vitendo vya ukatili na unyanyasaji wanavyofanyiwa majumbani.

Aidha sababu nyingine ni vifo vya wazazi kutokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo UKIMWI na hatimaye walezi kuwanyang'anya watoto mali zao walizoachiwa na marehemu wazazi wao na hivyo baadhi ya watoto kukimbilia mitaani.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, tabia za ujuma walizonazo watoto hawa ni kuzurura na kuomba kuomba mitaani, tabia ya wizi na udokozi, lugha ya matusi, uchokozi, ujeuri, kutumia na kuuza madawa ya kulevyta na ukahaba.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna utafiti maalum uliofanywa kwa ajili ya kupata idadi ya watoto wa mitaani kwa nchi nzima. Kumekuwa na juhudhi mbalimbali zinazofanywa na Wizara na taasisi za Serikali, Mashirikia Yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya dini na watu binafsi kwa ajili ya kupata idadi ya watoto wa mitaani katika maeneo yao. Wadau hawa wamekuwa wanafanya tafiti zao kwa miji tofauti kwa malengo tofauti hivyo kutoweza kuonesha sura ya kitaifa ya tatizo la watoto wanaishi mitaani. Hata hivyo mazungumzo yanaendelea kati ya Wizara yangu na Shirika la *Internation Consortu for Street Children* la Uingereza kwa kupitia ubalozi wa uingereza kwa kupitia ubalozi wa uingereza kwa kufanya utafiti wa nchi nzima kwa lengo la kubaini ukubwa wa tatizo hili ili kuwa na mpango endelevu wa kutatua tatizo la watoto wa mitaani.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nina swalii moja la nyingeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya wazee huwafanya watoto wao kuwa vitega uchumi kwa kuwapeleka mabarabarani asubuhi ili waombe na jioni kukusanya mapato kwa matumizi ya familia je, Serikali haioni kama ipo haja sasa ya kuwafuatilia wazee hao wenye tabia mbaya ya kuwadhalilisha watoto na kuwapa adhabu kali ili waache mtindo huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna wazazi wengine ambaa wanaishi mijini na kwa sababu hawana ajira na hawa namna yoyote ile ya kujipatia kipato wanawapeleka watoto wao mitaani kwenda kuomba na kuleta chakula. Hii imedhuhirishwa kwa utafiti uliofanyika katika Wilaya ya Morogoro Mjini Mtaa wa kwa mahita ambapo asilimia 60 ya wazazi wanaoishi eneo la Chamwino walikubali kwamba wanawapeleka watoto wao kwenye kufanya biashara, kuomba omba na kuwalettea chakula kwa sababu hawana namna ya kuishi.

Ili kuweza kupambana na tatizo hili tunaona kwamba ni umaskini unafanya hivyo. Sasa Serikali ina mikakati ya kuhakikisha kwamba watu kama hao wanafuatiliwa ili waweze kusaidiwa wajisaidie na ndiyo sababu Wizara yangu ikishirikiana na *International Consortium for Street Children* imeamua kufanya utafiti shirikishi katika maeneo yote ya mijini ili tuweze kujua sababu zote ambazo zinaleta watoto mitaani na tuweze kupanga mikakati endelevu ambayo inaweza ikatoa jibu ambalo litapunguza hili tatizo. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Hili moja la Wizara ya Elimu naona sekretarieti yetu imefanya makosa. Imeleta maswali kumi na moja. Katika hali yoyote ile maswali maswali kumi na moja katika saa moja huwezi kwa hiyo hili kesho lipewe priority kwa sababu liliongezwa kimakosa.

Sasa tuna matangazo ya wageni. Kwenye Speaker's Galleries tuna mgeni wetu ambaye ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoka Marekani ni Mheshimiwa Edwin Kindler akiambatana na mkewe Lily. *We like you to rise up hands. Welcome to Tanzania in particularly to our house. Thank you very much. (Makofi)*

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu kwa sababu leo ni siku yake kwa hiyo amekuja Mama Saumu Kawambwa pamoja na watoto wake. Naomba wasimame walipo. Karibuni sana.(*Makofi*)

Halafu tuna mgeni wa Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje ambaye ni Naibu Waziri wa Miundombinu naye amemleta partner wake, maana yake mke wake. Mama Violet Chibulunje. Karibu sana mama.

Tunawageni wa Mheshimiwa William Lukuvi ni mke wake Bibi Jemina Lukuvi na watoto wao. Karibu sana.

Wageni wa Mheshimiwa Maria Hewa hawakufika nadhani itakuwa kesho.

Tunawageni wa Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka ni Ndugu Isaac Kalaiya Katibu wa Umoja wa Vijana wa CCM Morogoro Mjini, Mheshimiwa Emmy Kiula (Diwani), Mheshimiwa Sija Lukwale (Diwani) wanafuatana na Mheshimiwa Mkuu wa Msafara Bwana Kudra Mung'ong'o Katibu Mwenezi wa CCM Morogoro Mjini. Naomba wasimame hao wote. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Mzeru Nibuka. Karibuni sana.(*Makofi*)

Tunawageni wa Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi ni dada yake na mtoto wa dada yake. Naomba wasimame walipo. Tuna wanafunzi 20 kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine SUA naomba wasimame pale walipo. Karibuni sana tunawashukuru kwa kazi mnayofanya na msome kwa bidii ili mje mtusaidie.

Tuna wanafunzi 21 kutoka *CBE* ambao wanaendelea na mafunzo kuhusu Bunge wanaongozwa na Mkuu wa Msafara wa Spika wa Bunge lao Bwana Adam Gidioni.

Karibuni sana, ahsante sana. Spika ndiyo yupi sasa. Huwezi kujua siku moja unaweza kuja kukaa kwenye Ukumbi huu, hapa tulipo.

Baada ya kusema hapa naomba nitangaze shughuli za kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Mheshimiwa Anne Kilango Malecela anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane kwa ajili ya Kikao kifupi mchana saa saba katika chumba namba 220.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge juzi wakati Mwenyekiti Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid anaongoza Kikao alikuwa ameahidi kwamba ufanuzi wa kuhusu Kanuni ya 63 ungetolewa. Kwa hiyo utatolewa kabla ya mwisho wa wiki hii.

Tunajaribu kuangalia Kanuni yote nzima kwa sababu inawachanganya Wabunge wengi. Kwa hiyo tunaiangalia vizuri tuweze hata kutoa hand out kuhusu Kanuni ile ya 63. Kwa hiyo muwe na subira majibu yatatolewa.

Baada ya kusema hivyo mnafahamu tunao wale wageni wa Tume ya Bunge kutoka Kenya tutakuwa na mazungumzo sasa na mimi kama mnavyofahamu mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Kwetu.

Kwa hiyo nitamwomba Mwenyekiti aweze kunipokea ili nihudhulie kile Kikao.

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Agenda inayofuata.

**HOJA ZA SERIKALI  
Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 Wizara ya  
Maendeleo ya Miundombinu**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kipindi cha maswali na majibu kukamilika, sasa nitamwita mtoa hoja wa asubuhi hii, naye ni Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ili aje mbele, asome hotuba yake ya bajeti, inayohusu Wizara yake ya Miundombinu, Mheshimiwa Waziri, karibu!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2008/2009. Awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika. Kuteuliwa kwake kumedhihirisha imani kubwa waliyo nayo viongozi wa nchi za Afrika kwake binafsi na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa heshima kubwa aliyonipa kwa kunateua kuongoza Wizara hii nyeti ya Miundombinu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na watanzania wote kwa ujumla kwamba nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kuhakikisha kuwa nafanikisha malengo ya Wizara hii na ya Taifa kwa ujumla. Aidha, naendelea kuwashukuru wananchi wa jimbo la Bagamoyo kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kuteuliwa na hatimaye kupitishwa kwa kura nyingi na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa 10 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliopewa nyadhifa za kuongoza Wizara hii pamoja na Wizara nyingine mbalimbali katika Serikali hii ya Awamu ya Nne. Napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Benedict Ole Nang'oro (Mb) kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto. Ushindi alioupata umeonyesha imani kubwa waliyo nayo wananchi kwa Chama Cha Mapinduzi na kwake pia. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Al-Shaymar Kwegyir (Mb) na Mchungaji Dr. Getrude Lwakatare (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa CCM.

Napenda pia kumpongeza Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kuchaguliwa kushiriki kwenye Kamati ya Sekta hii. Napenda kuishukuru kwa dhati Kamati hii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga (Mb), Mbunge wa Singida Kusini kwa ushirikiano na ushauri ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha utendaji wa Wizara na sekta kwa ujumla. Aidha, naishukuru pia Kamati ya Mahesabu ya Serikali (PAC) iliyoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. John Momose Cheyo (Mb) kwa kutembelea na kukagua Miradi hususan ile ya barabara. Ziara hizi zimetoa changamoto ambazo zinaisaidia Wizara kufikia malengo yake hivyo nawashukuru wanakamati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa: Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa ujumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009. Aidha, napenda kuwashukuru

Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba za Mawaziri waliotangulia. Maoni ya Wabunge hao yamesaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya Miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya ilani ya uchaguzi ya ccm ya mwaka 2005 na utekelezaji wake. Iani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilielekeza sekta ya Miundombinu, itekeleze maeneo muhimu yafuatayo::

“Barabara:

(a) Kuendeleza na kuimarisha Mfuko wa Barabara (*Tanzania Road Fund*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uimarishaji wa Mfuko wa Barabara, Serikali imeidhinisha mapendekezo ya jinsi ya kuongeza mapato ya Mfuko kwa ajili ya matumizi endelevu ya barabara ambapo tozo ya mafuta (*fuel levy*) kwa Mfuko wa Barabara iliongezwa kufikia shilingi 200 kwa lita badala ya shilingi 100 kuanzia mwaka 2007/08. Hatua hii imeongeza mapato ya Mfuko ambayo kwa sasa yanafikia shilingi bilioni 218 kwa mwaka. Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vingine vitakavyochangia mapato kwenye Mfuko huu ili kuongeza uwezo wa kuzifanyia matengenezo barabara zetu.

(b) Kukamilisha ukarabati wa barabara zote amba o unaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami amba o umekwishaanza katika barabara kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara iliyolekezwa kukamilishwa ambayo utekelezaji wake uliana toka Serikali ya awamu ya tatu ni 17. Kati ya miradi hiyo, miradi 11 imekamilika ikiwa ni asilimia 65 ya miradi iliyopangwa kutekelezwa. Aidha, miradi 6 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. (*Makofi*)

Serikali tayari imekamilisha ujenzi wa miradi ya barabara za:- Singida – Shelui (km 110), Shelui – Igunga (km 32), Igunga – Nzega – Ilula (km 215), Muhutwe – Kagoma (km 24), Nangurukuru – Mbwemkuru – Mingoyo (km 190), Mkuranga – Kibiti (km 79), Pugu – Kisarawe (km 6), Chalinze – Morogoro – Melela (km 130), Tunduma – Songwe (km 104), Kiabakari – Butiama (km 17) na Dodoma – Morogoro (km 256). Miradi sita (6) ambayo imeanza na inaendelea kujengwa ni:- Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 32), Mbeya – Chunya – Makongolosi (Mbeya – Lwanjiro km 36), Arusha – Namanga (km 105), ukarabati wa barabara ya Kilwa, DSM (km 11.6), Nelson Mandela DSM (km 115.6) na Sam Nujoma DSM (km 4). (*Makofi*)

(c) Kuendelea kuimarisha barabara nchini zitakazouunganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara za lami; zitakazouunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote pia kwa barabara za lami na kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya zote kwa barabara zinazopitika wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za kuiunganisha nchi yetu na nchi jirani zimeendelea kuimarishwa. Jitihada zinaendelea kuhakikisha kuwa kiungo cha barabara ya lami kati ya Tanzania na Msumbiji (Mangaka – Mtambaswala) kinaanza kujengwa kwa lami. (*Makofi*)

Aidha, nchi nyingine zilizobaki tayari zimeunganishwa kwa barabara za lami. Mikakati inaendelea ya kujenga barabara nyingine za mipakani kati ya Tanga na Horohoro (mpaka wa Kenya) na Mwandiga – Manyovu (mpaka wa Burundi) kwa kiwango cha lami. Aidha, Makao Makuu ya Mikoa yote ya Tanzania Bara imeunganishwa kwa barabara za lami isipokuwa Makao Makuu ya Mikoa minne tu ambayo ni:- Manyara, Rukwa, Tabora na Kigoma.

(d) Kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo; Tunduma – Sumbawanga, Marangu – Tarakea – Rongai, Minjingu – Babati – Singida, Rujewa – Madibira – Mafinga, Mbeya – Chunya – Makongorosi, Msimba – Ikokoto – Mafinga, Arusha – Namanga, Tanga – Horohoro na ukarabati wa barabara ya Kilwa, Dar es Salaam, barabara ya Mandela, Dar es Salaam na barabara ya Sam Nujoma, Dar es Salaam. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya miradi hiyo 11 mipyä ya barabara iliyoainishwa kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami, tayari miradi saba inaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami. Miradi hiyo ni:- Marangu – Tarakea – Rongai ambao uko katika hatua za kukamilishwa ujenzi, Minjingu – Babati – Singida tayari zabuni kwa ajili ya ujenzi zimekwishaitishwa na hivyo kutarajia kuanza kazi za ujenzi kabla ya mwisho wa mwaka 2008. Ujenzi wa barabara za Nelson Mandela na Kurasini – Mbagala (Kilwa Road) tayari umeanza kutekelezwa. Barabara ya Sam Nujoma ujenzi wake unaendelea na inatarajiwu kukamilika kabla ya mwisho wa Julai 2008. Katika barabara ya Mbeya – Chunya – Makongolosi, sehemu ya Mbeya – Lwanjilo tayari imepata mkandarasi na anaendelea na kazi za ujenzi. Kuhusu ukarabati wa barabara ya Arusha – Namanga, Mkandarasi yupo kwenye hatua ya kuanza kazi.

Miradi ambayo haijaanza ni: Tunduma – Sumbawanga (km 231), Singida – Babati - Minjingu (km 223), Rujewa – Madibira (km 146) na Tanga – Horohoro (km 65). Hata hivyo, kwa kutumia msaada wa Serikali ya Marekani kupitia ‘Millenium Challenge Corporation’ (MCC), Serikali imepanga kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara za Tunduma – Sumbawanga (km 224.5), Songea – Namtumbo (km 70), Peramiho – Mbinga (km 80) na Tanga – Horohoro (km 65).

(e) Kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu barabara kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zinazoendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu ni 8 kama ifuatavyo: Babati – Dodoma – Iringa (km528), Sumbawanga – Kigoma – Nyakanazi (km 829), Musoma – Fort Ikoma (km 64), Korogwe – Handeni – Kilosa – Mikumi (km 353), Nzega - Tabora – Sikonge - Chunya (km 599), Mtwara – Masasi – Songea -Mbamba Bay (km 829), Manyoni – Itigi - Tabora (km 249), na Ipole – Mpanda – Kigoma (km 582). Barabara zilizokamilisha upembuzi yakinifu ni 2 ambazo ni; Maganzo – Maswa – Bariadi – Mkula – Lamadi (km 171), na Bagamoyo – Saadan - Tanga (km150).

(f) Kuhimiza maandalizi na ujenzi wa Daraja la Kigamboni chini ya uongozi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kuunganisha Kigamboni na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshiniwa Mwenyekiti, mchakato wa maandalizi ya ujenzi wa daraja la Kigamboni limechukua muda mrefu. Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) bado liko katika mchakato wa kukamilisha taratibu za kumpata mbia kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili la Kigamboni. Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na NSSF kwa pamoja zinaendelea kukamilisha taratibu za kumpata mbia wa kushirikiana kwenye kazi ya ujenzi wa daraja hili.

(g) Kuhakikisha upatikanaji wa kivuko kipyga cha Kigongo – Busisi (Mwanza).

Mheshimiwa Spika, Kivuko kipyga cha Kigongo – Busisi kinachoitwa M.V. Misungwi chenye uwezo wa kubeba tani 250 kimekamilika na kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 12 Mei, 2008.

(h) Kukamilisha ujenzi wa daraja jipya la Mpiji ambalo litawezesha njia mbadala ya Dar es Salaam – Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba ujenzi wa daraja la Mto Mpiji katika barabara ya Dar es Salaam-Bagamoyo ulikamilika mwaka 2005.

(i) Kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na ujenzi wa daraja la mto Kilombero na kukamilisha ujenzi wa daraja la mto Mwatisi katika mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu wa daraja la Mto Kilombero umekamilika. Hatua inayoendelea ni usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni za ujenzi wa daraja. Kuhusu daraja la Mto Mwatisi kazi ya usanifu wa kina imekamilika na ujenzi utaanza mwaka 2008/09. (*Makofi*)

(j) Kufanya usanifu wa daraja jipya la Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa daraja la mto Ruvu ulianza Mei, 2006 na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2008.

(k) Kuendelea kuandaa mazingira mazuri ya kuishirikisha sekta binafsi katika ujenzi na matengenezo ya barabara kwa kutumia mfumo wa Jenga, Endesha na Kabidhi (BOT).

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasimu ya Sera ya Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika ujenzi na matengenezo ya barabara kwa kutumia mfumo wa Jenga, Endesha na Kabidhi (BOT) imekamilka. Sera hii itatoa mwongozo wa jinsi ya kuishirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(l) Kuanza ujenzi wa Daraja la Umoja (Tanzania na Msumbiji).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ujenzi wa Daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji ilianza mwaka 2005 na imekamilika kwa asilimia 63. Daraja hili linatarajiwu kukamilika mwaka 2009.

(m) Kuanzisha programu ya Taifa ya Usafiri Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuchangia katika Programu ya Taifa ya Usafiri Vijijini kwa kuendesha mafunzo ya matumizi ya nguvu kazi katika ujenzi wa barabara vijijini (*Upscaling of Labour Based Technology Programme*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri na Uchukuzi. kwa upande wa Usafiri na Uchukuzi, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilielekeza sekta hii kuchukua hatua zifuatazo:

(a) Kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa lengo la kulipa uwezo wa kutoa huduma bora kwa bidhaa na abiria wa ndani na wa nchi jirani. Pia Shirika litaendeleza kama mhimili wa mpango wa maendeleo wa eneo la Ukanda wa Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha mchakato wa kukodisha Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) ambayo ilianza kuendesha shughuli zake tarehe 1 Oktoba, 2007. Kampuni hii ni ya ubia kati ya Serikali ya Tanzania kwa asilimia 49 na M/S RITES ya India kwa asilimia 51. Aidha, Serikali imeanzisha Kampuni ya kusimamia rasilimali na miundombinu ya reli kwa niaba yake. Kampuni hiyo ijulikanayo kama “*Reli Assets Holding Company (RAHCO)*” ina jukumu pia la kuendeleza miundombinu ya reli kwa niaba ya Serikali.

(b) Kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (TAZARA) ili liweze kuhimili kwa uwezo mkubwa zaidi majukumu ya kuboresha huduma kwa bidhaa na abiria na kusaidia shughuli za uendelezaji wa mpango wa eneo la Ukanda wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Tanzania na Zambia zinaendelea na mchakato wa kuishirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za TAZARA. Mawasiliano yanaendelea kati ya nchi hizi na China pamoja na Wadau wengine ili wakubali kushiriki katika kuendesha shughuli za MAMLAKA.

(c) Kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya za Arusha – Musoma, Isaka – Kigali na eneo la Ukanda wa Mtwara, ambayo itaunganisha Bandari ya Mtwara, Songea, Mbamba Bay, Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa reli ya Arusha – Musoma umejumuishwa katika Mpango Kamambe wa Reli ya Afrika Mashariki (*East African Railway Master Plan*) ambao unaendelea kukamilishwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mpango huu utawezesha utafutaji wa fedha kwa pamoja kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya reli za Afrika Mashariki. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya reli ya Isaka – Kigali

ambayo itaziunganisha nchi za Tanzania, Rwanda, na Burundi inaendelea na Mtaalam Mwelekezi DB International wa Ujerumanu anatarajiwa kukamilisha kazi yake Agosti, 2008.

(d) Kuimarisha bandari za Kigoma na Kasanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*) imeendelea na kazi ya kuziboresha bandari za Kigoma na Kasanga katika Ziwa Tanganyika ili kuwa na uwezo wa kuhudumia abiria na mizigo kwa wingi zaidi. Kuhusu kuongeza kina cha maji, katika bandari ya Kigoma, *TPA* wamenunua mtambo wa kuondolea mchanga (*dredger*) ambao unategemewa kuwasili Julai, 2008 na kufanyiwa majoribio kabla ya kuanza kazi. Aidha, kazi ya kukarabati gati ya Kasanga ilikamilika Novemba, 2007. Kazi inayoendelea sasa ni kufanya usanifu kwa lengo la kupanua gati hii ili kuruhusu meli mbili kutia nanga kwa wakati mmoja.

(e) Kuvutia wawekezaji katika miundombinu ya uchukuzi ya reli, anga na maji katika kanda za maendeleo ili kuimarisha biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda za Maendeleo zimeendelea kuimarishwa kwa kuboresha miundombinu ya reli, barabara pamoja na bandari. Juhudi mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa za kuboresha barabara zinazounganisha nchi za Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Watu wa Kongo kuitia Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Kigoma na Kasanga. Aidha, katika kuendeleza Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara Serikali za Tanzania na Msumbiji zimeendelea na ujenzi wa Daraja la Umoja katika mto Ruvuma litakalounganisha nchi hizi mbili. Juhudi zinaendelea kuchukuliwa kuwezesha ujenzi wa barabara kutoka bandari ya Mtwara hadi bandari ya Mbamba Bay ili kufungua fursa za ushirikiano wa kibiashara na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia.

(f) Kuendelea kuutengenezea mazingira mazuri ya kibiashara Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (*JNIA*) inaendelea ikiwa ni pamoja na matengenezo ya maegesho ya ndege, upanuzi wa barabara ya pili ya kurukia na kutua ndege, mfumo wa umeme pamoja na uboreshaji wa mazingira. Miradi mingine ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa jengo la abiria (*Terminal 3* na jengo la mapokezi ya Viongozi Wakuu). Aidha, taratibu za kulipa fidia kwa viwanja vya Pugu, Majohe na Buyuni kwa ajili ya makazi ya wananchi wa Kipawa, Kigilagila na Kipunguni ili kupisha upanuzi wa Kiwanja zinaendelea.

(g) Kukamilisha ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe na kuimarisha viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe unaendelea. Kazi zinazoendelea ni kumalizia tabaka la mwisho la changarawe na kuweka lami katika barabara ya kutua na kurukia ndege pamoja na viungio na maegesho ya ndege, kuweka lami barabara ya kuingia kiwanjani (*access road*) pamoja na barabara nyingine ndani ya kiwanja. Kazi nyingine ni kukamilisha baadhi ya majengo ikijumuisha jengo la abiria na kununua mitambo ya mawasiliano. Kazi hizi zimepangwa kuanza Julai, 2008 na kukamilika ndani ya miezi 24.

Kuhusu viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora na Shinyanga, kwa sasa watalamu wanaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu katika viwanja hivyo vitatu. Kazi hii inatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, 2008 na kazi itakayofuata ni usanifu wa kina kabla ya ujenzi kuanza.

(h) Kutekeleza Mradi wa Mabasi ya Usafiri wa Haraka Dar es Salaam

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi zimeelekezwa katika kutekeleza mradi wa mabasi yaendayo kasi (*DART*) ambao utatekelezwa katika awamu sita. Awamu ya kwanza ya mradi inajumuisha upanuzi wa barabara za Morogoro, Kawawa na Msimbazi zote kwa pamoja zikiwa na urefu wa kilometra 20.9. Miundombinu ya mradi huu

itakayo jengwa ni njia maalum za mabasi, vituo vya mabasi 5, stesheni 29 na karakana 2 za mabasi. Ujenzi wa miundombinu unatarajiwu kuanza Septemba, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sekta ya miundombinu na changamoto zilizopo. Miundombinu ya uchukuzi imeendelea kuimariika. Hata hivyo huduma za uchukuzi na usafiri zimekuwa hazitoshelezi mahitaji. Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha miundombinu ya uchukuzi na huduma za usafiri ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Kwa upande wa miundombinu ya barabara changamoto ni kuhakikisha kuwa barabara zote zinapitika wakati wote pamoja na kupunguza msongamano wa magari katika miji. Aidha, Wizarainashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na wadau wengine katika kuhakikisha kuwa miundombinu na huduma za usafiri wa barabara zinaboreshwu hadi vijiji ambako wananchi wanategemea usafiri wa barabara katika shughuli za maendeleo.

Kwa upande wa miundombinu ya reli changamoto ni kuziimarisha na kuboresha njia za reli, mawasiliano na vitendea kazi vyake, na kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za usafiri wa reli. Jitihada zinazoendelea ni pamoja na kubadilisha mataruma yenye uwezo mdogo na kuweka mataruma yenye uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha huduma za usafiri wa Majini, Serikali inaendelea kujenga na kuimariisa magati katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Aidha, huduma za bandari zetu zinaendelea kuboreshwa kwa kuziongezea uwezo wa kuhudumia mizigo zaidi ikilinganishwa na hali ya sasa. Kwa mfano; katika bandari ya Dar es salaam kazi ya upanuzi wa eneo la bandari unaendelea ikiwa ni pamoja na kuanzisha maeneo mengine ya kuhifadhi kontena ndani na nje ya bandari. Maeneo hayo ni Ubungo na Kurasini ambayo yatasaidia kupunguza mlundikano wa mizigo na kontena bandarini.

Kuhusu usafiri wa anga changamoto zilizopo ni kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na viwanja vya ndege na mitambo ya mawasiliano ili kuimariisa usalama wa usafiri wa anga pamoja na kukidhi mahitaji ya watumiaji yatokanayo na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Katika sekta ndogo ya Huduma za Hali ya Hewa changamoto iliyopo ni kuboresha miundombinu iliyopo na kuongeza mingine pamoja na kuongeza idadi ya vituo vya utabiri wa Hali ya Hewa ili huduma hii iweze kuwafikia wananchi wengi na kwa wakati. Changamoto nyingine ni kupata Wataalamu wa kutosha na wenye ujuzi ili waweze kutumia miundombinu hiyo na kutoa taarifa sahihi kwa sekta za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2007/08 na malengo ya mwaka 2008/09. Katika mwaka 2007/08, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini yake na Wadau wa sekta iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kubuni Sera, Mikakati na programu za kisekta na kusimamia utekelezaji wake. Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za kisekta

zinaimarishwa na kuendelezwa kwa kuzingatia malengo ya kitaifa ambayo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (Vision 2025), MKUKUTA na Mkakati wa Kushirikiana na Wahisani (*Joint Assistance Strategy for Tanzania - JAST*). Wizara inaendelea na utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Bunge. Aidha, Wizara imezingatia miongozo na kanuni za kimataifa kama Malengo ya Milenia (*MDGs*), Mikataba na makubaliano ya Mashirika mbalimbali ya Kimataifa yanayohusu sekta zetu ikiwemo Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri Majini (*International Maritime Organisation- IMO*), Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga (*International Civil Aviation Organisation- ICAO*), Shirika la Kimataifa la Hali ya Hewa – (*World Meteorological Organisation – WMO*) na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji na ubunifu wa Sera za Sekta. Katika mwaka 2007/08, Wizara imeendelea na utekelezaji wa mikakati ya Sera zilizopo za Uchukuzi na Ujenzi. Utekelezaji wa mikakati umezingatia ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kuendeleza miundombinu ya uchukuzi. Aidha, Wizara inaendelea kuandaa Sera za sekta ikiwa ni pamoja na Sera ya Taifa ya Huduma za Hali ya Hewa, Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani na Sera ya Taifa ya Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi (*PPP*). Kwa ujumla Maandalizi ya Sera hizi yamefikia hatua nzuri na inategemewa kuwa zitapitishwa na Serikali na kuanza kutumika mwaka 2008/09. Madhumuni ya kutungwa kwa Sera hizi ni kuboresha utoaji huduma za Sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa anga, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi ili kuhakikisha kuwa huduma zinaboreshw. Mikakati mingine iliyotekelawa ni pamoja na kupitia upya makubaliano ya Usafiri wa Anga (*Bilateral Air Services Agreements-BASAs*) kati ya Tanzania na nchi nyingine au kuanzisha mikataba mipy ya usafiri wa anga. Aidha, Tanzania kwa kushirikiana na nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi chini ya Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kupitia mikataba ya usafiri wa anga kati ya nchi hizi ili kuioanisha na matakwa ya maamuzi ya Mawaziri wa Afrika wanaosimamia usafiri wa anga (*Yamoussoukrou Decision*) ya 1999 yanayohusu ulegezaji wa masharti ya usafiri wa anga kati ya nchi na nchi. Lengo ni kuweza kuvutia wawekezaji na kurahisisha usafiri wa anga katika nchi wanachama wa Jumuiya. Aidha Aprili, 2008, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China zilitiliana saini makubaliano ya usafiri wa anga yenye lengo la kutoa fursa kwa Kampuni za ndege za nchi hizi mbili kutoa huduma za usafiri wa anga kati ya Tanzania na China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urekebishaji wa taasisi za Wizara katika mwaka 2007/08, Wizara kwa kushirikiana na iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*) na sasa “*Consolidated Holding Corporation – CHC*” na wadau wengine iliendelea na zoezi la kurekebisha taasisi zilizo chini yake. Katika Mwaka 2007/08 Serikali ilikamilisha mchakato wa ukodishaji wa Shirika la Reli Tanzania kwa Kampuni ya Reli Tanzania (*TRL*) ambayo ni ya ubia kati ya Serikali ya Tanzania kwa asilimia 49 na *M/S RITES* ya India kwa asilimia 51. Aidha, Serikali ilianzisha Kampuni ijulikanayo kama “*Reli Assets Holding Company Ltd (RAHCO)*” yenye jukumu la kusimamia rasilimali na kuendeleza miundombinu ya reli kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Tanzania na Zambia zinaendelea na urekebishaji wa TAZARA, kwa kutafuta fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu na huduma. Hii ni kutohana na ukweli kwamba TAZARA inahitaji uwekezaji mkubwa na Serikali za Tanzania na Zambia hazina uwezo wa kifedha wa kuiendesha. Hivi sasa Serikali hizi zinaendelea na mazungumzo na Serikali na Wawekezaji wa China na wawekezaji wengine ili waweze kushiriki katika mchakato wa kuendesha TAZARA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Usafiri Dar es Salaam (*UDA*), Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa linakuwa na mtaji wa kutosha ikiwa ni pamoja na kulifutia madeni ili kusafisha Mizania ya Shirika na hivyo kuweza kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Programu ya Uwekezaji Katika Sekta ya Uchukuzi (*Transport Sector Investment Programme - TSIP*). Katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya mwaka 2007/08, Bunge lako Tukufu lilielezwa kwamba Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi (*TSIP*) imekamilika na utekelezaji wake umeanza. Lengo la Programu hii ya miaka kumi ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2018 barabara kuu zote zinakuwa katika kiwango cha lami na hivyo kufanya makao makuu ya Mikoa kuunganishwa kwa barabara za lami na makao makuu ya Wilaya kuunganishwa kwa barabara za changarawe au za lami nyepesi kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Aidha, bandari, reli na viwanja vya ndege vitaendelezwa ili kuwa na miundombinu inayowezesha utoaji wa huduma zenye viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizofikiwa kuhusu utekelezaji wa programu hii ni pamoja na kuainisha miradi inayotakiwa kutekelezwa katika sekta ndogo za Barabara, Reli, Usafiri wa majini na viwanja vya ndege. Miradi hii ilipewa kipaumbele (*prioritization*) kulingana na aina ya mradi na umuhimu wake katika jamii. Hatua nyingine ni kuoanisha program hii na Mpango wa muda wa kati wa Bajeti (*MTEF*) kwa vipindi vya utekelezaji vya miaka mitatu mitatu (*3 years Rolling Plan*). Hii inatokana na ukweli kwamba mpango huo wa miaka kumi hauwezi kutekelezwa nje ya utaratibu uliopo hivi sasa wa utayarishaji wa mpango wa kila mwaka. Kwa hiyo mpango wa MTEF wa mwaka 2007/08 na 2008/09 ni sehemu ya utekelezaji wa programu hiyo ya miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupata mwelekeo na hali halisi ya utendaji wa sekta ya Miundombinu kwa ujumla, Wizara imefanikiwa kufanya Kongamano la pamoja kati ya Serikali na Wahisani kuhusu mapitio ya Utendaji wa Sekta ya Miundombinu (*Joint Infrastructure Sector Review - JISR*). Kongamano hili ambalo lilifanyika Oktoba, 2007 ni la kwanza katika historia ya Wizara na Sekta ya uchukuzi. Lengo lake lilikuwa ni kufanya mapitio ya shughuli zinazofanyika katika sekta zetu ikiwa ni pamoja na zile ambazo tunawashirikisha Wahisani. Kutohana na Kongamano hilo suala la mabadiliko ya kisera na kimfumo katika sekta lilijitokeza bayana. Aidha, ilionekana kuwa kuna umuhimu wa kuwa na ushirikiano wa karibu na wadau wote katika utendaji wa sekta. Masuala mengine yaliyojitekeza ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha za matengenezo ya barabara zinatumwiwa ipasavyo, umuhimu wa kuweka mikakati ya kubuni vyanzo vipyta vya mapato kwa ajili ya kuendeleza sekta ya uchukuzi, umuhimu wa

kuboresha huduma za usafiri wa umma kwa kuhakikisha kwamba wadau wote wanahusishwa ipasavyo na umuhimu wa ushirikishwaji wa Sekta binafsi katika utekelezaji wa shughuli za sekta.

Ili kuweza kutathmini utendaji wa Sekta, Wizara imeendelea na zoezi la maandalizi ya viashiria muhimu vya kisera (*Sector Policy Level Monitoring Indicators*). Viashiria hivi vimeendelea kuainishwa kwa lengo la kuandaa takwimu (*Sector Database*) katika sekta za Uchukuzi, Ujenzi na Hali ya Hewa. Inatarajiwa kuwa database hiyo itakamilika mwishoni mwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za usafiri wa barabara. Katika mwaka 2007/08, sekta ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara imeendelea kuimarika katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kijamii hapa nchini. Huduma za usafiri kwa njia ya barabara zimeendelea kutolewa kwa kiasi kikubwa na sekta binafsi. Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya barabara ili iweze kukidhi mahitaji ya watumiaji wa huduma hii. Aidha, Wizara katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Uchukuzi imeweka mikakati ya kuishirikisha sekta binafsi ili iweze kuendelea kutoa mchango wake katika ukuzaji wa sekta ndogo ya barabara. Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Wizara nyingine, taasisi na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI iliendelea kuimarisha huduma ya usafiri wa barabara kuanzia ngazi ya kitaifa hadi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa mijini, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa huduma zinaboreshwu katika kiwango cha kuridhisha. Katika jiji la Dar es Salam, Shirika la Usafiri Dar es Salaam limeendelea kutoa huduma kwa kushirikiana na sekta binafsi. Katika mwaka 2007/08 Shirika lilikuwa na wastani wa mabasi 27 ambapo wastani wa mabasi yaliyokuwa barabarani kwa siku yalikuwa 19. Juhudi zinaendelea za kuboresha Shirika ili liweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama barabarani na uimarishaji wa usafiri mijini. Katika mwaka wa 2007/08, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa usalama barabarani iliendelea kuimarisha usalama barabarani kwa kutoa elimu ya Umma kuitia vyombo vya habari kama vile luninga na redio, vipeperushi na semina mbalimbali. Katika kipindi hiki ajali za barabarani zilipungua toka ajali 2873 mwaka 2006 hadi ajali 2586 mwaka 2007. Upungufu huu ni sawa na asilimia 10.

Ili kutatua tatizo la ajali za barabarani, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa ajali za barabarani zinaendelea kupungua kama sio kwisha kabisa. Mikakati hiyo ni pamoja na kuhakikisha kuwa watumiaji wa barabara wanapewa elimu ya kutosha kuhusu sheria za barabara na matumizi sahihi ya barabara. Kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na wadau wengine, Wizara inahakikisha kuwa elimu ya usalama barabarani inaendelea kufundishwa shulenji ili kuweza kuwaelimisha wanafunzi umuhimu wa kuzingatia matumizi sahihi ya barabara. Machi, 2008 Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (*TIE*) waliendesha mafunzo ya usalama barabarani katika mkoa wa Kilimanjaro ambapo Walimu 350 na wanafunzi 6,000 walishiriki. Lengo la

Wizara ni kuendesha mafunzo kama hayo kwa nchi nzima ili kuwapatia wananchi uelewa wa matumizi sahihi ya barabara na hivyo kupunguza ajali za barabarani. Aidha, Wizara inaendelea kuhakikisha kwamba madereva wanapatiwa mafunzo kama hayo kwa kuwa imeonekana kuwa ajali nyingi zinasababishwa na uendeshaji usiozingatia sheria za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua tatizo la ajali za barabarani kwa mwaka 2008/09 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa ajali za barabarani zinapungua. Mikakati hiyo ni pamoja na kuhakikisha kuwa watumiaji wa barabara wanapewa elimu ya kutosha kuhusu sheria za barabara na matumizi sahihi ya barabara. Mikakati mingine ni kufanya ukaguzi wa ajali za barabarani (*Road Safety Audit*), kuandaa eneo la mafunzo na utahini wa madereva na kuanzisha utaratibu wa ukaguzi wa magari kwa mujibu wa sheria. Aidha, Wizara itakamilisha utaratibu wa kuweka maeneo ya kupumzisha madereva, abiria na magari, kuboresha menejimenti ya usalama barabarani kwa kuwa na sekretarieti ya kudumu na kuweka mtandao wa kutunza kumbukumbu za ajali na vyanzo vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi (Usalama Barabarani) imeendelea kutekeleza agizo la Serikali la kuyataka mabasi ya abiria kuzingatia ratiba za kusafirisha abiria kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 4.00 usiku. Aidha, hatua zimeendelea kuchukuliwa ili kudhibiti ongezeko holela la nauli kuanzia kipindi cha Novemba, 2007 hadi Mei, 2008. Hatua hii inalenga kuwapunguzia wananchi mzigo wa gharama za usafiri.

Kuhusu leseni za usafiri katika kipindi cha Julai, 2007 hadi Desemba 2007, jumla ya leseni 10,054 na ratiba 1,335 zilitolewa. Hili ni ogezeko la asilimia 21.78 (kwa leseni) na asilimia 28.49 (kwa ratiba) ikilinganishwa na leseni na ratiba za mwaka 2006/07. Aidha, *SUMATRA* ilikamilisha maandalizi ya Kanuni za Usafirishaji kwa njia ya barabara [*The Transport Licensing (Road Passenger vehicles) Regulations, 2007*]. Utekelezaji wa kanuni hizi unatarajiwu kuanza katika mwaka 2008/2009.

Wizara kupitia *TANROADS* imeendelea kudhibiti uzito wa magari kwa kutumia mizani zisizohamishika na zinazohamishika katika barabara zote kuu. Udhibiti wa uzito wa magari umeendelea kutekelezwa kwa kutumia mizani ishirini na tisa (29). Kati ya hizo, mizani 15 ni zile ambazo hazihamishiki na mizani kumi na minne (14) zinazohamishika. Ili kuboresha udhibiti wa uzito wa magari, mizani 8 zilizokuwa katika mfumo wa “*mechanical*” zimegeuzwa kuwa katika mfumo wa “*digital*”. Mizani mbili (2) mpya zisizohamishika ziko katika hatua za mwisho za kuzinduliwa katika maeneo ya Nangurukuru na Mingoyo. Aidha, mizani 8 mipyä inayohamishika inatarajiwu kununuliwa katika mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza msongamano wa magari katika miji mikubwa, Serikali imeendelea na kutekeleza mipango yake ya muda mfupi na mrefu. Katika mpango wa muda mfupi Serikali ilianzisha utumiaji wa njia tatu katika kutoa huduma kwa barabara za Morogoro, Ali Hasani Mwinyi na Mandela za jijini Dar es salaam ikiwa ni pamoja na kuanza upanuzi wa baadhi ya barabara.

Wizara imeendelea na utaratibu wa kutumia eneo maalum kati ya Mbezi Luis na Kimara kwa ajili ya maegesho ya magari ya mizigo. Aidha, mkakati wa ukarabati wa barabara na uanzishwaji wa barabara za mzunguko (*Ring roads*) pia umeendelea kupewa umuhimu mkubwa ili kupunguza msongamano wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mrefu, juhudhi zimeelekezwa katika kutekeleza mradi wa mabasi yaendayo kasi (*DART*) ambao utatekelezwa katika awamu sita. Awamu ya kwanza ya mradi inajumuisha barabara ya Morogoro, Kawawa na Msimbazi zote kwa pamoja zikiwa na urefu wa kilomita 21. Miundombinu ya mradi huu itakayojengwa ni njia maalum za mabasi, vituo vya mabasi 5, stesheni 29 na karakana 2 za mabasi.

Awamu ya kwanza ya mradi huo inakadiriwa kugharimu dola za Kimarekani milioni 158.2. Kati ya fedha hizo Serikali ya Tanzania itatoa dola za kimarekani milioni 10, Benki ya dunia itatoa Dola za

Kimarekani milioni 110 na sekta binafsi itawekeza kiasi cha dola milioni 38.2 kwa kununua mabasi na kujenga mfumo imara wa kukusanya nauli. Ujenzi wa miundombinu una urefu wa kilomita 21 za barabara na ina vituo vidogo 29, vituo vikubwa 5 na maeneo mawili ya maegesho na matengenezo. Ujenzi wa miundombinu ya *DART* unatarajiwa kuanza Septemba, 2008. Huduma ya usafiri chini ya mfumo huu mpya inatarajiwa kuanza kutolewa Julai, 2010. Zoezi la ulipaji wa fidia linaendelea vizuri. Kazi nyingine za msingi zitakazotekeliza ni pamoja na kukamilisha mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi wa miundombinu na kukamilisha upatikanaji wa mkopo toka Benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa utekelezaji wa mradi huu. Majukumu mengine ni kupata wazabuni watakaohusika na shughuli za uendeshaji mabasi, ukusanyaji nauli na usimamizi wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Barabara Kuu na Barabara za Mikoa na Matengenezo ya Barabara. Katika mwaka 2007/08, Wizara ililenga kujenga na kukamilisha barabara zenyne urefu wa kilometra 527.5 kwa kiwango cha lami. Kati ya hizo, kilometra 470.5 ni za Barabara Kuu na kilomita 57 ni za Barabara za Mikoa. Hadi kufikia Juni, 2008 jumla ya kilometra 410 za Barabara Kuu sawa na asilimia 78 ya lengo zimekamilika. Kilomita zilizobaki bado zinaendelea kujengwa. Miradi ambayo ujenzi wake umekamilika kwa kiwango cha lami ni pamoja na Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95), Mbwemkuru – Mingoyo (km 95), Singida – Shelui (km 110), Geita – Buzirayombo (km 100), Buzirayombo – Kyamiorwa (km 110), Singida – Isuna (km 63) na Mkuranga – Kibiti (km 79). Aidha, Barabara za Mikoa zenyne urefu wa kilomita 1,020 zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe na kilometra 26 kwa kiwango cha lami. Ukarabati wa barabara za mikoa unafanyika katika mikoa yote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara ambayo ujenzi wake unaendelea ni pamoja na barabara ya Sam Nujoma (km 4.0), DSM – Mbagala (km 11.6), Tarakea – Kamwanga (km 32), Mbeya – Makongorosi (sehemu ya Mbeya – Lwanjilo, km 36), Nelson Mandela (km 15.6), Masasi – Mangaka (km 54), Usagara – Geita (km 90), Dodoma – Manyoni (km 127) na Isuna – Manyoni (km 55), Daraja la Umoja, Daraja la

mto Ruvu, Daraja la mto Nanganga. Aidha barabara ambazo ujenzi wake unatarajiwa kuanza katika mwaka 2008/09 ni pamoja na barabara ya Kigoma – Kidahwe (km 36), Bagamoyo – Msata (km 64), Mwandiga – Manyovu (km 58), Ndundu – Somanga (km 60), Sumbawanga – Mpanda, sehemu ya Sumbawanga – Chala (km 60), Singida – Babati – Minjingu (km 223), Tanga - Horohoro (km 65), Songea – Namtumbo (km 70), Tunduma – Sumbawanga (km 231), DSM – Mbogala awamu ya pili (km 6.6) na Songea – Mbinga (km 100).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, mgawanyo wa rasilimali umeelekezwa kwenye miradi ya barabara kuu ambayo utekelezaji wake unaendelea. Wizara imepanga kuendelea na utekelezaji wa miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara za lami. Jumla ya kilomita 208.1 zinatarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kilomita 80 za lami zitafanyiwa ukarabati. Utekelezaji wa miradi hii unajumuisha barabara zitakazofadhiliwa na washirika mbalimbali wa maendeleo ikiwa ni pamoja na mfuko wa “*Millenium Challenge Cooperation (MCC)*” wa Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matengenezo ya barabara. Katika mwaka 2007/08, Wizara kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ilipanga kuzifanyia matengenezo barabara kuu na za mikoa zenye urefu wa kilomita 30,013.9 na madaraja 2,098. Hadi kufikia Juni, 2008, jumla ya kilomita 5,940.1 na madaraja 580 ya Barabara Kuu na kilomita 11,985.9 na madaraja 492 ya Barabara za Mikoa zilifanyiwa matengenezo ikiwa ni asilimia 60 ya lengo. Aidha, sababu ya kutofikia lengo ni ongezeko kubwa la gharama za matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wizara kupitia *TANROADS* itaendelea kuzifanyia matengenezo Barabara za Mikoa, Barabara Kuu pamoja na Madaraja. Lengo ni kuzifanyia matengenezo Barabara Kuu na za Mikoa zenye urefu wa kilomita 27,743.04 na madaraja 2,239. Kuhusu Barabara za Mikoa jumla ya kilomita 929 za barabara za changarawe na kilomita 16 za lami zitafanyiwa ukarabati kwa kutumia fedha za maendeleo. Aidha, kilomita 175 za changarawe na kilomita 17 za lami zitafanyiwa ukarabati kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa Mpango wa Matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa kwa mwaka 2008/2009 ni kama unavyoonyeshwa katika Kiambatanisho Na. 1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa 2008/09. Katika mwaka 2008/09, jumla ya shilingi milioni 321,402.49 fedha za ndani zimetengwa kutoka mfuko mkuu wa Serikali kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo ya Barabara Kuu. Kati ya hizo, shilingi milioni 190,000 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya makandarasi. Kiasi kinachobaki cha shilingi milioni 131,402.49 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ambayo utekelezaji wake unaendelea. Aidha, shilingi milioni 7,949.9 kutoka Mfuko wa Barabara zimetengwa kuchangia miradi ya maendeleo.

Kwa upande wa Barabara za Mikoa jumla ya kilomita 1,127 zitakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe na jumla ya kilomita 34.5 zitajengwa kwa kiwango cha lami.

Aidha, Madaraja 14 yamepangwa kujengwa katika mikoa ya Lindi (1), Mbeya (2), Morogoro (3), Ruvuma (5), Singida (1), Arusha (1) na Mwanza (1). Jumla ya shilingi milioni 48,797.07 kutoka mfuko wa maendeleo zimetengwa kugharamia miradi hiyo ambapo kati ya hizo shilingi milioni 13,884.17 ni fedha za ndani na shilingi milioni 34,912.9 ni fedha za nje. Aidha, Mfuko wa Barabara umetenga shilingi milioni 6, 291.0 kwa ajili ya kukarabati Barabara za Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa Vivuko Wizara kwa kupitia Wakala wa Ufundu na Huduma za Umeme (*TEMESA*), imeendelea na mkakati wake wa kuimarisha usafiri wa maeneo yanayohitaji vivuko. Katika mwaka 2007/08, vivuko vipya vilivyonunuliwa ni pamoja na Kivuko cha Kigamboni (Dar es salaam) chenye uwezo wa kubeba tani 500 (sawa na abiria 2,000 na magari madogo 60 kwa mara moja). Kazi ya ujenzi wa kivuko hiki ilianza Novemba, 2007 ambapo hadi hivi sasa asilimia 70 ya kazi imekamilika. Inatarajiwa kuwa kivuko hicho kitaanza kazi Septemba, 2008. Aidha, ukarabati wa vivuko vya zamani vya MV Alina (DSM), na MV Sengerema (Mwanza) unaendelea vizuri kwa kununua vifaa kwa ajili ya ukarabati kupitia “Mpango wa ukarabati wa vivuko.”

Katika hotuba ya mwaka 2007/08 ilielezwa kuwa Kivuko cha Kigongo/Busisi (Mwanza) kiitwacho MV Misungwi kilikuwa kinajengwa. Ninayo furaha kutoa taarifa kuwa kivuko hicho chenye uwezo wa kubeba tani 250 yaani abiria 1,000 na magari 36 kwa wakati mmoja kilikamilika Januari, 2008 na kuzinduliwa rasmi na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 12 Mei, 2008. Aidha, Kivuko kipyta cha Ruhuhu (Ruvuma) chenye uwezo wa kubeba tani 50 kilikamilika Machi, 2008 na kinasubiri kuzinduliwa rasmi. Kivuko hiki ni kwa ajili ya kuwashudumia wananchi wa Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma na Ludewa mkoani Iringa. Kivuko kingine kipyta kilichonunuliwa ni cha Kilombero mkoani Morogoro ambacho kina uwezo wa kubeba tani 50 (yaani abiria 100 na magari madogo 6 kwa wakati mmoja). Ukamilikaji wa vivuko hivi ni hatua nzuri katika kuboresha huduma za usafiri kwa wakazi wa maeneo husika hivyo kurahisisha utekelezaji wa shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kivuko kipyta cha Mto Pangani kitanunuliwa kwa kupitia msaada wa Benki ya Dunia. Mkataba wa kukijenga kivuko hicho ulisainiwa Mei, 2008 kati ya Wizara na mkandarasi aitwaye Jons Gram Hanssen AS kutoka Denmark ambaye anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo ifikapo Mei, 2009. Kwa upande wa vivuko vya Utete (Pwani), Musoma – Kinesi (Mara) na Rugezi-Kisorya (Ukerewe, Mwanza) zabuni za ununuzi zilitangazwa na Wakandarasi wa kuleta vivuko hivyo wameshapatikana. Mkataba wa kuleta vivuko hivyo ulisainiwa Juni, 2008 kati ya Wizara na kampuni ya *N.N. Shipbuilders & Engineers PVT. Ltd* ya India (kwa ajili ya Kivuko cha Utete) na Scheepsbouw Noard Nederland B.V. ya Uholanzi (kwa ajili ya Vivuko vya Kinesi na Kisorya). Vivuko vya Kinesi, Kisorya na Utete vinatarajiwa kukamilika Juni, 2009. Ujenzi wa Kivuko kipyta cha Rufiji kupitia Mpango wa Ukarabati wa Vivuko Vitano umekamilika na kitahamishiwa Nyakaliro/Kome wilayani Sengerema. Kivuko hiki kitaanza kazi Septemba, 2008.

Katika mwaka 2008/09 Wizara ina mpango wa kukamilisha ujenzi wa vivuko vipyta vya Utete (Pwani), Musoma- Kinesi (Mara), na Rugezi- Kisorya (Mwanza) na Kivuko cha Mto Pangani (Tanga).

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa Majini huduma za Uchukuzi kwa njia ya maji zimegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni: (i) uchukuzi baharini na katika maziwa na (ii) huduma za bandari. Huduma za uchukuzi wa baharini zinatolewa na Kampuni za nje ya nchi wakati Kampuni za ndani ya nchi hutoa kiasi kidogo cha huduma hizo. Kampuni za nje ni pamoja na Kampuni ya Meli ya Serikali za China na Tanzania (*SINOTASHIP*). Uchukuzi katika maziwa unatolewa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri na Uchukuzi Katika Maziwa. Katika mwaka 2007/08 Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) iliendelea kutoa huduma za uchukuzi na usafiri kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ikishirikiana na sekta binafsi. Katika kipindi hiki Kampuni iliweka lengo la kusafirisha mizigo yenyewe uzito wa tani 210,941 na jumla ya abiria 574,986. Hata hivyo, jumla ya tani 203,135 zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 109,603 zilizosafirishwa mwaka 2006/07 ikiwa ni ongezeko la asilimia 1. Aidha, katika kipindi hiki abiria 569,442 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 543,359 waliosafirishwa mwaka 2006/07 ikiwa ni ongezeko la asilimia 5. Kwa utendaji huo Kampuni ilipata faida ya shilingi milioni 504.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchukuzi wa masafa marefu baharini umeendelea kutolewa na Kampuni ya Meli inayomilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China ijulikanayo kama *SINOTASHIP*. Katika mwaka 2007/08 Kampuni ilikuwa na meli mbili zenyewe uwezo wa kubeba jumla ya tani 31,000 kwa wakati mmoja. Meli za Kampuni zilifanya safari 14 ikilinganishwa na safari 16 zilizokuwa zimepangwa. Lengo la idadi ya safari halikufikiwa kutokana na baadhi ya safari kuwa za umbali mrefu kuliko ilivyokuwa imekadiria. Aidha, jumla ya tani 178,002 za shehena zilisafirishwa, ambazo ni zaidi kwa asilimia 0.32 ikilinganishwa na lengo la tani 177,400 ambalo Kampuni ilikuwa imejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 mapato ya Kampuni yalipungua kwa asilimia 1 kutoka Dola za Marekani 8,800,022 zilizopatikana mwaka 2006 hadi Dola 8,703,799. Kwa kulinganisha na makadirio ya mwaka 2007 ya dola 6,315,000. Mapato hayo yameongezeka kwa asilimia 38. Sababu kubwa ya kupanda kwa mapato ukilinganishwa na makadirio ni kuimarika kwa soko la usafirishaji wa shehena ulimwenguni kote katika mwaka 2007.

Katika mwaka 2008, Kampuni itaendelea kutumia meli zake mbili na imejiwekea lengo la kusafirisha tani 140,000 kwa kukamilisha safari 16 ambapo faida itakuwa dola za kimarekani 350,000. Aidha, Kampuni ina mpango wa kujenga meli mbili kubwa zenyewe uzito wa tani (*DWT*) 57,000 na tani 34,000 na hivyo kuongeza idadi ya meli zake kufikia

nne ifikapo mwaka 2009. Ili kutekeleza mpango huu Kampuni inakamilisha mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya China (China Development Bank) ili kupata mkopo kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, usalama wa Vyombo vya Majini Wizara imeendelea kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Sheria ya Usafiri majini ya mwaka 2003 (*Merchant Shipping Act, 2003*) ambayo inahusu usimamizi wa masuala ya usafiri majini. Katika kutekeleza Sheria hii, Serikali imeendelea kuwa na makubaliano na nchi mbali mbali kuhusu uboreshaji wa usalama wa vyombo vya majini. Makubaliano na Serikali ya Malawi kuhusu uboreshaji wa uchukuzi katika Ziwa Nyasa yako kwenye hatua za mwisho. Aidha, majadiliano na Serikali ya Msumbiji kuhusu uchukuzi katika Ziwa Nyasa na majadiliano na Serikali ya Kiislamu ya Iran kuhusu uchukuzi baharini yako kwenye hatua za awali. Lengo la makubaliano hayo ni kuboresha ushirikiano baina ya nchi hizi katika masuala ya usalama wa vyombo na biashara ya uchukuzi wa majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuzingatia mikataba mbalimbali ya kimataifa inayosimamiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (*International Maritime Organization - IMO*). Wizara kuitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) imeandaa kanuni na taratibu zipatazo 15 katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usafiri Majini ya 2003 (*Merchant Shipping Act, 2003*). Kanuni zilizoandaliwa zitasaidia kuongeza usalama wa usafiri majini. Aidha, maeneo mengine yanayozingatiwa katika kusimamia usalama wa usafiri majini ni pamoja na ukaguzi wa vyombo vya usafiri majini na mabaharia na kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya usafiri majini kwa kufungua ofisi ya ukaguzi huko Sumbawanga. Hatua nyingine ni kufunga vifaa vya mawasiliano katika bandari za Itungi, Mwanza na Kigoma na kutoa semina kwa wadau wa usafiri wa majini kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMATRA imeendelea kudhibiti upandaji kiholela wa gharama za watoa huduma katika sekta ya usafiri nchi kavu na majini. Kabla ya kurekebisha viwango vya gharama za huduma Mamlaka hufanya tathmini na wadau hushirikishwa kutoa maoni yao. Katika mwaka 2007/08 Mamlaka ilipokea maombi ya kurekebisha viwango vya gharama za huduma kutoka kwa watoa huduma za usafiri wa mabasi, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Kampuni za Wakala wa Meli (Shipping Agents) na Kampuni ya Reli Tanzania (TRL). Mamlaka ilitathmini mapendekezo yao kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya gharama za uendeshaji na kuongeza gharama kwa viwango mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2008/09, SUMATRA itaandaa kanuni na taratibu za usimamizi wa usalama wa usafiri katika nchi kavu na majini, kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya majini, kuimarisha ofisi za ukaguzi wa vyombo vya majini ambazo zimefunguliwa katika miji ya Mwanza, Bukoba, Kigoma, Sumbawanga na Itungi. Mamlaka pia itaboresha uratibu wa shughuli za utafutaji na uokoaji kwa kutumia kituo cha kisasa cha kuongozea meli kilichoko Dar es salaam. Hatua nyingine ni pamoja na kuhimiza matumizi ya mabasi makubwa kwa usafiri wa mijini, kuratibu utekelezaji wa

mapendekezo ya utafiti wa ajali barabarani na kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya utafiti wa usafiri wa wanafunzi katika Miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za Bandari. Katika mwaka 2007/08 Serikali imeendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa inaongeza uwezo wa bandari zetu kuhudumia mizigo zaidi ikilinganishwa na hali ya sasa ili kukabiliana na ongezeko la shehena hususan shehena ya kontena. Lengo la TPA wamelenga kuhudumia tani milioni 10 ifikapo mwaka 2015 ikilinganishwa na tani milioni 7 zinazohudumiwa sasa. Aidha, utekelezaji wa mradi wa utafiti wa Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Bandari zote nchini (*Port Master Plan Study*) unaendelea kutekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Mradi huu ulianza kutekelezwa Aprili, 2008 na unatarajiwa kukamilika Januari 2009. Mkakati wa kuendeleza Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ambapo utafiti wa awali (*Geotechnical Survey*) ulikamilika Machi, 2008. Katika Bandari ya Tanga, mkakati wa kujenga bandari sehemu ya Mwambani, Tanga na kuendeleza maeneo ya Uwekezaji (*Export Processing Zones – EPZ*) katika Bandari ya Mtwara unaendelea vizuri.

Katika kipindi hicho, TPA ilielekeza nguvu zake katika kuboresha bandari na magati. Aidha, Mamlaka iliendelea na juhudzi za kushirikisha sekta binafsi katika maeneo mengine ya uendeshaji ikiwemo ukodishaji wa uendeshaji wa vitengo vya kuhudumia mizigo katika bandari za Kigoma na Kasanga. Mazungumzo na kampuni mbalimbali zinazotaka kuwekeza katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Mamlaka ililenga kuhudumia tani za mapato 6,384,100. Katika kipindi cha Julai, 2007 hadi Machi, 2008 jumla ya tani za mapato 4,952,825 zilihudumiwa ikilinganishwa na lengo la kuhudumia tani za mapato 4,860,400 katika kipindi hicho na hivyo kuvuka lengo kwa tani za mapato 92,425 sawa na asilimia 1.9. Aidha, Mamlaka ilifanikiwa kukamilisha utekelezaji wa miradi mbali mbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mnara wa kuongozea meli (*New Port Control Tower*) katika Bandari ya Dar es Salaam. Mnara ambao pia utatumika kama kituo cha mawasiliano cha shughuli za Utafutaji na Uokoaji baharini. Mradi wa kuboresha maeneo ya kuhudumia shehena ya magari na kontena, ukarabati wa gati la Kasanga, ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kuhudumia mizigo, mradi wa kubadilisha bomba la mafuta la inchi 18 kwenye gati la kupokea mafuta Kurasini (*18" Submarine Oil Pipeline*) na ukarabati wa barabara ya Kajunjumele inayounganisha bandari ya Kiwira hadi Bandari ya Itungi. Miradi mingine ambayo utekelezaji wake unaendelea ni ujenzi wa Bomba kubwa la mafuta (*SBM*), kuendelea na ujenzi wa awamu ya pili wa gati la Mbamba Bay, ujenzi wa gati la Mafia na upanuzi wa gati la Bandari ya Kasanga. Ukarabati wa gati la Nansio pia utatekelezwa katika mwaka wa 2008/09.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TPA* kuitia Kitengo cha Kontena kilicho chini ya Mwekezaji binafsi (*TICTS*) katika kipindi cha Julai 2007 hadi Machi 2008, ililenga kuhudumia kontena (*TEUs*) 302,000. Katika kipindi hicho shehena ya kontena iliyohudumiwa ni *TEUs* 290,759 ikiwa ni pungufu ya lengo kwa *TEUs* 11,241 sawa na asilimia 3.7. Kupungua kwa shehena ya kontena kulitokana na kukosekana kwa nafasi ya kutosha ya kufanya kazi ya kupakia na kupakua. Aidha, uwezo wa Kitengo cha Kontena ni kuhudumia kontena 250,000 kwa mwaka, hivyo kuongezeka kwa shehena ya kontena

kumesababisha ukosefu wa nafasi ya kufanya kazi, hali ambayo inasababisha mlundikano wa kontena na msongamano wa meli zinazosubiri nje ya bandari kabla ya kuingia bandarini kuhudumiwa. Katika kukabiliana na hali hii, hatua mbali mbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na wadau wote muhimu wa bandari wakiwemo *TPA*, *TICTS* na *TRA* kufanya kazi kwa saa 24 kwa siku. *TRA*, *TICTS* na *TPA* wameboresha mtiririko wa nyaraka za uondoshaji wa mizigo bandarini ambapo sasa nyaraka zinatumia njia ya ‘electronic’ baada ya kukamilika kwa mradi wa *ASYCUDA ++* na mtandao wa “*Port View*” wa *TPA*. *TICTS* na *TPA* wanatekeleza mpango wa kuboresha hali ya vifaa kwa kununua vifaa vipyta vya kuhudumia kontena. Baadhi ya vifaa vimeshawasili na kuanza kazi. Kuanzia Juni, 2007 kwa makubaliano na *TICTS*, *TPA* ilianza kuhudumia meli ndogo “*feeder Vessels*” zinazobeba kontena zisizozidi 500. Utaratibu huu umesaidia sana kupunguza idadi ya meli ambazo zinasubiri huduma katika Kitengo cha Kontena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyine ni uendeshaji wa minada kwa kontena zote ambazo zimekaa muda mrefu bandarini bila kuchukuliwa na wenyewe. Kwa mujibu wa sheria na taratibu kontena zilizokaa bandarini zaidi ya siku 21 hustahili kupigwa mnada na Mamlaka ya Mapato. Kuhusu kontena tupu kukaa muda mrefu bandarini, Wenye meli/wakala wao wameagizwa kuondoa kontena hizo bandarini ili nafasi itumike kuweka kontena zenye mizigo. Utaratibu ni kuwa kontena tupu zitaruhusiwa kuletwa bandarini saa 48 kabla ya kupakiwa melini. Ili kuongeza nafasi ya kuweka kontena nje ya bandari, Mamlaka ya Mapato imetoa leseni kwa Waendeshaji sita wa vituo vya mizigo (*Inland Container Depots – ICDs*). Vituo hivyo ni pamoja na vituo vya Kurasini na Ubungo ambavyo vina uwezo wa kuhifadhi kontena 8,500. Utaratibu huu wa kuendesha *ICDs* umesaidia kupunguza mlundikano wa kontena bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza nafasi ya kuhudumia kontena bandarini *TICTS* wamepewa eneo la yaliyokuwa maghala ya *TPA* na kituo cha mafuta ndani ya kituo cha kontena. Maeneo haya yana ukubwa wa hekta 5 na uwezo wa kuhudumia kontena zaidi ya 3,000. Ili kuweza kupata nafasi zaidi *TPA* wana mpango wa kujenga jengo litakalotumika kuweka magari, eneo linalotumika sasa kuweka magari litatumika kuweka kontena. Ujenzi wa jengo hilo unategemewa kuanza mwaka 2009. Ujenzi wa Gati namba 13 na 14 katika bandari ya Dar es Salaam pia utasaidia kuongeza nafasi ya kuhudumia kontena bandarini. Mamlaka inaendelea kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huu. Ujenzi umepangwa kufanya katika utaratibu wa “*Fast Track*” ili uweze kukamilika ndani ya miaka minne kuanzia sasa. Matumizi ya Bandari Kavu (dry ports) pia yamepewa msukumo wa pekee ili kufanikisha upatikanaji wa nafasi za kuhudumia makontena na mizigo mingine. Bandari Kavu za Isaka na Mbeya zinaboreshw. Hatua zote hizi zimechukuliwa ili kuongeza ufanisi, kupunguza mlundikano wa kontena, kupunguza muda wa meli kukaa bandarini na kupunguza gharama za njia na hivyo kuongeza biashara kwa mizigo kupita kwenye bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/09, Mamlaka inatarajia kuhudumia jumla ya tani 7, 490,500 katika bandari kuu. Aidha, Mamlaka itahudumia kontena 438,500. Mamlaka pia inatarajia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuboresha miundombinu na huduma katika Bandari. Miradi mipyta iliyopangwa ni pamoja na ukarabati wa magati katika ziwa Tanganyika, Victoria na Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri na Uchukuzi wa Reli. Baada ya shughuli za uendeshaji wa Shirika la Reli (*TRC*) kukodishwa kwa Kampuni ya Reli Tanzania (*TRL*) kiwango cha utoaji huduma kimeendelea kuwa cha wastani. Tangu ilipoanzishwa Oktoba, 2007, *TRL* imeweza kusafirisha tani 452,457 za mizigo ambapo 332,399 ni mizigo ya ndani na tani 120,058 ni mizigo ya nchi jirani. Aidha, katika kipindi hiki kampuni ilisafirisha jumla ya abiria 572,000. Hata hivyo *TRL* bado inakabiliwa na matatizo ya uchakavu wa mabehewa, injini, pamoja na miundombinu hafifu ya reli. Hivi sasa Kampuni iko katika taratibu za kukarabati mabehewa na injini na kununua nyingine mpya ili kuboresha huduma za usafiri wa reli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, *TRL* imepanga kufanya safari nne kwa wiki toka Dar es Salaam hadi Kigoma na Mwanza badala ya safari mbili za sasa. Aidha, itakodi mabehewa 23 ya daraja la tatu na mabehewa mengine 30 yatafanyiwa ukarabati. Hatua nyingine ni kupunguza muda unaotumiwa na mabehewa kwenda na kurudi kutokana na kukodi injini 15 zeny uwezo wa *class 73xx*. Mipango mingine ni pamoja na kukarabati injini 15 za *class 88xx*, kuboresha miundombinu ya mawasiliano na kununua vipuri kwa ajili ya kukarabati mabehewa. Inatarajiwa kwamba Kampuni itaweza kuboresha huduma za usafiri wa mizigo na abiria baada ya kukamilika kwa mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *RAHCO* iliyoanzishwa Oktoba, 2007 iliendelea na jukumu la kusimamia na kuendeleza miundombinu ya reli kwa niaba ya Serikali. Kampuni iliendelea na ukamilishaji wa kazi ya kubadilisha mataruma ya uzito wa ratili 80 kwa yadi ya reli kati ya Kintinku - Makutopora (km16) na Itigi - Malongwe (km 31) na kufanya uchambuzi wa zabuni ya ujenzi wa vituo vya kontena vya Ilala, Shinyanga na Mwanza. Aidha, Benki ya Dunia imekubali kufadhili ununuaji wa mataruma na reli kwa ajili ya kilomita 150 za Reli ya Kati. Taratibu za kumpata mzabuni wa kuuza reli na mataruma zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, *RAHCO* itaendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya rasilimali za reli, kufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya kuimarisha njia ya reli na madaraja kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma. Aidha, kazi nyingine ni kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya ya Reli kati ya Arusha na Ziwa Natron, ujenzi wa reli ya kuunganisha bandari ya Mbegani - Bagamoyo na Kidomole (*Link line*). Kazi nyingine ni ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza mataruma na uimarishaji wa njia ya reli kutoka Moshi hadi Arusha kwa kuweka reli za ratili 95 kwa yadi. Miradi mingine itakayoteklezwa ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya ujenzi wa reli kati ya bandari ya Mwambani hadi Tanga, majengo ya kitega uchumi katika viwanja vitano Jijini Dar es Salaam, ujenzi wa bandari kavu ya Katosho katika reli ya Kigoma na ujenzi wa yadi ya kupanga mabehewa eneo la Pugu (*Pugu Marshalling Yard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha nusu ya mwaka cha 2007/08, *TAZARA* ilisafirisha tani 290,570 za mizigo ikilinganishwa na tani 330,000 zilizopangwa

kusafirishwa, ambayo ni asilimia 88.1 ya lengo. Pia Mamlaka ilisafirisha abiria 592,209 kati ya abiria 550,000 waliokadiriwa kusafirishwa hivyo kuvuka lengo lililokadiriwa kwa asilimia 7.7. Serikali ya Tanzania imeendelea kuipatia *TAZARA* fedha kwa ajili ya kuboresha eneo la mmomonyoko wa ardhi kama hatua za muda hususan matengenezo ya reli kati ya Mpanga – Kitete yaani umbali wa km 561 toka Dar es salaam. Sehemu inayofanyiwa ukarabati ina urefu wa mita 500.

Serikali ya Zambia imepata wafadhili ambao wamesaidia kuboresha mawasiliano ya reli baada ya kununua na kufunga mitambo mingine ya *HF Radio* kwa upande wa Zambia. Matengenezo ya injini 6 za treni yanaendelea ambapo ukarabati wa injini mbili kati ya 6 zilizopangwa umekamilika. Aidha, zoezi la kubadilisha reli chakavu limekamilika ambapo jumla ya mataruma ya reli 13,813 yamebadilishwa kati ya 17,000 yaliyokubaliwa na Jamhuri ya watu wa China chini ya Mpango wa Itifaki ya 12 ya ushirikiano wa kiufundi baina ya nchi tatu za China, Tanzania na Zambia. Reli zilizobaki zimehifadhiwa kwa ajili ya matengenezo ya dharura.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili *TAZARA* ni pamoja na kukabiliwa na uhaba wa fedha za uendeshaji ambao umeathiri utendaji kwa kushindwa kufanya matengenezo makubwa ya injini za treni. Changamoto nyingine ni mmomonyoko wa ardhi na ubovu wa reli hasa kwa upande wa Tanzania. Katika mwaka 2008/09, *TAZARA* ina lengo la kukarabati injini pamoja na kuboresha miundombinu ya mawasiliano ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Reli. Katika mwaka 2007/08, *SUMATRA* imeendelea kusimamia usalama na ubora wa huduma za usafiri wa reli nchini. Katika kuimarisha na kuboresha huduma na usalama wa usafiri wa reli, ukaguzi na tathmini ya hali ya usalama katika usafiri wa reli ulifanyika. Ukaguzi ulifanyika katika reli ya *TRL* kati ya Ruvu - Tanga na Tanga – Arusha na ukaguzi wa breki katika injini na mabehewa ya abiria ya reli ya *TAZARA*. Aidha, ulifanyika ukaguzi wa injini tisa zilizoingizwa nchini na *TRL* na ukaguzi wa njia ya reli, miundombinu na vyombo vyta usafiri wa reli za *TAZARA* na *TRL*. Lengo ni kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa reli zinatolewa kwa usalama wa kutosha. Kazi nyingine zilizofanywa ni pamoja na utoaji wa leseni kwa kampuni ya *TRL* kama mwekezaji mpya na uandaaji wa kanuni za usafirishaji katika reli. Kanuni hizo zinahusu usimamizi wa usafirishaji wa bidhaa hatari kwa njia ya reli, viwango vyta ujuzi na afya vinavyohitajika wawe navyo wafanyakazi wa maeneo nyeti ya kiusalama na breki, mawasiliano na abiria na viunganishi vyta mabehewa. Lengo la Kanuni hizi ni kuimarisha ulinzi na usalama katika usafiri wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri wa Anga. Katika kuimarisha na kuboresha huduma za usafiri wa anga, Serikali imeendelea kuzingatia vigezo na kanuni za usalama wa anga kama inavyoshauriwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*The International Civil Aviation Organisation-ICAO*). Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCAA*) imeendelea kutoa huduma za uongozaji ndege kwenye anga na pia kwenye viwanja kumi na vitatu (13) nchini kwa kiwango cha kuridhisha. Viwanja hivyo ni pamoja na *JNIA*, Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Tabora, Kigoma, Pemba, Zanzibar, Tanga, na Songea. Zabuni kwa ajili ya kufunga mtambo mpya wa

kuwezesha ndege kutua salama (*VOR/DME*) katika Kiwanja wa Ndege cha Mwanza imetangazwa. Ufungaji wa mtambo huo unatarajiwa kukamilika Desemba, 2008. Mamlaka inaendelea na kazi ya matayarisho kwa ajili ya ukaguzi utakaofanywa na *ICAO* Novemba, 2008. Ukaguzi huu ni muhimu kwa nchi yetu kwani matokeo yake ndiyo yanayoithibitishia Jumuiya ya kimataifa kuhusu uwezo wa nchi kuhakikisha na kuzingatia usalama wa usafiri wa anga ndani na nje ya nchi. Aidha, Mamlaka iko kwenye taratibu za kuandaa kanuni za kuendesha Mfuko maalumu kwa ajili ya mafunzo ya marubani na wahandisi wa ndege. Kanuni hizo zitaweka utaratibu wa kuweza kuwapatia mafunzo wataalamu wazalendo hapa nchini ambapo wanafunzi wataweza kuchangia baadhi ya gharama bila kutegemea misaada toka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kupitia *TCAA* inashiriki kikamilifu katika mipango mbalimbali ya kikanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) katika kuoainisha kanuni zake ili hatimaye kuwezesha ubadilishanaji wa wakaguzi wa ndege. Kuhusu ushirikiano kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, uimarikaji wa Wakala wa Udhibiti wa Kikanda ulioanzishwa Juni, 2007 (*Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency CASSOA - EAC*) utasaidia kuiongezea Mamlaka uwezo wa udhibiti kwa kutumia wataalamu wa kanda. Itifaki ya kuanzisha Wakala huu italetwa katika Bunge lako Tukufu ili iweze kuridhiwa. Aidha, usimikaji wa mitambo muhimu ya mradi wa satellite kwa ajili ya kuboresha mawasiliano ya anga Kaskazini mwa eneo la Afrika ya Mashariki na Bahari ya Hindi (*NAFISAT*) umekamilika. Mawasiliano ya anga kwa njia ya satellite yamekamilika pia katika nchi za *SADC*, Burundi, Rwanda na Uganda. Mara nchi za Kenya na Seychelles zitakapomaliza kusimika mitambo, mradi huu utakuwa umekamilika katika ukanda mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea na jitahada za kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa anga zinaboreshw na kuzingatia kanuni za usalama wa anga. Katika mwaka 2007/08 kulitokea ajali 2 zilizosababisha vifo vya watu 4 akiwemo rubani wa ndege mmoja. Mamlaka ya Usalama wa Anga inaendelea kuimarisha udhibiti wa usafiri wa anga, kampuni za ndege, waendeshaji wa viwanja na marubani ili kupunguza ajali za ndege. Lengo la Mamlaka ni kuhakikisha kuwa Kampuni za ndege na wenye viwanja wanazingatia usalama katika utendaji wao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za usalama wa usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, *TCAA* ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa wakaguzi wa ndege hasa kwenye uendeshaji (*flight operations inspectors*) pamoja na mitambo michakavu. Kutokana na upungufu wa wataalamu hawa kwenye soko la ajira, Mamlaka inabidi ishindane na Kampuni za ndege za ndani na nje ili kuwapata wataalamu hao. Kulingana na viwango vya mishahara vilivyopo, Mamlaka inashindwa kupata wataalamu hawa kwa ikama iliyopo. Ili kutatua changamoto hizo, katika mwaka 2008/09, Mamlaka itakamilisha kanuni za uendeshaji wa Mfuko Maalum wa mafunzo ya marubani na wahandisi wa ndege. Mfuko huu utaanza kwa kudhamini wataalamu wa Kitanzania kwa ajili ya kusomea taaluma hii. Aidha, Mamlaka inatarajia kusimika mitambo mipy ya “*VHF Relay Stations*” kwenye vituo sita vya Tabora, Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Mtwara. Vituo hivi vitasaidia kuboresha huduma ya mawasiliano kati ya marubani na waongoza ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08 idadi ya abiria waliosafiri kwa kutumia usafiri wa anga iliongezeka kutoka abiria 2,649,664 mwaka 2006/07 na kufikia abiria 2,912,432 kwa mwaka 2007/08 ikiwa ni ongezeko la asilimia 10. Aidha, idadi ya abiria waliosafiri ndani na nje ya nchi iliongezeka kutoka abiria 1,145,310 mwaka 2006/07 na kufikia abiria 1,307,561 mwaka 2007/08, hii ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.2. Idadi ya abiria waliosafiri ndani na nje ya nchi kupitia Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere iliongezeka kutoka abiria 1,195,275 mwaka 2006/07 hadi kufikia abiria 1,418,896 mwaka 2007/08, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 18.7. Idadi ya abiria waliosafiri humu nchini iliongezeka kwa asilimia 6.7, kutoka abiria 1,504,354 mwaka 2006/07 hadi kufikia abiria 1,604,871 mwaka 2007/08.

Safari za ndege ziliongezeka kutoka safari 163,341 mwaka 2006/07 hadi kufikia safari 175,711 mwaka 2007/08 ikiwa ni sawa na asilimia 7.5. Safari za ratiba (*scheduled frequencies*) ziliongezeka kutoka safari 96 katika mwaka 2006/07 hadi safari 113 katika mwaka 2007/08. Kuongezeka kwa abiria ndani na nje kumetokana na kuongezeka kwa huduma za kiuchumi na kijamii katika sekta ndogo ya usafiri wa anga. Katika mwaka 2007/08 kiasi cha mizigo kilipungua kutoka tani 34,711.4 zilizobebwa mwaka 2006/07 hadi tani 29,961.5. Sababu za kupungua kwa mizigo ni upungufu wa minofu ya samaki toka Mwanza, kupungua kwa shughuli za ujenzi katika maeneo ya migodi kwa kuwa shughuli nyingi zimekamilika. Sababu nyingine ni kupungua kwa bidhaa mbalimbali zinazopitia Zanzibar baada ya Shirika la Oman Air kusitisha safari zake hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuisaidia Kampuni ya Ndege ya Tanzania (*ATCL*) ili iweze kuboresha huduma zake ipasavyo na kuijiendesha kibiashara. Baada ya kutengana na Shirika la Ndege la Afrika Kusini (*SAA*), *ATCL* ilifanikiwa kuzindua rasmi nembo yake mpya tarehe 1 Oktoba, 2007. Nembo hii ina picha ya Twiga na kilele cha mlima Kilimanjaro. Ili kudhibiti mapato ya Kampuni, *ATCL* imeingia mkataba na Kampuni ya Mercator ili kufanikisha usimamizi wa mapato ya ndani kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Katika mwaka 2007/08 *ATCL* iliweza kununua ndege mbili aina ya Dash 8-300 zenye uwezo wa kubeba abiria 50 kila moja. Ndege hizi ziliwasili nchini Machi, 2008.

Aidha, *ATCL* ilikodisha ndege kubwa aina ya Airbus A320-214 yenye uwezo wa kuchukua abiria 150 kwa mkataba wa miaka sita iliyowasili nchini Aprili, 2008. Kampuni ina jumla ya ndege 6, 3 za kukodi na 3 za Kampuni yenyewe. Kampuni inatarajia kutumia ndege hizo kwa safari za kwenda Tabora, Kagera, Mtwara, Kilimanjaro na Zanzibar. Aidha, kampuni inatarajia kutumia ndege hizo kwa safari katika maeneo ya Maziwa Makuu kwa kwenda Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08 Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*) iliweza kubeba wastani wa abiria 254,000 (*Revenue passengers*) ikilinganishwa na uwezo wa abiria 251,000 mwaka 2006/07. Aidha, ndege za Kampuni zilifanikiwa kuondoka kwa wakati (*On Time Performance*) kwa kiwango cha asilimia 80 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 75 cha mwaka 2006/07.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, *ATCL* inatarajia kupanua huduma zake hadi katika miji ya Bukoba, Shinyanga, Lindi na Pemba, kuongeza safari

zake za nje hadi katika mji wa Mumbai (India) na kufanya ushirikiano wa kibashara na Kampuni nyingine ili abiria wake wachukuliwe na Kampuni hizo kuwapeleka kule ambako ATCL haifiki. Mikakati mingine ni kununua ndege mbili zeny uwezo wa kuchukua abiria 72 kila moja. Aidha, katika kutimiza mkakati wa kuifanya JNIA kuwa kiungo cha usafiri katika nchi za Afrika Mashariki na Kati, Kampuni inatarajia kukodi ndege nyingine ya B737-200 au ndege nyingine yenye ukubwa huo. Ndege hii itawezesha Kampuni kupanua safari zake hadi Zambia na Zimbabwe ili kubeba abiria waendao Dubai na kwingineko ili kuunga safari zao Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kampuni binafsi ya Ndege ya Precisionair, katika mwaka 2007/08 Kampuni ilibeba abiria 465,152 ikilinganishwa na abiria 425,306 wa mwaka 2006/07 ikiwa ni ongezeko la asilimia 10. Kampuni iliingia mkataba na Kampuni ya ATR ya Ufaransa wa kununua ndege mpya saba, (tatu ATR 42-500 na nne ATR 72-500). Machi, 2008 Kampuni ilipokea ndege moja aina ya ATR 72-500 na ndege nyingine kama hiyo inatarajiwa kuwasili hapa nchini Oktoba, 2008. Kampuni inatarajia kupokea ndege mbili kila mwaka kuanzia 2009 hadi 2011.

Aidha, April 2008, Kampuni ilikodisha ndege nyingine aina ya Boeing 737-300 yenye uwezo wa kubeba abiria 116. Hatua hii imewezesha Kampuni kuwa na ndege tisa, nne ATR 42, nne ATR 72 na Boeing 737-300 moja. Ndege ya pili ya Boeing 737-300 inatarajiwa kuwasili nchini Oktoba, 2008. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya ndege Kampuni iko kwenye mchakato wa kujenga Karakana ya matengenezo ya Ndege (Hangar) kwenye Kiwanja cha Ndege Cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Ujenzi wa Karakana hii unatarajiwa kukamilika baada ya miaka miwili.

Matarajio ya Kampuni ni kubeba abiria 616,354 mwaka 2008/09. Ili kufikia lengo hilo Kampuni ina mikakati ya kuongeza safari za ndani ya nchi za kwenda Songea, Tanga na Pemba. Aidha, Kampuni inatarajia kuongeza safari za kikanda kwenda Luanda nchini Angola, Lubumbashi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Johannesburg, Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) ulitekeleza majukumu yake ya kuwashudumia viongozi wakuu wa Serikali na kupata mapato ya shilingi bilioni 4.6, ambapo hadi Mei, 2008 jumla ya shilingi bilioni 3.0 zilikusanywa. Aidha, TGFA iliweza kupunguza ukaaji wa ndege chini kwa asilimia 90. Wakala umeweza kuboresha ndege zake hadi kufikia kiwango cha “Business Class” ili kuwavutia zaidi wateja wao na kuwezesha ndege zote kuruka kwa wastani wa asilimia 95 ya saa zilizokuwa zimekadiriwa.

Pamoja na mafanikio hayo, Wakala ulikabiliwa na changamoto za upungufu wa marubani, uchakavu wa ndege na uhaba wa fedha. Katika kutatua changamoto hizi, katika mwaka 2008/09, Wakala una lengo la kufanya matengenezo makubwa ndege zake ili kuimarisha na kuboresha usalama katika utoaji wa huduma zake. Aidha, Wakala utaajiri marubani wapya na wahandisi wa ndege pamoja na kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa Viwanja vya Ndege. Wizara inaendelea kuboresha hali ya viwanja vya ndege nchini. Katika mwaka 2007/08, awamu ya pili ya ukarabati wa *JNIA* uliendelea ambapo kazi zilizoteklezwa ni pamoja na matengenezo ya maegesho ya ndege, upanuzi wa barabara ya pili ya kurukia na kutua ndege, mfumo wa umeme pamoja na uboreshaji wa mazingira. Miradi mingine ni pamoja na kufanya upembusi yakinifu na usanifu wa jengo la abiria (*Terminal 3*) na jengo la mapokezi ya viongozi wakuu. Viwanja vingine vilivyofanyiwa ukarabati ni Musoma na Lake Manyara ambavyo vilifanyiwa ukarabati wa njia za kurukia ndege kwa kiwango cha changarawe.

Aidha, kazi za ujenzi wa uzio zilifanyika katika viwanja vya Musoma, Arusha na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanja cha Mwanza kazi zinazoendelea ni ujenzi wa maegesho ya ndege za mizigo na ukamilishaji wa mchakato wa kumpata mkandarasi kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanja hicho. Aidha, ukarabati wa maegesho na viungio vyake katika Kiwanja cha Ndege cha Arusha unaendelea. Kuhusu kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe, Mbeya awamu ya mwisho ya ujenzi inaendelea. Kazi zilizoteklezwa katika mwaka 2007/08 ni pamoja na ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa viungio na ujenzi wa mfumo wa kuondoa maji ya mvua kiwanjani. Aidha, usanifu wa ukarabati mkubwa wa Viwanja vya Ndege vya Bukoba, Shinyanga, Tabora, Sumbawanga, Mafia, Kigoma na Arusha umeendelea kutekelezwa kwa Msada wa Benki ya Dunia. Serikali ya Marekani kupitia mfuko wake wa '*Millenium Challenge Cooperation*' (*MCC*) utafadhilli ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na ajali za ndege zinazotokea majini, Serikali imekamilisha mipango ya uokoaji majini (*water rescue plans*) katika viwanja vya ndege vya Mwanza, Mtwara, Kigoma, Musoma, Bukoba na Tanga. Lengo la mipango hii ni kuiwezesha Serikali kuwa na uwezo wa kukabiliana na matukio ya ajali za ndege haraka na hivyo kuokoa maisha ya watu na mali. Mipango hii itafanyiwa majoribio katika mwaka 2008/09 ili kupima uwezo wa wadau na kurekebisha upungufu utakaobainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2008/09, kazi zitakazoteklezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa uzio wa Viwanja vya ndege vya Mtwara, Tabora, Kigoma na Lake Manyara. Kazi nyingine ni ununuzi na ufungaji wa mitambo ya ukaguzi wa abiria na mizigo katika viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora, Bukoba, Mwanza, Musoma, Arusha, Shinyanga Dodoma na Mtwara. Aidha, Serikali itaendelea na taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa viwanja vya Pugu, Majohi na Buyuni kwa ajili ya makazi ya wananchi wa Kigilagila na Kipunguni. Wananchi wa Kigilagila na Kipunguni wanahamishwa ili kupisha upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere pamoja na miradi mingine ya maendeleo. Miradi mingine itakayoteklezwa ni pamoja na ukamilishaji wa ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege za mizigo na viungio vyake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itafanya upanuzi na uendelezaji wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Upanuzi huo utahusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo jipya la mizigo, jengo la kuongozea ndege, kurekebisha mifumo ya maji ya mvua na maji safi, kuweka taa za kuongozea ndege, ujenzi wa jengo la kituo cha umeme, ujenzi

wa miundombinu ya mafuta ya ndege na ujenzi wa viungio (*turning loops*). Mradi huu mkubwa utakaogharimu zaidi ya Dola za Marekani milioni 14 zitatolewa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania, BADEA na *OPEC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Hali ya Hewa. Katika mwaka 2007/08, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kuboresha huduma zake ili ziweze kufikia matarajio ya watumiaji wa huduma hizo. Katika kuboresha huduma hizo, Mamlaka imefunga mitambo na vifaa mbalimbali katika maeneo kadhaa hapa nchini ili kuboresha huduma zake. Mitambo ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe imefungwa katika vituo vya Mtwara na Bukoba. Vifaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na vifaa vya kupimia mvua (*rain gauge & cylinders*), redio za mawasiliano na Kompyuta vimefungwa katika maeneo ya Morogoro, Iringa, Songea, Musoma na Mahenge. Aidha, mitambo ya kisasa ya mawasiliano na ya kuchambua taarifa na takwimu za hali ya hewa imefungwa katika viwanja vya ndege vya Mwanza, KIA, JNIA na Zanzíbar. Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imefufua vituo 220 na kuanzisha vituo vipyta 120 vya kupima mvua nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutekeleza wajibu na majukumu yake ya kukusanya, kuhakiki, kuratibu taarifa za hali ya hewa na kusambaza taarifa hizo nchini. Mamlaka pia imeendelea kutoa utabiri wa kila siku na wa msimu. Aidha, utoaji tahadhari dhidi ya hali mbaya ya hewa na majanga yanayohusiana na hali ya hewa imeendelea kutolewa. Mamlaka imeendelea kutoa huduma za hali ya hewa kwa sekta za kiuchumi na kijamii hususan sekta za usafiri, kilimo, maji, mazingira na ujenzi. Katika mwaka 2007/08, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa kituo cha hali ya hewa kilichopo Mpanda na huduma za hali ya hewa zitaanza kutolewa mwaka 2008/09. Aidha, Mamlaka imepata hati ya umiliki (*title deed*) ya eneo litalotumika kujenga Makao Makuu ya Mamlaka. Eneo hilo lipo Barabara ya Sam Nujoma, Dar es salaam. Hivi sasa Mamlaka inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Mamlaka itaendelea na majukumu yake ya kutoa huduma na taarifa za hali ya hewa kwa wananchi na sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Mamlaka itaongeza vituo vya kupima hali ya hewa na kuimariswa vilivyopo kwa kiviongezea vifaa. Ujenzi wa ofisi mpya kwa ajili ya vituo vya Manyara na Pemba utaanza na mafunzo kwa wafanyakazi yataendelea kutolewa ndani na nje ya nchi kwa nia ya kuwaongezea uwezo wa kutoa huduma bora. Ujenzi wa Nyumba za Viongozi na Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08, Serikali kupitia Wakala wa Majengo ya Serikali (*TBA*) imeendelea kutekeleza azma yake ya kujenga na kuboresha makazi ya watumishi wa umma na ofisi za Serikali. Hadi sasa Wakala umeweza kukamilisha ujenzi wa nyumba 278 za watumishi wa umma katika Mikoa 21 ya Tanzania Bara. Aidha, Serikali kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 imehakikisha kuwa ujenzi wa majengo ya ofisi za umma unafanyika kwa kuzingatia mahitaji na

matakwa halisi ya watu wenyewe ulemavu. Ujenzi na matengenezo ya nyumba za Viongozi, pamoja na ununuzi wa samani zinazohitajika unaendelea vizuri. Katika juhudini za kuendelea kujiimarisha kiuchumi Wakala umeanza kujenga Majengo matatu ya ghorofa kwa njia ya ubia. Majengo hayo ni pamoja na jengo la ghorofa nane lenye nyumba (flats) 16 katika Kiwanja na. 93/1 Ada Estate na majengo mawili ya ghorofa tatu (yenye nyumba 8 kila moja) katika kiwanja Na. 76 Ada Estate Jijini Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine inayoendelea ni kufanya upembuzi yakinifu wa eneo la iliyokuwa Kampuni ya Mabasi ya Taifa (KAMATA) ili eneo hilo liweze kutumika ipasavyo. Aidha, Wakala unaendelea na ujenzi wa majengo 12 ya ghorofa katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Morogoro, na Dodoma. Pamoja na Wakala kuwa na vyanzo vya mapato vitokanavyo na mauzo ya nyumba, pango la nyumba na ada za ushauri, kasi ya ujenzi wa nyumba mpya kwa ajili ya watumishi wa Umma ni ndogo. Hii ni kutokana na kodi ya nyumba (pango la nyumba) kwa nyumba zilizopangishwa kwa watumishi kuwa ndogo na baadhi ya watumishi wa umma waliokopeshwa kushindwa kurejesha mkopo kwa wakati na ongezeko kubwa la gharama za ujenzi. Katika kutatua changamoto hizo, Wakala umeazimia kuendelea kuboresha usimamizi na udhibiti wa fedha na manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa wadau kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Wakala umepanga kuendelea kujenga nyumba za watumishi wa Serikali na kuongeza jitihada ya kununua viwanja zaidi hususan eneo la Kigamboni. Wakala utatoa huduma bora za ushauri wa kitaalam kwa miradi ya ujenzi wa nyumba za watumishi na ofisi za Serikali zitakazozingatia mahitaji na matakwa ya watu wenyewe ulemavu. Aidha, Wakala utatekeleza ujenzi wa nyumba tano 5 za Viongozi kwa kila wilaya za Bariadi, Nkasi, Simanjiro na Kilindi. Wakala utanunua nusu ya hisa ya asilimia ishirini na tano katika miradi mitatu ya ubia katika viwanja Na. 45 na 46 Chimara na Ex- NEDCO Plot Chole/Haile Sellasie-Dar es Salaam. Pia, Wakala utaendelea na Ujenzi wa jengo la ghorofa nane lenye nyumba (flats) 16 katika kiwanja Na. 93/1 Ada Estate-Dar es Salaam, na Ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa tatu yenye nyumba (flats) 8 kila moja katika kiwanja Na. 76 Ada Estate- Dar es Salaam. Wakala itajenga jengo la ghorofa lenye nyumba (flats) 6 katika kiwanja Na. 5 Mtaa wa Moshi-Dodoma. Aidha, Wakala umepanga kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali hasa kutoka kwa watumishi wa umma waliokopeshwa nyumba na kubuni vyanzo vipyta vya kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji wa Taaluma na Shughuli za Ujenzi. Wizara inasimamia Baraza na Bodi mbalimbali zinazohusika na uratibu wa shughuli za kisekta kama vile uhandisi, ukandarasi, usimamizi wa vifaa, ubunifu wa majengo na ukadiriaji wa majenzi.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Ujenzi (*NCC*), limeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Katika mwaka 2007/08 Baraza kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali limeendelea na maandalizi ya miongozo ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa njia ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnerships - PPPs*). Shughuli nyingine ni kuanza ujenzi wa jengo la ofisi la ghorofa 14 kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) na mwekezaji binafsi. Majukumu

mengine ni kuendelea kutunisha Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund - CIDF*) na kwa kushirikiana na kitengo cha Ukaguzi wa Kiufundi cha Wizara ya Fedha, Baraza lilifanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi 23. Miradi hiyo ilijumuisha miradi 10 ya barabara, miradi 8 ya majengo na miradi 5 ya maji. Katika ukaguzi huo Baraza lilibaini upungufu katika miradi hiyo amba ni pamoja na kutokutumika ipasavyo kwa utekelezaji wa mikataba ya miradi, kutokukidhi mahitaji ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na usimamizi duni wa miradi. Kasoro hizo zimerekebishwa na mamlaka husika na kuhakikisha kuwa wahusika wanachukuliwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2008/09, Baraza litaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa 14, kutoa mafunzo na ushauri wa kiufundi na kutatua migogoro. Shughuli nyingine ni ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi, kuhamasisha mikakati ya kukuza ubora na tija katika utekelezaji wa shughuli za ujenzi. Aidha, Baraza litaendelea kuhamasisha ushirikiano katika sekta ya Ujenzi nchini na mahusiano ya kanda na kimataifa yenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa sekta ya Ujenzi. Mpango mwingine ni pamoja na uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi (*Construction Industry Development Fund - CIDF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mfuko wa Barabara (*RFB*). Katika mwaka 2007/08, Bodi ya Mfuko wa Barabara (*RFB*) ilipokea toka HAZINA jumla ya shilingi bilioni 149.762 na kuzigawa kwa taasisi zinazotumia fedha za Mfuko huu hadi kufikia Machi, 2008, ikilinganishwa na shilingi bilioni 91.90 zilizopokelewa mwaka 2006/07. Bodi ilifanikiwa kufanya mapititio ya Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Barabara “*Road Toll (amendment) Act No.2 of 1998*” kwa lengo la kuifanya marekebisho. Lengo ni kuifanya sheria hiyo iweze kuendana na mabadiliko yaliyopo hivi sasa ikiwa ni pamoja na kuongeza vifungu vyta sheria vitakavyotoa adhabu kwa watakaobainika kutumia vibaya fedha za Mfuko.

Aidha, Bodi ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kucheleta kukamilika kwa taarifa za ukaguzi za Halmashauri kwa upande wa Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa hesabu za Serikali. Kutokamilika mapema kwa taarifa za ukaguzi hususani kwa Halmashauri kunachelewesha uchukuaji wa hatua sahihi mapema na uwezo mdogo wa kutumia fedha za Mfuko katika kipindi kilichopangiwa (*Full absorption capacity*) kwa Mawakala wa Barabara. Hali hii husababisha fedha zilizotengwa kwa mwaka wa fedha husika kuendelea kuwepo mpaka mwaka wa fedha unaofuata. Hali hii husababisha kazi za barabara kutokamilika kwa mwaka uliopangwa. Katika kutatua changamoto hizo, katika mwaka 2008/09 Bodi imejiwekea mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuziba mianya ya ukwepajhi wa kulipa ushuru wa mafuta ya Petroli ili kuongeza mapato. Aidha, Bodi inatarajia kuongeza ufuutiliaji wa matumizi ya Mfuko wa Barabara kwa Mawakala wa Barabara ili kazi zikamilike kwa wakati uliopangwa na kupata thamani halisi ya kazi iliyofanywa (*Value for Money*).

Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, mkiwa wajumbe wa Bodi za Barabara za Mikoa, tusaidiane kuzitaka taasisi zinazotumia fedha za Mfuko huu kuzitumia fedha hizi katika shughuli za matengenezo ya barabara na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*). Katika mwaka 2007/08, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, ilisajili wahandisi 444 na Kampuni za ushauri wa kihandisi 17 ikilinganishwa na mwaka 2006/07 ambapo ilisajili wahandisi 543 na Kampuni za ushauri wa kihandisi 10. Idadi hii inafanya jumla ya wahandisi waliosajiliwa kufikia 7,937 na Kampuni za ushauri wa kihandisi zilizosajiliwa kufikia 151. Aidha, Bodi imeendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu. Lengo la mpango huu ambao unagharamiwa na Serikali ni kuwawezesha wahandisi wahitimu kupata uzoefu wa kutosha wa kufanya kazi za kihandisi na hivyo kuweza kutoa michango yao kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.

Katika mwaka 2007/08, Bodi ilisimamia mafunzo ya wahandisi wahitimu 515. Kati ya wahandisi hao, 169 wanafadhiliwa na Kampuni binafsi. Jumla ya Wahandisi wahitimu 78 toka Serikali za mitaa na Taasisi za Serikali wamehitimu mafunzo hayo na kusajiliwa na Bodi.

Katika kipindi hiki, Bodi imetembelea miradi ya ujenzi wa barabara na migodi yote mikubwa ili kuhakikisha kuwa wahandisi wa kigeni walioajiriwa katika miradi hiyo wanautaalamu wa kutosha na wamesajiliwa na Bodi. Jumla ya wahandisi wageni 22 walisajiliwa, na 8 walikataliwa usajili kwa sababu hawakuwa na sifa za kutosha. Bodi iliweza kukagua shughuli za kihandisi pamoja na maendeleo ya wahandisi katika Halmashauri za Wilaya, Manispaa, na Majiji katika mikoa 17 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Bodi inatarajia kusajili wahandisi 800, Mafundi Sanifu 200 na Kampuni za ushauri wa kihandisi 25. Bodi pia itaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu 800. Idadi hii ni pamoja na wahandisi wahitimu 400 wanaoendelea na mafunzo wakiwa ni wenye ufadhili wa Serikali na watu binafsi. Aidha, Bodi itaendelea kufanya ukaguzi kwa shughuli za kihandisi nchini ili hatimaye shughuli zote za kihandisi ziwe zinafanywa na wahandisi waliosajiliwa kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi. Bodi imepanga kutembelea mikoa yote ya Tanzania Bara ili kuhamasisha utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa wahandisi baada ya kufanyiwa marekebisho yaliyopitishwa na Bunge mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa (*NBMM*). Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa (*NBMM*) iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kukuza, kusimamia na kuratibu mafunzo na Elimu inayohusu fani ya ununuzi na ugavi. Katika mwaka 2007/08 Bodi ilisajili wataalamu 187 na kuwatahini wataalamu 1980 wa ngazi mbalimbali ikilinganishwa na mwaka 2006/07 ambapo ilisajili wataalamu 149 na kuwatahini wataalamu 1,684. Hii inafanya idadi ya wataalamu waliosajiliwa na kupewa miongozo ya maadili kufikia 1850. Miongozo hii inawaasa wataalamu kufuata mienendo mizuri katika utekelezaji wa majukumu yao na kuepukana na vitendo vya ubadhififi, wizi na rushwa. Aidha, Bodi iliendesha mafunzo endelevu (*Continued Professional Development*) ambapo warsha na semina 10 zilifanywa kwa watendaji wa ununuzi na ugavi katika Serikali Kuu, Mashirika ya Umma, Idara za Serikali na Asasi zake. Mafanikio mengine yanahusu Bodi kuanzisha ushirikiano na Bodi kama hii ya nchini India ijulikanayo kama *Indian Institute of Materials Management (IIMM)* ambapo taasisi

hizi zilisaini mkataba wa ushirikiano. Kupitia mkataba huo Bodi imefanikiwa kununua vitabu 480 vya taaluma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, malengo ya Bodi ni pamoja na kuuhamasisha Umma juu ya sheria mpya ya Bodi iliyopitishwa na Bunge mwaka 2007 juu ya uboreshaji wa taaluma ya ununuzi na ugavi, kuandaa kanuni za kutekeleza sheria mpya ya Taaluma ya Ununuzi na Ugavi. Pia, kuongeza idadi ya watahiniwa wa mitihani na kuendelea kuishauri Serikali juu ya masuala ya Ugavi na kuandaa mitaala mipyä ili iendane na mabadiliko ya taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Usajili wa Makandarasi (*CRB*). Katika mwaka 2007/08, CRB ilisajili makandarasi wapya 662 na hivyo kufanya jumla ya idadi ya makandarasi wote kufikia 4,630. Katika kutekeleza majukumu yake ya kuratibu shughuli za makandarasi, Bodi ilifanya ukaguzi katika miradi 1,251 ya ujenzi katika mwaka 2007/08 ambayo ni ongezeko la asilimia 14 zaidi ya ile iliyokaguliwa mwaka 2006/07. Katika miradi iliyokaguliwa asilimia 78.4 ilikutwa haina upungufu. Makandarasi waliokutwa na upungufu walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Bodi pia ilisajili jumla ya miradi 2,084 ya ujenzi ikilinganishwa na miradi 1989 iliyosajiliwa mwaka 2006/07.

Aidha, *CRB* imeendelea kutekeleza mkakati wa kuendeleza makandarasi wazalendo ambapo kozi 6 ziliendeshwa nchini kote chini ya mpango wa mafunzo endelevu wa makandarasi. Jumla ya makandarasi 246 walihudhuria kozi hizi. Bodi imeendelea kutoa malipo ya awali kwa makandarasi chini ya mfuko wa kusaidia makandarasi (*Contractors Assistance Fund*). Wanachama wa mfuko huo wameongezeka hadi kufikia 508 na mfuko umekusanya jumla ya shilingi bilioni 1.26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09, Bodi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuendeleza makandarasi na kuratibu shughuli zao. Pia, Bodi itafungua ofisi mpya ya kanda huko Arusha ikiwa njia mojawapo ya kusogea huduma zake karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (*AQSRB*). Katika mwaka 2007/08, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilifanikiwa kusajili Wabunifu Majengo 35 na Wakadiriaji Majenzi 15, ikilinganishwa na mwaka 2006/07 ambapo Wabunifu Majengo 16 na Wakadiriaji Majenzi 13 walisajiliwa. Aidha, Wataalamu 28 wenye sifa za kati walisajiliwa ikilinganishwa na wataalamu kama hao 38 waliosajiliwa mwaka 2006/07. Kampuni za Ubunifu Majengo 15 na Ukadiriaji Majenzi 12 zilisajiliwa na kufikisha jumla ya Kampuni kuwa 180, kati ya hizo 10 zikiwa ni Kampuni za kigeni. Bodi ilitembelea na kukagua miradi 296 katika mikoa 8 ya Tanzania Bara ili kuhakikisha kuwa kazi za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi zinabuniwa na kusimamiwa na wataalamu waliosajiliwa. Aidha, Bodi iliendelea kusimamia programu ya mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa fani za ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi kwa lengo la kuwapa uzoefu ili wasajiliwe. Programu hii ina wahitimu 60. Bodi ilisajili miradi mipyä ya ujenzi 429,

kwa lengo la kuhakikisha kwamba miradi yote ya ujenzi inasimamiwa na wabunifu majengo na kupata ushauri wa wakadiriaji majenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, Bodi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja kutokamilika kwa sheria ya majengo, ambayo ingeweza kusaidia kuainisha viwango mbalimbali vyta ujenzi na kuweka ubora unaotakiwa kwa kila aina ya matumizi ya jengo hasa ya shughuli za kijamii na pia kuainisha ujenzi sawia na mipango ya miji mbalimbali. Aidha, bado jamii hajatambua umuhimu wa kuwatumia wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi katika miradi yao ya ujenzi, hasa baada ya kupata kibali cha ujenzi. Katika kutatua changamoto hizi Wizara inaendelea na taratibu za kukamilisha mchakato mzima wa kurekebisha Sheria namba 16 ya mwaka 1997 iliyounda Bodi hiyo na kutunga Sheria mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Bodi inatarajia kusajili wataalamu 70 na wale wenye sifa za kati 53. Bodi inatarajia kusajili Kampuni za kitaalamu 53 na kutahini wataalam 112. Bodi pia itaendeleza mpango wa mafunzo maalum ya vitendo kwa ajili ya kuwasaidia wahitim 60 wa taaluma husika ili wawze kusajiliwa kwa mujibu wa sheria. Bodi imepanga kukagua sehemu 270 katika mikoa yote ya Tanzania Bara ili kuhakikisha kwamba wadau wote wanaelewa umuhimu wa kuwatumia wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi katika kuendeleza miradi ya majengo na majenzi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda za Maendeleo (*Development Corridors*). Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kufanya jitihada za kuendeleza miundombinu ya usafiri katika kuchochea matumizi ya rasilimali za kiuchumi na kijamii zilizobainishwa kuwepo katika kanda za maendeleo. Tanzania ina kanda nne za maendeleo; Kanda hizo ni: (i) Ukanda wa Kati, (ii) Ukanda wa Mtwara, (iii) Ukanda wa Tanga na (iv) Ukanda wa Dar es salaam.

Ukanda wa Maendeleo wa Kati umeendelea kuimashwa kwa kuboresha miundombinu ya reli, barabara pamoja na bandari za Dar es Salaam na Tanga na Ziwa Victoria. Aidha, ukodishaji wa uendeshaji wa shughuli za reli ya kati ambayo inatoa huduma za usafiri katika ukanda huo ni hatua mojawapo ya kuendeleza ukanda huo. Hatua nyingine ambazo Serikali za Tanzania, Rwanda na Burundi zimekusudia kuchukua ni kujenga njia ya reli ya kati kutoka Isaka hadi Kigali na kuunganisha nchi ya Burundi. Upembuzi yakinifu kwa utekelezaji wa mradi huu unaendelea na unatarajiwa kukamilika Agosti, 2008.

Juhudi zinaendelea kuchukuliwa kwa nia ya kuboresha barabara zinazounganisha nchi za Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Watu wa Kongo kuitia Bandari za Dar es Salaam na Tanga. Hii ni pamoja na kuimashwa na kupanua daraja la mto Ruvu, ujenzi wa barabara zilizo katika ukanda huu kwa kiwango cha lami, na kuweka kivuko chenye uwezo mkubwa katika rasi ya Kigongo-Busisi katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara Serikali za Tanzania na Msambiji zimeendelea na ujenzi wa Daraja la Umoja katika mto Ruvuma litakalounganisha nchi hizi mbili na hivyo kusaidia kukuza shughuli za

kiuchumi na maendeleo. Ujenzi wa daraja hili unaendelea ambapo nguzo 19 zimekamilika, sawia na ujenzi wa barabara ya urefu wa kilometa 5 kila upande kwa kiwango cha lami. Juhudi zinaendelea kuchukuliwa kuwezesha ujenzi wa barabara kutoka bandari ya Mtwara hadi bandari ya Mbamba Bay ili kufungua fursa za ushirikiano wa kibiashara na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia kwa kutumia bandari ya Mtwara. Aidha, Serikali ya Marekani kwa kupitia *MCC* imekubali kufadhili ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Namtumbo kupitia Songea hadi Mbinga chenye urefu wa kilomita 139. Maandalizi ya kumpata mkandarasi wa kujenga barabara hii yanaendelea na yanatarajiwा kukamilika Agosti, 2008. Mazungumzo kati ya Serikali na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) yanaendelea ili Benki hiyo iweze kufadhili ujenzi wa kipande cha barabara chenye urefu wa kilomita 200 kati ya Mangaka - Tunduru hadi kufikia daraja la Diaca nchini Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi mingine iliyo katika ukanda wa Tanga, pia Serikali inakusudia kuvuna magadi (Soda Ash) katika Ziwa Natron. Mradi huu wa uvunaji magadi unasimamiwa na Shirika la TATA Chemicals la India na NDC la Tanzania. Nia ni kuvuna kiasi cha tani 500,000 kwa mwaka. Mzigo huu ni mkubwa na hivyo unahitaji mpangilio sahihi wa miundombinu kuweza kuuhudumia. Tathmini ya njia muafaka za usafirishaji wa tani hizo imeshafanywa ambapo upembusi yakinifu umeonyesha kuwa ipo haja ya kuimarisha njia ya reli iliyopo kati ya Tanga, Moshi na Arusha, ikiwa ni pamoja na kuimarisha madaraja. Aidha, kuna umuhimu wa kujenga reli na barabara mpya zitakazounganisha maeneo ya mradi na mji wa Arusha pamoja na kupanua uwezo wa bandari ya Tanga. Hii itasaidia kuhimili ongezeko la mizigo litakalosababishwa na kuboreka kwa miundombinu ya uchukuzi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukanda wa Dar es Salaam unaendelea kuimarishwa kwa kuboresha miundombinu ya reli ya *TAZARA*, barabara na Bandari ya Dar es Salaam. Miradi iliyo katika ukanda huu ni pamoja na barabara ya Msimba-Ruaha/Ikokoto-Mafinga (km 167) ambapo hatua za utekelezaji zilizofikiwa ni kuwa usanifu wa kina umekamilika na mchakato wa kumpata Mkandarasi wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami unaendelea. Miradi mingine ni ukarabati wa barabara za Songea-Makambako na Mafinga- Mgololo. Aidha mradi mwingine ni ujenzi wa daraja jipya la Ruvu ambapo utekelezaji wake ni kuwa ujenzi wa mihimili ya kubeba nguzo za daraja jipya na nguzo za pembeni umekamilika. Matayarisho ya ujenzi wa nguzo za katikati (piers) yanaendelea. Mradi mwingine ni uimarishaji wa njia ya reli ya *TAZARA* eneo la Kitete-Mpanga ambalo linaendelea kufanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushiriki katika Jumuiya Mbalimbali katika mwaka 2007/08 Wizara iliendelea kushiriki katika mikutano, semina, kongamano na warsha mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Mikutano hiyo ilifanyika kwa lengo mahsusil la kukuza mashirikiano ili kuendeleza miundombinu na huduma zake. Mikutano hiyo ni pamoja na ile ya ushirikiano kati ya Serikali ya Muungano (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Maziwa Makuu (*Great Lakes*).

Kuhusu ushirikiano wa *SMT* na *SMZ*, Wizara imefanya mikutano Oktoba, 2007 na Machi, 2008. Lengo ni kutathmini utendaji wa sekta zetu za mawasiliano na uchukuzi

hasa kwenye masuala yote yanayohusu Muungano. Aidha, mikutano hii, pia ina lengo la kukuza na kuimarisha ushirikiano katika sekta za uchukuzi na mawasiliano.

Ili kuimarisha usalama wa usafiri majini, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia taasisi zake zinazosimamia usafiri wa majini zinafanya kazi kwa ushirikiano. Katika kufanya hivyo, ushauri wa Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri Baharini (International Maritime Organization - IMO) unazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushiriki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Wizara imeendelea kushiriki kwenye miradi ya pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika sekta ya usafiri wa barabara, maji, reli, anga, na sekta ya hali ya hewa. Katika sekta ya barabara, miradi inayohusika ni Mradi wa Barabara za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East Africa Road Network Project - EARNP*). Mradi huu ulianzishwa mwaka 1998 kwa lengo la kujenga barabara kwa kiwango cha lami ambazo sifa zake ni lazima ziwe ni zile zinazounganisha nchi mbili au zaidi. Sekretariati ya Jumuiya kwa kushirikiana na nchi wanachama zinatafuta fedha ili kujenga na kukarabati barabara hizo. Dola za kimarekani milioni 142 za ujenzi wa barabara ya Arusha - Namanga – Athi River zimepatikana kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Benki ya Japan ya Ushirikiano wa Kimataifa (JBIC). Ujenzi wa barabara hii umeanza. Mradi huu wa kilomita 240 utaunganisha Tanzania na Kenya ambapo kilomita ziko Tanzania na kilomita 136 ziko Kenya. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) imetoa fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya Arusha – Moshi – Holili/Teveta – Mwatati - Voi na Tanga – Horohoro – Saadan – Bagamoyo. Taratibu za kumpata Mtaalamu Mwelekezi zinaendelea.

Katika kuendeleza usafiri wa majini kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sheria ya Usafiri katika Ziwa Victoria imekamilika na kuridhiwa na Bunge la Afrika Mashariki. Sheria hii inaandaliwa sanjari na Sheria ya Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria. Aidha, Kamati ya Wakuu wa Mamlaka za Usafiri wa Majini na huduma za Bandari ya kuratibu maendeleo na kuoanisha Sera za usafiri wa majini imeanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa reli, nchi za Afrika Mashariki zimeamua kuwa na Mpango Kamambe (*Railway Master Plan*) wa kuendeleza usafiri wa reli utakaouniganisha nchi hizi. Mtaalam Mwelekezi yuko katika hatua za mwisho za kukamilisha kuandaa mpango huu. Mpango huu unajumuisha reli ya Tanga -Arusha – Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushiriki katika Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*). Wizara imeendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali zinazotekelizwa na nchi wanachama wa SADC. Katika mkutano wa Wakuu wa nchi uliofanyika Agosti, 2007 huko Lusaka, Zambia uliazimia kuweka kipaumbele katika uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi. Tanzania ikiwa ni mwanachama wa jumuiya hiyo imewasilisha miradi hiyo ambayo mingi inagusa uendelezaji wa ukanda wa Mtwara.

Miradi hiyo inalenga kuboresha huduma za usafiri katika bandari za Mtwara, Kasanga na Mbamba Bay na ujenzi wa barabara ya Mtwara – Mbamba Bay.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Watumishi. Katika mwaka 2007/08 Wizara imeendelea na jukumu lake la kuwaendeleza na kuwahudumia wafanyakazi wake kijamii na kitaaluma. Katika kipindi hiki Wizara imeweza kuwapandisha vyeo Watumishi 130 wa kada mbali mbali, kuwathibitisha kazini watumishi 31 na kuwaajiri katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni watumishi 25. Aidha, watumishi waliopelekwa katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi walikuwa 77 ambapo kati yao watumishi 17 wanaendelea kupata mafunzo ya muda mrefu hapa nchini na watumishi 60 walipata mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

Katika mwaka 2008/09, Wizara itaendelea na utaratibu wa kupima utendaji wa kazi kwa njia ya uwazi. Aidha, itaendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi 30 na kuwapatia mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi watumishi 80. Lengo ni kuwaongezea ujuzi na ufanisi katika kazi zao. Aidha, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 176 wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mtambuka, Habari, Elimu na Mawasiliano. Ili kuweza kuelimisha Umma na jamii kwa ujumla kuhusu shughuli za Sekta zetu Wizara imeendelea kukitumia kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano. Kitengo hiki ni kiungo muhimu kati ya Wizara, Vyombo vya Habari na jamii. Wizara imeweza kuwa na mawasiliano na jamii kwa njia za mikutano, taarifa kwenye magazeti, Luninga (TV), radio, na pia kupitia tovuti ya Wizara. Hivi sasa tovuti ya Wizara inaendelea kuboreshwa kwa kuzingatia mabadiliko yanayoendelea kufanyika katika muundo wa Wizara.

Kitengo kimeendelea kuboresha kumbukumbu za miradi inayosimamiwa na Wizara ikiwa ni pamoja na Barabara, Viwanja vya Ndege, Reli, Bandari, na Vivuko. Kumbukumbu hizo pia zitajumuisha ramani zitakazoonyesha barabara zinazosimamiwa na Wizara ya Miundombinu, reli, bandari na vivuko. Aidha, Kitengo kimeanza utaratibu wa kuandaa vipindi maalum vitakavyoonyesha na kuelezea matukio mbalimbali ya sekta kwa ajili ya matumizi ya vipindi vya Televisheni na radio.

Katika mwaka 2008/09 Kitengo kinatarajia kuanzisha utaratibu wa kudumu wa kuendesa kampeni za upashaji habari kupitia vyombo vya habari na majukwaa mengine. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mfumo wa TOVUTI pamoja na taarifa zinazohusu shughuli zinazotekelawa ili ziweze kuendana na mabadiliko yanayoendelea kufanyika katika sekta nzima ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rushwa, Jinsia na UKIMWI. Kwa kutambua athari na matokeo mabaya ya rushwa, Wizara iliendelea kusisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa uwazi na uaminifu ili kuziba mianya ya rushwa. Katika kufanya hivyo watumishi wa Sekta wanaohusika na masuala ya manunuzi mbalimbali wametakiwa kutekeleza majukumu yao kwa kufuata taratibu zilizowekwa. Aidha Wizara imekuwa ikifuatilia mikataba yote ya manunuzi ili kuhakikisha kwamba inafanyika kwa haki na uwazi na bila upendeleo.

Kuhusu jinsia, idara ya Barabara kwa kupitia kitengo cha Ushirikishwaji wa Wanawake kinaendelea kuhamasisha na kuelimisha wanawake na jamii kwa ujumla ili wanawake waweze kushiriki kwa wingi zaidi katika kazi za ujenzi wa barabara. Ushirikishwaji huu unatofautiana kati ya mkoa na mkoa kulingana na mila na desturi, jitihada za wataalamu walioko kwenye mikoa na uelewa wa jamii husika. Hivi sasa ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara umefikia asilimia 30, lengo ni kufikia asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kushirikiana na *TACAIDS* na wadau wengine katika kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanapata kinga za kutosha za ugonjwa hatari wa UKIMWI. Katika kipindi cha 2007/08 Wafanyakazi wameweza kupata mafunzo ya jinsi ya kijikinga na UKIMWI, matumizi ya dawa za kurefusha maisha na kuishi kwa matumaini na vifaa vya kinga. Aidha, Wizara imeendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya zao na kwa walioathirika na virusi vya UKIMWI wameendelea kupatiwa huduma za dawa kwa magonjwa nyemelezi, dawa za kurefusha maisha (*ARV*) na lishe bora. Katika mwaka 2007/08 Wizara ilitengewa shilingi milioni 65.0 ikiwa ni fedha zinazotolewa na Benki ya Dunia kwa ajili ya Mradi wa Kupambana na janga la UKIMWI. Kazi zilizofanyika katika kipindi hiki ni pamoja na kufanya tathmini ya tabia na mienendo ya watumishi ili kuona wanabadilika kwa kiasi gani ili kupunguza maambukizo ya UKIMWI. Katika mwaka 2008/09, Wizara itaandaa mwongozo wa Sera ya UKIMWI (*HIV/AIDS Policy Guidelines*) sehemu ya kazi ambayo itatumika kama mwongozo wa kuendesha shughuli za UKIMWI pamoja na kutoa huduma kwa waathirika wa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za mafunzo, Wizara ya Miundombinu inasimamia vyuo vinavyotoa mafunzo yanayohusika na sekta. Vyuo hivyo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT). Serikali imeendelea kuboresha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ili kiwe kituo bora kinachokidhi mahitaji ya Sekta ya Uchukuzi. Katika mwaka 2007/08, Chuo kimesajili wanafunzi 442 ambaa ni pungufu kwa asilimia 2 ikilinganishwa na mwaka 2006/07 ambapo wanafunzi 450 walisajiliwa. Chuo kimeendesha kozi fupi na ndefu katika ngazi ya Stashahada ya juu na Stashahada ya kawaida kwenye nyanja za Uongozi katika usafirishaji, uondoshaji na usafirishaji mizigo na ufundi wa magari. Aidha, Chuo kinaendelea kufanya kazi za utafiti na uelekezi katika masuala ya usafirishaji. Chuo kimeendelea kuimarisha ushirikiano na Vyuo vingine ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09 Chuo kimepanga kujitangaza zaidi ndani na nje ya nchi ili kuweza kuongeza idadi ya wanafunzi. Aidha, chuo kitaongeza majengo ya madarasa, hosteli na kuendelea na ujenzi wa maktaba. Chuo kimedhamiria kujiendeleza ili kuweza kufikia lengo la kutoa shahada ya Uzamili na baadaye hadi Shahada ya Uadtari wa Falsafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ujenzi – Morogoro. Katika mwaka 2007/08, Chuo kilifundisha mafundi Sanifu 73 wa fani mbalimbali, kiliendesha mafunzo ya mafundi stadi 51 na madereva wapya 201 na madereva wa taasisi za umma 18. Katika

mwaka 2008/09, Chuo kinatarajia kutoa mafunzo kwa mafundi sanifu 120, madereva wa vyombo vya Umma 40, madereva wapya 230 na mafundi stadi 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Bahari – Dar es Salaam (*DMI*). Katika mwaka 2007/08, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya kuendeleza rasilimali watu katika sekta ya usafiri wa majini. Mafunzo hayo yanatolewa kwa kuzingatia Mikataba wa kimataifa inayosimamiwa na Shirika la Kimataifa la Usimamizi wa Usafiri wa Majini (*International Maritime Organisation- IMO*) na kwa kuzingatia viwango vinavyohakikiwa na Shirika la Ukagazi wa Ubora wa Masuala yanayohusu Bahari. Shughuli nyine za Chuo ni pamoja na utoaji wa huduma ya ukarabati wa vifaa vya kuokolea majini (liferafts) na Wakala wa kutafuta ajira kwa mabaharia (*DMI Crew Agency*) ulioanza kazi Mei, 2007. Katika mwaka 2007/08, idadi ya wanafunzi waliojiunga na chuo ni 5,451, kati ya hao wanafunzi wa mafunzo ya muda mrefu 262 na muda mfupi ni 5,189.

Aidha, wanafunzi wa mafunzo ya muda mrefu ni pamoja na fani ya uongozi wa meli 83, wahandisi wa meli 90, uongozi wa usafirishaji 19, mabaharia wa kawaida 70. Chuo kimeweza kutafuta ajira 252 katika meli zilizosajiliwa ndani na nje ya nchi. Jumla ya meli 14 zimeweza kufanyiwa ukarabati wa vifaa vya kuokolea (*life rafts*). Pamoja na shughuli hizo chuo kimeendelea kuwa na ushirikiano na vyuo vingine kutoka ndani na nje ya nchi ili kukuza mitaala yake. Aidha, chuo kiliweza kuanzisha mahusiano ya kimasomo na Chuo Kikuu cha Dalian cha Jamhuri ya Watu wa China, Chuo Kikuu cha Stord-Haugesund cha Norway na Chuo cha *Namibia Maritime and Fisheries Institute (NAMFI)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, Chuo kilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na idadi ndogo ya wanafunzi wa kitanzania kutokana na kutopewa mikopo ya elimu kutoka katika Bodi ya Mikopo na ukosefu wa nafasi za mafunzo kwa vitendo. Mikakati ya Chuo ni kutoa mafunzo ya ubaharia katika ngazi ya Shahada (*NTA Level 7 & 8*) na kununua vifaa vya kufundishia vinavyokidhi matakwa ya Mikataba ya Kimataifa ya masuala ya bahari (*International Maritime Conventions*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/09 chuo kitaanza kutoa huduma ya kuwapatia wenye meli vifaa vya kuainisha sehemu meli ilipozama au ilipopotea. Vifaa hivi vinaitwa '*Emergency Position Indicating Radio Beacons*' (*EPIRBs*). Katika ukanda huu wa Afrika huduma hii inatolewa katika nchi mbili Misri na Afrika Kusini. Hii ni hatua nzuri kwa Chuo kwa kuweza kutoa huduma hii kwenye meli ambazo zinasafiri kwenye Maziwa na Bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Hali ya Hewa- Kigoma. Katika mwaka 2007/08, Mamlaka ya Hali ya Hewa, iliendelea kutoa mafunzo ya daraja la tatu katika Chuo cha Hali ya Hewa, Kigoma na mafunzo ya daraja la pili katika tawi la Chuo hicho

lililopo kwenye Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Jumla ya wanafunzi 46 walimaliza mafunzo na wengine 44 wanaendelea na mafunzo ya daraja la tatu. Wanafunzi 26 wamemaliza masomo ya utabiri wa hali ya hewa daraja la pili na wengine 28 wanaendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Chuo cha Usalama wa Usafiri wa Anga (Civil Aviation Training Center - CATC) - DAR ES SALAAM*. Chuo kimeendelea kutoa mafunzo yahusuyo shughuli za usafiri wa anga na uendeshaji wa viwanja vyta ndege. Mafunzo haya hutolewa kwa wanafunzi wa ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2007/08 jumla ya idadi ya wahitimu kutoka chuo cha CATC walikuwa 276 ambapo ni ongozeko la asilimia 0.36 ikilinganishwa na mwaka 2006/07. Kati ya wahitimu hao 276, idadi ya wahitimu wa kike ni 86, sawa na ongezeko la wanafunzi 28 (au asilimia 48) ya wahitimu wa kike ikilinganishwa na mwaka 2006/07.

Aidha, Chuo kimeweza kuongeza idadi ya kozi zinazotolewa kutoka 41 hadi kufikia 44 na kuwaendeleza kielimu na kitaaluma wakufunzi 8. Chuo kilipokea wanafunzi 33 kutoka nchi za Botswana, Namibia, Uganda, Msumbiji, Zambia, Liberia na Nigeria na hivyo kuingizia nchi fedha za kigeni.

Katika mwaka 2008/09 chuo kimepanga kujitangaza zaidi, ndani na nje ya nchi ili kuongeza idadi ya wanafunzi pamoja na kufunga “*simulator*” ya kisasa kwa mafunzo ya waongoza ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahili ya Nguvu Kazi (*Appropriate Technology Training Institute – ATT*I) – *MBEYA*. Katika mwaka 2007/08, Chuo cha Matumizi ya teknolojia Stahili ya Nguvu Kazi (*ATT*I) kiliendelea kufundisha matumizi ya teknolojia stahili inayotegemea nguvu kazi katika ukarabati na matengenezo ya barabara, hivyo kutoa ajira na kipato kwa wananchi. Aidha, kitengo cha “*Labour Based technology Unit*” kiliendelea kuratibu matumizi ya teknolojia stahili, kutoa maelekezo, ushauri na miongozo mbalimbali kwa wadau wa kazi za barabara kuhusu matumizi bora ya teknolojia stahili ya nguvu kazi na mafunzo. Katika mwaka 2008/09 Chuo kitaendelea na usimamiaji wa utekelezaji wa mpango wa “*Taking Labour Based Technology (LBT) to Scale*”. Pia kitaendelea kutoa elimu kwa njia ya uhamasishaji, kutoa mafunzo kwa watumishi mbalimbali ili waweze kuwa na utaalamu wa kusimamia kazi na kukiendeleza kituo cha utunzaji habari zinazohusu teknolojia ya nguvu kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani, kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu, napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha 2007/08 katika kutimiza malengo yetu. Shukrani zetu pia ziwaendee Washiriki wetu wa maendeleo (*Development Partners*) wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza programu na mipango yetu ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Hali ya Hewa. Wahisani hao wanajumuisha mashirika na taasisi za kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta zetu. Nchi na mashirika hayo ni pamoja na; Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Baharini (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), OPEC Fund, Umoja wa nchi za Ulaya, “Third World Organization for Women in

Science” (TWOWS), UNESCO, Nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uhlanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubelijiji, Ujerumani na wengine wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya sekta zetu. Shukurani za pekee ziwaendee Waheshimiwa wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imechangia katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Naomba waendelee na moyo huo ili tuweze kuendeleza sekta hii ambayo ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani zangu hazitakuwa kamili bila kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekia Chibulunje (Mb.), Katibu Mkuu Eng. Omar Abdallah Chambo na Naibu Katibu Mkuu Bi. Joyce K. G. Mapunjo. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara, Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na Wataalamu wote wa Wizara kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara. Naomba waendelee na juhudhi hizo katika kipindi kijacho ili tuweze kutekeleza malengo tuliojiwekea kwenye sekta zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2008/09, ili Wizara ya Miundombinu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2008/09, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 801,961,340,900 kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa mwaka 2008/09. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni shilingi 208,784,558,000 ambapo shilingi 2,342,662,000 ni mishahara ya watumishi wa Wizara (PE), na shilingi 206,441,896,000 ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC). Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi 593,176,782,900 ambapo kati ya hizo, shilingi 356,156,302,000 ni fedha za ndani na shilingi 237,026,480,900 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: [www.infrastructure.go.tz](http://www.infrastructure.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii nimeambatisha orodha ya Miradi itakayotekelawa katika mwaka 2008/09 pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo (Kiambatanisho Na. 2). Aidha, Kiambatanisho Na. 3 ni mchanganuo wa Miradi ya Barabara za Mikoa itakayotekelawa katika mwaka 2008/09 pamoja na fedha zilizotengwa katika kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Bajeti hii, nafikiri mtakubaliana na mimi nikisema kwamba hotuba yake leo imekuwa ni ya kimsingi kabisa kwa sababu imechambua utekelezaji wa Ilani ya

Uchaguzi kwa hatua moja baada ya nyingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, niseme tu kwamba tunakupongeza sana. Inatakiwa kuwaonesha Watanzania ni namna gani Ilani imeshatekelezwa kwa hatua moja hadi nyingine.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ili naye aje kutoa maoni ya Kamati ya Miundombinu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU (MHE. MOHAMED H. MISSANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa fedha wa 2007/2008, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2008/09

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichukue fursa hii, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kufanya hivyo, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa wa Marehemu waliopata ajali ya Helikopita, iliyotokea hivi karibuni huko Mkoani Arusha. Tunaungana na ndugu wa Marehemu katika kuomboleza msiba huu, kwani nchi imepoteza wapiganaji hodari katika kuleta maendeleo kwa Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke Roho za Marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati yangu ya Miundombinu, naipongeza Wizara ya Miundombinu kwa maandalizi, ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hiyo mbele ya Kamati yangu kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya 2008/2009. Aidha, Wizara iliwasilisha pia Taarifa ya Utekelezaji wa maagizo ya Kamati na Mipango ya Bajeti ya 2007/2008 na kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya muundo wa Wizara ya Miundombinu, shughuli za mawasiliano kama vile Shirika la Posta, Kampuni ya Simu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania, zilihamishiwa kwenye Wizara mpya ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wizara ya Miundombinu inaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kuititia Sera ya Taifa ya Ujenzi iliyopitishwa Mwaka 2003. Kamati ya Miundombinu sasa hivi inashughulikia Wizara mbili za Miundombinu na Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Aidha, katika kujielimisha shughuli za Wizara, Wajumbe walipata fursa ya kujielimisha kuhusu:-

- Majukumu ya Wizara;
- Muundo wa Wizara;

- Dira ya Wizara;
- Malengo ya muda mrefu ya Wizara
- Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara
- Matatizo/changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata pia fursa ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka 2008/2009 kama yalivyowasilishwa na Wizara ya Miundombinu mbele ya Kamati tarehe 5 – 6 Juni, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili bajeti ya wizara ya miundombinu kwa mwaka 2007/2008. Katika kikao cha mwezi Juni 2007, baina ya Kamati na Uongozi wa Wizara, jumla ya maagizo Ishirini (20) yalitolewa kwa utekelezaji. Wizara iliyafanya kazi maagizo hayo na hatimaye kufikia hatua mbalimbali za utekelezaji.

Aidha, yapo maagizo ambayo yametekelezwa kwa ukamilifu na yapo maagizo, ambayo utekelezaji wake, ni wa muda mrefu na bado Wizara inaendelea kuyafanya kazi. Kamati kimsingi imeridhika na hali ya utendaji wa Wizara hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Wizara iliweka malengo ya kukusanya mapato ya shilingi milioni 321,944. Mpaka kufikia Machi 2008, jumla ya shilingi milioni 352.72 zilikuwa zimekusanywa na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia mia moja na tisa (10%). Ongezeko hilo limetokana na uuzaaji wa hati za Zabuni na usajili wa magari ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Wizara ilitengewa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 208.582 ikiwa ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na ruzuku kwa Taasisi na Matumizi Mengineyo.

Aidha mpaka kufikia mwezi Aprili 2008, kiasi kilichopokelewa ni shilingi bilioni 126,661 sawa na asilimia 60.73 ya Bajeti nzima. Hali hii inamaanisha kwamba, kiasi kikubwa cha fedha kilikuwa bado hakijatolewa na Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa malengo yaliyopangwa na kwa kuwa mpaka kufikia kipindi hicho, ni miezi miwili kufika mwisho wa mwaka wa fedha, hali ya kiutendaji wa Wizara na Taasisi zake, zitakuwa zimeathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo 2007/2008, Katika mwaka 2007/2008, Serikali ilitenga shilingi bilioni 478.445 kwa ajili

ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 225,516 ziliwa ni fedha za ndani na shilingi bilioni 252.929 ziliwa ni fedha za nje. Mpaka kufikia Aprili 2008 jumla ya shilingi bilioni 166.476 za ndani ziliwa zimetolewa ikiwa ni sawa na asilimia 73 ya fedha zote za ndani zilizotengwa kwa mwaka 2007/2008. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na kukamilisha ujenzi/ukarabati wa barabara kuu kwa kiwango cha lami kwa jumla ya kilometa 377. Kilometra 741 za barabara za Mikoa ziliwa zimekamilika kujengwa na ukarabati kwa kiwango cha changarawe na kilometra 26.1 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango wa mwaka 2007/2008. Kwa ujumla, Wizara imepata mafanikio katika utekelezaji wa mipango ya mwaka 2007/08, kama ilivyofafanuliwa katika taarifa ya utekelezaji wa mradi kwa mradi. Aidha, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:-

(i) Kuandaa na kukamilisha Rasimu ya Sera ya Taifa ya Huduma ya Hali ya Hewa; Rasimu ya Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani, Rasimu ya Sera ya Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi na Serikali katika ujenzi wa Miundombinu (*PPPs*) na Rasimu ya Sera ya Majengo;

(ii) Kukamilika kwa mchakato wa ukodishwaji wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), ambapo Kampuni ya India inayoitwa *RITES* ilikabidhiwa jukumu la kuendesha Shirika hili kwa ubia na Serikali;

(iii) Kukamilika kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami na baadhi yake zimefunguliwa rasmi kama vile Mbemkuru - Mingoyo (km 95); Singida - Shelui (km 110); Singida – Isuna (km 63); Kyamiorwa – Buzirayombo (km 120); Buzirayombo - Geita (km 100) na Tarakea – Rongai - Kamwanga (km 32);

(iv) Kukamilika kwa maandalizi ya Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Miundombinu ya Uchukuzi (*TSIP*) ya miaka kumi ya uwekezaji katika Miundombinu ya Uchukuzi, kuwa na miundombinu endelevu, yenye ufanisi wa hali ya juu na ya gharama nafuu ifikapo Mwaka 2016. Programu hii inatekelezwa kwa awamu mbili za kipindi cha miaka mitano mitano na awamu ya kwanza ilianza mwaka 2007/08; na

(v) Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imekamilisha mchakato wa kuifanya Bohari Kuu kuwa Wakala wa Serikali. Wakala huu utajulikana kwa jina la *Government Procurement Services Agency (GPSA)* na itachukuwa majukumu yote yaliyokuwa yanashughulikiwa na Bohari Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2007/2008 ni pamoja na:-

(i) Serikali kutokuwa na uwezo wa kifedha ikilinganishwa na mahitaji halisi ya miradi ya maendeleo;

(ii) Uhaba pamoja na uduni wa mitambo ya kuwezesha Wakandarasi Wazalendo kumudu utekelezaji wa kazi za barabara;

(iii) Uwezo mdogo wa Wahandisi wa Halmashauri zetu kushindwa kushughulikia miradi ya ujenzi na ushirikishwaji duni wa Wahandisi katika ujenzi na matengenezo ya miundombinu;

(iv) Mlundikano mkubwa wa madeni ya miradi ya barabara ambayo ulipaji wake uliathiri kwa kiasi kikubwa miradi ya ujenzi wa barabara kwa mwaka 2007/08;

(v) Ujenzi usio halali katika maeneo ya hifadhi ya barabara (*Road Reserve*);

(vi) Uwezo mdogo wa baadhi ya Wakandarasi katika kutekeleza kazi za barabara hivyo kuchelewesha ukamilishwaji wa miradi;

(vii) Baadhi ya Wahisani kuwa na urasimu mrefu wa kutoa fedha wanazotoa kufuatana na ratiba iliyowekwa hivyo kuchelewesha miradi kuanza malipo kwa Makandarasi kwa muda uliokubaliwa katika Mikataba;

(viii) Utaratibu mrefu wa kutoa Zabuni (hasa kwa miradi ya Wahisani) umekuwa ukichelewesha kuanza kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi; na

(ix) Ubovu wa miundombinu ya uchukuzi hususani Barabara, Reli, na Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka wa fedha 2008/2009. Malengo na mpango wa Maendeleo wa Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2008/2009, ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Aidha, Mpango huu umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (*Vision 2025*), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (*MKUKUTA*), Mkakati wa Kushirikiana na Wahisani (*Tanzania Joint Assistance Strategy*), pamoja na mikakati mbalimbali ya Kitaifa na Kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2008/2009 na kwa kuzingatia Mwongozo wa Matayarisho ya Bajeti, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mwongozo huo kwa upande wa Wizara ya Miundombinu ni pamoja na:- (i) Ujenzi na ukarabati wa barabara Kuu, barabara za Mikoa na Barabara zingine muhimu;

(ii) Ujenzi wa Barabara ya Sumbawanga–Mpanda –Kanyani-Nyakanazi;

(iii) Ujenzi wa Barabara ya Sumbawanga – Kasesya/Matai-

(iv) Barabara ya Kigoma-Kidahwe-Uvinza-Liunde;

(v) Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora;

(vi) Barabara ya Mangaka – Tunduru;

- (vii) Barabara ya Singida - Babati – Minjingu; na
- (viii) Ujenzi wa Daraja la Kilombero na Malagarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imejulishwa kuwa baadhi ya maeneo hayo mbali na umuhimu wake katika kuendeleza uchukuzi na kukuza uchumi wa nchi kwa haraka zaidi, hayakuweza kutengewa fedha kutohana na ufinyu wa Bajeti. Kati ya miradi hiyo, miradi iliyotengewa fedha katika Mwaka 2008/09 ni pamoja na:-

- (i) Ujenzi/Ukarabati wa barabara Kuu, barabara za Mikoa na Barabara zingine muhimu kwa miradi inayoendelea;
- (ii) Ujenzi wa Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Nyakanazi;
- (iii) Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Ilunde;
- (iv) Barabara ya Mangaka – Tunduru;
- (v) Barabara ya Singida - Babati – Minjingu; na
- (vi) Ujenzi wa Daraja la Kilombero na Malagarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara kupitia Idara mbalimbali na Vitengo vyake, inatarajia kukusanya jumla ya shilingi Bilioni 100.18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya Matumizi ya Kawaida katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 208,785 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa ajili ya kulipia Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake shilingi bil.18.07 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 190.714. Aidha, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 152.932 ni kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Kwa mantiki hiyo, fedha zilizobaki kwa ajili ya matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 37.78 kiasi ambacho ni kidogo kikilinganishwa na shilingi bilioni 42.60 zilizotolewa mwaka 2007/2008 wakati gharama za ujenzi na uendeshaji zimepanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2008/2009; katika mwaka 2008/2009, Wizara imetengewa shilingi bilioni 592.182 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 355.156 fedha za ndani na shilingi bilioni 237.026 ni fedha za kigeni. Kati ya fedha za ndani shilingi bilioni 163.556 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi inayoendelea, shilingi bilioni 190 ni kwa ajili ya kulipia madeni ya Wakandarasi mbalimbali na shilingi bilioni 1.6 ni kwa ajili ya kulipia fidia kwa wakazi wa Msalato-Dodoma ili kupisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati, baada ya kupitia na kujadili Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka 2007/2008 na kujadili Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka 2008/2009, Kamati imeendelea kuusisitizia uongozi wa Wizara kutekeleza mipango ya kazi zake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi kama Dira ya Maendeleo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishukuru Serikali, kwa kuthamini maoni na ushauri uliotolewa wakati wa vikao vilivyofanyika tarehe 5 - 6 Juni, 2008, wakati wa kupitia na kujadili mwelekeo wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujadili kwa kina mwelekeo wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2008/2009, Kamati imebaini kuwa, Wizara ya Miundombinu inakabiliwa na ufinyu wa Bajeti, isiyokidhi utekelezaji wa mipango ya miradi ya maendeleo kama inavyostahili. Aidha, Kamati imetafakari hali hii na kubaini kuwa bado jitihada zinahitajika katika kupata vyanzo vya ziada vya mapato ya ndani hususan katika kutunisha Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati bado inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kupata fedha za ndani na nje ili kuiwezesha Wizara hii iweze kutekeleza mipango ya miradi ya maendeleo kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ili ifikapo mwaka 2010 miradi hiyo iwe imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa madeni ya Wakandarasi yanafikia shilingi bilioni 190, Kamati inasisitiza kuwa, madeni hayo yalipwe mara moja ili kuwawezesha Wakandarasi kuendelea na ujenzi wa barabara badala ya hali ya kusikitisha ya Wakandarasi kusimamisha kazi kama walivyofanya KONOIKE na hivyo barabara hizo kutomalizika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa, Serikali itafute kila njia ili kuweza kulipia maombi yaliyokosa fedha lakini yakiwa na umuhimu sana kwa Taasisi husika. Kwa mfano Shirika la Ndege la Tanzania liliomba shilingi bilioni 4 na shilingi bilioni 5 kwa Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA), kwa ajili ya matengenezo ya ndege za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza na kuishauri Serikali ifanye jitihada kuendeleza miundombinu iliyopo katika Mikoa ya pembezoni, kwa mfano Mikoa ya Kusini na Magharibi, kwani kwa kufanya hivyo, kutawezesha matumizi ya rasilimali zilizoko katika Mikoa hiyo kama vile Makaa ya Mawe ya Mchuchuma, Gesi ya Songosongo na Mnazi-Bay, ili kuinua uchumi wa nchi. Lakini pia itatuwezesha kutumia fursa ya kijiografia tulio nayo kuhamasisha biashara na nchi jirani hasa za Burundi, Rwanda na DRC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya ujenzi wa barabara na majengo, kwa kuwa miradi mingi ya maendeleo hususan katika sekta ya ujenzi wa barabara imeshindwa kutekelezwa, hali iliyosababishwa na kutopatikana kwa fedha zinazoahidiwa na Wahisani na ambazo upatikanaji wake unaambatana na masharti magumu, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango mkakati utakaowezesha kupatikana kwa fedha za ndani. Fedha

zitakazotumika kupanga Bajeti itakayokidhi kutekeleza mipango ya miradi ya maendeleo kwa vigezo vya kuweka vipaumbele (*priorities*) na pale wahisani watakapochangia Bajeti ya Maendeleo, basi *Min-Budget* iletwe Bungeni kwa ajili ya kuidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara zinazohitajika kujengwa ni nyingi na kwa kuwa Serikali haina fedha za kutosha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha mapema mpango wa BOT (*Build - Operate and Transfer*), *BOOT* (*Build – Own - Operate and Transfer*) na ule wa *PPP* (*Public Private Partnership*), kwa uwazi na kuharakisha kutunga Sera husika. Hii itahamasisha Wawekezaji kujitokeza kushiriki katika ujenzi wa miundombinu.

Aidha, kwa kuwa uwezo wa kujenga barabara kwa fedha zetu ni mdogo na kwa kuwa sasa Serikali ya Awamu ya Nne, imefanya kazi nzuri kiasi kwamba nchi sasa inakopesheka, Serikali isiogope kukopa kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa barabara, kwani badhi ya madeni tunayolipa sasa ni ya miaka 1950 iliyokopwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ya kutenga shilingi bilioni 10 kwa ajili ya barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora na kwamba, fedha hizo zitumike kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami; kwa kuwa usanifu na upembuzi ulikwishafanyika. Iwapo Wafadhili watatoa fedha nyingine, ziingizwe katika barabara hiyo kutokana na umuhimu wake na kwamba mwakani itengewe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imejulishwa kuwa , kwa mwaka huu wa fedha miradi ifuatayo inayofadhiliwa na Mfuko wa *MCC*, kupitia Hazina itaanza kutekelezwa, kwa kuzijenga kwa kiwango cha lami:-

- (i) Barabara ya Tunduma – Sumbawanga;
- (ii) Barabara ya Namtumbo – Songea; na
- (iii) Barabara ya Tanga – Horohoro.

Hivyo basi, tunaitaka Serikali ifanye kila jitihada ili barabarahizi zipate Makandarasi wazuri na wengi, ili kuharakisha ujenzi wa barabara hizo kwa kuwa fedha zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati bado inaendelea kuisisitizia Serikali itoe kipaumbele katika ujenzi wa barabara kwa Mikoa, ambayo haina barabara zinazopitika badala ya kuendeleza barabara ambazo tayari ni nzuri na zinapitika.

Aidha, Serikali ifanye kila jitihada kuweza kukamilisha miradi yake ya maendeleo kama *Mtwara Development Corridor* na kufungua barabara za Mikoa kama vile barabara

ya Babati – Kondoa – Dodoma – Iringa; pamoja na zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani. Hii itawezesha bandari zetu kupata mizigo ya kutosha na kutoa huduma nyinginezo kwa mizigo na abiria ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuboresha mishahara na marupurupu ya watumishi wa *TANROADS* ili kuwapa motisha ya kufanya kazi kwa ufanisi. Kamati imebaini mafao wanayopata watumishi hawa ni madogo ikilinganishwa na taasisi nyingine za umma.

Aidha, Kamati inaitaka Serikali, kuwawezesha watumishi wa *TANROADS* kwa kuwapa nyenzo na vitendea kazi vya uhakika kama vile magari kwa vile Ofisi za *TANROADS* hazipo Wilayani na hivyo kuhitaji usafiri wa kutokea Mikoani ili kuwafikisha katika miradi, kukagua na kuwasimamia Wakandarasi wanaojenga barabara, madaraja na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuwapongeza Watumishi wa *TANROADS*, kwa jitihada nzuri za kazi, licha ya tatizo la kucheleweshewa fedha za barabara kwa vipindi virefu sana. Serikali iharakishe kutoa fedha za barabara mara tu bajeti ikimalizika na kabla ya msimu wa mvua kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali za kuongeza Mfuko wa Barabara, ambapo Halmashauri za Wilaya zimeongezewa fedha pia; bado yapo malalamiko mengi kuhusu namna barabara za Wilaya na vijijini zinavyojengwa, kwani *value for money* haionekani.

Aidha barabara nyingine za Wilayani na vijijini, ni mbovu na ndefu kiasi kwamba Halmashauri hazina uwezo wa kifedha wa kuzijenga au kuzikarabati. Ipo haja ya kulitazama tatizo hili ikiwezekana kuwa na fungu maalum kwenye ofisi ya Waziri Mkuu (*TAMISEMI*), ili kusaidia ujenzi wa barabara hizo pale wanapoombwa na Halmashauri za wilaya zenye matatizo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia wingi wa malalamiko wa Wabunge kuhusu ujenzi wa barabara katika Halmashauri zetu, pamoja na ukweli kuwa uwezo wa kifedha, ni mdogo na utaalami pia ni tatizo; Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuangalia upya Sera ya ujenzi wa barabara ili kuiwezesha *TANROADS* kushughulikia miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara zote nchini (za Kitaifa, Mikoa na Wilayani), kwa kuwa uwezo wanao na wataalam wa kutosha wapo. Hii itaokoa fedha nyingi, ambazo hupelekwa katika Halmashauri, ambako hakuna ufanisi kutokana na kutokuwa na wataalamu wanaokidhi sifa na viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zoezi la bomoa bomoa nyumba za wananchi ili kupisha upanuzi wa barabara, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza zoezi hili kwa umakini ili kuepusha manung’unico ya wananchi hasa pale wanapocheleweshwa kulipwa haki zao za fidia punde zoezi hilo linapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa matukio ya kuporomoka kwa majengo yaliyojengwa bila kufuata taratibu za ujenzi zinazozingatia mipango-miji au kuzingatia viwango vinavyotakiwa (mfano jengo la ghorofa kumi lililodondoka mjini Dar

es Salaam katika mtaa wa Kisutu); Kamati inaishauri Serikali kuwashirikisha wadau wote kama vile Baraza la Ujenzi la Taifa (*NCC*), Bodi ya Usajili wa Makandarasi (*CRB*), Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*), Bodi ya Usajili ya Wasanifu na Wakadiria Majenzi (*AQSRB*) pamoja na Wataalamu wa Mipango-Miji kuhakikisha kuwa vibali vya ujenzi vinatolewa kwa Wakandarasi wenyе sifa na waliosajiliwa tu na kwamba sheria, kanuni na viwango vya ujenzi vinazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara ya Miundombinu kuongeza juhudи katika kuzisimamia Bodi zake zinazohusika na sekta ya ujenzi, ambazo ni Baraza la Ujenzi la Taifa (*NCC*), Bodi ya Usajili Wahandisi (*ERB*), Bodi ya Usajili Wakandarasi (*CRB*), Bodi ya Usajili ya Wakadiria Majenzi (*AQSRB*) pamoja na Wataalamu wengine wa Mipango-Miji, kujenga uhusiano mzuri wa kikazi baina yao ili kazi za sekta ya ujenzi ziwe za viwango na ubora unaokusudiwa. Kwa wanaokiuka taratibu na sheria za ujenzi wachukuliwe hatua kali kukomesha tabia ya ujenzi holela unaosababisha maafa kwa watu na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo na sheria rasmi ya majengo (*Bulding Act*), kunachangia kuwepo kwa matukio ya ujenzi usiokuwa na viwango. Hivyo Kamati inaitaka Serikali kuharakisha kutunga sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawapa pole wale wote waliopatwa na mkasa wa kuangukiwa na jengo la ghoroga kumi na kupoteza maisha na mali zao. Serikali itoe adhabu kali kwa wale watakaobainika kuhusika na uzembe huo, ili iwe fundisho kwa wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwawezesha Wahandisi Wazalendo kupewa kazi kwa upendeleo maalum hasa kwa miradi inayogharamiwa na Serikali, ili waweze kupata vifaa, mtaji na ushindani wa kibiashara katika sekta ya uhndisi na ujenzi. Mpango huu utatoa fursa na kuwajengea uwezo wataalamu hawa Wazalendo katika ushindani, ambao kwa hivi sasa haupo. Uwepo utaratibu maalum wa kuwakopesha fedha na vifaa Wahandisi, Wakandarasi na wataalam wengine wa sekta ya ujenzi ili kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vile vile inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni na kutoa kipaumbele kama ilivyoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua alizochukua kuhusu ujenzi wa Daraja la Kigamboni na hivyo kuleta matumaini kuwa litajengwa kama Ilani ya uchaguzi ya CCM inavyoolekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya usafiri wa majini, Kamati inaitaka *SUMATRA* kuwajibika zaidi katika kukabiliana na matukio ya ajali za barabarani na majini kwa bado ajali zinaendelea kukithiri. Ajali ambazo zinasababishwa na

uzembe wa wamiliki wa vyombo nya usafiri kwa kuweka ujazo mkubwa wa mizigo na abiria. Hii pia huchangiwa na ubovu wa vyombo vyenyewe nya usafiri. Kamati inaishauri *SUMATRA* kuweka mikakati endelevu ya kuvisimamia na kuvifanya ukaguzi wa mara kwa mara vyombo hivyo. Aidha kwa vile vitakavyobainika kusababisha ajali kwa uzembe, adhabu kali zitolewe kwa wahusika ikiwa ni pamoja na kufungiwa leseni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzindua kivuko kipywa ajili ya eneo la Busisi. Kwa vivuko na magati mengine ambayo bado yanahitaji ukarabati, Kamati inaishauri Serikali itenge fedha za kutosha ili miradi hiyo ikamilike na kuwaondolea wananchi kero kama vile Kivuko cha Mv. Sengerema, Ukala, Ukerewe, Kinesi, Pangani na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kukarabati na kuziboresha Bandari za Lindi, Mtwara, Tanga, Kasanga, Kigoma, Mwanza na Itungi.

Aidha kwa msisitizo wa kipekee Kamati inaishauri Serikali kuanza ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, ambayo tayari upembuzi yakinifu umekwishafanyika ili kuondoa msongamano wa meli katika bandari ya Dar es Salaam.

Kadhalika Kamati inashauri Serikali kuwa mazungumzo yaliyopo kati ya *TRA* na *TPA* juu ya matumizi ya Bandari ya Mtwara yakamilishwe mapema ili Bandari hiyo iweze kutumika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuhusu ushauri wake wa mwaka jana ilipokuwa ikiwasilisha taarifa yake ya mwaka 2007, kuwa imefika wakati sasa kuangalia upya uwezekano wa ujenzi wa reli kutoka Tanga hadi Musoma, ili kuiwezesha Bandari ya Tanga kupata mizigo na kuijendesha. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kupunguza pia msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam na kuvutia wafanyabiashara wanaotumia bandari ya Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mazingira ya bandari zetu hayavutii na nyingi kukosa vitendea kazi, kwa mfano Bandari ya Mtwara na Tanga, ambazo zinaendeshwa kwa kusaidiwa na Bandari ya Dar es Salaam; Kamati inashauri kuwa Serikali iwekeze kwanza katika bandari hizi kabla ya kukodishwa ili kuvutia Wawekezaji.

Aidha ufanyike utafiti wa kutosha kuhusu gharama za ukarabati na uendelezaji wa Bandari zote za Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la ubinafsishaji /uwekezaji, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja kuhusu marekebisho ya baadhi ya vipengele nya Mkataba wa *TICTS* vyenye upungufu, ikiwa ni pamoja na kusitisha nyongeza ya miaka 15 zaidi, iliyoongezwa bila kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004.

Hata hivyo, Kamati ya Miundombinu inaitaka Serikali kuwa makini na kufuata sheria na taratibu ilizojiwekea ili zoezi la ubinafsishaji/uwekezaji lifanyike kwa uwazi na haki kwa lengo la kuleta ufanisi na maendeleo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika suala zima la kuingia mikataba au ubia na Makampuni, Wawekezaji na Wakodishaji wa kutoka nje ya nchi.

Aidha, hatua kali ziwe zikichukuliwa kwa Watendaji wanaaoingiza nchi yetu katika mikataba mibovu inayolitia hasara Taifa pamoja na kulikosesha mapato ya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa zoezi la ubinafsishaji lisichukue muda mrefu kwani dhana hii huwaathiri wafanyakazi na kupunguza morali ya kazi kwa kujua ubinafsishaji unatarajiwa.

Aidha, pale inapowezekana, Serikali ijiwekee utaratibu wa kuwekeza kwanza katika Mashirika inayotarajia kuyaiza au kuyabinafsisha ili yanapouzwa yawe katika hali ya kushindaniwa na kuuzwa kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya usafiri wa anga, Kamati inaipongeza Serikali kwa kurejesha ATCL chini ya umiliki wa Umma. Lakini imepatwa na wasiwasi juu ya hali ya kifedha za kuendesha Shirika hili. Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua ya kusafisha mizania ya Hesabu za ATC, kwa nia ya kuvutia wabia watakaowekeza mtaji wa kutosha, utakaotosheleza kununua ndege mpya na kuajiri Watumishi wenye uzoefu na wenye sifa zinazostahili. Kutotekeleza hayo, kunaweza kuifanya nia nzuri ya kurejesha ATC kutokuwa na maana yoyote kwa wananchi, ambao wanahitaji sana huduma hii ya usafiri wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri pia Serikali kuliangalia upya suala la kuwasomesha na kuwaendeleza wataalamu wa nchini hasa Marubani, Wahandisi wa ndege, Wahudumu wa kwenye ndege pamoja na wengineo ili kuboresha huduma za usafiri wa anga na kuingia katika soko la ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha Hanga za kutengenezea ndege zilizomo nchini ili ziweze kufanyiwa matengenezo hapa hapa nchini, kwa lengo la kupunguza gharama na kujenga uwezo wa ndani kwa kuwatumia wataalam wa hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kazi za ukarabati wa viwanja vya ndege na nyingine kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vipyta. Aidha ujenzi wa viwanja vipyta uanzo mwaka huu wa fedha 2008/2009. Viwanja vingine Tisa (9) ambavyo Benki ya Dunia imekwishatoa fedha kwa ajili ya usanifu na upembuzi yakinifu ni pamoja na viwanja vya Kigoma, Tabora,

Sumbawanga, Mafia, Arusha, Shinyanga na Bukoba. Kwa upande wa ujenzi wa viwanja vipyta ni pamoja na Msalato, Dodoma na Mwanza ambacho kinafadhiliwa na BADEA na OPEC. Ujenzi wa Uwanja wa Songwe uendelee kusimamiwa kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudhi za Serikali katika kuendeleza miundombinu nchini hasa barabara, Kamati inashauri kuwa ni vema mkazo huo huo ukawekwa kwenye miundombinu mingine ya reli na viwanja vya ndege ili kukuza uchumi wa nchi kwani miundombinu ya barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege inatumika kwa kutegemeana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kukua kwa kasi kwa usafiri wa anga kati ya Tanzania na nchi nyingine, Kamati inashauri Wizara iandae mipango ya muda mfupi, kati na mrefu kuhusu uendelezaji na uboreshaji wa miundombinu katika viwanja vya ndege, ambayo itakidhi matakwa ya soko la Kimataifa katika usafiri wa anga.

Aidha, Serikali iharakishe mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege mpya wa Kimataifa Bagamoyo au Mkuranga ili kuupunguzia mzigoto uwanja wa Kimataifa wa Mwl. Julius Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati yangu kuwa, Serikali wakati ikiendelea na mchakato wa ujenzi wa Uwanja mpya wa kimataifa (Mkuranga au Bagamoyo); uwanja wa sasa wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (*Terminal II*) uboreshwe miundombinu yake na ubaki kutumika kwa ajili ya usafiri wa ndege za kimataifa (*International flights*), na ule uwanja wa ndege wa zamani (*Terminal I*) ujengewe uwezo na kuboreshwa miundombinu yake ili utumike kwa ajili ya usafiri wa ndege za humu humu nchini (*Domestic Flights*). Mpango huu utapunguza kero kwa wasafiri na kupunguza msongamano, ambao unajitokeza sasa katika uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ukiritimba wa Kampuni inayotoa huduma katika viwanja vya ndege ya *Swissport*, unakaribia kumalizika mwishoni mwa mwaka huu; na kwa kuwa Serikali itakaribisha wawekezaji wengine katika huduma hiyo, Kamati inaitaka Serikali kuandaa na kuweka mazingira mazuri ya miundombinu ya viwanja vya ndege hasa maeneo ya wasafiri na sehemu za kutolea mizigo ili kuruhusu Makampuni yanayotoa huduma katika viwanja vya ndege kufanya kazi kwa ushindaji na kuboresha huduma hizo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisistiza kuwa Serikali ikamilishae zoezi la ulipaji wa fidia kwa wakazi wa maeneo yanayozunguka uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, ambayo ni Kipawa, Kipunguni na Kigilagila na kuondokana na kero hii ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya kuendeleza miradi ya viwanja vya ndege hazitoshi kulingana na mahitaji; Kamati inashauri Serikali kuwa makusanyo ya ada ya huduma za viwanja vya ndege inayokwenda hazina (*Passenger's service charges*), ambayo hukusanywa kupitia *TRA*, iwe ikirudi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*) kwa asilimia 100% na

kutumika kwa ajili ya huduma za viwanja vya ndege. Utaratibu huu umekuwa ukitumika pia kwa sekta nyingine kama ilivyo Maliasili, ambapo makusanyo ya Ngorongoro huenda moja kwa moja kwao badala ya kupitia kwenye mfuko mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wakala wa Ndege za Serikali (*TGFA*), Kamati inaendelea kusisitizia ushauri wake wa awali kuwa, Watumishi hasa Marubani na Wahandisi waboreshewe maslahi yao.

Aidha, fedha walizoomba *TGFA* kwa ajili ya uendeshaji pamoja na matengenezo kiasi cha sh. bilioni 5 wapewe ili kulinda usalama wa viongozi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama wa anga, Kamati inashauri Wizara kuititia Mamlaka yake ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania (*TCAA*) kuhakikisha kuwa, Wataalamu wake wanachukua hatua za makusudi za kuhakikisha ndege zinazonunuliwa na Mashirika ya Serikali na yale ya binafsi kuwa ni za usalama. Aidha, *TCAA* wafanye ukaguzi wa mara kwa mara na kutoa taarifa yake kwa umma ili kuwaondolea mashaka watumiaji wa usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa reli, ubinafsishaji wa Shirika la Reli Tanzania, ulikamilika mwaka 2007, *TRL* inamilikiwa na Kampuni ya India yenye 51% ya hisa zote na Serikali ya Tanzania inayomiliki 49% ya hisa zote. Kamati imesikitishwa kwa kubaini kuwa, uongozi wa juu unashikiliwa na wawekezaji pekee yao amba ni Waasia. Kamati inashauri Serikaki kuangalia upya mgawanyo wa uongozi ndani ya *TRL* ili Watanzania wazalendo waweze kushirikishwa katika uongozi wa juu wa Shirika hili. Suala hili ni la muhimu kwa usalama na mafanikio ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya usafiri wa reli nchini yamekuwa sugu na kutokana na malalamiko mengi ya Watumishi wa Shirika la Reli Tanzania kutokana na ufanisi mbaya wa reli nchini, Kamati inashauri kuwa suluhisho pekee ni kukaa pamoja kwa pande husika ili kujadili njia nzuri ya kuboresha huduma hii kwa wakazi wote wa reli ya Kati, ambao hawana njia mbadala ya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, Kamati haijaridhishwa na mipango inayofanywa ya kufufua usafiri wa reli ya Dar es salaam – Tanga - Arusha na kuimarisha ile ya Tabora – Mpanda na Manyoni - Singida. Hazionekani dalili dhahiri kuwa miapanngo hiyo itakamilika hivi karibuni. Serikali itoe kipaumbele hasa kwa reli ya Tabora – Mpanda, kwani wananchi wa eneo hilo hawana usafiri wa kuaminika unaoweza kuitika mwaka mzima, barabara zao ni mbovu na wanaathirika kiuchumi kwa kukosa miundombinu ya uhakika. Aidha mwekezaji wa wa *TRL* hana budi kuzingatia mkataba kuhakikisha usafiri wa reli ya Tabora, Mpanda na Manyoni – Singida, unaendelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo kubwa linaloikabili *TRL*, ni ukosefu wa fedha za kuijendesha, Kamati inashauri kuwa *TRL* itumie fursa ya Mkataba wa Makubaliano ya Kuanzisha Wakala wa Uwezesaji Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati (*Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency – TTFA*) ambao Tanzania imeridhia, kuweza kukopa fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli za reli, kupanua

miundombinu na kuboresha huduma za reli nchini. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha majibu ya hoja ya *TRL*, kama ilivyoazimiwa na Bunge katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya *TAZARA*, ni Mamlaka inayomilikiwa na Serikali mbili za Tanzania na Zambia, Shirika hili limekuwa linajientesha kwa kusuasua. Kamati inaishauri Serikali ikae na upande wa pili, yaani Zambia na kuweka mikakati endelevu ya kuiimarisha reli hii ya kihistoria ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi na faida ya nchi hizi mbili. Kamati inaishauri Serikali ione uwezekanao wa kuunganisha reli kutoka Tunduma hadi Kasanga ili kuboresha matumizi ya reli hii kwa nchi jirani ya DRC.

Aidha, Kamati imebaini kuwa uongozi wa juu wa *TAZARA*, hususan *CEO* umekuwa ni wa upande mmoja wa Zambia kwa muda mrefu sasa. Serikali ifanye rejea ya makubaliano ya umiliki wa *TAZARA* na kufanya mabadiliko ya sheria ili uongozi wa juu uwe wa mzunguko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati kwa muda mrefu imekuwa ikisikiliza kilio cha wafanyakazi wa *TAZARA* kuhusu maslahi yao duni. Wafanyakazi wa *TAZARA* upande wa Tanzania, mbali ya kufanya kazi katika mazingira magumu, lakini mishahara yao ni midogo mno ikilinganishwa na wenzao wa upande wa pili. Serikali iangalie upya mishahara ya wafanyakazi wa *TAZARA* hasa upande wa Tanzania na kuiboresha. Aidha, kwa wanaodai malimbikizo na viinua mgongo baada ya kupunguzwa au kustaafu nao walipwe mafao yao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2008/2009, ili kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka 2008/09, Wizara ya Miundombinu inaomba iidhinishiwe jumla ya shilingi  $800,667,340,900/=$ . Kati ya hizo shilingi  $563,940,860,000/=$  ni za hapa na shilingi  $237,026,480,900$  ni za nje. Fedha za hapa zinajumuisha fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi  $208,784,558,000/=$  na Fedha za Maendeleo shilingi  $355,156,302,000/=$ .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na kuitia kifungu kwa kifungu na kuipitisha na sasa Kamati yangu inaliomba Bunge lako Tukufu kukubali kuitisha maombi ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Nawashukuru pia Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa; Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Ezekiah Ndahani Chibulunje; Naibu Waziri wa Miundombinu, Bwana Omar Abdallah Chambo; Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu na watumishi wote Wizarani kwa kuiwezesha Kamati yangu kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa wa kuitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na

hivyo kufanikisha Taarifa hii, ambayo kwa niaba yao naiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya kipekee niwapongeze na kuwatambua Wajumbe wote wanaouna Kamati ya Miundombinu mimi niliyesimama, ni Mheshimiwa Alhaji Mohamed Hamis Missanga, Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Paschal Costantine Degera, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa. Wengine ni Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Herbet James Mntangi, Mheshimiwa Dkt. Gertrude Ibengwa Mongella, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mheshimiwa Sigsfrid Seleman Ng'itu, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Phillemon Mikol Sarungi na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nachukua fursa hii, pia kumshukuru Kaimu Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashillilah, Makatibu wa Kamati, Bibi Justina Mwaja Shauri na Bwana James John Warburg kwa kuihudumia Kamati kwa umakini mkubwa na kuanda Taarifa hii pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba sasa kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na Kamati yao nzima kwa ujumla kwa kutoa maoni na ushauri kuhusu Wizara husika. (*Makofi*)

Sasa ninaomba niwape taarifa ndogo kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, waliokwishakuomba kuchangia katika hotuba hii, ni Waheshimiwa Wabunge 82, lakini kati yao hao 82 Waheshimiwa Wabunge 25 hawajawahi kuchangia hoja hata moja toka wamekuja hapa Bungeni, nadhani mnanielewa. Kipaumbele watapata kwanza wale ambao hawajawahi kuchangia hata mara moja na kama nafasi yetu itaturuhusu basi tutaendelea na wale ambao wamechangia mara moja tu hapa Bungeni.

Kwa hiyo, ninaomba basi niwaite kabisa wale wasemaji wa mwanzo kama wapo nje waweze kuingia ndani na wajiandae halafu nitampa nafasi Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Lekule Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzukwanko, atafuatiwa na Mheshimiwa Capt. John Komba.

Baada ya kuwataja hao wasemaji wa mwanzo, sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani ili aje atoe maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Kabwe Zitto. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kutoa Maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni, kuhusiana na Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu.

Lakini kabla sijatoa maoni haya, napenda kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma, kuzipongeza Asasi zisizo za Kiserikali za Mkoa wa Kigoma ambazo jana zimechukua ushindi dhidi ya Asasi za Mikoa mingine yote zilizokuwa zinafanya maonyesho hapa Bungeni. (*Makofi*)

Napenda kutoa Pongezi za dhati kwa Mwenyekiti wetu wa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi kwa kuhakikisha kwamba AZAKI yetu inapata ushindi unaostahili. (*Makofi*)

Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka wa fedha 2008/2009, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa kwa takribani miaka miwili iliyopita nilikuwa Waziri Kivuli wa Mipango na Uchumi. Kufuatia mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kujiuzulu kwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Upinzani Bungeni naye ilimbidi kupanga upya timu yake na akaniteua kuwa Waziri Kivuli wa Miundombinu.

Kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kama Msemaji Mkuu wa Wizara ya Miundombinu, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed (Mb) na Naibu wake Dr. Wilibrod Peter Slaa (Mb), kwa kunituea kushika nafasi hii. (*Makofi*)

Vile vile napenda kuwashukuru kwa kunipatia msaиди mahiri na mwenye uzalendo wa dhati kwa nchi yetu, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki (Mb) kama Naibu Waziri Kivuli wa Miundombinu. Hotuba hii imefika hapa kwa msaada mkubwa sana wa Mheshimiwa Bakari Shamis Faki. (*Makofî*)

Nawashukuru pia Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani walio katika Kamati ya Bunge ya Miundombinu ambao ni Mheshimiwa Bi. Khadija Al-Quassmy wa Viti Maalumu na Mheshimiwa Said Amour Arfi wa Mpanda Kati, kwa msaada mkubwa walionipa katika kuandaa hotuba hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sio Mhandisi, ni Mchumi tu, tena Mchumi wa Biashara, hivyo imani walionayo viongozi wangu na Wabunge wenzangu kwangu ni faraja sana hasa ukizingatia kuwa Wizara hii ni Wizara nyeti sana kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu na hasa katika nyakati za sasa ambapo Tanzania inapaswa kuchukua nafasi yake katika Eneo la Maziwa Makuu kama nchi kiongozi kiuchumi (Uchumi wa Jiografia).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikisha Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Watanzania wote wazalendo kuwa nitafanya kazi hii, kwa kushirikiana na Naibu wangu Mheshimiwa Bakari Shamis Faki (Mb), kwa uwezo wangu wote kwa lengo la kusaidia maendeleo ya Taifa letu zuri la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kaskazini, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kazi zangu. Najua kuna changamoto nyingi sana zinazotukabili lakini tumeanza kuona mwanga kwani tayari mkataba wa ujenzi wa barabara yetu ya Mwandiga – Manyovu na ile ya Kigoma – Kidahwe, umesainiwa na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka huu. Tumekuwa Jimbo la kwanza katika Mkoa wa Kigoma kupata barabara ya lami toka nchi yetu ipate uhuru!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ujenzi wa barabara hii, ndugu zetu wa Kasulu Magharibi nao watafaidika na mradi huu kwani barabara hii pia itafika kwao. Kwa niaba ya wananchi wa Kigoma Kaskazini, napenda kuishukuru Serikali kwa kutimiza wajibu wake bila kujali itikadi za kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawataka wananchi wa Kigoma Kaskazini, kuhakikisha kuwa wanajiandaa na mabadiliko ya kiuchumi yatakayotokana na ujenzi wa barabara hii na hivyo kushika ardhi ya kutosha na kuongeza uzalishaji mashambani kwani soko la bidhaa zetu sasa litapanuka. Vilevile wakulima wa Kahawa wa Kata za Kalinzi, Mukigo na Bitale, waongeze uzalishaji na ubora wa kahawa yetu uongezeka zaidi kwani sasa gharama za usafiri wa kahawa itapungua kufuatia ujenzi wa barabara hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya jumla katika Taarifa ya Hali ya Umasikini ya mwaka 2007 (*Poverty and Human Development Report 2007*), imeonekana kuwa itakuwa ni vigumu sana kwa Tanzania kufikia malengo ya MKUKUTA kwani kasi ya ukuaji wa uchumi imekuwa chini ya viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya suala ambalo limeainishwa katika Sura ya Tatu ya Taarifa hiyo ni kuwa kama Taifa tumekuwa na rasilimali chache sana za kuweza kufikia malengo ya ukuaji uchumi lakini zaidi ni kuwa rasilimali chache tulizonazo tunazitawanya kila mahali ili mradi kila mtu apate bila mkakati maalumu. Tunarithishana! (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo, kwa mara ya kwanza, imesema ukweli na kuonya kuwa bila kuweka mkakati mpya wa kutumia rasilimali za nchi kwa malengo mahususi, hatutapiga hatua katika maendeleo ya uchumi (*Given our limited resources there is need for a clear direction for resource mobilization and a concentration of efforts – Tanzania needs a well focused national growth strategy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Hali ya Umasikini, imeshauri kuwa sasa ni lazima tuchague sekta *ongozi* (*growth drivers*) na sekta ambayo taarifa hii imeipendekeza ni sekta ya miundombinu (*Transport services for landlocked neighbours* Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zambia, Malawi and Uganda). Sekta hii ina mahusiano mazuri na chanya (*strong linkages*) na shughuli nyingine za kiuchumi pia inagawa vizuri faida za ukuaji uchumi (*strongly supportive of broad based enabling environment*) na inaweza kutengeneza ajira nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Hali ya Umasikini, inatuonya kuwa iwapo hatutaenda haraka katika suala hili nchi nyingine zenye bahari zaweza kuchukua mkakati huo na kuutekeleza haraka na Tanzania ikapoteza fursa hii na kuendelea na lindi la umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu hapa Bungeni, nilisema pia mkakati huu unaanza kuchukuliwa na Msumbiji na Angola. Tuwe makini na tusome taarifa hizi muhimu sana na kuzifanyia kazi. Ninashauri kwa nguvu kubwa kuwa Taarifa ya Hali ya Umasikini (*Poverty and Human Development Report*) na brief zake ziwe ni nyaraka muhimu kwa kila Mbunge kuanzia sasa (*a must read reports*). (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2008/2009, Kambi ya Upinzani, itajikita katika maeneo machache yenye umuhimu wa kipekee katika Wizara ya Miundombinu. Maeneo hayo ni barabara, viwanja vya ndege na usafiri wa anga, bandari na usafiri wa maji, reli na usafiri wa reli na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji Dar es Salaam. Tutajikita kutoa mapendekezo maalumu katika maeneo hayo ili kuifanya

Serikali iliyopo madarakani iangalie upya mipango yake na kwa kushirikiana tujenge nchi yetu nzuri ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inatambua kuwa sekta ya ujenzi imekua ikichangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Ukiangalia taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2007, utakutana na takwimu ambazo zinaonesha kuwa sekta ya ujenzi na maendeleo ya ardhi imekuwa zaidi ukilinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka 2006. Mwaka 2007, kiwango cha ukuaji wa shughuli za ujenzi kilikuwa asilimia 9.7 ikilinganishwa na asilimia 9.5 mwaka 2006. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa ujenzi wa majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi.

Aidha mchango wa shughuli za ujenzi katika pato la Taifa ulikuwa asilimia 6.5 mwaka 2007 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2006. Ukuaji wa sekta ya ujenzi katika uchumi wa nchi ni ishara njema sana kutokana na sababu nilizoleza hapo juu na hasa suala la ajira kwa wananchi na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuongezeka kwa ukuaji wa sekta ya ujenzi katika uchumi, Serikali imekiri kuwa kuna wasiwasi wa kutoweza kufikia malengo ya Program ya Maendeleo ya Sekta ya Uchukuzi (*TSIP*). Program hii kama mnavyofahamu, ni ya miaka kumi na huu ni mwaka wake wa kwanza wa utekelezaji (2007/2008).

Hata hivyo, miradi yote mipya iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka huo wa kwanza haikutekelezwa na wala haitatekelezwa katika mwaka huu wa fedha ambao umeanza (2008/2009). Habari hii sio njema hata kidogo na ni ya kukatisha tamaa sana kwa mpenda maendeleo ye yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali niliyoeleza hapo juu, ni dhahiri kuwa miradi mingi iliyopo katika Ilani ya uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005 ambayo ilikuwa imepangwa kutekelezwa, haitatekelezeka kwani Taifa halina fedha za kutekeleza. Sasa mtu atajiuliza hivi wakati wa uchaguzi CCM iliandika *wish list* ili kuomba kura tu? Imefikia wakati sasa ni vizuri vyama vya siasa viwe makini vinapoandika Ilani zao kwani hii tabia ya kurundika miradi mingi kwenye Ilani halafu utekelezaji wake unakwama, ni doa katika mchakato wa siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni, inawaomba Wabunge tujikite katika mjadala wetu katika suala zima la fedha za ujenzi wa miundombinu (*financing Infrastructure*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata woga sana, ninaposoma ripoti mbalimbali za Serikali kuhusiana na maendeleo ya miundombinu yetu ya kuwezesha ukuaji wa uchumi. Inabidi sasa tuache kujadili kila mtu na kabarabara kake na badala yake tuwe na mjadala mpana sana kuhusu ni vipi tunapata fedha za ujenzi wa miundombinu ya nchi. Kupiga kelele, tunapiga kila mwaka, ni jukumu sasa la viongozi wote wa kisiasa kukaa na

kuangalia kwa mapana, tunafanya nini kuhusu suala hili la ufinyu wa fedha za miundo mbinu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo ya miundombinu kwa mwaka 2008/2009, zinazoombwu kuidhinishwa hapa ni Tshs.592.182 bilioni na kati ya fedha hizo Tshs.355.156 billioni ni fedha za ndani na Tshs.237.026 billioni, ni fedha za nje. Katika fedha hizi Tshs.164 bilioni, ni kwa ajili ya kutekeleza miradi inayoendelea na Tshs.190 bilioni ni kwa ajili ya kulipia madeni ya Wakandarasi waliokeleza miradi ya barabara. Mahitaji halisi ya miradi inayoendelea bila kuweka miradi mipyä ni Tshs.357 bilioni. Hii maana yake ni kuwa Bunge hili linajadili asilimia 46 tu ya mahitaji halisi ya ujenzi wa miundombinu hapa nchini kwa mwaka 2008/2009. Hakuna miradi mipyä na hata ile ya zamani, tunaweza kuigharimia kwa 46% peke yake. Hatutafika hata kidogo. Ninashauri na kupendekeza kwamba tujielekeze katika mjadala mpana wa fedha za miundombinu vinginevyo Taifa hili litadumaa. Lazima tutafute vyanzo vingine vyä fedha ili kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitatu iliyopita, tumepisha jumla ya shilingi trilioni 1.12 yaani bilioni 1120 katika Bajeti ya Wizara ya Miundombinu, mwaka 2006/2007, tulipitisha bilioni 223, mwaka 2007/2008 tulipitisha bilioni 305 na 2008/2009, tunapitisha sasa bilioni 592. Ukiangalia sehemu kubwa ya hizi fedha zimechukuliwa na mvua kwa sababu barabara nyingi ambazo tumezijenga hazikuwa za kuweza kudumu kipindi kimoja cha msimu wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inatambua kuwa kuna juhudzi za Serikali kutohakana na fedha za Serikali ya Marekani za *MCC*, kutatua tatizo hili kwa kujenga barabara na kiwanja kimoja cha ndege. Bado fedha za *MCC*, hazitamaliza tatizo letu. Ninashauri Serikali ikae na kuleta hapa Bungeni mpango mbadala wa kupata fedha za kujenga miundombinu hapa nchini. Kabla ya Bunge la mwezi wa Novemba, Serikali iwe imemaliza kazi hiyo na kuieleza Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Kamati ya Bunge ya Fedha juu ya mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hatuwezi kukwepa kuweka *Sovereign Bond* ya angalau Tshs. 800 bilioni ili tupate fedha za miradi yote ya sasa na kutengeneza miradi mipyä. Miradi hii mipyä lazima itokane na mjadala wa kina kuzingatia ushauri wa Taarifa ya Hali ya Umasikini (*Poverty and Human Development Report 2007*), kuhusiana na Mkakati Mpyä wa Kukuza Uchumi (*A new Framework for a Tanzanian Growth Strategy*). (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya barabara zetu (*State of Roads*), matengenezo ya kawaida ya barabara kuu ya kilometa 4,677.7, yalikamilishwa mwaka 2007, ikilinganishwa na kilometa 5,080.3 mwaka 2006. Hapa panaonyesha upungufu wa kilometa zipatazo 402.6 ukilinganisha na mwaka 2006. Hoja inayotolewa na Serikali

kwenye upungufu huu wa kupungua kwa ujenzi kwenye sekta ya barabara eti ni kutokana na utekelezaji wa Sheria mpya ya Manunuzi ambapo mchakato wa kutafuta Wakandarasi unachukua muda mrefu. Ninaomba tupate maelezo ya kina zaidi kuhusiana na ucheleweshaji huu wa ujenzi wa barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 barabara za Mikoa zenye urefu wa kilometra 5,062.4 zilifanyiwa matengenezo ikilinganishwa na kilometra 8611 mwaka 2006, kwenye eneo hili pia palitokea upungufu wa ujenzi wa zaidi ya kilomita 3548.6, hii inaonyesha wazi kuwa kwa kipindi cha mwaka 2007, sekta ya miundombinu haikuwekewa mkazo unaostahili kwani kasi ya ukuaji wake ilipungua japokuwa Bunge lako Tukufu lilipitisha fedha nyingi zaidi ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2006. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri wa Miundombinu atoe sababu za kujitosheleza ni kwa nini kasi ya ujenzi wa barabara ilipungua kwa kipindi cha mwaka 2007? Kuna mkakati gani wa kuhakikisha kuwa kasi ya ujenzi wa barabara kwa mwaka huu inakua kwa kasi inayostahili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inataka kupata maelezo ya kina kutoka Serikalini, ni kwa nini sekta ya ujenzi kwa mwaka 2007/2008, imetumia Shillingi bilioni 596.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 777.2 zilizotengwa kwa sekta ya miundombinu ya barabara peke yake sawa na asilimia 76.7, ya fedha zilizotengwa. Mpaka mwaka wa fedha unaisha iliweza kufikia asilimia 100?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali, nimeshauri kuwe na mkakati mpya wa ujenzi wa miundo mbinu ya nchi. Hapa ninapenda kupendekeza kwa upande wa barabara ili kuhakikisha mkakati mpya unaoweza kurejesha gharama za ujenzi baada ya muda mfupi. Mkakati mpya uzingatie kuunganisha Mikoa ifuatayo kama hatua ya haraka kwa barabara za lami.

1. Mkoa wa Mbeya na Mwanza kwa maana ya barabara ya Chunya, Sikonge, Tabora, Nzega mpaka Mwanza;
2. Kuunganisha Mkoa wa Mbeya na Kigoma kwa maana ya barabara ya Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma;
3. Mkoa wa Mtwara na Ruvuma kwa maana ya barabara ya Mtwara – Tunduru – Songea – Mbamba Bay;
4. Mkoa wa Arusha na Iringa kwa Maana ya barabara ya Arusha – Babati – Kondoa – Dodoma – Iringa; na
5. Mkoa wa Kigoma na Dar es Salaam kwa maana ya barabara ya Kigoma, kwa maana Dodoma – Manyoni – Itigi – Tabora – Urambo – Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizo nilizozitaja, ni za kimkakati kiuchumi. Mkopo wowote utakaochukuliwa kwa ajili ya barabara hizi, unaweza kulipika kwa muda wa miaka 20 mpaka 30 na mkopo unaokubalika kwani utachochaea ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuongeza shughuli za kiuchumi na hivyo kupelekea nchi kupiga hatua na kuchukua fursa ya uchumi wa Jiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasihi Wabunge tuelekeze mjadala katika suala hili la *financing infrastructure* kwani kama hakuna fedha hata tupige kelele VIP pesa hazitakuja maana tutajenga barabara lakini lazima tuendelee kulipia elimu, afya, huduma za Serikali, pensheni kwa wastaafu wetu ambazo tunataka ziongezeke mpaka ngazi ya kima cha chini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nzungumzie kidogo mradi mmoja wa barabara, nayo ni barabara ya Sam Nujoma. Ujenzi wa barabara ya Sam Nujoma ambao ni kutokea Mwenge hadi Ubungo, umeshachukua muda mrefu sana na bado ujenzi wake haujakamilika, pamoja na Mheshimiwa Rais kuahidiwa kuwa ujenzi wake ungekamilika mwaka 2006 mwezi November mpaka leo hii, ujenzi huo bado haujakamilika. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutoa majibu ya kina, nini kimesababisha ujenzi wa barabara hiyo kuchelewa kwa kiasi hicho? Tatizo liko wapi? Mkandarasi ama ni Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Bandari zetu na usafiri wa majini (*The state of our ports and marine transport*). Nchi yetu imejaaliwa na Mungu kwa kuzungukwa na Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu matatu ambayo ni Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Mungu angeweza kutunyima rasilimali nyingine zote na akatuacha na rasilimali hizi tu na tungeweza kukua kama Taifa kutokana na utajiri unaoweza kuzalishwa na rasilimali hizi. Hata hivyo, Mungu ametujaalia mengine mengi sana kama Madini, Mito yenye kuzalisha Umeme na Watu wapenda amani na wakarimu. Hata hivyo bado hatujaweza kutumia rasilimali hizi kujiendeleza inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi, katika mwaka wa 2007, bandari ya Dar es Salaam, ilihudumia shehena zenyenye jumla ya tani 5,703 milioni ikilinganishwa na tani 6,320 milioni mwaka wa 2006, sawa na upungufu wa asilimia 9.8. Vile vile, jumla ya meli 4,380 zilihudumiwa katika kipindi cha 2007, ikilinganishwa na meli 4,147 mwaka wa 2006, sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Kambi ya Upinzani, imeshtushwa na hali hii ya kushuka kwa idadi ya makontena ambayo yamehudumiwa na bandari yetu kuperomoka kwa takribani asilimia 10 katika kipindi cha mwaka mmoja, kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007, Kitengo cha Kontena kilihudumia tani 3,327 milioni kati ya shehena yote iliyohudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam. Aidha, mwaka 2007, kitengo hiki kilihudumia kontena 333,980 zenyenye urefu wa futi ishirini kila moja, ikilinganishwa na kontena 273,128 mwaka wa 2006, sawa na ongezeko

la asilimia 22.3. Katika mwaka wa 2007, muda wa kukaa bandarini kwa kontena zilizoingia nchini uliongezeka toka wastani wa siku 14.5 mwaka wa 2006 hadi siku 23. Aidha, ufanisi katika Kitengo cha Kontena, ulipungua hadi kufikia mizunguko 18 kwa saa ikilinganishwa na mizunguko 21 kwa saa mwaka 2006. Taarifa hizi sio nzuri kwa Bandari ambayo ingeweza kuleta utajiri mkubwa kwa nchi yetu. Tunataka kupata maelezo ya kutatua matatizo haya ili Kitengo cha Makontena kiwe na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007, bandari za Tanga na Mtwara, zilihudumia shehena zenye jumla ya tani 542 milioni na 112 milioni ikilinganishwa na tani 519 milioni na 153 milioni mwaka 2006 kwa mtiririko huo. Bandari hizi za Mtwara na Tanga, ni lulu kwa nchi lakini hatutumii lulu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima pawepo na mkakati madhubuti wa kuziimrisha Bandari za Mtwara na Tanga, ili kuhakikisha kuwa Meli kubwa za mizigo zinaweza kutia nanga kwenye maeneo hayo. Hatua hii inalenga kwenye kuongeza mapato zaidi na hata kupanua wigo wa soko la malighafi zinazozalishwa hapa nchini, kwa mfano Kama bandari ya Tanga itaimarishwa, itawezesha usafirishaji wa malighafi yatokanayo na mkonge kusafirishwa kwa urahisi zaidi kuliko hali ilivyo hivi sasa kwani ni lazima malighafi hizo zisafirishwe kwanza kwa njia ya barabara hadi Dar es Salaam, ndipo zinapakiwa kwenye meli. Lakini pia mkakati wa Bandari ya Tanga, ni lazima ufungamanishwe na mkakati wa sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 Tanzania itakuwa ni nchi yenyewe kuzalisha madini ya Nikeli kuliko nchi nydingine zote duniani kama mipango ya uchimbaji wa Nikeli kule Kabanga Wilayani Ngara itakamilika. Ni muhimu sasa kuweka mikakati ili Bandari ya Tanga iwe *Port of Choice*, kwa kusafirisha Nikeli na madini mengine yanayochimbwa nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo suala linaloitwa fungaminisho linapopata maelezo rahisi. Tutakapoimrisha Reli ya Kati ili iwe *Railway of Choice* kwa usafiri wa Shaba na Kobalti kutoka Mashariki ya Kongo, maana yake ni kuwa mizigo kwa ajili ya Bandari ya Tanga kama *Port of Choice* kwa usafirishaji wa Madini itaongezeka. Shughuli za kiuchumi zitapanuka, ajira zitakuwa bwelele na vijana hawataimba tena ‘Tanga Kunani’. Serikali itapata mapato na kuhudumia sekta za kijamii. Hii ndio inaitwa *Strategic Thinking* ambayo Kambi ya Upinzani, inaimba kila mwaka. Tubadili *mindset* kwa kupanga mipango yetu kwa kuangalia mbele kuna fursa zippi kwa upande wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Mtwara, maelezo yake hayatofautiani na ya Tanga. Licha ya kusafirisha Korosho na mazao ya misitu, Bandari ya Mtwara, ni muhimu

sana kufungamanishwa na miradi ya Mchuchuma na Liganga. Vilevile Bandari hii yaweza kuwa ni Bandari ya nanga kwa uvuvi wa Bahari Kuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri na haswa kwa njia ya maji Ziwa Victoria umekuwa hauridhishi kwani meli ambazo zinatumika kuwasafirisha abiria zimekuwa zikilalamikiwa kila mara kutokana na meli hizo kuwa ama ni chakavu sana kutokana na kukaa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo au kutokana na kuwa ni za zamani sana. Meli hizi zinahatarisha maisha ya wananchi wetu kila wanaposafiri, hivyo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina juu ya hali hii ya kuhatarisha maisha ya wananchi wetu na kuna mkakati gani wa kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanakuwa salama kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa sasa huu ni wakati muafaka wa kuwa na Bandari za nchi kavu (*Dry Ports*) ili kuweza kupunguza msongamano wa makontena katika Bandari ya Dar es Salaam na pia kukuza uchumi maeneo mengine ya nchi kwa kukuza nafasi za ajira. Serikali inapaswa kuweka mkakati wa kina kuwa Bandari ya Dar es Salaam iwe ni kwa ajili ya kuitisha mizigo yote ambayo inakwenda nje ya nchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mizigo yote ambayo inakwenda nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (*DRC*) na Burundi ijengewe bandari ya nchi kavu Kigoma na hapo ni kuwa mizigo yote ambayo inaingia bandarini kwa ajili ya kupelekwa kwenye nchi hizo, basi isafirishwe moja kwa moja hadi Kigoma na ndipo iweze kuchukuliwa kutokea pale kwenda katika nchi zinazokwenda. Jambo hili litasaidia kuinua uchumi wa Kigoma na pia litawezesha kuimarishe Shirika letu la Reli kwani litatumika kusafirisha mizigo hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma na wananchi wataweza kupata ajira kwenye Mkoa huo na pia litawezesha kuharakisha ukarabati wa miundombinu katika Mkoa huo, biashara itaimarika na pia litapunguza wingi wa mizigo ama makontena kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mizigo yote ambayo inakwenda nchi za Uganda na Rwanda, Bandari ya Nchi Kavu iwe Isaka, Shinyanga na hili litaharakikisha kukua kwa uchumi katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwani ajira nyingi zitawenza kupatikana na hatimaye kuimarishe kwa uchumi katika maeneo husika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mizigo yote inayokwenda nchi za Zambia na Malawi, pajengwe bandari ya nchi kavu Mbeya ili kuhakikisha kuwa mizigo hiyo inachukuliwa kwenye eneo husika. Hii itasadia kasi ya ukuaji wa uchumi kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu kusini kama vile Iringa, Mbeya na Ruvuma. Pia kwenye maeneo haya Makampuni yote yanayohusika na *clearing and forwarding* yawe yanafanya shughuli zake kwenye maeneo hayo ambayo yana bandari hizo za nchi kavu. Dar es Salaam iachwe na kuwa ni kwa ajili ya mizigo ya ndani na ambayo haiendi kwenye Mikoa na nchi husika na pia liwe ni eneo la kupokelea mizigo husika na kuisafirisha kwa maeneo hayo. Yaani Dar es Salaam ibaki kuwa ni (*Transit port*). (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa nimetenda haki iwapo sitazungumzia matatizo ya wafanyakazi wa bandarini Kigoma *AMI* na nilikuwa naomba Waziri wa

Miundombinu aweze kutolea maelezo matatizo haya vijana hawa na watu wengine pia waliochishwa baada ya *AMI* kukosa *contract* ya pale bandarini na hawajalipwa mafao yao, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aweze kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Reli na Usafiri wa Reli (*The State of our Railways and Rail Transport*). Usafiri wa Reli ni usafiri muhimu sana kwa nchi na hasa kuhusiana na usafiri wa mizigo yenye uzito mkubwa. Hatuwezi kuendelea kamwe kwa kutegemea usafiri wa barabara kusafirisha mizigo yenye uzito mkubwa kama Madini na bidhaa nyine.

Tanzania tuna reli mbili, yaani ya *TAZARA* na ile ya Kati. Wabunge wamezugumza humu Bungeni kuhusiana na adha ya usafiri wa Reli. Waziri Mkuu ametoa majibu kuhusiana na suala hili na ameeleza kwamba kwa kiasi kikubwa sisi ni chanzo cha matatizo haya na siyo mwekezaji ambaye amekodisha Reli hii kwa ubia kati ya hawa *RITES* na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa Nguruka Mkoani Kigoma watu wa Nguruka waliniambia kwamba ukitaka kusafiri kwa reli inabidi uweke sahihi hukumu ya kifo. Kuna taarifa za vifo vilivyotokea maeneno ya Uvinza kufuatia mwanamke mmoja kukosa hewa alipokuwa akisafiri na treni ya abiria kwenda Kigoma. Serikali ifuatilie kujua usahihi wa taarifa hizi. Vile vile kumekuwa na ugumu mkubwa wa kupata tiketi za kusafiria katika stesheni karibu zote za reli na kuwa usumbufu mkubwa sana kwa wananchi wetu. Hali ya reli inasikitisha mno kwa wananchi wa Mikoa ya Kigoma na Tabora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Kumi na Moja, Mheshimiwa Said Amour Arfi - Mbunge wa Mpanda Kati, CHADEMA alitoa hoja binafsi hapa Bungeni kuhusu hali ya Shirika la Reli na Serikali iliahidi kutoa majibu. Ni vizuri basi Serikali itoe majibu kama nyongeza ya majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na tatizo la usafiri wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2007, Shirika la Reli Tanzania lilisafirisha mizigo tani 714,000, ikilinganishwa na tani 775,281 mwaka 2006, sawa na upungufu wa asilimia 7.9. Kati ya hizo, tani 173,516 ilikuwa ya nchi jirani za Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Rwanda, Burundi na Uganda. Hivi sasa kuna kitu kinaitwa *mineral boom* kule Kongo ya Mashariki. Inakuwaje tena usafiri wa mizigo unashuka kiasi hiki? Kwa kuwa Shirika hili bado Serikali ina hisa za kutosha, ni vyema Serikali kuititia Wakurugenzi wake ambao wengine ni Wabunge wenzetu iwe na mkakati wa kutangaza huduma ya reli kwa nchi hizi. Hata hivyo, ni lazima tuboreshe kwanza huduma hizi na kupanua reli hii ili kupata biashara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Reli lilipata mapato ya shilingi bilioni 33.6 mwaka 2007, ikilinganishwa na shilingi bilioni 42.6 mwaka wa 2006, sawa na upungufu wa asilimia 21.1. Huku ni kuporomoka kwa kasi kwa mapato ya shirika ambapo ni lazima Serikali itolee maelezo. Kambi ya Upinzani pia inapenda kufahamu kama Shirika lina *Corporate Plan* na kama inafuatwa katika kuboresha huduma za reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo viwanja vyta ndege kwa usafiri wa anga, Stesheni za Reli zina umuhimu mkubwa sana kwa usafiri wa reli. Kwa muda mrefu sana Stesheni za Reli zimekuwa ndio maofisi ya Shirika la Reli na pia zimekuwa zinamilikiwa kwa pamoja na reli. Stesheni za Reli, hasa zile stesheni kubwa kama vile Tabora, Kigoma, Urambo, Mpanda, Kilosa, Dodoma, Morogoro, Tanga, Mwanza na Dar es Salaam zimekuwa hazitumiki kwa asilimia 100 na kwa kweli stesheni nyingine zimekuwa chafu na hazihudumiwi ipasavyo. Sijui kama katika mkataba wa kukodisha reli na pia makubaliano ya wanahisa, yaani *Share holders agreement* wamesema nini kuhusu Stesheni hizi na hasa umilliki wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri tuwe na mwono tofauti na kugeuza Stesheni hizi kuwa vituo vyta Biashara katika Miji yetu. Stesheni nyingine kama ile ya Kigoma, Tabora, Dodoma na Dar es Salaam zinaweza pia kuwa ni *Tourist Attractions* hasa kwa watalii kutoka Ujerumani kutokana na ukweli kuwa Stesheni hizi ni moja ya usanifu wa Kijerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Stesheni hizi zina zaidi ya miaka 100 na baadhi ya vyumba vyake vyaweza kugeuzwa kuwa hoteli na migahawa na maduka ya vitu mbali mbali na hivyo kuzifanya hizi stesheni kuwa *live usiku* na mchana. Ninaiomba Wizara ya Miundombinu itafakari hili na kualika Makampuni ya Kitanzania *private sector* kuangalia uwezekano wa kuzibadili Stesheni hizi kwa maana ya majengo kuwa maeneo ya Biashara. Inawezekana, hebu tujaribu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa kwa ATC Serikali iliunda *RAHCO* kwa ajili ya kuuza mali za iliyokuwa *TRC*. Moja ya mali zilizouzwa ni pamoja na *Gerezani Railway Social Club* ambayo kimsingi ilikuwa ni mali ya Wafanyakazi. Ninapenda kupata maelezo ya Serikali kuhusiana na uuzwaji wa mali hizi. Vile vile tunapenda kujua hatua zilizochukuliwa kutokana na mataruma ya reli yaliyokatwa na kukutwa katika Kiwanda cha Nondo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la daraja la Kigamboni ni suala linalosemwa kila mwaka na wala hatuoni aibu kuendelea kulisemea. Naomba Waziri wa Miundombinu alieleza Bunge hili, ni lini tutaacha kusema na kutenda kuhusiana na suala hili? Suala hili sasa liishe maana tumekuwa Taifa la maneno matupu mpaka inakuwa ni aibu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya viwanja vyta ndege na usafiri wa anga (*The state of our Airports and Air Transport*), nafasi ya Tanzania kijiografia inatoa fursa kubwa kwa usafiri wa anga kuwa na manufaa kwa Taifa. Hivi sasa Taifa letu lina viwanja vyta ndege viwili vyta kimataifa, yaani *Julius Nyerere International Airport* na *Kilimanjaro International Airport*. Kiwanja cha Songwe kinamaliziwa kujengwa. Viwanja vyta ndege vyta Mwanza, Kigoma, Tanga, Mtwara, Bukoba na Mafia ni viwanja muhimu sana kwa ukuaji wa sekta na uchumi kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Nchi, huduma za usafiri wa anga nchini ziliendelea kutolewa na mashirika kadhaa ya ndege na

idadi kubwa ni makampuni binafsi. Makampuni hayo nimeyataja katika hotuba yangu na idadi ya abiria ambao wamesafirishwa ni pamoja na *Air Tanzania Company Limited, Precision Air, Coastal Travel, Regional Air Services, Eagle Air, Air Excel, Flight Link, Zan Air* na kampuni kadhaa nyinginezo. Abiria wa ndani waliosafiri kwa ndege hizo ni jumla ya watu 1,074,424 mwaka 2007 ikilinganisha na abiria 1,011,265 mwaka 2006.

Kampuni ya *Precision* ilisafirisha takriban abiria 470,000 kati ya abiria wote walisafiri ndani ya nchi kwa ndege. Hii ni sawa na asilimia 43 ya wasafiri wote. Tanzania hatuna tabia ya kutambua mchango wa Watanzania wenzetu wanaofanya vizuri katika nyanja mbalimbali. Tunapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wamiliki na wafanyakazi wa Kampuni ya *Precision* kwa huduma wanayotoa kwa Watanzania. Licha ya mapungufu kadhaa yaliyopo, lakini hivi tukijiuliza kama hawa *Precision* wasingekuwepo hali ya sasa wa usafiri wa anga Tanzania ingekuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni yetu ya Umma ya *Air Tanzania* ambayo ilianzishwa baada ya kuvunjwa kwa mkataba na Kampuni ya *South Africa Airways* iliendelea kusucasua katika mwaka uliopita. ATCL ilisafirisha nusu ya abiria waliosafirishwa na *Precision*. Ni mategemeo ya Watanzania kuiona ATCL kama fahari ya Taifa (*The National Pride*). Hata hivyo, hali ya ATCL inatia simanzi sana kwa sisi wapenzi wa sekta ya umma katika maeneo nyeti kama usafiri wa anga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu ya kina juu ya hali ya ndege na ni kwanini eneo limeendelea kupata matatizo ya kifedha? Tatio ni nini hasa? Ni menejiment, ni hujuma au kuna ujisadi? Shirika letu la ndege limekuwa katika wakati mgumu sana kwa kipindi kirefu kutokana na ukata na ukosefu wa fedha kutokana na Serikali na hali ngumu ya kiuchumi ambayo inalikumba shirika hilo na hii inatokana na Serikali kutenga kiasi kidogo sana cha fedha kujiendesha.

Kitendo cha ATCL kusafirisha nusu ya abiria waliosafirishwa na kampuni moja binafsi na robo tu ya abiria waliosafiri kwa ndege nchini ni aibu kwa Shirika letu la Ndege kwani kama abiria wanaongezeka ilitegemewa kuwa ni shirika letu la ndege lingeweza kuiongezea faida na mapato zaidi kutokana na ongezeko hili la wateja, ila badala yake shirika letu limekuwa na wakati mgumu zaidi kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu ya kina juu ya hali ya shirika letu la ndege na ni kwanini shirika hilo limeendelea kupata matatizo ya kifedha? Tatizo ni nini hasa? Menejimenti, hujuma au kuna ujisadi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna taarifa kuwa katika mwaka 2007 kampuni ya ndege Tanzania iliendelea kujiimarisha kwa kukodi ndege nne ambazo kati ya hizo mbili ni za aina ya B737-200 na nyingine aina ya B737-700/800. Kambi ya Upinzani imepata taarifa kuwa ndege zote hizo ni mbovu na zilinunuliwa kifisadi. Sisi tunatoa *benefit of doubt* kwa ATCL na hivyo tunataka maelezo kutoka Serikalini kuhusiana na ununuzi wa ndege hizi na hasara ambayo ATCL imepata. Tunahitaji maelezo ya kina na majibu yasiyofinyangwa finyangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchakato wa kubinafsisha ATC Serikali iliunda kitu kinachoitwa *ATHCO* ili kuuza mali za iliyokuwa *ATC*. Katika michango mbali mbali ya wabunge Kambi ya upinzani humu Bungeni, tuliulizia kuhusu nyumba za *ATC* zilizouzwa ama kuachwa kinyemela katika nchi mbalimbali duniani. Tulihoji mwaka 2006/2007 kuhusiana na nyumba za *ATC* huko Johannesburg, Harare, Lusaka, Comoro na mali kadha wa kadha huko Oman na Riadha Saudia. Serikali likiri kuwapo kwa mali hizo na kuahidi kutolea majibu. Mpaka sasa Watanzania hawajapata majibu kutoka Serikalini. Tunataka kujua mali za Watanzania hizi ni nini hatma yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi wa viwanja vya ndege ni eneo ambalo halijatiliwa mkazo wa kutosha na pia halipewi kipaumbele cha kutosha. Kutokana na kukua kwa kasi ya usafiri wa anga hapa nchini na ikizingatiwa kuwa sekta ya utalii inakua kwa kasi kubwa, basi haina budi kuboresha viwanja vyetu vya ndege na kuvientesha kibashara. Hili litawezesha kuvutia watalii wengi kuja nchini moja kwa moja kwani kwa sasa watalii wengi wanapitia Nairobi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inakubaliana na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwamba tozo ya *passengers service charges* inayotozwa hivi sasa na *TRA* na kwenda Mfuko Mkuu iende *Tanzania Airport Authority* yote ili mamlaka iweze kuwekeza katika kuboresha viwanja vya ndege. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa sasa ni wakati muafaka tukaamua kutumia *terminal one* kwa ajili ya wasafiri wa ndani na *terminal two* ikatumika kwa ajili ya wasafiri wa nje na hatua hii itawezesha mamlaka husika kuweza kukarabati kiwanja cha *Julius Nyerere International Airport* na hivyo kuweza kuvutia mashirika mengi ya kimataifa.

Pia kama tukiweza kukarabati viwanja vyetu kwa sasa ni wakati muafaka sana kwani kutokana na mashindano ya mpira wa miguu kombe la dunia ambayo kwa mara ya kwanza yatafanyika Barani Afrika mwaka 2010. Lazima tuboreshe viwanja vyetu ili kuhakikisha kuwa timu nyingi zinakuja kuweka kambi nchini na ikizingatiwa kuwa kwa sasa tuna kiwanja cha mpira wa miguu cha kisasa nchini. Kambi ya Upinzani inapenda kupata maelezo ya kina kuhusu utayari wa Serikali kufaidika na Mashindano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika nchini Afrika Kusini miaka miwili ijayo na sekta ya *aviation* imejiandaa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapenda pia kusisitiza umuhimu wa viwanja vya ndege vya pembezoni mwa nchi. Uwanja wa Ndege wa Mwanza na ule wa Kigoma ni viwanja muhimu sana katika eneo la Maziwa makuu. Ni muhimu uwanja wa ndege wa Kigoma ukapewa kipaumbele pekee kwani uwanja huu ukitangazwa vizuri utakuwa ni *stop over* ya ndege kutoka Congo na Burundi kwa ajili ya kuleta abiria Uwanja wa ndege wa Dar es Salaam na kwenda ughaibuni. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iliangular suala hili na kuweka mkakati wa pekee wa uendeshaji wa uwanja huu ili Taifa lifaidike, lakini pia kampuni za ndege nchini nazo zifaidike.

Kambi ya Upinzani pia inapendekeza kuwa sasa ni wakati muafaka tukaamua kutumia *terminal one* kwa ajili ya wasafiri wa ndani na *terminal two* ikatumika kwa ajili ya wasafiri wa nje na kwa maana ya ndege za kimataifa na hatua hii itawezesha Mamlaka

husika kuweza kukarabati kiwanja cha *Julius Nyerere Internal Airport* hivyo kuweza kuvutia mashirika mengi ya kimataifa.

Pia kama tukiweza kukarabati viwanja vyetu kwa sasa ni wakati muafaka sasa kwani kutockana na mashindano ya mpira wa miguu ya kombe la dunia ambayo kwa mara ya kwanza yanafanyika Barani Afrika mwaka 2010 lazima tuboreshe viwanja vyetu ili kuhakikisha kuwa timu nyingi zinakuja kuweka kambi nchini ikizingatiwa kuwa kwa sasa tuna kiwanja cha mpira wa miguu cha kisasa nchini. Kambi ya Upinzani inapenda kupata maelezo ya kina kuhusu utayari wa Serikali kufaidika na mashindano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika nchini Afrika Kusini miaka miwili ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la ukiritimba wa Kampuni ya *Swissport* katika viwanja vyetu na hasa uwanja wa ndege wa Dar es Salaam. Zama hizi kuwa na kampuni ya huduma moja katika uwanja ni hatari sana na wala sio tija. Kuna haja kubwa ya kuweka ushindani katika huduma hii kwa kuondoa ukiritimba wa Kampuni ya *Swissport*. Ninamtaka Mheshimiwa Waziri atengue mara moja ukiritimba huu na kuruhusu ushindani. Hili lifanyike haraka kwani hakuna mantiki hata kidogo kuwa na kampuni moja pekee katika huduma ya mizigo katika viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitaje muhtasari wa mapendekezo ambayo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweze kuyafanya kazi.

Serikali izingatie taarifa ya hali ya umasikini kwamba sekta ya miundombinu na hasa sekta ndogo ya huduma za uchukuzi ni sekta ya kwanza kimkakati katika kukuza uchumi wa nchi wa nchi ili kuhudumia nchi jirani zisizo na bandari. Hivyo vipaumbele vya barabara zipi za kujengwa, viwanja vipi vya ndege vya kuboreshwa, bandari zipi kuimashwa lazima vizingatie ushauri huo.

Serikali ilete Bungeni mpango mbadala wa ujenzi wa miundombinu na kuwa na mjadala mpanga wa Bunge kuhusu jinsi ya kugharamia miundombinu yetu (*financing infrastructure in Tanzania for development*). Kwa kushauriana na Kamati ya Bunge ya Fedha na uchumi na pia Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Serikali iharakishe mchakato wa kuchukua *sovereign bond* ili kugharamia ujenzi wa miundombinu na kuleta taarifa Bungeni katika Mkutano wa 13 wa Bunge la tisa.

Serikali iamue kwa makusudi kabisa kuifanya bandari ya Dar es Salaam kuwa ni Transit Port kwa mizigo yote inayokwenda nchi za Zambia na Malawi (Bandari yake iwe Mbeya), Burundi na congo DRC (Bandari yake iwe Kigoma) na Rwand na Uganda (Bandari yake iwe Shinyanga – Isaka).

Viwanja vya ndege vya Mbeya, Mwanza na Kigoma viboreshwe kwa haraka ili kukidhi haja ya ukuaji wa Sekta ya uchukuzi na mabadiliko yatakayoletwa na maamuzi niliyataja hapo juu. Uwanja wa Ndege wa Kigoma katika siku chache zijazo na kwa mikakati maalum utakuwa ni hub ya ukanda wa maziwa makuu. Umuhimu ni huo huo kwa Mbeya na Mwanza.

Katika hali ya haraka sana kwa vyovyyote vile, barabara na reli kuelekea Ngara zijengwe ili kuhakikisha kuwa uzalishaji na Nikeli utakapoanza kule Kabanga kuwe na miundombinu stahili na huduma hii ya miundombinu itafungamanisha Sekta ya Madini na Sekta ya Miundombinu na hivyo Taifa kufaidika na raslimali madini na vile vile kuchocheo maendeleo ya kiuchumi ya eneo la ziwa magharibi.

Serikali ifikirie kuanzisha wakala wa barabara za vijijini katika kila Mkoa (*Rural Roads Agency*) ili kuwa na jukumu la kisheria kuejnga na kukarabati barabara za vijijini na kuondoa jukumu hilo katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii itaongeza ufanisi na utaalamu na pia kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama za ujenzi wa barabara (*economies of scale*) badala ya sasa ambapo kila Halmahsauri katika Mkoa inajijengea barabara bila kuwiana na mipango ya maendeleo ya Mikoa. Ushauri huu unaimarisha  $D$  by  $D$  badala ya kuua kwani bado jukumu la Baraza la Madiwani litakuwepo lakini wakala huu utafanya kazi chini ya Bodi ya Barabara ya Mkoa na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*).

Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kushirikiana na Kamati ya Bunge ya Uwekezaji Umma (*Public Investments Committee/POAC*) ifanye tathmini ya ubinafsishaji *TRC* na *ATC* na kuhakiki mali za mashirika haya na kuleta taarifa Bungeni il ikuweza kuokoa baadhi ya mali za umma zilizopotea katika zoezi hili kama nyumba za *ATC* zilizokuwa katika nchi za Afrika Kusini, Zambia, Comoro, Zimbabwe na Oman. Vile vile mali za *TRC* kama vile *Gerezani Railway Social Club* na kadhalika. Hii ni kutokana na *ATHCO* na *RAHCO* kuuza mali hizi kama wendawazimu.

Serikali iache kwa sasa mpango wowote wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege mpya na badala yake ifanye marekebisho makubwa katika *Terminal One* ya sasa na kuanzia mwakani mwezi Januari, *Terminal One* itumike kwa ndege za ndani na *Terminal Two* itumike kwa ndege za nje. (*Makofit*)

Napenda kutoa ushauri kwamba Serikali iimarishe Chuo cha Usafirishaji as a matter of Agencey. Maana kama tutataka nchi ichukue fursa ya huduma za usafiri kwa nchi za Maziwai Makuu ni lazima kuwa na wataalam wa usafiri ili waweze kuishauri nchi vyema kuiendeleza Sekta hii. Chuo sasa kitatoa wachumi usafiri wengi na pia kijikite katika kada ya logistics kweni kutokana na ukujali wa Sekta wanahitajika wataalam wengi sana. Naomba tu kwamba Hansard ichukue yote ambayo yameandikwa kwa sababu siwezi kuyasoma yote kwa muda wote.

Stesheni za Reli zote katika Miji mikubwa zisiwe mali ya *TRL* na kama ipo hivyo katika mikataba na ibadilishwe ili Stesheni hizo ziendeshwe na Sekta binafsi za kitanzania kama vituo vya kibashara na *TRL* wapange kama ilivyo katika nchi nyingine. Hii itafanya majengo hay akutumika kw aufanisi kwa hivyo kukuza biashara katika Miji ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Tabora na Kigoma kwa kuanzia. Tathmini ya kina ifanyike kuhusu suala hili.

Serikali itengue mara moja ukiritiba wa *Swissport* katika huduma za mizigo katika viwanja vya ndege vya Tanzania na badala yake iruhusu ushindani wenye tija. Ushiriki wa Watanzania upewe kipaumbele katika biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hoja za majibu ya Upinzania inahitaji majibu katika masuala yafuatayo kutoka Serikalini.

- Serikali ilete taarifa Bungeni kuhusiana na mapitio ya Mkataba wa ukodishwaji wa Uwanja wa Ndege wa *KIA* kwa kampuni ya *KADCO* ili tujue kama katika marekebisho ya Mkataba maslahi ya Taifa yamezingatiwa. Je, mapitio hayo tayari?
- Serikali itoe maelezo ya kina Bungeni kuhusiana na maswali yanayoulizwa na umma juu ya ukodishwaji wa ndege mbovu na za gharama kubwa unaofanywa na *ATCL*.
- Serikali itoe majibu iliyonayo kuhusiana na mali za *ATC* zilizoko nje ya nchi.
- Tanzania na hasa sekta ya usafiri wa anga imejipangaje kuhusiana na fursa zitakazoletwa na kufanyika kwa Mashindano ya kombe la Dunia la Mpira wa Miguu huko nchini Afrika ya Kusini?
- Serikali itoe maelezo kuhusiana na mafao ya waliokuwa na wafanyakazi wa AMI wakati wanaendesa Bandari ya Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kambi ya Upinzani inatekeleza wajibu wake wa kidemokrasia wa kutoa maoni na hoja ili Kambi ya Chama kinachotawala ifanyie kazi kwa maslahi ya Taifa. Ninawatahadharisha wenzetu kuwa hali ya kisiasa ya nchi imebadilika sana na kwa kasi.

Iwapo walio na Serikali watashindwa kutekeleza mabadiliko muhimu ya kisera ili kuendena na upopo wa mabadiliko ya kiuchumi, wananchi watawapumzisha. Sisi tunasubiri tupewe ridhaa na wananchi ili tutekeleze mipango hii ambayo wenzetu mmeshindwa kutekeleza. Mawazo mbadala tunayo, nguvu ya kutekeleza mawazo haya tunayo na tunaweza! (*Makofi*)

Wanasiasa wa Kambi ya Upinzani wana macho na wanaona, wana ngozi na wanahisi, wana masikio na wanasikia, wana pua na wananusa, wana mdomo na wanasema, ndiyo maana tuhuma zote za ubadirifu na ufisadi ambazo tumezisema zimethibitika kwamba ni za kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii uliyonipa na naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge namshukuru Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Miundombinu.

Kwa muda tulio bakiwa nao Waheshimiwa Wabunge tunaweza sasa kuanza kuwaruhusu wachangiaji kadhaa waanze kuchangia mada tuliyonayo na kama nilivyosema tutaanza na Mheshimiwa Michael Laizer na Mheshimiwa Daniel Msanzugwanko ajiandae na kama muda utaendelea kutruhusu, basi Mheshimiwa Capt. John Damian Komba naye atapata nafasi. Mheshimiwa Laizer tafadhali.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Waziri wa Miundombinu. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri walioifanya kufuta mikataba wa *Dowans*. Nawapongeza Serikali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie mikataba mingine mibovu, ifute kama ilivyofuta hii na Wizara hii ya Miundombinu iige Wizara ya Nishati na Madini. Ndugu yangu, Mheshimiwa Ngeleja, ifute tusione tena mikataba mibovu inayonyanyasa na kuwahujumu wananchi na kunufaisha wachache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie katika barabara za Mkoa hasa nianze na barabara ya Arusha-Namanga. Barabara hii ya Arusha-Namanga tangu mimi nilipoingia Bungeni nilikuta ikiitwa Himo-Moshi-Arusha-Namanga. Nina miaka 13 sasa, hiyo barabara imeishia Arusha. Ina miaka minane sasa tangu ifike Arusha. Lakini mpaka sasa bado barabara ya Arusha-Namanga inakarabatiwa kuwekwa viraka tu na kila bajeti ukiangalia barabara ipo. Itatengenezwa mwezi wa tano, itatengenezwa mwezi wa saba mpaka leo ni danadana. Nataka leo kupata jibu kwamba sasa imeanza Nairobi, imeanza *Athi River*, badala kwanza Arusha, imeanza *Athi River*. Itafika Longido lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuzungumzia barabara hii ya Rombo-Tarakea-Rongai-Kamwanga. Nadhani Wabunge wenzangu mnafahamu kila siku kwamba ninachangia barabara hii. Barabara hii ina matatizo makubwa sana. Imewagawa wananchi, ni barabara ya kisiasa.

Niliwahi kusema kwamba hebu mniambie ni barabara ipi ya lami inatoka Makao Makuu ya Wilaya nyingine na kuishia kijiji cha mpakani cha Wilaya nyingine. Hii nasema ni barabara ya Kijiji kwa sababu ingezunguka mpaka Hai ndiyo tungejua kwamba hiyo ndiyo barabara ya Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara imetoka Rombo mpaka kwenye kijiji cha Kamwanga ambacho kiko mpakani, kiko Wilaya ya Longido. Cha ajabu sana lami imefikia hapo, na baya zaidi wananchi wamevunjiwa nyumba zao. Wananchi wa Rombo, Tarakea, Rongai wamelipwa fidia. Lakini wa Kamwanga wa Jimbo langu hawakulipwa fidia. Ndugu zangu Mawaziri nyinyi ni Wabunge kama sisi, uteuzi ndiyo umewafanya muwe Mawaziri. Huo uwaziri unatumia vibaya kuangalia Jimbo lako. (*Makofi*)

Hata Rais aliyekuchagua, Rais hajakuchagua utumikie Jimbo lako. Unatumikia nchi nzima. Hatukubali kuona kwamba sisi Wabunge ambaio sio Mawaziri, Mawaziri tunaopakana nao wanajenga kwao, wanaacha kwetu.

Kwa hiyo, mimi nikaona barabara inakuja kuishia kwenye kijiji kingine, tena barabara ya lami. Nimeleta orodha ya watu waliovunjiwa nyumba, nimempa aliyekuwa Waziri Mkuu, nimempa aliyekuwa Waziri wa Miundombinu, nadhani kilio cha watu wa Kamwanga ndiyo imefanya mabadiliko makubwa yaliyofanyika yatokee. (*Kicheko/Makofi*)

Watu wengine wa Jimbo la Rombo wamelipwa fidia, lakini wa Jimbo la Longido hawakulipwa fidia na wamevunjiwa nyumba na hawana pa kuishi mpaka sasa hawana pa kuishi. Naomba Serikali itoe maelezo kwamba kwa nini watu wa Longido wa Kamwanga hawakulipwa fidia na wengine wamelipwa fidia na barabara ni hiyo hiyo moja iliyosababisha kuvunjiwa nyumba zote. Naomba njue ni lini barabara hiyo itaendelea kupita Longido na kwenda Siha. (*Makofi*)

Niliwahi kuuliza kwamba hii barabara inaonyesha mpaka wa makabila? Niliwahi kuuliza hapa hapa Bungeni, hivi hii barabara inasubiri mpaka na mimi niwe Waziri wa Fedha ndiyo iendelee. Naomba maelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona baadhi ya Mawaziri hawatekelezi kazi waliopewa na Rais vizuri. Tukifanya kazi kwa kutumia siasa, kwa kufuata kura, hivi mnataka Jimbo la Longido liwe kama Jimbo la Rombo kuwa jimbo la Upinzani? Kama mnalitaka kulirudisha ili wananchi watoe kura mnataka wananchi wa Longido nao waende upinzani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamenipa kura kwa imani, wananiamini. La sivyo nisingepata kura. Lakini wananiamini kwamba naweza kuwatetea na ndiyo sasa nawatetea nataka Serikali iwalipe fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuzungumzia barabara za Mikoa. Niliomba katika Mkutano wa *Road Board* Mkoani barabara za Longido zipandishwe hadhi ziwe barabara za Mkoa. Niliomba barabara kutoka Longido-Ketumbene mpaka Lengai iunganishe Wilaya ya Longido na Wilaya ya Ngorongoro. Kwa sasa sisi hatuunganiki kabisa, hakuna barabara inayounganisha Wilaya hizo pamoja na kwamba ni Wilaya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha kwenye *Road Board* tumepitisha kwenye Kikao cha *RCC*, barabara zilizopandishwa hadhi zimesomwa hapa na aliyekuwa Waziri wa Miundombinu. Nimesimama kwenye vifungu na kuelezea barabara hiyo kwamba mbona tumepitisha, aliyekuwa Mhandisi hakuleta barabara za Wilaya Longido. Ameleta barabara za Wilaya ya Monduli akaacha barabara za Wilaya ya Longido. (*Makofi*)

Nimesimama hapa kwenye vifungu. Mheshimiwa Chenge ndiye aliye kuwa anasoma, ndiye Waziri wa Miundombinu. Aliye kuwa Waziri Mkuu akasimama akaniunga mkono kwamba ni kweli hiyo barabara ipo, ireke bishwe. Hiyo barabara haikureke bishwa. Mpaka juzi nikamwomba nikamfuata Waziri wa Miundombinu wa sasa pamoja na Katibu wake, nikamweleza hayo na akakumbuka kwamba nimesema hilo Bungeni. Waziri pamoja na Katibu wake nawashukuru sana kwa sababu nimeona kwenye vitabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nimelisema hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema isahihishwe, haikusahihishwa. Ndugu zangu nawaambia wengine tunateseka! Kuna barabara ambazo zimepandishwa hadhi za vijiji. Inatoka kijiji kwenda kijiji lakini za kwangu inayotoka katika Wilaya kwenda Wilaya nyine haipandishwi, kwa sababu ni za Lekule. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, naomba ndugu zangu, tutakuja kuleta hoja hapa tuombe Mawaziri watoke nje ya Bunge, wasiwe Wabunge. Ndiyo tutakuja kufanana upendeleo huu uishe. (*Makofi*)

Nimesemea Wizara moja tu. Ningesema Maji, ningesema Wizara nyine. Kwa hiyo, ningependa kuzungumzia barabara nyine ambayo tumeomba ipandishwe hadhi. Kuna barabara tulioomba kutoka Olmoloki mpaka Namanga. Ni barabara ya mpakani. Wenzetu wa Kenya wana barabara inayoambaa mpakani kutoka Namanga mpaka Rombo. Lakini huku kwetu hakuna barabara. Tuliomba hiyo barabara ipandishwe hadhi kwa sababu ni barabara ya mpakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wanajenga, sasa barabara kutoka Rombo mpaka Nairobi, barabara ya lami, watu ambao hawaangalii kwamba hili jimbo ni la nani. Wanaangalia maslahi ya Taifa. Hawaangalii kura, kwa sababu tukiangalia kura, tutaacha maeneo mengine. Itakuwa ni Majimbo ya Waziri tu ndiyo yanaendelea. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, hiyo barabara ya kutoka Olmoloki kwenda Namanga. Nadhani hata hiyo barabara naomba nayo iwe barabara ya Mkoa kama ilivyopitishwa na *Road Board*, ilivyopitishwa na *RCC* ya Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kusema kwamba nitaunga mkono baada ya kupata majibu ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lekule Laizer na ninaamini wapiga kura wamekusikia ipasavyo. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko na Mheshimiwa *Capt. John Komba* ajiandae.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia tangu nimekuwa Mbunge, napenda kwa namna ya pekee niwapongeze wapiga kura wangu wa Jimbo kubwa la Kasulu Mashariki. Kwa kunisa dia sana kufanya kazi katika Jimbo langu la

uchaguzi. Nawashukuru sana. Changamoto tunazo nyingi lakini tunasonga mbele kwa ari mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe pongezi kwa ndugu zetu, mlioteuliwa kushika nafasi mbalimbali katika Serikali yetu, Mawaziri, Manaibu Mawaziri, *protocol* imezingatiwa hongereni sana. Lakini nije kwa ndugu yangu Kawambwa, nikupe hongera ya pekee kabisa na ndugu yangu Chibulunje, kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii muhimu sana ya Miundombinu.

Miundombinu ni Wizara ambayo inasimamia uhai wa Taifa letu, inasimamia reli zetu, barabara zetu, bandari zetu, viwanja vya ndege, nyumba za Serikali na hata mawasiliano. Ni Wizara muhimu sana na Mheshimiwa Kawambwa wewe na Naibu wako, mmepewaa kazi kubwa. Fanyeni kazi bila kuchoka mbadilishe sura ya Wizara hii. Hii Wizara ndio kilimo, ndio viwanda, ndio uhai wa Taifa letu na kwa maneno nyingine niseme tu Wizara ya Miundombinu kwa kweli ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Kawambwa, ni Mhandisi, Naibu wake ni Mwanaharakati wa muda mrefu sana, mpambanaji, Katibu Mkuu wake ni Mhandisi mzoefu, hebu badilisheni sura ya Wizara hii iweze kweli kufanana na usasa na uleo na kwamba miradi ya maendeleo ya barabara izingatie vipaumbele vya kiuchumi ili nchi yetu iweze kuondoka hapa ilipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba na mimi niseme kwamba sisi wananchi wa Mkoa wa Kigoma, kwa kweli, tangu tumepata uhuru hii ndio bajeti yetu ya historia. Ndio bajeti ambayo sasa inatujengea barabara ya lami kutoka Mwandiga mpaka Manyovu na niseme tu hii barabara ni mkakati wa muda mrefu wa sera za *CCM* na wala sio Kambi ya Upinzani, maana wenzetu wana tabia ya kujitapa, maneno mengi.

Nirejee ukurasa wa nne wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imeeleza *Maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi* na utekelezaji wake na kamwe sio utekelezaji wa Ilani ya chama kingine. Sasa alikuja mdogo wangu hapa, Mbunge mwenzangu, yeeye! Yeeye! Yeeye! Maneno mengi, kana kwamba barabara hizi zinajengwa kama nyumba za miti. Barabara za lami zina mchakato mrefu na zinahitaji muda kuzijenga. Barabara ya Mwandiga – Manyovu, ni mkakati wa *CCM* wa tangu awamu ya tatu. Ndugu zangu wa Kigoma, msisikilize maneno ya barabarani haya, ujenzi wa barabara ya Mwandiga – Manyovu, kilomita 60.2 ni mkakati endelevu wa Chama Cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda katika jimbo hilo katika miji ya Kalinzi, miji ya Bitale, Matyazo, kunakolimwa kahawa, nikawaeleza mkakati wa ujenzi wa barabara hii ya lami. Ndugu zangu wa Kigoma Kaskazini, barabara ya lami mchakato wake ni mrefu na Mbunge wa miaka miwili hawezi kujitapa kwamba yeeye ndio kajenga barabara ya lami, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ndugu zangu wa Kigoma tuelewe. Lakini niseme kwamba sisi watu wa Kigoma kwa kweli, bajeti hii ni nzuri kabisa kwa sababu sasa imekumbuka Mkoa wa Kigoma.

Barabara ya lami Mwandiga – Manyovu, inajengwa kwa kiwango cha lami, barabara ya lami kutoka Kigoma mjini, pale *railways* mpaka Kidahwe, inajengwa kwa kiwango cha lami na barabara ya kutoka Kidahwe mpaka Ilunde – Malagarasi *bridge* nayo inajengwa kwa kiwango cha lami na daraja lenyewe la Malagarasi. *I mean*, daraja na *aproan* yake kilometra 48, pande zote mbili za daraja nazo zinajengwa kwa kiwango cha lami. Nasema tena, huu ni mkakati wa muda mrefu wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba ukurasa wa 4, 5, 6 na 7, umeeleza kwa mahsus i maelekezo ya ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia wapinzani hapa wanajigamba na orodha ya barabara ndefu kwenye hotuba yao, ukurasa wa 10, wameorodhesha barabara nyingi pale. Barabara zote zile ni barabara zimeorodhesha kwenye ilani ya *CCM*. Tena kwa sababu wanazikosea labda nisahihishe kidogo, kwenye ilani ya *CCM* hakuna barabara inaitwa Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma, haiko. Barabara hiyo inaitwa Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Kasulu. Kibondo – Nyakanazi. Sasa kwa sababu barabara sio zao hizi, basi wana tabia ya kudandia dandia mambo yasiyowahuusu na matokeo yake ndio hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliyasema hayo makusudi kwa sababu kumekuwa na upotoshaji mwingi sana hasa katika maeneo ambayo tumesubiri muda mrefu miundombinu hii. Kumekuwa na upotoshaji mwingi sana, wenzetu wanapitapita wanasema, hizi barabara Nsanzugwanko, hawesi kuzileta wala Mporogomy, ni mimi tu. Haiwezekani! Barabara wala haijengwi na Mbunge mmoja, ni Chama chake na Serikali yake. Napenda niseme haya makusudi ili kuweka rekodi sawasawa na wenzetu wa Kigoma wanatusikia na tutakwenda kuwaeleza hali halisi ya mambo ilivyo. Uzoefu wa Mbunge wa miaka miwili hauwezi kujenga barabara ya lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie barabara ya *central corridor*. Hii imesemwa sana na mpaka Mbunge, mwenzetu alishawahidi kuleta hoja binafsi kuhusu barabara hii ya katikati hapa. Niseme tu kwamba barabara hii ya Itigi – Tabora – Kigoma ni barabara ya kiuchumi na hii barabara naomba itizamwe kwa macho mawili. Hii barabara ikijengwa leo, itajenga barabara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na dhana ya kwamba tusikimbilie kujenga kila barabara, tuangalie zile barabara ambazo zina *economic impact* na zikijengwa vizuri zitajenga barabara nyingine. Hii barabara ya katikati, Tabora – Itigi mpaka Kigoma, ina umuhimu mkubwa wa aina mbili. Aina ya kwanza, ni mkakati wa kiuchumi kwa sababu nchi tajiri pekee inayotuzunguka katika nchi yetu ni nchi moja tu. Nchi ya *DRC*, nchi nyingine zote zinazotuzunguka hazina uchumi mkubwa kiasi hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya *DRC* ina mzigo mkubwa ambao mzigo huo ili ufile nchi za nje ni lazima upite Bandari ya Dar-es-Salaam, kwasababu andari ya Matadi iko mbali. Sasa ukijenga barabara hii ya Itigi – Tabora – Kigoma, kama ambavyo tumeanza sasa kuanzia Kigoma mpaka Kidahwe na pengine tukapata hata wakandarasi watatu wanne kujenga barabara hii kimkakati, kama jambo la dharura ili ku-*tape resources* zilizoko katika *DRC* ambazo ni mzigo takribani tani milioni 300, tani hizo tukizisafirisha sisi kupitia kwenye barabara zetu na reli ya kati maana yake nchi itapata takribani shilingi trilioni tatu. Sasa barabara hii itajenga barabara nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali, kwa kweli hebu rekebisheni mambo mjenge barabara hii kwa udharura. Wekeni Makandarasi hata kama ni watatu au wanenili tujenge barabara nyingine. Hizo barabara nyingine zinaweza zikajengwa tu kimkakati, lakini barabara moja ina *trigger* na inaweza ikajenga barabara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya barabara ni jambo kubwa ambalo kila Mbunge anasema. Reli ya kati imezungumzwa sana. Mimi nitoe ushauri tu, mengi yamezungumzwa kuhusu *TRL* na bughudha, usumbufu, wanaopata wasafiri. Mimi niseme tu mapendekezo mawili. Pendekezo la kwanza, hebu imarisheni usalama wa raia katika reli ya kati kwa sasa kwa udharura ili watu wasafiri kwa amani na pia msongamano kwenye treni ya reli ya kati unaweza ukaondoka kesho, kama Mheshimiwa Waziri, wewe ukikaa na watu wa *TRL* leo au kesho baada ya hotuba yako ili watu wasafiri kwa utaratibu wasisongamane na hatimaye kupata majanga na hata vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa nizungumze na hili kwa kweli nitapenda nipaye maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni barabara zinazotuunganisha sisi na nchi jirani. Kule Kigoma, tuna barabara tatu kubwa zinazotuunganisha sisi na nchi jirani. Kwa mfano kwenye ilani ya *CCM*, tumeeleza wazi kwamba barabara zinazotuunganisha na nchi jirani tunajenga kwa kiwango cha lami. *Okey*, hata kama bado, basi tuzijenge kwa kiwango cha changarawe ili zipitike wakati wote.

Kuna barabara yetu ya Makere – Nyarugusu – Herushingo – Kitanga – Burundi, nayo ni barabara ya kiulinzi, ni barabara ya kimkakati. Barabara ya Heru juu – Munyegera – Muyama – Burundi, hizi ni muhimu sana na tulishaomba kwamba barabara hizi zipewe kipaumbele na zipandishwe daraja zisiwe barabara za Halmashauri, ziwe barabara za Mkoa.

Tangu tumeomba tangu enzi za Mheshimiwa Mramba, akiwa Waziri wa Miundombinu mpaka leo, nitapenda kujua sasa *status* ya barabara hizi kuzipandisha hadhi ili ziwe barabara za Mkoa na zina sifa kwa sababu zinatuunganisha na nchi jirani ya Burundi. Jambo lingine ni rushwa katika mikataba ya ujenzi. Hili limezungumzwa sana. Hebu Mheshimiwa Waziri na wenzako hebu fanyeni kazi kwa karibu na *TAKUKURU*, ili fedha zetu katika barabara ziweze kuleta tija inayohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumzie suala la maghorofa yanayobomoka katika miji ya Dar-es-Salaam. Wenzetu wa Bodi ya Uhandisi wametulalamikia, naomba Mheshimiwa Waziri akasome katika gazeti la mwananchi la tarehe 30 tafadhalii. Kuna sababu za maghorofa kuporomoka zimeelezwa, Mwenyekiti wa *Registration Board*, Amandus Chaki, ameeleza mambo ya msingi, lakini kubwa ninalotaka kulisema ni kwamba amesema wamepeleka marekebisho ya sheria Serikalini, lakini Wizara ya Miundombinu imeyakalia. Haya maghorofa yatatuua. Naomba Mheshimiwa Waziri jambo hili aliye udharura, hiyo sheria iletwe Bungeni, pengine hata katika kipindi hiki kwa udharura ili tusiendelee kupata matataizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na mimi sasa niwapongeze timu ya mpira wa miguu ya Kigoma, timu ya Coca cola, kwa kufanya vizuri na hatimaye imekuwa timu ya kwanza kupeleka wachezaji sita wa chini ya miaka 17 Brazil, wachezaji kutoka Mkoa mmoja. Hiyo ni dhahiri kwamba Kigoma kuna vipaji nya kila aina.

Nami niungane na Mbunge wa Kigoma Kaskazini kuwapongeza *AZAKi* ya Kigoma kwa kuwa *AZAKi* ya kwanza kushinda na niseme hiyo ndiyo Kigoma, kila mara iko *number one* na ni kwa sababu tu imeshindwa kuwezeshwa kwa kipindi kirefu kilichopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nakushukuru wewe, nimshukuru Waziri na timu yake, nasema tena hebu badilishi sura ya Wizara hii. Hii Wizara ndiyo roho. Haiwezekani uzungumze kilimo, uzungumze viwanda bila kuzungumzia *infrastructure* na nina hakika Mheshimiwa Waziri, nasema tena wewe ni Mhandisi, Katibu wako ni Mhandisi na wahandisi mahiri kama ninyi tena bado vijana hebu fanyeni kazi mambo yabadilike. Yaonekane kabissa ni tofauti. Nina hakika itatujengea heshima kabisa katika nchi yetu. Kengele ya pili hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, kwa sababu hii ni bajeti ya kihistoria kwa mkoa wa kigoma. Asante sana.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITU:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 64(1) (f) na (g)

**MWENYEKITU:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 64(1)(f) na (g) kwamba Mbunge, hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine na sikutaka tu kusimama wakati Mheshimiwa, ndugu yangu, kaka yangu, Nsanzugwanko, anazungumza na ni kwa sababu ni mtu ambaye ninamheshimu sana.

Lakini katika baadhi ya yote aliyoyazungumza, sijali vijembe vyatia kiasiasa kwa sababu ni kawaida, sisi Wabunge ni wanasiyasi, lakini katika yote aliyoyazungumza amesema kwamba watu wasisikie maneno ya barabarani akiwa anafanya *reference* kwangu. Hotuba yangu bahati nzuri ipo kwa maandishi na imegawiwa kwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Nsanzugwanko, aoneshe sentensi yoyote ya barabarani katika maoni ya Kambi ya Upinzani, ambayo nimeyazungumza na kama haitakuwepo nilikuwa naomba afute kauli yake na aniombe radhi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninapokea mwongozo wa Mheshimiwa Zitto Kabwe. Kwa mujibu wa kanuni yuko sahihi, lakini nilikuwa naomba niseme kitu kimoja. Wakati, sijui Mheshimiwa Nsanzugwanko nitampa nafasi atoe maelekezo yake, lakini wakati Mheshimiwa Nsanzugwanko akichangia amechangia hotuba ya Kiongozi wa Upinzani lakini pia ame-quote mambo yanayoendelea katika Jimbo na mahali aliko. Sasa

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tu tukubaliane kwamba wakati unapochangia yako mambo ambayo ndiyo yanayoendelea ndani ya Bunge, lakini yako mambo ambayo lazima mtu atafanya *reference* kutoka katika eneo analotoka. Sasa kwa kuwa hotuba hii iliyokuwa hapa mbele imechangia pia na hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, lakini mimi nafikiri kwamba tunapotaka kupata ufanuzi ni lazima tutenganishe haya mambo mawili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninaomba kusema tu kwamba, Mheshimiwa Zitto, mchango wa Mheshimiwa Nsanzugwanko kwa kadiri ya maadili ya Kiti changu, ulihusianisha mazingira ya ndani ya mazingira ya Mbunge, alikotoka na hivyo baada ya maamuzi hayo, ninamwomba *Captain* John Komba, aendelee.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kumshukuru sana mtoa hoja hii, Mheshimiwa Kawambwa na wizara nzima ya Miundombinu.

Pia, namshukuru sana Rais, kwa kufanya mabadiliko katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Baraza la Mawaziri na kumpata Mheshimiwa Kawambwa, ambaye kwa kweli kanivutia katika kutoa hoja yake. Kwanza ameeleza ilani ya uchaguzi, amesema katika ilani ya uchaguzi yapi yametekelawa, yapi hayajatekelawa, kwa hiyo, naomba hata Mawaziri wengine watakapoanza kusimama hapa, waseme hivyo hivyo katika Wizara yake, kipi kimesemwa kwenye ilani, kipi kimetekelezwa, kipi bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna hii sikupenda sana mchango wa Kambi ya Upinzani, iliposema kwamba hatujatekeleza ilani ya uchaguzi, ama tumeweka mambo mengi zaidi kwa hiyo, tumeshindwa kutekeleza. Mimi nina hakika katika nchi hii tumetekelawa ilani ya uchaguzi zaidi ya asilimia 60 kwa kuangalia tu unaona asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ambaye atashangaa kwamba mashule mengi katika nchi hii yamejengwa kwa kipindi kifupi, hakuna atakayeshangaa vituo vya afya, zahanati, zimejengwa katika kipindi hiki, hakuna atakayeshangaa kwamba bei za mazao ya korosho, kahawa zimepanda katika kipindi hiki, barabara nyngi sana zimejengwa katika kipindi hiki na bahati nzuri katika mchango wa Upinzani, amesema mwenyewe hapa, ukurasa wa tatu: “*Kwa niaba ya wananchi wa Kigoma Kaskazini, napenda kuishukuru Serikali kwa kutimiza wajibu wake bila kujali itikadi za kisiasa.*” Wajibu gani huo? Kwa kujenga mabarabara Kigoma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namimi nasisitiza wananchi wasisikilize maneno ya barabarani, maneno ya barabarani hayasaidii sana, kwa sababu haya yanayozungumzwa hapa pia barabarani huko wanafanya mikutano Wapinzani, wanasema maneno ya uwongo uwongo tu kama haya na wakati katika maandishi wanakiri kwamba tumetekeleza ilani ya uchaguzi. Kwa hiyo Mheshimiwa Nsanzugwanko yuko sahihi kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nirudi kwenye michango yangu mimi mwenyewe. Nikianzia kwa upande wa shirika letu la ndege, kwa kweli hili shirika liko hoi, linahitaji kusaidiwa sana. Kwa sababu unajua ATC sasa hivi ina ndege tano tu. *Boeing* mbili, *Airbus* moja, *Q 300*, ziko mbili na kwa kweli hizo ndege zinatumia mafuta ambapo mafuta yake bei ni ghali sana. Kwa namna hiyo ni kwamba, hata kulipa madeni ya ile kampuni ya *South Africa Airways* ya bilioni nne, ni tatizo. Kwa hiyo mimi nilikuwa naiomba Serikali iisaidie sana ATC kuipa mtaji ili iweze kukidhi matakwa ya usafiri wa anga. Ikitanya hivyo tutakuwa tumeendelea kutekeleza ilani yetu ya uchaguzi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye barabara zetu za Mbinga. Tunaishukuru Serikali kwa kupitia *MCC* kutusaidia na kutupa mradi huu wa barabara kuanzia Namtumbo mpaka Mbambabay na kwa taarifa ambazo ninazo ni kwamba tayari mambo yameanza kutoka Songea, Peramiho kwenda Mbinga na kutoka Namtumbo kwenda Songea. Kwa namna hiyo, tunaishukuru sana Serikali. Lakini liko tatizo la bandari. Bandari ya Dar-es-Salaam sasa hivi inahemewa, matumizi ya bandari ya Mtwara ni muhimu sana. Lakini unapohimiza matumizi ya bandari ya Mtwara, ili bidhaa ziende Mtwara, zikitoka Mtwara ziende wapi?

Nina hakika zikitoka Mtwara ziende Kusini mwa Afrika, *land locked countries* zilizo Kusini mwa Afrika. Nchi kama Malawi, nchi kama Zambia, nchi kama Kongo Kusini, sehemu za Lubumbashi, Botswana, Msumbiji, nchi zaidi ya sita au saba, lakini zikifika Mtwara, hazijafika huko ninakokusema, lazima bandari ya Mtwara uihusianishe na bandari ya *Mbambabay* ambayo ndio itakuwa kiungo kutoka Mtwara *Mbambabay*, *Mbambabay* na kuelekea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa kweli Bandari ya *Mbambabay* inatia huzuni sana. Ni jina refu, mtu mwengine ambaye hajafika *Mbambabay* atafikiri kweli hiyo bandari ni kubwa. Hakuna bandari pale! Pale kuna shimo tu refu, maji mazuri sana

watu wanakuja mpaka kwenye ufukwe wanapakuwa bidhaa lakini hakuna bandari inayoitwa bandari ya *Mbambabay*.

Kwa kweli, hata tukiangalia bajeti ya mwaka huu kwa Bandari ya *Mbambabay*, Serikali imetoa shilingi milioni 50 tu. Shilingi milioni 50 utajenga gati gani? Imeandikwa kujenga gati, gati gani utajengwa kwa shilingi milioni 50? Na mnataka mwongeze uchumi kupitia nchi hizi ambazo hazina bandari ya bahari ama ya maziwa. Sasa shilingi milioni 50 itabeba mzigo gani wa kupeleka huko?

Kwa hiyo, mwaka huu nitasamehe, lakini ninaomba wakati mwengine, mwakani kama tunataka kuinua uchumi kweli kweli ni lazima tuzingatie Bandari ya Mtwara, kwa uzito wake na tuzingatie Bandari ya *Mbambabay* kwa uzito wake ili tuweze kuinua uchumi kupitia barabara hizo, ama sivyo barabara ya lami kutoka Mtwara mpaka *Mbambabay* itakuwa haina faida. Ukiondoa watu wa kusafiri kwa mabasi, tunasafiri mpaka sasa kwa shida, lakini tunasafiri. Lakini mazao hayawezi kusafiri, vifaa vyta ujenzi haviwezi kusafiri, mitambo mbalimbali haiwezi kusafiri. Kwa hiyo, ninaomba tuisaidie bandari ya Mtwara, sambamba na bandari hii ya *Mbambabay* ili tuweze kusafirisha bidhaa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni meli. Angalau kule Kigoma kuna *MV Liemba*, Ziwa Victoria kuna *MV Victoria*, lakini ukienda ziwa Nyasa ni huzuni kabisa. Hizo zinazoitwa meli sio meli ni boti. Kulikuwa na boti tatu zamani miaka ya 1970. Kulikuwa na boti inaitwa *MV Iringa* na *MV Mbeya*. *MV Mbeya*, ikazama, *MV Iringa* imekwisha, imebaki meli moja ya mizigo na hiyo ndio meli ya usafiri na lile ziwa lina mawimbi makubwa kama bahari. Inakuwa shida wakati mwengine unafikiri juu ya hii meli, itafika kwenye kituo cha pili! Lakini Mungu yupo na wale watu kule ndio maana wanapona, lakini kwa kweli hali ya usafiri wa Ziwa Nyasa, ni mbaya sana. Naomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili na atoe kipaumbele angalau wale watu wapate usafiri wa uhakika katika ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uwanja wa ndege wa Songea. Naona wengine wanataka tu tuimarishe viwanja vya Dar-es-Salaam, sijui vya Kigoma, Bukoba, Mbeya, wanasahau Songea, halafu wanataka Songea tuvutie wawekezaji. Songea kama hamjui wengine ni kwamba ni kilometra 1,200 kutoka Dar-es-Salaam. Kilometra 1,500 kutoka Dodoma kwenda Songea. Mwekezaji gani huyo atakayetoka Dar-es-Saalam kwa barabara kutoka saa 12:00 aingie saa 2:00 usiku awe na hamu ya kuwekeza *Mbambabay*, Lituhi, Liuli na maeneo mengine ya Songea? Mwekezaji gani huyo? Hayupo!

Kwa hiyo, kama hatutaimarisha kiwanja chetu cha ndege na kiwanja chetu kimeimarishwa, katika viwanja vizuri katika nchi yetu kimojawapo ni cha Songea. Ni kiwanja cha lami chote, hakuna vumbi, ndege ikitua ni lami *chirrrrrrr*, mpaka unafika, lami tupu, hakuna vumbi. Lakini kwa nini ndege hazitui Songea? Ni kitendawili ambacho sijui nani atategua. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Kawambwa, afike Songea aone kiwanja kile halafu aone namna gani ambavyo watu wanaumia. Wametengeneza kiwanja vizuri kwa kujitolea na Serikali imetoa pesa kidogo lakini hakitumiki. Ni kama

*White elephant* ya maonyesho tu imewekwa mahali pale. Naomba mtumie kikamilifu kiwanja cha Songea. Mtu akifika Songea, mzalishaji mali au mwekezaji atapata raha ya kwenda sehemu nyingine za Ruvuma. Lakini hawesi kuja kwa *bus* halafu ukamtegemea kwamba kesho aende akatafute maeneo ya kuwekeza. Tuna vivutio vingi sisi, tuna ziwa Nyasa zuri tu, tuna mito mizuri tu, tunamadini mengi tu, lakini mtu hawesi kwenda kuwekeza kule. Tuna *Selous*, mbuga za wanyama kule, lakini atakwendaje *Selous*? Atakwenda kwa *bus*? Haiwezekani, naomba tuimarishe viwanja vyetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi ya mwaka 2005 ya kutusaidia umeme katika mji wa Mbanga, kero ambayo ilikuwa ni ya kudumu katika mji wetu. Leo Mbanga tuna umeme wa uhakika kuliko maeneo mengi katika nchi yetu. Tunamshukuru sana Rais na kupitia hiyo nimshukuru pia Waziri wake wa Madini na Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, dakika zilizobaki ni tano na dakika hizi tano hazitaweza kutosha kwa msemeji yejote. Basi ninaomba tu nitoe matangazo mafupi kabla sijasitisha shughuli za Bunge.

Kuna ufunguo wa gari, mwenzetu mmoja alisahau ufunguo wake kwenye *security point*, kwa hiyo, kama kuna mtu amepoteza ufunguo, atawaona Makatibu wetu waweze kumpa maelekezo. Halafu labda ningesoma pia orodha ya wachangiaji watakaoanza kuchangia jioni ili waweze kuijandaa na kuwahi kwenye ukumbi wa Bunge. Atakayeanza ni Mheshimiwa Shah, kama atakuwa amemaliza shughuli za kukutana na wageni wetu wa Bunge, kutoka Kenya. Kama atakuwa bado ana shughuli hiyo na wote tunafahamu kwamba Mheshimiwa Shah, ni Kamishna wa Bunge letu, kwa hiyo, yuko na makamishna wenzake kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile atakayefuata baada ya Mheshimiwa Shah, atakuwa Mheshimiwa Nimrod Mkono, lakini kama Mheshimiwa Shah, hatakuwepo, basi Mheshimiwa Nimrod Mkono, ujiandae kwa sababu utaanza. Atakayefuatia baada ya Mheshimiwa Nimrod Mkono, atakuwa Mheshimiwa Brigedia General Hassan Ngwilizi. Kwa hiyo, hao ndio wasemeji wetu watakaoanza leo jioni, saa 11:00.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaomba nisitishe shughuli za Bunge kwa asubuhi ya leo na tutaonana tena saa 11:00 jioni.

(*Saa 06:53 mchana Bunge, lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji wa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu wakati alipokuwa akiwasilisha leo asubuhi na aliposoma bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya Wizara yake, sasa mchana huu wa leo tutaanza na Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah na Mheshimiwa Nimrod E. Mkono ajiandae.

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ya kuweza kuchangia kwa mchana huu wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hapa na kutupa afya njema katika kuhakikisha kwamba tupo hapa na tunachangia hoja hii ya Wizara ya Miundombinu ambayo ni Wizara nyeti kabisa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Mafia nasema ahsanteni sana Serikali na sina budi kutoa shukrani kwa Serikali kupitia Wizara hii kwa yale yote ambayo wameamua kuyafanya katika Wilaya ya Mafia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia katika kusoma *Quran* kidogo, hivyo nafahamu *Quran* kwa uchache na baadhi ya hadithi zilizosemwa na Mahalifa wetu kupitia kwa Mtume kwa yale aliyoyafanya Mtume wetu, *Swalallah Alayhi Wasallam*. Kwa sababu kuna hadithi moja inayosema mara nyingi napenda kuisoma kwamba: “*Man lam yashkur nnasu la yashkur-llah.*” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeote asiyeweza kumshukuru binadamu mwenzake kwa jambo lolote jema lile ambalo amelifanya juu yake, basi hata Mola wake ambaye haonekani hawezi kumshukuru. Kwa hiyo, kwa kupitia hadidhi hiyo nasema na kushukuruni na *inshallah* na ninyi Mwenyezi Mungu atakujalieni mambo yenu yatakwenda vizuri na yanyooke kwa njia za kheri ninyi pamoja na vizazi vyenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hofu kubwa sana kuhusu baada ya kuvipitia vile vitabu vya mwanzo vya bajeti hii ya Serikali, lakini nimefurahi kwamba mwaka jana lile *tractor (grader)* ambalo mmeahidi lilishanunuliwa na liko Kibaha linasubiri kusafirishwa kwenda Mafia. Nasema ahsante sana. (*Makofi*)

Lakini pia mwaka huu Serikali ilipoona umuhimu wa lile *grader* kutofanya kazi peke yake bila kupata shindilia ikaamua kutupatia tena milioni 71 na laki kadhaa kwa ajili ya ununuzi wa lile *vibrator machine (compactor)*. Kwa hiyo, narejea tena kusema shukrani na Mwenyezi Mungu atakuzidishieni.

Ninayasema haya kwa nini? Nayasema haya kwa sababu hata Mwenyezi Mungu aliyetuumba anatuambia hivi:

“*Audhubillah mina shaitwan rajiim. Waama biniimat rabika fahdith*”, anasema, ama neema za Mola wenu zitangazeni. Kwa hiyo, kwa kila jambo jema lile ambalo

linafanyika ni wajibu kwamba tuliseme na litangazwe, jamii ifahamu na dunia nzima kwa ujumla iweze kuelewa yale mema yaliyofanywa na Serikali. Isiwe makombora tu yanapigwa na mema yapo. Kwa hiyo, tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani nyingi sana hasa kwa watu wa Mamlaka ya Bandari, awamu ya kwanza ya upembuzi yakinifu, umeshapita, fidia imeshalipwa, uwanja umeshasafishwa na sasa tunasubiri ujenzi. Nitakachomwomba tu Mheshimiwa Waziri aseme lini ujenzi huu utaanza? Naamini pesa zipo, pesa za mwaka jana shilingi bilioni nne zipo na kwa hekima za watu wa *TPA* kupitia kwako Mheshimiwa Waziri kwamba kuna shilingi bilioni nne nyingine, kwa hiyo, shilingi bilioni nane zinatosheleza kabisa kuanza kazi na ninaamini hata asilimia 75 kama sio asilimia 85 ujenzi wa gati itakuwa pesa zake zipo. Kwa hiyo, nasema shukrani na ninakushukuru sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena niseme upande wa uwanja wa ndege. Narejea tena kusema nashukuru. Uwanja unakwenda vizuri, uwanja unajengwa lakini nilikuwa nataka nifahamu jambo moja kwamba lini yule Mkandarasi atatukabidhi na lini awamu ya pili ya mradi huu utaweza kuanza ujenzi ule kupitia pesa za *MCC*? Lakini ninaamini baada ya kesho Mheshimiwa Waziri kumaliza na kufanya *winding-up* shughuli yake, basi naamini kwamba pesa zetu zile za *MCC* zitaanza kusambazwa na ujenzi wa uwanja wa ndege kama ulivyoahidi na hata alivyosema Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kwamba uwanja wa ndege utajengwa, basi ninaamini utakamilika kwa zile siku ambazo mmeweza kuzipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi sana ya kusema kwa sababu leo nimesimama kutoa shukrani na msione taabu nitamaliza dakika zangu 15 kwa kutoa shukrani tu, kwa sababu ni haki yangu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo kuna aya moja inasema hivi: “*Ahiba l-nnas ma tuhib linafsika.*” *Ipende nafsi yako unasikia eeeh! Mpendelee mwenzio kama unavyoipenda nafsi yako.*”

Kwa hiyo, nasema nawashukuruni sana na ninaishukuru Serikali, Mheshimiwa waziri Mkuu pokea salamu hizi kwa niaba ya wananchi wa Mafia kumpelekeaa Mheshimiwa Rais pamoja na jamii nzima ya Serikali kwa wale waliokuwepo sasa na hata wale waliokuwepo katika Bunge lile lililopita yaani awamu iliyopita kwa sababu ndiyo na wao walianza katika kutoa pesa na kusema kwamba tunashukuru na tunaamini kwamba shughuli yetu hii itaweza kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Mafia ni mbaya sana, lakini ninaamini katika kipindi hiki cha uchaguzi huu ukimalizika mpaka 2010 hali itakuwa nzuri na hao wanaojitayarisha sijui watakuja kusema nini jipya ambalo wao watakuja kulileta katika dunia ile ya Mafia kwamba wao watabadilisha nini. Kama kuwabadilisha watu au kufanya nini, lakini naamini mengi yale ambayo yanawaumiza wananchi basi yatakuwa yametatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa aya. Naomba ninukuu na kusema kwamba haya ni mambo yaliyotamkwa ndani ya *Qur'ani* Mungu alituambia baada ya kumwogopa yeye tumtii Mtume wake, tuitii Serikali na kuwatii wazazi wawili. Kwa hiyo, hata uongozi huu tunapaswa kuutii na kuushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna aya inasema hivi: “*Walain shakartun laazida-nnakum*”, yaani mkinishukuru nitawazidishieni. “*Walain kafartum inna adhabu la shadidu*” na mkinikufuru au mkinikanusha, basi adhabu kali juu yake itakufikieni.

Sasa mimi maana ya kusema aya hii ni kitu gani? Ni kwamba ninashukuru kwa sababu yeye anasema tukimshukuru atatuzidishia. Kwa hiyo, nami nawashukuru. Sasa shukrani hii isiwe mwisho wa shughuli zile za matatizo mengi yaliyokuwepo pale Mafia, lipo tatizo moja sasa ndiyo ninalileta ili kwa kupitia shukrani hizi na aya hii mwone kwamba ni wajibu wenu Serikali katika kulitenda lile tendo ili liweze kukamilika na adhabu ile iweze kupungua.

Tuna tatizo la barabara ndogo tu kipande cha Kilomita mbili kutoka Kijiji cha Jimbo kwenda Kijiji cha Banja. Hivyo vijiji vya Banja na Jojo ni visiwa. Sasa pana jangwa linalopita maji chumvi, wakati wa bamvua, yaani wakati *high tide* magari huwa hayawezi kupita, kwa hiyo, tumeomba lijengwe tuta na Mheshimiwa Rais alipokuja kutoa shukrani na kuangalia shughuli za kimaendeleo za Wilaya ya Mafia alifika pale akaongea na wananchi na akaahidi kwamba Mungu akipenda, basi bajeti hii tutahakikisha hili eneo linatengezwa, ni kilomita mbili na ni tuta tu la kuweka udongo, kuliweka imara. Sidhani kama litachukua hela nyngi sana, lakini kutockana na uzito wa tuta lile, Halmashauri yetu ya Wilaya ya Mafia haina uwezo wa kuhimili kishindo cha ujenzi wa tuta lile.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali upande wa ujenzi wa barabara, basi itusaidie na hata Meneja wa Mfuko wa barabara nilimpeleka Bwana Haule alipaona na akasema, basi Mheshimiwa Rais akisema, basi hiyo kwetu sisi ni amri. Sasa Rais kasema kupitia kwake leo nakuambieni kwa sababu ninyi mlikuwa hampo, basi iwe amri kupitia kwake kwenu ninyi muweze kutusaidia kutekeleza yale ambayo Mheshimiwa Rais ameyasema ili wananchi wasiweze kupata adhabu ya kupita wakati wa majimana tu, na wakati wa bamvua kushindwa kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasimama tena mbele yenu hapa kwa niaba ya wananchi wa Mafia. Mheshimiwa Waziri, nakuomba ninyi na Viongozi wote wa Serikali pamoja na Mtukufu Rais wetu kuwaombea kila la kheri na Mwenyezi Mungu atakuondolea matatizo yote na Mwenyezi Mungu atakunyoosheeni.

Najua ninyi hamuwezi kusema, tunafahamu mna kero kwenye majimbo yenu, lakini Serikali kwa kupitia hekima zake itaweza kutekeleza yale ambayo ninyi yamekuwa kero katika majimbo yenu, basi waone kwamba wana wajibu wa kuyatekeleza kwa kuwa hamna kauli ya kusema na hamna mtu wa kuwasemea. Kwa hiyo, mimi nasema Mungu atasaidia na tumwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba awaone wale wanaoshindwa

kusema, basi waweze kuangaliwa pia majimbo yao maana yake wanaonekana kama vile hawasemi kitu, kumbe wako kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema nawashukuru sana Viongozi wote wa Mamlaka ya Bandari, Menejimenti Kuu, Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi wake na Watumishi wote. Namshukuru Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, namshukuru sana na *Engineer* wake Bwana Suleiman, Bwana Tesha - Mkurugenzi Mkuu na wote wale ambao wako katika Idara hii ya Viwanja vya Ndege na sitaacha kumshukuru pia Meneja wa Mfuko wa Barabara pamoja na Bodi nzima na ninaishukuru kabisa Serikali kwa heshima zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, laiti kungekuwa na uwezo wa kusema zaidi ya asilimia mia, basi sijui unaweza ukajumlisha wote wanaosema wanaunga mkono, zizidishe mara kumi, nasema nimeziungu mara milioni kuliko hiyo mia mnayosema. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nawashukuru, naishukuru Serikali na *inshallah* na wananchi wa Mafia semeni Serikali inatujali. Matatizo ya Zahanati zitnjengwa, msiwe na wasiwasi tumbakisha Zahanati tano tu, Zahanati zinakuja na ahadi zote kama hatukuzitimiza kwa asilimia mia, basi asilimia themanini nakuhakikishieni kauli zangu nilizozitoa kama Mbunge, kauli alizozitoa Mheshimiwa Rais kwa maana ya pamoja na Waheshimiwa Madiwani wenzangu nawachukulia jukumu hilo kwamba tutatekeleza na Serikali yetu itakuwa na nia ya kukamilisha ahadi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na hili halina umuhimu sana, lakini kwa sababu yuko mbele yangu, nasema naomba Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi au Naibu wake waende Mafia tukazungumze na wavuvi kabla ya kusoma bajeti yake. Kuna tatizo kubwa kule, watu hawaendi baharini, watu wana njaa, kumekuwa na wizi. Katika hili. Nasema nafikisha ujumbe, naomba Mheshimiwa kwa heshima kubwa atusaidie, huyu mtu niende naye ili tuweze kumaliza tatizo dogo lililokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru na wewe Mwenyezi Mungu atakujalia salama. Ahsante sana. (*Makofit*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninamshukuru Mheshimiwa Shah kwa mchango wake, lakini kabla sijamruhusu msemaji anayefuata, Waheshimiwa Wabunge naomba nitambue uwepo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa takribani siku kadhaa, hatukuwa naye hapa Bungeni na alikuwa katika shughuli maalum za kikazi kulingana na majukumu aliyopewa na Mheshimiwa Rais lakini tunafurahi kwamba leo amerejea tena na tuko naye hapa. Karibu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini mchana leo kabla sijasitisha shughuli za Bunge, nilipokea taarifa kutoka kwa *Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani na yeche aliniarifu kwamba Kiongozi wa Kambi ya Upinzani atakuwepo Bungeni leo jioni. Kwa hiyo, naomba kutambua uwepo wa Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Naomba niwakaribishe sana.

Baada ya tangazo hilo fupi sasa, naomba tuendelee na msemaji anayefuata, naye ni Mheshimiwa Nimrod E. Mkono. Karibu!

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi kama hii niweze kuchangia katika bajeti hii ya ujenzi ambayo ni muhimu sana katika nchi nzima.

Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa Musoma Vijijini ambao wanani pa ushirikiano mkubwa sana na wa karibu kwa miaka saba sasa, wanafanya kazi usiku na mchana, mkono kwa mkono, kama wanansikia, naomba Mungu awaweke salama, vizuri kabisa, tufanye kazi, tumalize kabla kipindi hakijakwisha.

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu na ni mara yangu ya kwanza kusimama na kumpongeza Waziri Mkuu kwa kuchukua nafasi nzuri na ameianza kwa kasi mpya tena na mazoea ambayo sio ya kawaida. Nampongeza na ninadhani atatuongoza na kutufikisha vizuri katika mwaka 2010.

Baada ya kusema hivi, narejea kwenye hoja iliyonifanya nisimame. Mimi nasema kwa sasa siungi mkono hoja hii. Narudia tena siungi mkono bajeti hii mpaka nitakapopata maelezo ambayo naomba Waziri ayashughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameanza kwa kusoma bajeti yake kwa kutaja ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na utekelezaji wake na amegusia jambo nyeti kweli CCM kama ikiahidi kitu ni lazima itekeleze. Sasa kwangu Musoma Vijijini ahadi iliyopewa ya kwanza ya mwaka 1995 ndani ya ilani ya Chama cha TANU miaka hiyo, mwaka 1975 kuhusu Barabara ya kutoka Musoma kwenda *Fort Ikoma* mpaka leo haijashughulikiwa. Hiyo ilikuwa ni Ilani ya Chama na walihidi watafanya barabara hiyo wakati Marehemu Baba wa Taifa bado yupo, wakati ahadi hii inatolewa mimi nilikuwa ndiyo namaliza Chuo Kikuu, leo nataka kustaafu na hiyo barabara haijaanza hata kupimwa.

Sasa kama kweli tunasema Ilani ya Chama inatekelezwa mia kwa mia, nami kwangu nasema hapana, wananchi wanasema haijatekelezwa kwa miaka 45 itakuwaje niunge mkono bajeti hii leo? Mpaka mniambie: Je, mmesahau?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajerumani walijenga barabara kutoka Musoma kwenda *Fort Ikoma*, miaka hiyo ya Wajerumani, waliona umuhimu wa Barabara hiyo, walijenga na *Fort* kule. Tangu Wajerumani waondoke, Serikali ya CCM na Serikali ya TANU haijafanya chochote wakati huu, nitawaambiaje wananchi wangu? Barabara inayopita Butiama imekufa sasa wananchi wao wenye we ndiyo wanahangaika kulima barabara kutoka Makutano kwenda Butiama, imekufa. Sasa nitaungaje bajeti hii na kwa misingi ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeunga ukurasa wa 9 nitankuu kama alivyosema:

“Mheshimiwa Spika, barabara zinazoendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu ni nane, kama ifuatavyo: Musoma – *Fort Ikoma*”. Anasema: “Kilomita 64”! amezipata Kilomita 64 kutoka wapi? Musoma mpaka Butiama ni Kilomita 40, Musoma hadi Ikizu ni kilomita nyingine 20 zinafika kilomita 64, *Fort Ikoma* ni zaidi ya kilomita 100.

Sasa kama Mheshimiwa Waziri mwenyewe hajui hizo kilomita ni ngapi kutoka Musoma kwenda *Fort Ikoma* itakuwa ni usanii ama ni nini? Hata kama hujui umbali gani ina maana hata barabara yenye hujui iko wapi. Nataka nipaye maelekezo na ufanuzi kabisa hizo ni kilomita ama maili? Ni kilomita 64 ama ni maili 64? Haziwezi kuwa chini ya kilomita 70.

Lakini pia anazungumzia juu ya upembuzi yakinifu, siyo ujenzi wa barabara, lakini huko nyuma, mwaka hadi mwaka bajeti ilikuwa inasema Barabara ya *Fort Ikoma* mpaka Musoma itajengwa, itajengwa, itajengwa na itajengwa. Mwalimu walimauhidi mpaka leo hayupo, lakini barabara haijajengwa. Sasa wewe unaniambiaje Mheshimiwa Waziri? Unasema niunge bajeti hii ama unafuata kipengele hicho? Hiyo ndiyo kazi kubwa ninayotaka kujua.

Lakini pia barabara tuliyoahidiwa ya kutoka Bunda inapita Ikizu, inakwenda *Fort Ikoma* inaunganika na ile ya kutoka Musoma kwenda Butiama, kwenda Ikizu na inaunganika kwenda *Fort Ikoma* na huko Serengeti ikifika tuliahidiwa pia tutajengewa uwanja wa ndege. Kwa bajeti hii sisikii chochote kinachozungumziwa juu ya uwanja wa ndege, hakuna.

Sasa Mkoa wa mara uko jirani kabisa na Kenya na Uganda, upande wa kushoto ni Ziwa, wananchi wetu wanahangaika sana kwa kuuza mali zao na bidhaa zao. Hawawezi kwenda Arusha kwa kuwa pale kuna wanyama na tumeambiwa wale wanyama usiwapige wala usipitishe barabara pale. Barabara pekee ya kutuleta Dar es Salaam ni mpaka upitie Kenya. Tukiwa na mahindi ya kuuza ni lazima tupite Sirari, ukifika Sirari unakutana na Askari wanalinda usipeleke bidhaa zako. Sasa wananchi wapeleke wapi bidhaa zao? Hatuna barabara wala ndege kwa miaka 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii bajeti ina maana gani? Nimesikia upande wa upinzani wanasema tuanze kuangalia kwenye *connectivity* tuone nchi na watu wa miundombinu ni sehemu gani tuweze kufiti vizuri katika hali ya leo. Lakini sikusikia hata wao wanataja Musoma. Hata wapinzani pia Musoma hawajui. Hawajui kabisa Musoma kuna Baba wa Taifa pale tulimzika, hawajui, lakini wanazungumza juu ya Mtwara, Ujiji na kadhalika.

Lakini pia naambiwa niunge mkono bajeti hii mia kwa mia, nadhani nataka maelekezo kwanza ama maelezo mazuri kabla sijasema natoa shilingi kwako Waziri wewe ili uniambie vizuri. Najua Wizara ni mpya kwako na wewe ni rafiki yangu tunaelewana vizuri sana, lakini nadhani safari hii kuna uwezekano ukakosa mshahara. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona bajeti sehemu nyingine imeanza kusemewa vizuri, kuna ahadi ya reli kutoka Tanga kwenda Mara. Nasikia hiyo, lakini itapita wapi sikuelezwa maana kuna wanyama pale na Wazungu wanasema hakuna reli kupita pale. Mtaipitisha wapi? Kenya nao wanashabikia kweli maana wao wanataka kutoka Mombasa iende ipeleke bidhaa Uganda na sehemu jirani. Je, watu wa Mara mnasemaje? Hatuna Reli, hatuna barabara wala uwanja wa ndege, miaka 45. Nataka maelezo mazuri.

Baada ya hapo naomba maelezo ya kina. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nimrod E. Mkono. Nafikiri Makofi haya yanaashiria kwamba Wabunge wanakuunga mkono katika hilo. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge baada ya kuunga mkono hoja hiyo ya Mheshimiwa Nimrod Mkono tumsikilize sasa Mheshimiwa . Brg. Gen. Hassan Athumani Ngwilizi na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya.

**MHE. BRG. GEN. HASSAN ATHUMANI NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo amewasilisha hoja yake, nami naamini kwamba kulingana na fedha tulizokwishampatia katika Wizara yake, mipango yake itaweza kutekelezeka. Kwa hiyo, naomba nasema moja kwa moja naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Pia nachukua nafasi hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa uteuzi wake, lakini vilevile kwa alivyowasilisha hotuba yake ambayo ilitoa picha ya utekelezaji wa Serikali katika kipindi hiki kijacho. Ilikuwa ni nzuri imejieleza vizuri na ninaamini inakidhi mahitaji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kukubali kuunda Tume ya Mipango. Tume hii itasaidia kutoa dira ambayo tumekuwa tukiizungumza tu. Sasa nadhani tutapata utaratibu mzuri wa utekelezaji wa mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba nianze sasa kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Nawapongeza wananchi wa Jimbo la Mlalo kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kujilettea maendeleo yao wenye. Nasema kwa kujilettea maendeleo yao wenye kwa sababu kwa wengi ambao hawajafika eneo lile, Mlalo ni mwisho wa safu ya milima Usambara. Mara nyingi watu wanapofika Lushoto wanadhania wameshafika Mlalo. Hawajafika Mlalo. Wako mwisho kule lakini Mlalo kuna maendeleo. Maendeleo yale yametokana na juhudzi za wananchi wenye kwa asilimia 90, kama *input* ya Serikali pale labda ni asilimia 10. Kwa hiyo, lazima tuwapongeze watu wa Mlalo kwa juhudzi zao hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna shule, tumejenga shule za kutosha, watoto wetu sisi wanapomaliza darasa la saba hatuna haja ya kuhangaika sana, madarasa tayari

yapo. Walimu wanajitahidi katika mazingira magumu, lakini naamini kwamba wataendelea kuongeza juhudzi zao. Ndugu zangu watu wa Mlalo hawapo nyuma kwa sababu wanajua maendeleo ni lazima wayalete wenyewe. Nawapongeza hasa ndugu zangu wa Kata ya Shume, wanajua nini maana ya elimu na ni Kata peke yake sidhani kama kuna Kata nyingine katika nchi hii ambayo wamediriki kujenga sekondari za wananchi saba katika Kata moja. Hii ni kwa sababu ya kujua wajibu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa juhudzi za wananchi ni lazima vilevile tuziunge mkono Kitaifa! Kwa ndugu zangu wa Mlalo wanapoomba mara nyingi kuungwa mkono ni katika ujenzi wa barabara. Jimbo la Mlalo kama ilivyo Wilaya ya Lushoto ipo milimani Maeneo ya milima ni maeneo maalum kama ambavyo tumewahi kusema barabara ambazo zipo katika maeneo ya tambarare ikiharibika mtu unaweza kutafuta eneo la kupitapita na ukapita, lakini maeneo ya milimani barabara ikijifunga, basi huna njia nyingine ya kufanya ni lazima utengeneze hapo ndiyo uweze kupita. Kama hutengenezi hupiti. Kwa hiyo, hiyo ndiyo sura ya hali ya barabara zetu zilizo katika Wilaya yetu ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Mhandisi wa barabara *TANROADS* wa Mkoa wa Tanga anajitahidi sana. Kwa hilo, tunapongeza sana, lakini ili aweze kufanya kazi yake vizuri ni lazima Serikali iangalie maeneo haya ambayo ni maalum ya milimani kwa jicho la pekee. Nashukuru kwamba barabara ya Lushoto hadi Mlalo imetengenezwa sasa hivi angalau inakidhi, kwa wakati huu wa kiangazi, lakini mvua zinaponyesha tunarudi ‘A’ kwa sababu maji yanazoa makalvati na usumbuwa wa usafiri unarudi pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Malindi kwenda Tarafa ya Mtae inapitia Kata ya Rangwi na Kata ya Sunga. Najua kwamba fedha zimetengwa kidogo, lakini bado haijaanza kutengenezwa. Tunaomba *TANROADS* kwa sababu ni barabara ya Mkoa waharakishe matengenezo kwa sababu kama nilivyosema wakati wa mvua barabara kule zinajifunga, kwa hiyo, muda wa wananchi kusafirisha mazao yao kirahisi ni wakati huu wa kiangazi. Sasa tusipozitengeneza haraka wakati huu, mvua zitatukuta tena mwezi Oktoba na wananchi hawataweza kusafiri kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kutokea Lukozi kwenda Viti kuitia Manolo, nayo hii ni ya Mkoa. Eneo lile la Manolo lipo katika hali mbaya, nayo tunaomba itengenezwe kwa haraka iwezekanavyo. Lakini kuna barabara ya Mlalo kwenda Mng’aro, hii inashuka Mlalo *Escarpe*, barabara hii Mkoa uliomba ipandishwe daraja. Maombi yapo Wizarani. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha hoja yake, atueleze hatma ya barabara hii kwa sababu kwa hali ya barabara ile inapanda *escarpment* ile kwa kilomita kumi na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazotengwa kwa Halmashauri kwa ajili ya barabara hazitoshelezi na mara nyingi unakuta mvua zinaponyesha mpaka msimu unaofuata magari hayapiti. Barabara ile ni muhimu kwa sababu watu wa Mlalo wanaitegemea kwenda kwenye eneo la tambarare ndiko wanakolima, sasa isipopitika maana yake ni lazima wapandishe mazao yao kwa kichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atupatie jibu: Barabara hii imekwishapandishwa daraja kama ilivyoombwa na Mkoa au bado? Kama bado, kuna sababu gani? Kwa sababu sisi Wilayani tukishazungumza na Mkoa, tunaamini kwamba Mkoa ndiyo unelewa vizuri na kazi ya Wizara ni kukubaliana na Mkoa. Sasa kuna mtaalam gani mwingine huko katika Wizara ambaye anadhani kwamba anajua vizuri zaidi kuliko uongozi wa Mkoa wa Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaje barabara. Najua hii siyo ya *TANROADS*, lakini kwa vile watu wa Jimbo la Mlalo wanansikiliza, watataka kujua nasema nini kuhusu barabara hii. Ipo barabara inayotakiwa kutoka Kata ya Mbaramo kwenda Kata ya Mlalo, ni barabara fupi ambayo itawaunganisha watu wa Kata ya Mbaramo kwenda Makao Makuu ya Wilaya, inahitaji kama kilomita kumi na sita kupita kwenye msitu. Kinachogomba katika barabara hii ni kwa sababu Wizara ya Maliasili wamesema eti vyanzo vya maji vitaharibiwa, lakini barabara ile iliombwa na wananchi na Halmashauri yao ikakubali, ikaenda Mkoani na Mkoa wakaomba Taifani na Wizara ya Maliasili haijatoa kibali hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wa Maliasili atakapowasilisha hoja yake, naomba atueleze hatma ya barabara hii ni nini? Imebidi niingize hapa kwa sababu tunazungumzia masuala ya barabara na ni barabara muhimu, inatakiwa kuwashudumia wananchi wengi zaidi ya elfu kumi kule, sasa kuwaacha wananchi wale bila ya usafiri wa uhakika sio busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ipo barabara ya kutoka Lushoto kwenda Magamba ambayo Serikali ilikwishaahidi itajengwa kwa kiwango cha lami. Zilikuwa ni kilomita sita tu na ilianza tayari kujenga kilomita hizo, mpaka hivi sasa kilomita tatu zimeshatengenezwa, lakini kiwango ama kiasi cha fedha kinachotolewa kila mwaka kinasikitisha. Zinatolewa fedha za kutengeneza nusu kilomita au kilomita moja kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Lushoto ni milimani, huyo mkandarasi ambaye anahitaji kufanya *mobilization* ya vifaa aje atengeneze nusu kilomita ama kilomita moja fedha zote zilizotengwa zitatumika kwa ajili ya *mobilization* tu. Kwa hiyo, tunaomba barabara itengewe fedha za kutosha ili ikamilike ni kilomita kumi na mbili tu mpaka pacha ya Magamba kwenda Mlalo na Magamba kwenda Viti.

Nia ya barabara ile ilikuwa itoke Lushoto ifike angalau eneo la Ikulu pale Lushoto. Ikulu ya Lushoto ni mojawapo ya Ikulu ndogo ambazo ni nzuri katika Tanzania hii na viongozi wetu wanapenda kufika kule. Sasa haiwezekani viongozi watoke na lami kutoka huko wanapotoka mpaka Lushoto wanaingia kwenye vumbi, ndiyo mantiki ya kutengeneza barabara ile. Kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Waziri amesikiliza maombi haya ya watu wa Lushoto na hususan Jimbo la Mlalo kwa sababu nao vilevile wanayo haki ya kupata huduma ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wangu uliobakia nizungumze kwa ujumla tu. Tumezungumza kwa kirefu sana mahitaji ya kuunganisha barabara katika nchi yetu, reli na bandari. Hivi sasa hata ukitaka kurudia tunahitaji reli ya Mtwara kwenda Songea kupitia Masasi tunarudia tu, lakini kama unavyoona, haipo katika mpango kabisa. Tunahitaji reli ya Tanga *line* iimarishwe. Mtu ambaye tumemkodisha ameamua kuifunga kabisa, maana yake tumemkubalia aje hapa ili atufungie huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inanikumbusha mtu mmoja aliyewuliza kiongozi wake wa dini vipi, nitakwenda peponi? Akaambiwa, aaah, ili uende peponi lazima ufe. Akasema ah, subiri kidogo. Wote tunajua tunataka kwenda wapi, tunataka barabara na reli hizi zijengwe, fedha hatuna, wafadhili hawatupi fedha.

Naomba nikubaliane na Kamati ya Miundombinu iliyopendekeza kwamba tukakope, hatuna njia nyingine. Wafadhili wapo, fedha za ndani tutazitafuta sawa, lakini tukakope, maendeleo hayana haja ya kungojea miaka arobaini, tumechelewa kama ilivyo hivi sasa. Ni muhimu wenzetu mnaokaa kutengeneza mipango mlione hili na nashukuru Mheshimiwa Rais ameanzisha tena *Planning Commission*, basi wafanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi jioni hii ili nami niweze kuchangia kwa ufupi tu hoja iliyo mbele yetu, hoja nzuri iliyotolewa na Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuelezea kwa ufupi jinsi gani ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe, Mbeya unavyokwenda taratibu. Kilio chetu Mkoa wa Mbeya ni Uwanja wa Ndege ambao ni wa Kimataifa na sio kama wengine wanavyodhani kuwa ni ukarabati, sio ukarabati ni ujenzi mpya. Hadi sasa ujenzi huo unakwenda taratibu sana wakati Serikali imeshatoa fedha nyingi. Kwa hiyo, naomba msukumo uwewe. Lakini nimefarijika niliposoma kitabu cha hotuba ya Waziri wa Miundombinu ukurasa wa 17. Kwa kweli ameleta matumaini makubwa sana kwamba kazi inaanza mwezi huu Julai na itakamilika baada ya miezi ishirini na nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndivyo ilivyo, basi ni shukrani kubwa sana. Naomba ieleteke tu kwamba mradi huu ulizinduliwa rasmi mwaka 2001. Kwa kuwa mradi huu ni mkubwa, ulihitaji fedha nyingi, hivyo iliamuliwa utekelezwe kwa awamu tatu. Awamu mbili zilikwishatekelezwa na zilishakamilika, ilibaki awamu ya tatu. Ili kukamilisha awamu ya tatu, Serikali ilishampata Mhandisi Mshauri, alipatikana tarehe 15 Juni, 2006. Baada ya hapo, ukapatikana mkopo wa fedha za Kimarekani dola milioni 11.6 kwa ajili ya kukamilisha awamu ya tatu. Lakini ikashangaza kwamba mpaka hivi sasa huo mradi bado haujaendelezwa, umesimama, lakini kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameahidi kwamba utaanza mwezi Julai, basi nina matumaini makubwa kwamba kweli utaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya fedha hizo za Kimarekani dola milioni 11.6 mradi huo ulikuwa utekelezwe ndani ya miezi kumi na nane ili ukamilike mwezi Agosti,

2008 lakini kwa kweli mpaka sasa bado haujaanza, labda umeanza siku mbili tatu zilizopita kwa sababu ndiyo kilio kikubwa sana cha wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuhusu mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu uwanja wa Songwe Mbeya sio kama ni mradi wa wananchi wa Mkoa wa Mbeya peke yao, hapana. Huu mradi tunasema ni bandari na sisi katika Mkoa wa Mbeya na Mikoa ya jirani na nchi za Ukanda wa Kusini ambazo ni Zambia, Botswana, Afrika Kusini kama vile wenzetu wa Mtwara wanavyopigania Bandari ya Mtwara, watu wa Tanga Bandari ya Mbeya na sisi wa Mbeya ni Uwanja ule wa Songwe ndiyo bandari yetu kwa sababu ndege itakuwa inabeba mizigo mikubwa na tutanufaika watu wa Mkoa wa Mbeya na hata Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Rukwa mnapopita kwenda Rukwa mpitie maana yake uko barabarani tu mnaweza kuuangalia huo uwanja na hasa Mbunge wa Mpanda Mashariki, akipata nafasi ya kwenda Mbeya ningewomba ajaribu kuupitia ule uwanja auone kwa sababu Jimbo lake la Mpanda Mashiriki wananchi wake ni wakulima wazuri sana wa mahindi, kwa hiyo, ule uwanja utawasaidia sana hata wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Kawambwa bado ni kijana na ana nguvu tena ni mpole sana, mungwana, namwomba baada ya Bunge hili mguu kwa mguu niongozane naye kwenda Mbeya ili tukauone wote uwanja ule unavyoendelea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika ujenzi mwingine wa barabara ya kutoka Mbeya – Luhanjilo – Chunya – Makongorosi. Barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami. Naipongeza sana Serikali kwa kutuwekea hiyo barabara. Mwaka jana hiyo barabara ilitengewa Shilingi bilioni sita, mwaka huu wa fedha 2008/2009 mkoaa umetengewa Shilingi bilioni nane, hazitoshi kabisa! Kwa jiografia ya barabara ile kwa kweli ni ya miamba na kona. Mimi sio *engineer* lakini hata *engineers* wataona kweli hizo Shilingi bilioni nane hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Kawambwa atakapokuja kuangalia Uwanja wa Kimataifa wa Mbeya, basi tufuatane pia mpaka barabara ya Chunya. Mguu kwa mguu nitakuwa naye, mimi ni mama yake asiwe na wasiwasi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo barabara sasa hivi imeanza kutengenezwa na itatengenezwa kwa kilomita thelathini na sita, yaani kutoka Mbeya Mjini mpaka Luhanjilo kitabaki kipande cha Chunya kwenda Makongorosi. Naamini Serikali itatuangalia kwa jicho la huruma kuhusu kipande hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niongelee kidogo kuhusu Ziwa letu la Nyasa. Ingawa sio la Miundombinu, lakini ni la Miundombinu kwa sababu naomba wasaidiwe kuboreshewa huduma za uvuvi wananchi wanaovua kwenye Ziwa Nyasa kule Kyela. Mpaka sasa hivi wanavua ule uvuvi wa kizamani. Ili kujipatia kipato na wao

waweze kuvua uvuvi wa kisasa, basi naomba Miundombinu itusaidie kuweka ile ..., wanasemaje?

**WABUNGE FULANI:** Gati.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Enhee, hiyo hiyo ili na wao waweze kuboresha kipato chao. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kuzungumzia kuhusu ongezeko la bei ya mafuta. Ongezeko la bei ya mafuta limesababisha ongezeko la bei ya chakula, upande mwingine wakasema ni *EPA* sijui, ni *Richmond*, lakini uhakika na ongezeko la mafuta kwa sababu mazao mengi yapo vijijini. Wajasiriamali wanapokwenda kuchukua mazao yao kutoka vijijini kuja mijini wanatumia gharama kubwa sana na ikizingatiwa kwamba wajasiriamali wengi hasa katika Mkoa wa Mbeya ni wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ndizo mnazoziona zinatoka Mbeya kwenda Dar es Salaam kwa kweli ni kutokana na nguvu za wanawake. Mahindi mnayoyaona ni kutokana na nguvu za wanawake, lakini gharama za usafirishaji kwa kweli zinawaumiza sana na ndiyo hilo lilopelekea gharama ya chakula kupanda bei, wala sio mambo ya *EPA* wala *Richmond*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya ongezeko la chakula, kutokana na ongezeko la mafuta pia nauli za kawaida zimeongezeka. Kitu kinachonishangaza ni kwamba shule zinapofungwa au kufunguliwa nauli inakwenda juu. Shule zikishafunguliwa wanafunzi wapo shulenii angalau zinakuwa za wastani, watoto wetu wanaumia sana. Naomba Serikali kwa kweli isimamie, kwa sababu kuna mamlaka ya *SUMATRA*, itumike kusaidia suala hili la ongezeko la nauli kiholela. Nasema kiholela kwa sababu utakuta leo kutoka Dodoma kwenda Mbeya Sh. 30,000/=, siku nyingine utakuta Sh. 25,000/= au 27,000/= hasa shule zinapofunguliwa. Naomba hili...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mama Kyendesya samahani kidogo. Waheshimiwa Wabunge, labda tu nimpongeze Mama Kyendesya kwa sababu amekuwa na mambo na hoja nyingi za kuchangia. Lakini kwa mujibu wa Kanuni yetu, inatuambia hoja iliyoko mbele yetu ni hoja ya Miundombinu. Kwa hiyo, yale ambayo yanahu hoja za bajeti zinazokuja, ningeomba sana Waheshimiwa Wabunge tusubiri, kama ni mambo ya Elimu, Ziwa au Samaki yasubiri hotuba zinazohusika zinazokuja. Mama Kyendesya naomba sasa uendelee.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilikuwa naongelea kuhusu *SUMATRA*.

**MWENYEKITI:** Kuhusu *SUMATRA* sawa sawa, lakini yale mengine yalikuwa hayahuksiki, usije ukaendelea na mengine ambayo hayahuksiki na bajeti husika.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naheshimu sana. Kwa kweli nilikuwa naongelea habari ya nauli kwamba, tunaomba

Serikali isimamie ili *SUMATRA* ifanye kazi yake sawa sawa, ili kuongezeka kwa nauli kiholela kupungue, wanafunzi wetu wanaumia kwa sababu shule zinapofungwa na kufunguliwa ndipo ongezeko la nauli linapokuja juu. Langu hasa lilikuwa ni hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipozungumzia kuhusu wajasiriamali kwamba wengi ni wanawake ni lile ongezeko la nauli tu. Kuchukua mazao mashambani, magari makubwa huwa yanawatoza nauli kubwa sana. Ilikuwa ni kuhusu hilo tu katika mambo ya nauli hasa wenyewe magari makubwa wanasema miundombinu huko sio mizuri, magari yao yanaharibika sana. Kwa hiyo, nilikuwa nakwenda kimiundombinu miundombinu tu. Nadhani nimeeleweka na Waziri anayehusika amenisikia na Mheshimiwa Mbunge wa Mpanda Mashariki amenisikia na amenielewa. Akipata nafasi kwenda Mbeya akaangalie Uwanja wa Songwe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana mama Kyendesya, kwa kweli mchango wako umekuwa ni wa kimiundombinu hasa na nadhani Mbunge uliyemtaja amekusikia kabisa na ye ye aliкуwa anafurahia sana jinsi ulivyokuwa unatambua uwepo wake. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mhonga na Mheshimiwa John Paul Lwanji ajiandae.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya nikaweza kusimama hapa mbele siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nina maneno ya utangulizi, nimepokea meseji nyingi sana kutoka kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma wakimshangaa Mheshimiwa mwenzetu, tunatoka Mkoa huo huo anaposimama ndani ya Bunge, badala ya kuongelea matatizo ambayo yanawahusu wananchi wake au yanayohusu mkoa kwa ujumla na nchi nzima anasimama na kuanza kumponda Mbunge mwenzake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hali ambayo hatuwezi kuikataa, ni kweli. Serikali imeamua kutenga pesa kwa ajili ya barabara ya Mwandiga – Manyovu, naishukuru sana na kwa kweli ni mara ya kwanza kwa Kigoma Vijijini kupata lami. Watoto wengi leo ukiwaliza lami ni kitu gani katika maeneo mengi hawajawahi kuona kabisa. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali na tunaamini hatufanyi kazi kwa itikadi hiyo, mipango ya Serikali ipo na itatekelezwa tu, nashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze kuchangia. Hakuna asiyejua kwamba, miundombinu ni kitu cha msingi sana katika kukuza uchumi wa nchi yoyote ile. Ni sawa sawa na *veins* au mishipa ya damu katika mwili wa mwanadamu na ndiyo maana Wabunge wengi sana wameomba kuchangia katika hii bajeti kwa sababu miundombinu ni kitu cha msingi sana. Tunazo changamoto nyingi kwa sababu uchumi wetu ni mdogo, hatuwezi kukamilisha barabara nyingi kama zilivyopangwa, lakini naamini Serikali ina juhudhi mbalimbali inafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ku-*refer* kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Mkullo. Alisema changamoto inayotukumba ni kwamba, miradi yetu mingi inategemea wafadhili kutoka nje, lakini kwa bahati mbaya sana kuna baadhi ya miradi ambayo haitekelezeki kwa sababu hatuna pesa za ndani. Kwa hiyo, hiyo ni changamoto tuangalie jinsi gani tunavyoweza kufanya kuhakikisha kwamba tunapata fedha ili kukamilisha miradi yetu ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwa na miundombinu ambayo ni madhubuti kwa mfano, barabara za kueleweka ni ngumu sana hata katika masuala haya ya kiuchumi, naweza kuchukua mfano kwa Mkoa wa Kigoma peke yake, Kigoma hatuna reli ya kueleweka, barabara hazipitiki, unakuta ukipata mfuko mmoja wa sementi ni Sh. 21,000/= mpaka Sh. 22,000/=, yaani huwezi kupata chini ya hapo labda u-*bargain* sana unaweza kupata kwa Sh. 20,000/=.

Kwa hiyo, si rahisi mwananchi wa Mkoa wa Kigoma kupata maendeleo kwa mtindo huo, lazima ataamua kujenga nyumba ya matofali ya kuchoma na wengi wanajengea chokaa. Sasa hiyo sijui ni teknolojia ya wapi. Wanatumia chokaa kama sementi kutokana na hali ngumu ya kiuchumi kwa sababu kule kumekuwa ni mbali sana kufikisha mizigo, kwa kweli ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni kwamba hata bidhaa zao zinauzwa kwa bei ndogo kwa sababu mtu anakwambia nimeifuata kutoka mbali. Kwa hiyo, unakuta bidhaa za kule zinauzwa kwa bei ndogo kwa sababu ya ule umbali. Nitatoa mfano, mwaka 2004 niliwahi kwenda Wilaya ya Kilolo sikumbuki Kijiji, lakini walitushangilia wakisema hawajawahi kupata wageni kutoka maeneo mengine kwa kipindi kirefu. Pale mfuko mmoja, yaani *sulphate* ya kabichi ilikuwa inauzwa Sh. 2,000/=, tulishangaa na matunda yanaoza. Wakatuambia kwamba huku watu hawafiki kwa sababu barabara ni mbaya sana. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba wale watu hawawezи kujikomboa kiuchumi kwa sababu hawana miundombinu ya kueleweka kufikisha mazao hayo sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikitika kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliainisha baadhi ya barabara ambazo zitajengwa, kwa kweli barabara ya Nyakanazi Kigoma sikuiona na wakati sijawa Mbunge nilikuwa nikijiuliza hivi hawa Wabunge wanafanya nini huku ndani mbona barabara zetu hazijengwi? Nami tangu nimeingia mwaka 2005/2006 nimeuliza maswali mengi sana yanayohusu barabara na reli, majibu tunayopewa na Serikali tupo kwenye upembuzi yakinifu, majibu yanayotoka Serikalini, vuta subira, fedha zikipatikana tutajenga. Yanakupa matumaini, lakini hayatoi mwelekeo wowote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naishauri Serikali itafute *alternative* na hata Kamati wameshauri kwamba tukope, nashangaa mbona mpango wa *MMEM* au *MMES* umekopewa fedha na tumeweza kujenga shule! Kwa hiyo, nilikuwa naomba tukope kwa sababu ya kuhakikisha kwamba tunafungua miundombinu ili uchumi wetu ukue. Hatutajali jina lolote utakaoitwa huo mkopo maana yake mkopo wa *MMEM* na *MMES*

tulikuwa tunaita fedha za Mkapa. Sasa ziiwe jina lolote, lakini barabara zijengwe. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano eneo la Kasulu, pale ukitandika shuka yako nyeupe ujue jioni huwezi kulilalia. Lile vumbi linaingia hadi ndani na mfano ikinyesha mvua sijui uvae kiatu gani maana utatoka hapo na kiatu kingine. Kwa hiyo, tuna hali mbaya sana. Tunaomba Serikali ihakikishe inatafuta *alternative* ya kuhakikisha barabara nyingi zinajengwa ili kuweza kutuokoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Reli ya Kati. Hapa ndiyo kuna tatizo kubwa; mwaka 2006 niliuliza maswali mengi ya Barabara na Reli, aliyekuwa Waziri kipindi hicho, Mheshimiwa Basil Mramba alituita Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma, tukaenda ofisini kwake, hapa hapa Dodoma, tukakaa naye kikao pamoja na wataalam. Alitupa hali halisi ya reli jinsi ilivyo na aliniambia mwanangu, maana yake wewe nakuona kama mwanangu, naona ningekuwa na uwezo ningesimamisha hiyo reli isifanye kazi, lakini hakuna *alternative* inabidi tuwaachie hivyo hivyo. Lakini ni *disaster* na kweli ni *disaster*.

Nilikuwa kwenye treini ile mwaka 2002 katika ile ajali ya Igando Msagali, namshukuru Mungu ni mionganoni mwa waliopona. Kwa kweli mpaka leo, mimi nina *forbear* kuhusiana na hiyo treni na ninapokwenda kusindikiza hata watu nikiangalia mle ndani ni hali ambayo inasikitisha. Aliyoyasema Mheshimiwa Tatu Ntimizi kwamba, watu wanakufa kwenye hiyo treni ni kweli watu wanakufa kwa sababu ya kukosa hewa. Watu wanakaa hadi chooni, sasa hawawezi hata kujisaidia.

Kinachosikitisha zaidi, tiketi zenyewe hazipatikani. Pale Mkoani Kigoma kwa mtu anayemfahamu *DC* au mtu yejote mkubwa mwenye cheo, unampigia simu kwa sababu yeye kidogo ana sauti, anapiga simu kwa *station master* unapata tiketi kiurahisi. Tiketi hazipatikani kabisa. Kwa wafuatiliaji wa vyombo vya habari; *Channel Ten* hapa siku moja walionyesha wananchi wanalamika, wamejaa pale *station* wanatafuta tiketi hawazipati, wamepanga mstari kuanzia asubuhi watu wanane ndiyo waliopata tiketi, lakini Ukienda kwenye treini watu wamejaa. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie tatizo hasa la msingi ni nini?

Kwa sababu Serikali nayo ina asilimia zake 49, hebu waulize hawa *RITES* kwa nini wanawajaza watu namna ile, maana yake hali ile ni mbaya mno inasikitisha. Halafu wamepandisha bei ya mizigo, ukisema ukodishe behewa moja siyo ile zamani mlikuwa mna mizigo yenu wengi mnapandisha tu kwenye behewa mnalipia, sasa hivi unatakiwa uchukue behewa zima ulipie na behewa zima ni shilingi 4,266,000. Kwa mtu wa kawaida hawezi, lazima uwe na biashara kubwa ndio unaweza kutuma mzigoto kutumia reli ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati tukiongea na Mheshimiwa Mramba kipindi hicho, alituambia tusubiri *RITES* wachukue hali itakuwa bora. Kwa kweli naona hali imezidi kuwa mbaya, Serikali iangalie. Namshukuru Waziri Mkuu, alisema wazi hapa ndani kwamba, tatizo haliko kwa *RITES* peke yake, lipo hata kwa watendaji wetu. Kwa

hiyo, Serikali ichukue hatua kwa sababu yenye ina mkono mrefu, inaweza ikalifuatilia hili suala na likatatuliwa. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu au *group* la Mawaziri wengine, wahakikishe tunayoyasema. Treni inapita hapa Dodoma, wakaangalie tu *situation* mle ndani, yaani hata ukiambiwa wewe uingie huwezi kufika mbali, unaweza ukazimia kutokana na hali hiyo. Watu wanakaa hadi chini, wanaweka watoto chini ya viti; kwa kweli ni hali ngumu sana tunaomba sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kilichonishangaza kabla sijahama hapa kwenye reli nirudi tena kwenye barabara. Waheshimiwa Wabunge wa Tabora walipolalamika fedha zilipatikana. Sasa sijui na sisi leo tutaambiwa tumetengewa kiasi gani kwa ajili ya Barabara ya Nyakanazi. Ina maana fedha zipo, mipangilio ndiyo hakuna au nini na ile shilingi bilioni kumi ilitoka wapi ya kuingiza hapo, sikatai isiingie kwa sababu hata sisi inaturahisishia inatupunguzia safari, lakini nilikuwa naomba njue utaratibu ukoje; kwa nini mtu unatokea siku zote unaomba barabara fedha haitengwi, siku ambayo unaongea fedha inatolewa hapo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye *ATC*, tunaipongeza Serikali kwa kuirudisha mikononi mwa Watanzania. Tatizo ni kwamba, bado sielewi ni Menejimenti au ni Serikali inatoa fedha ndogo? Hali bado ni mbaya sana kwa upande wa Shirika letu la Ndege, yaani safari haziko *reliable*, utaambiwa njoo ndege zinaondoka labda saa 12, mtakwenda mkifika pale, hata haupigiwi simu kuambiwa ndege hakuna, unaambiwa mtaondoka sasa nne. Saa nyngine saa nne tena usiku msiondoke iwe mpaka kesho; utaratibu wa hii ndege haueleweki. Sasa sielewi ni kitu gain? Nadhani tunaweza kupata majibu ya kijitosheleza.

Tumekuwa tukihoji Kambi ya Upinzani katika michango yetu mbalimbali kuhusiana na mali ambazo zilikuwa za *ATC*; kuna nyumba za *ATC* huko Johannesburg, Harare, Lusaka, Comoro na Riyadh Oman, lakini hatujapata majibu ya kujitosheleza. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atuelezee, mpaka sasa kuna kitu gain; tunataka kujua kitu gani kimetokea kutokana na utelekezwaji maana tunaona kama zile nyumba zimetelekezwa tu? Kwa hiyo, tunaomba Serikali ituambie kuna kitu gani hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma tunao Mpango wa *Special Economic Zone* kwa ajili ya angalau na sisi kujikwamua kiuchumi. Mradi huu ni mzuri sana na ni mkubwa lakini hatuwezi kufanikiwa kama bandari yetu haitafanya kazi vizuri. Sisi pale tumepakana na Kongo upande wa Mashariki, nazipongeza juhudzi za awali za kutoa mchanga kwa sababu mvua ilipokuwa ikinyesha pale mchanga mwangi ulikuwa unajaa kwenye *port* pale. Serikali imejitahidi imetoa, lakini bado hata hivyo ile bandari yetu haitumiki ipasavyo. Hotuba ya Kambi ya Upinzani imeelezea jinsi tunavyowezwa kufanikiwa kutokana na utumiaji mzuri wa bandari zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo tumewahi kulizungumzia sana hapa watu wa Kigoma. Nadhani mnafahamu kwamba, Kagunga ni eneo ambalo tunapakana kabisa na Burundi na ni eneo ambalo tulikuwa tunapendekeza lijengwe soko ambalo linaweza likatusaidia kufikisha sisi bidhaa zetu pale ziweze kutoka nje. Tulikuwa tunaomba gati lijengwe kwa sababu pale kuna ziwa Tanganyika, tunatenganishwa na

Ziwa na vilevile tukijenga gati pale itatusaidia sana hasa huu mpango wetu mzima wa *SEZ*. (*Makofi*)

Kitu kingine ni Kivuko cha Ilagala, pale tunalo Ziwa na tunao Mto Malagarasi ni mto mkubwa sana, si rahisi kuvuka hivi hivi una mamba. Tuna kivuko ambacho hakifanyi kazi, yaani kipo tu pale kimetulia, watu wanatumia maboti ambayo hayana uhakika. Sasa nilikuwa naomba Serikali ituambie ina mkakati gain, kwa sababu hili suala la kivuko siyo siku ya kwanza kuongelewa?

Kwa hiyo, tunaomba wakati akijibu atuelezee Mikakati ya Serikali kama wanakitengeneza au tunapata kingine, kwa sababu wananchi wanapata tabu sana kutoka eneo moja kwenda lingine. Hiki ndiyo kivuko wanachokitegemea ili waweze kuvuka upande wa pili wapande gari kuja Kigoma Mjini hospitali, kama mnavyojua tena Kigoma hatuna Hospitali ya Wilaya wanatumia hiyo hiyo ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri anaweza akanijibu hayo machache ambayo nimechangia. Nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, nakushukuru sana kwa mchango wako ambao umeuwasilisha muda mchache uliopita. Kwenye utata wa Kiswahili, nakushauri umwone tu Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, anaweza kukusaidia pia kupata ufanuzi wa mambo mengine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa John Paul Lwanji na Mheshimiwa Zabein Mhita ajiandae.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi ninaunga mkono hoja na kama alivyosema dada yangu, Mheshimiwa Florence Kyendesya, kwa kweli hao watu ni wa taratibu na ni wasikivu. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake, majukumu hayo waliyokabidhiwa nadhani watayafanya kwa uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuupongeza Uongozi wa Mkoa wangu na Serikali kwa ujumla, kwa kazi waliyoifanya ya kurekebisha barabara muhimu kabisa ya kutoka Sanza - Chikola - Manyoni - Itigi. Kwenye barabara hii, kazi waliyoifanya ilimwezesha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa *Africa Union* kulala Itigi. Tarehe 2 Mei, 2008 alisafiri kutoka Sanza kukagua shughuli za maendeleo na kuona barabara hiyo na mwisho jioni akafika Itigi na kupumzika hapo mpaka kesho yake asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nadra kupata Mheshimiwa Rais anayeweza kulala kijijini na ni wachache sana. Pamoja na wadhifa wa Uenyekiti wa *Africa Union*, alitoka Addis Ababa kwa shughuli muhimu akaenda Uganda Kampala, halafu akaenda Dar es Salaam akalala Itigi. Kwa hiyo, sisi Wananchi wa Itigi tunashukuru sana kwa hilo, lakini iliwezekana kwa sababu ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuishukuru sana Serikali kwa kusikia kilio chetu cha barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora na kwenda Kigoma. Itatuletea ahueni kubwa sana na Serikali nadhani kwenye miundombinu ya reli, itapunguza sana lawama. Kwa sababu kama itatokea kwamba hiyo barabara ikatengenezwa kwa kiwango cha lami mapema, watu watachagua kupanda mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuwaambia kitu kimoja; angalieni tu mfano wa barabara ya lami iliyofika pale Chikuyu, maisha ya watu wa Bahi na wa Chikuyu yamebadilika ghafla. Kwa hiyo, miundombinu ni kitu muhimu na hasa barabara kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina barabara zinazokisiwa kufikia kilomita 29,000 mpaka 30,000, lakini ni asilimia 16 tu ndiyo zenyelami kwa maana ya kwamba, kilomita 5,000. Sasa utaona jinsi gani ambavyo tuko nyuma. Wiki iliyopita, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anawasilisha hotuba yake hapa, labda ninukuu alisema hivi: "Maendeleo ya Uchumi wa Nchi yoyote ile hutegemea sana mtandao mzuri wa barabara. Barabara husaidia shughuli za kiuchumi na kijamii kustawi, kushamiri, na kuchangia katika ukuaji wa uchumi na mapato ya watu. Aidha, barabara ni muhimu katika kuwasaidia wananchi wanaishi vijijini hasa wakulima kusafirisha mazao yao kutoka mashambani hadi kwenye masoko."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge 88 waliochangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, walisisitiza masuala ya miundombinu. Mimi nadhani Serikali ya Awamu ya Tatu, ilijizolea umaarufu sana ilipoweka kipaumbele zaidi kwenye miundombinu. Nadhani hapa ni kweli tumekuja na elimu, tumekuja na afya, nafikiri ndiyo miundombinu inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu mwaka jana wanafunzi hawakusoma wakati wa masika. Tulifungua shule za sekondari na za msingi, lakini walimu walipofuata mishahara mwezi Desemba, ile mvua ya mwanzo iliponyesha walipofika Manyoni hawakuweza kurudi katika maeneo ya kazi, kwa mfano, Mgandu na Rungwa. Kwa hiyo, wanafunzi wakawa hawana walimu kwa sababu walipofuata mishahara barabara zikawa hazipitiki. Sasa unaona ni kitendawili hapo *which comes first*, maana shule ndiyo zipo lakini sasa tumejaribu kadiri tulivyoweza lakini watoto hawakusoma kwa kipindi cha miezi mitatu, minne na walimu ilibidi wapangiwe shule za Mjini Manyoni na Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ndiyo maana ninaunga mkono hii hoja kwa sababu Serikali sasa hivi ninavyoona katika hii bajeti imejaribu kutambua. Mimi ninaomba mwakani hiki kipaumbele kisisitizwe, ikiwezekana ije namba mbili au iwe ya kwanza kabisa. Kwa sababu tunashindwa kufika kwenye hospitali zetu, tunashindwa kufika kwenye shule zetu kwa sababu hatuna barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunalalamika tuko nyuma, lakini hatuwezi kulalamika kwa sababu wakati wa ukoloni hatukujengewa barabara. Sisi hatukuwa koloni kama Kenya, wenzetu walijengewa barabara kwa sababu wale watu walifikiri

kwamba, hawawezi kuondoka. Sisi hapa tulikuwa *trusteeship*, Serikali ya Uingereza iliambiwa kwamba, ikae ituangalie kwa muda, walikuwa hawakufanya kitu chochote. Sasa ni lazima hata hizi nchi mnazosema za *Asian Tigers* kama Malaysia na wapi zimewekeza katika elimu, afya na nini, lakini zilianza kwanza kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninasisitiza kwamba, mwakani tutengee fedha za kutosha tuweze kuimarisha barabara zetu. Watu watajajiri *automatically*, hatuwezi kuajiri kila mtu. Sasa kama kuna barabara za kutosha vijijini na ni nzuri na kuna barabara zenye lami, *definitely* watu watajajiri, mazao yao watayafikisha katika soko ambalo wanaweza kupata bei nzuri na watafanya shughuli zenye tija. Sasa hivi wanakuwa katika *Zero Grazing* kwa sababu wakipata mazao watayapeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima watafanya biashara kama kuna barabara nzuri. Kama nilivosema, maisha ya Watu wa Bahi sasa hivi na Chikuyu wanakwenda kuchukua samaki na mpunga; hayo ndiyo maendeleo. Serikali *automatically* inajipunguzia mzigo wa kufikiria namna ya kuwatafutia watu ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunesema tunajiondoa kwenye utegemezi kutoka asilimia 42 mpaka asilimia 34. Mimi ninaungana na Mbunge mwenzangu wa Mlalo kwamba, lazima tuendelee kukopa. Tunasema tumeondokana na utegemezi kwa asilimia 42 mpaka asilimia 34, lakini wakati huo huo tukatangaza kwamba, barabara kadhaa muhimu tumeziacha kama hii inayoleta kilio ya kutoka Manyoni - Itigi - Tabora, lakini barabara nyingi ziliachwa tu. Nashangaa iweje sasa? Lazima tuendelee kukopa na tuwekeze katika miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Dodoma - Manyoni - Isuna inakwenda lakini kasi yake hairidhishi. Tumeambiwa kutoka Manyoni kwenda Isuna ni kilomita 54, lakini barabara hii ipo *scheduled* kumalizika baada ya miezi 33. Miezi 33 nafikiri ni mwezi Desemba, 2010. *You can imagine* ni kipande tu hicho kinasimamisha shughuli zote, kwa sababu iliyahi kunyesha mvua magari yote yalikwama pale Kamenyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeiomba Serikali ijaribu kufikiria hili, maana hii miezi 33 ni *tentative*. *This is tentative* kwa sababu kuna *variations* hapo zitakazotkea na nini. Kwa hiyo, *definitely* unaweza hata kuongeza miezi kumi mingine hapo. Kwa hiyo, barabara hii inaweza kumalizika hata mwaka 2011 au 2012. Naomba hata hizo fedha za *Millennium Challenge Account* kwa nini wazisichukue kule, maana Mkoa huu hakupangiwa kabisa hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeliomba Serikali ijaribu kulitazama hilo, kama ambavyo tunalia kuhusu barabara ya Somanga - Ndundu kipande hicho tukikamilishe. Walisema tutasafiri kwa teksi kutoka Mtwara mpaka Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeiomba sana Serikali iweze kuwa makini kwa hilo, ikamilishe hivyo vipande vilivyobaki. Barabara hiyo ya kutoka Chikuyu kwenda Manyoni inakwenda, ingawa mara nyingine inasuasusa kwa sababu ya kukosa fedha,

lakini wamepata fedha wanaendelea. Manyoni mpaka Isuna wamepata mkandarasi, tafadhalii sana tunaomba muda huo uangaliwe ili barabara hiyo iweze kumalizika mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Itigi - Rungwa kwenda Chunya imetengewa shilingi milioni 400, mwaka jana ilitengewa shilingi milioni 500 na wameweza kujenga madaraja madogo madogo katika zile sehemu sugu, lakini fedha hizo ni chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya hii barabara ni kwamba, mwaka 1998 iliwekwa katika Mradi wa *El-Nino*, iliharibika kabisa mpaka Serikali ikaamua kuiweka katika Mradi wa *El-Nino*, akapewa mkandarasi mmoja anayeitwa *Badri East Africa*. Mtu huyu akafanya sehemu fupi ya kutoka Kirumbi mpaka Mwamagembe lakini ikamshinda, kwa hiyo, akasimamishwa fedha zikarudishwa Serikalini. Sasa baada ya kuurudisha ule Mradi, zimekuwa zikitolewa fedha kiasi hicho kidogo kidogo kwa ajili ya *ku-maintain*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba hiyo barabara itengewe fedha za kutosha, maeneo hayo ni muhimu sana ukitoka Itigi kuna vijiji karibu 20; Mlonghojii, Lulanga, Itagata, Kayui, Uspesanoni, Mtakuja, Makale, Mitundu, Ipalalyuu, Iatagali, Kiyombo, Kirumbi, Mwamagembe, Kintanula, mpaka Rungwa, Kambi Katoto, Makongorosi, Chunya, Mkwajuni mpaka Mbeya. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Wapinzani katika ukurasa wa kumi wa Taarifa yao wameitaja barabara hiyo wanasema kwamba ni muhimu. Mbeya - Chunya - Tabora - Mwanza. Sasa hapo wameingia mitini, ukisema Barabara ya Chunya - Tabora bila kutaja Itigi, kwa sababu pale ndiyo CCM imeshamiri sana na wale wamepinda hapo, sijui wanataka kuipitisha wapi hiyo barabara? Ukweli ni huo kwamba, barabara hiyo ni muhimu sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Reli ya Kati, Ijumaa ile kabla hatujaanza Kikao cha Bunge hapa, treni ndogo inayokwenda Singida ilipofika katika Mlima wa Saranda ilishindwa, ikaanza kurudi nyuma mpaka Stesheni ya Saranda. Bahati nzuri kule walimanage kuondoa treni nyingine iliyokuwa pale na ilipokosa nguvu kidogo ikaenda kuanguka na watu waliumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaona tungejaribu sana Reli sasa hivi tuiache kwa ajili ya mizigo, tukamilishe hizo barabara, watu watumie mabasi. Mimi ndivyo ninavyoona na ni maoni yangu, kwa sababu reli bado inakarabatiwa itachukua muda mrefu. Sasa hivyo vipande vya barabara vilivyobakia vimaliziwe ili watu waweze kutumia kwa ajili ya kuokoa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumalizia kwa kusositiza tu kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ana-*wind up* alikuwa amesisitiza kuwaonya wenzetu wale ambao hawataki kufanya kazi. Wale wenzetu wanaotukwamisha, kwa hiyo, lilikuwa na uzito sana na alitoa mfano wa kitu kimoja sijui kwa *Attorney General* na

ndivyo ilivyo, kuna watu wa aina mbili katika utumishi wetu; wale wanaotaka kufanya kazi na wale ambao hawataki kufanya kazi; wale wanaopokea rushwa na wale ambao hawapokei rushwa. *We have two strange bad fellows.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeliomba sasa Wizara zote zichukue wito wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa ku-single out hao watupunguzie mzigo ili tuweze kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Lwanji, nakushukuru sana. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita na Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Miundombinu.

Awali ya yote, naomba niwapongeze kwa dhati; Waziri Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu, Injinia Omar Chambo, Naibu Katibu Mkuu, Bi Joyce Mapunjo na Wakurugenzi wote, kwa hotuba ilioandalialiwa kisayansi. Matumaini yetu ni kuwa utekelezaji wake pia utakuwa wa kisayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, mchango wangu nitauelekeza kwenye tatizo sugu ambalo ni barabara ya kutoka Minjingu, Babati, Kondoa, Haneti, Jimbo la Chilonwa, ambalo Mbunge wake ni Mheshimiwa Kalumbu Hezekiah Chibulunje mpaka Dodoma na hadi kufika Iringa. (*Makofi/Kicheko*)

Sera ya Wizara ya Miundombinu, inatoa kipaumbele katika ujenzi wa barabara Kuu, yaani *Trunk Roads*. Barabara niliyoitaja ni barabara kuu hivyo ujenzi wake kwa kulingana na sera hiyo, hauna mjadala. Barabara hii si tu kwamba inaunganisha Mkoo wa Dodoma na Mikoa mingine, bali pia inaunganisha nchi yetu na nchi nyingine. Barabara hii inafahamika kwa jina la *The Great North Road*, inatoka *Cairo, Egypt* mpaka *Cape Town*, Afrika ya Kusini. Katika nchi nyingine zote inapopita barabara hii, imejengwa kwa kiwango cha lami isipokuwa katika eneo ambalo nimelitaja. Kibaya zaidi ni kuwa, sehemu niliyoitaja barabara hii ipo katika hali mbaya sana. Labda nitoe mfano, kutoka hapa Dodoma mpaka Kondoa ni kilomita 160 tu, lakini kutokana na ubovu wa barabara hii magari yanachukua saa nne, yaani wastani wa kilomita 40 kwa saa. Athari yake ni ucheleweshwaji wa wasafiri, ikizingatiwa kuwa wasafiri wengi wanaunganisha usafiri huu na mwingine. Wakati wa masika barabara hii inachukua zaidi hata ya siku moja. *Wear and tear* ni kubwa, magari hutumia mafuta mengi zaidi ikizingatiwa kupanda kwa bei ya mafuta na hii pia inasababisha nauli kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru wenyewe mabasi yanayopita katika barabara hiyo; Machame *Investment, Satellite, King Cross* na Mareja, yanatoa huduma kwa abiria katika barabara hii pamoja na ubovu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara hiyo kwenye Kijiji cha Kolo kuna daraja ambalo livilunjika tangu mwaka 1997 mpaka hivi leo daraja hili halijatengenezwa, lakini badala yake imejenga *drift* mtoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui iwapo kitaalam ujenzi wa *drift* katika barabara kuu unakubalika. Kuvunjika kwa daraja hilo ni hatari kwa wasafiri na hasa ukizingatia kuwa, daraja hilo lipo katika mteremko. Aidha, wakati wa mvua mto unapojaa, inabidi magari yasubiri mpaka maji yanapopungua wakati mwingine inakuwa hata zaidi ya saa tatu. Kuna madaraja kati ya Kondoaa na Kijiji cha Kilema ambayo hayana kingo. Madaraja haya ni hatari sana kwa usalama wa madereva, wasafiri na mali zao na usafiri wenyewe na hasa madaraja haya yanapokuwa katika mteremko. Labda nitoe mfano, katika Kitongoji cha Ausia zimeshatokea ajali zaidi ya nne. Pia ningependa kufahamu iwapo kitalaam inakubalika katika barabara kuu kuwa na madaraja ambayo hayana kingo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya leo, miundombinu duni ni moja ya vikwazo vikubwa ambavyo hukwamisha na kudumaza harakati za maendeleo. Ubovu wa barabara hii umeathiri kwa kiwango kikubwa sekta nyingi, mfano sekta ya Elimu, Afya, Maliasili na Utalii na hususan kilimo. Kutokana na ubovu wa barabara hiyo, wakulima wanashindwa kusafirisha mazao yao kwenye masoko na hiyo inatoa mwanya kwa walangazi kwenda vijijini na kununua mazao kwa bei ndogo sana. Hivyo, kuwakatisha tamaa kabisa wakulima. Naamini kwamba, iwapo barabara hii itatengenezwa itakuwa changamoto na motisha kwa wakulima hivyo kuongeza uzalishaji kwa kuwa wataweza kusafirisha mazao yao kwenye masoko na kuyauza kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Jimbo la Kondoaa Kaskazini ni wakulima hodari. Pamoja na mazao wanayolima ya mahindi, mtama, karanga na ulezi, katika miaka ya hivi karibuni wamejikita zaidi katika kilimo cha alizeti tena kwa wingi sana. Wakulima hawa hawajanufaika na zao hilo la kibiashara hata kidogo, kutokana na sababu ambazo nimezieleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kondoaa Kaskazini pia lina vivutio vingi na *unique*, yaani vyta kipekee kabisa. Labda nitoe mfano, kuna michoro ya miambani iliyoko Kolo ambayo imeingizwa katika orodha ya urithi wa dunia (*World Heritage Site*), kuna daraja la kunesa lililojengwa na Wajerumani ambalo sasa hivi halitumiki tena, nalo ni kivutio kikubwa sana. Kuna chemchemi ya maji ambayo ni chanzo cha maji katika Mji wa Kondoaa. Hivi ni vivutio ambavyo vingeweza kuvutia watalii wengi na kuliingizia Taifa letu pato kubwa, pamoja na wananchi lakini hali halisi si hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Wizara ya Miundombinu zimetengwa shilingi bilioni 12.01 kwa ajili ya barabara kutoka Dodoma mpaka Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa hatua hii inayotoa mwanga na kuleta matumaini kwa wananchi wa Kondo. Hata hivyo, tunaomba sana fedha iliyotengwa ifanye kazi iliyokusudiwa na kazi hiyo ionekane, yaani tuone *value for money*, isiwe tu ni pesa katika kitabu lakini kazi haionekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana fedha hizo ni kiini macho tu kwa Wananchi wa Kondo Kaskazini. Tunaomba fedha hizo zisihamishwe na kupelekwa sehemu nyingine kwa kisingizio chochote kile. Barabara hii ninayoizungumzia, ilishafanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 1991 kutokana na kumbukumbu nilizonazo. Vilevile mwaka 2006 ilifanyiwa tena upembuzi yakinifu. Katika ukurasa wa tisa katika kitabu cha bajeti kinaleza tena itaendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu. Sasa ninachosema ni kwamba, tangu mwaka 1991 iwapo hatua za kujenga barabara zingefanyika hivi sasa tungakuwa tunaongea lugha nyingine. Tungekuwa tunaomba pengine tu kufanyiwa ukarabati mdogo mdogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara hii upo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhita, nimeletewa taarifa hapa kwamba una-refer notes zako moja kwa moja kutoka kwenye karatasi zaidi ya kusema. Kwa hiyo, ningombua uzungumze na Kiti zaidi ya kusoma kwenye karatasi uliyonayo.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda kwa kuwa ninatazama chini na kuinua uso, isieleweke kwamba nasoma, pengine ni tabia tu kwamba ninapoongea napenda kutazama chini na kuinua uso. Lakini hii haina maana ninasoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ipo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, vilevile Mheshimiwa Rais wetu mpewa alitoa ahadi wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu kuwa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Mpaka sasa hivi haijajengwa, sasa anayezuia barabara hii kujengwa ni nani? Pamoja na kwamba ipo kwenye Ilani, Mheshimiwa Rais wetu alitoa ahadi tangu mwaka 2005 bado haijajengwa; nani huyu anaizuia?

Kwa msingi huu, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kondo Kaskazini, ningependa nipewe maelezo ya kina wakati Mheshimiwa Waziri akifanya majumuisho katika Bajeti yake, kuhusu masuala niliyohoji ikiwa ni pamoja na kufahamishwa lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Tunaomba tupate *time frame*. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana utufahamishe lini pamoja na kwamba kumekuwa na upembuzi yakinifu tangu mwaka 1991, sasa ujenzi unaanza lini? Naomba nilifahamu hilo.

Baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja, nikiwa na mategemeo kwamba hoja zangu zitajibowi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja hii. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi alivyoiwasilisha hoja yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumze machache katika hoja hii lakini si kwa uzito , lakini kwa jinsi pengine ambavyo nitakuwa nimeyapangilia kama ifuatavyo: Kabla ya kuja Bungeni, nilipata nafasi ya kutembelea mpaka wetu wa Tanzania na Uganda Mutukula. Siku ninatoka Uganda naingia Tanzania na gari langu kulikuwa hakuna njia ya kupita kwa maana ya kwamba, malori yalikuwa yameziba pande zote za barabara. Hoja ninayotaka kuzungumza hapa ni kwamba, ramani za ujenzi wa barabara zizingatie mazingira. Mutukula pale ni sehemu ya mpakani, magari ni mengi inapaswa yawe upande na upande. Kuwe na nafasi iliyojengwa ambayo ni ya magari ya malori mazito yanayotoka Tanzania na yanayoingia toka Uganda. Hali hii kwa pale mpakani hata hali ya usalama haikai vizuri. Nilipenda niliseme hilo kwamba, ule msongamano uliopo pale Mutukula si mzuri lakini tatizo kubwa pale miundombinu haikuzingatia ukuaji wa lile eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kulizungumzia ni la pongezi. Napenda niipongeze *SIDO*, jana imeshinda katika Maonyesho ya Biashara ya Dar es Salaam, lakini napenda niipongeze Magereza pia jana imeshinda nayo; ambapo ndipo hoja yangu ilipo hapo katika matengenezo ya samani. Wizara hii inahusika pia na masuala ya kutafuta samani za maofisi kwa Serikalini. Wamekuwa wanapenda kununua samani kutoka nje. Jana mshindi wa kwanza ni Magereza, mshindi wa pili ni Jeshi la wa Wananchi na JKT ndiyo anafuatia mshindi wa tatu ambaye simfahamu. Kwa nini kama hawa wanaweza kushinda katika matengenezo ya samani nchini katika biashara kubwa namna hii, iliyoshirikisha nadhani wafanyabiashara kutoka katika nchi karibu mia moja na washindani walikuwa ni wengi; kwa nini Serikali isiente kununua kule samani? Napenda kuishauri Serikali kwamba, katika hili *furniture* za kuanzia sasa hebu waanze kwenda kule Magereza *then* Jeshi la Wananchi na JKT halafu ndiyo waende maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, sasa nataka nizungumze kwa ufupi tena kuhusu shukrani. Asubuhi Serikali ilipokuwa inajibu swalı langu, ilielezea masuala mazima kuhusu ujenzi wa barabara ya Mutukula – Kagoma, naipongeza sana. Kwa upande wangu, Mutukula mpaka Kagoma ilimalizika mwaka 2004. Kwa hiyo, huko hatuna hoja tunashukuru na upungufu mwagine upo chini ya *TANROAD* wanaendelea nayo. Hoja sasa iliyopo kwetu ni namna gani unavyoweza kutoka Kagoma kuelekea mbele?

Nitazungumzia hapo vizuri baadae wakati nitakaporudi nyuma huko; kwanza nitoe shukrani zangu nyingine kidogo tu. Kati ya Ahadi za Rais alizozitoa alipokuja Kagera wakati anaomba Urais ni pamoja na namna ya kuitengeneza barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo, yenye kilomita 58. Kitabu cha Bajeti cha mwaka huu kimekuja na matengenezo ya km 3. Ninaishukuru sana Serikali, imeweza kututengea kiasi cha shilingi 550 milioni. Karagwe na Ngara zipo mpakani. Kwa kweli ukiangalia hapo, hakuna ahadi kwamba walau kipindi kinachokuja lakini angalia ni kilomita tatu tu. Tungepata kilomita

20 au 30 tingesema walau tumepunguziwa kwa kiasi kikubwa na wakati mwingine tunaamini kwamba, tunaweza kumaliza Ahadi ya Rais. Ninaomba Serikali ituambie; je, lini inaweza kutuongezea pesa na kumaliza barabara hii kwa kilomita 55 zilizobaki na ku-*extend* kufika mpaka Ngara? Nilipenda Serikali inisaidie jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikitoka hapo, naomba nirejee kwenye hoja yangu ya Kagoma - Lusahunga niliyoleta asubuhi. Kwanza, napenda niseme sikuridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri asubuhi. Lakini kwa sababu sheria inasema kwamba ukishauliza maswali yako mawili umemaliza, sikuridhika na nilitaka kuleta Mwongozo wa Spika, nikaona nisicheleweshe shughuli kwa sababu leo nilikuwa nimeomba kuchangia. Sasa naomba nieleze mambo mawili ambayo sikuridhika nayo. Jambo la kwanza, niliuliza Serikali hiki kipindi cha kwanza ambacho imetutengea pesa kutoka Kagoma kwenda mpaka Lusahunga ikamsimamisha Mkandarasi inasema kwamba ni kilomita 154 ambazo ni nyingi kuliko 138 ambazo zilizokwisha malizika lakini ilizitenga mara mbili. Kwa nini inapotaka kujenga kilomita 154 isingetoa vipande viwili hata vitatu kuwapa makandarasi watatu tofauti? Ndiyo lilikuwa swali langu, Mheshimiwa Waziri hakutaka hata kuligusa akaenda kurukia la wafanyakazi ambalo nitalizungumzia baadae.

Ninamtaka katika kujibu, aniambie hivi atakapoenda kurejesha hao wajenzi mwezi wa kumi atakuja tena kuwaomba watoke Kagoma waende mpaka Lusahunga kilomita 154 kwa kuendelea kusuasua kama sasa? Ninaomba barabara hii itengwe angalau mapande matatu ili iweze kupewa makandarasi tofauti na kuweza kujengwa ikamilike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali hilo hilo langu la asubuhi niliuliza pesa za wale ambao walikuwa vibarua ziko wapi? Jibu nililopewa nalo sikuridhika, mimi alishanilettea majibu haya hapa wakati anajibu pale. Kwa hiyo, nilipata nafasi ya kuyasoma na nikajua kabisa kwamba, Serikali ilikiri yenye hapa kwamba kukosekana kwa vielelezo kumefanya kuwe vigumu kwa Serikali kufuatilia malalamiko ya vibarua. Mimi nikauliza kwa kuwa Serikali yetu inakuwa inaingia mikataba hii na imeshaizoea inafahamu kwamba lazima wafanyakazi wa Tanzania wataingia kufanya kazi za vibarua na wengine za kiutaalam, lakini nani anayeshughulikia haki za wafanyakazi, hapa ni haki za wafanyakazi? Kwa sababu kibarua akishafanya kwa mfululizo miezi minane si kibarua tena lakini haki yake iko wapi?

Ndicho nilichotaka kusema hicho na ninachotaka katika mikataba ya barabara inayoendelea. Inapokuwa tayari mkandarasi ameshaingia mkataba, ninaomba wafanyakazi wa Tanzania wahakikishe kwamba, Wizara inayohusika iweke na sehemu ya wafanyakazi ili waweze kuwa na haki zao. Waorodheshwe wajulikane ni haki wanastahili. Unatoka wapi, jina lako nani, umri wako, unafanya kazi gani, unalipwa nini na nani anaingia na huo mkataba. Ninaomba suala hili mimi nijulishwe kwamba Serikali ikubali kwamba itashirikiana na mimi kupata orodha ya wale wananchi ambao walikuwa vibarua kwenye hii barabara kabla ya ku-*terminate* huu mkataba ambao hawajui watapata wapi haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo nisemee hili la usafiri na usafirishaji katika Mkoa wa Kagera limekuwa ni kero. Nina hakika limefanya maisha ya Wananchi wa Kagera yawe magumu. Wamekwamishwa kiuchumi na kijamii. Mkoa wa Kagera una matatizo ambayo siwezi kuyaeleza nikayamaliza. Labda tu niseme zile hisia za kuhisi kwamba labda Mkoa wa Kagera umetengwa. Sisi Mkoa wetu ndiyo tulipata matatizo ya UKIMWI, sote tunafahamu UKIMWI ulianzia Mkoani Kagera. Lakini mpaka leo hii bado *attention* haijaweza kufika kwenye maeneo yote, kwa sababu kubwa ya usafiri. Sisi Mkoa wa Kagera una Wilaya ya Muleba na Biharamulo, sipajui vizuri lakini nasemea Muleba ninakokufahamu. Muleba sisi tunazo Kata tatu zilizo ndani ya Ziwa Victoria na hizi Kata ni za Kiserikali. Kwangu mimi kuna vijiji vinane kwa mwezangu sikuju kuna vijiji vingapi, unafikaje kuwashudumia wananchi waliopo Goziba, waliopo Kerebe, Mazinga huko Muleba Kusini kama hakuna usafiri wa uhakika? (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichopita tangu alipokuwepo Mheshimiwa Mwandosya, tulioomba usafiri ikaenda ujenzi ikarudi. Hata leo nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Maua Daftari, namwambia sisi bado tunahangaika na masuala ya usafiri katika Ziwa Victoria. Usafiri katika Ziwa Victoria unaathiri maisha ya wananchi kiuchumi na kijamii. Niambie jinsi ambavyo utaweza kupeleka huduma ya elimu. Wananchi kule wamekwama kusoma, nimekwenda juzi nimelia machozi, shule tulioianzisha ilitakiwa kuwa na darasa la sita leo hii ipo darasa la kwanza, wanafunzi wote wameshatawanyika wamekusanywa kuingizwa katika darasa moja. Mwalimu akienda kupokea mshahara harudi, mpaka mwezi mzima upite. Suala hili linanisikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tatizo lingine ambalo lipo hapo ni suala la usafiri wa reli. Wenzangu wamezungumza vizuri sana kuhusu usafiri wa reli. Kweli kama reli haijaboreshwa sijui unawasaidiaje wananchi wanaokwenda Kanda ya Ziwa. Kwa sisi kutoka Dar es Salaam kwa treni, ukafika Dodoma ukaenda mpaka Mwanza na Mwanza ukapanda meli ukaenda mpaka Bukoba, hatuna namna ya kufika huko. Imekuwa ni matatizo; je, Serikali ina mpango gani wa kutununulia meli mpya sisi wa Mkoa wa Kagera, tutabaki na MV Victoria kila siku inayoharibika na kutengenezwa mwaka mzima ikitirudi siku mbili tena inarudi kwenye matengenezo? Hivi kwa nini maisha yetu yanawekwa rehani? Ninaomba Serikali inipe majibu na iniambie inatafuta fungu gani la *emergency* kuhakikisha kwamba inanunua meli kwa ajili ya Wananchi wa Mkoa wa Kagera. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili sasa si la kuendelea kujadiliana tunahitaji majibu, kwa sababu meli hii haihudumii tu Wananchi wa Kagera. Ilikuwa inaeleweka na ilikuwa inafanya safari za kwenda Kisumu na Jinja, Mara na Mwanza mpaka Shinyanga waliitegemea. Leo huduma hii hakuna. Naomba Serikali inipe majibu. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nilitaka kusema hivi hakuna kigugumizi katika kuzungumza suala zima la ufisadi, umetufika rohoni. Ufisadi umetoka kwenye ngazi za juu ambapo bado kuna vitu tunahangaika navyo lakini kuna ufisadi mkubwa sana vijijini. Fedha za Serikali kwa ajili ya wananchi vijijini hazifiki, eti tusizungumze! Hivi kweli ni sawa sawa? Wananchi wanachanga pesa zao hazifiki, shule hazijengwi,

miradi haiendi, zahanati hazijengwi fedha ziko mfukoni tuiseme? Lazima tuendelee kusema suala hili ili wanaohusika wajue kwamba halipendezi na fedha hizi si zao ni za wananchi na za maendeleo. Lazima fedha hizo zirudi na kila anayezipata ahakikishe amezifanya kazi inayotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo niliyozungumza nakushukuru, nitaunga mkono hoja baada ya kupata majibu. (*Makofi*)

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii. Vilevile nampongeza Waziri wa Miundombinu, pamoja na Naibu wake na watumishi wa Wizara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda niwaambie Waheshimiwa Wabunge katika Bunge hili hatutaki malumbano, inatakiwa tufanye kazi zilizotuleta. Barabara ya Mwandiga - Manyovu ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi tangu mwaka 1995, 2000 na 2005. Wakati huo ilikuwa ni wakati wa Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, ambaye ni mstaafu na si kwa ajili ya Mheshimiwa Zitto Kabwe ambaye ni Mbunge wa Jimbo hilo hivi sasa. Hii ilikuwa ni kwa ajili ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia bandari. Bandari ya Kigoma ilishabinafishwa, siku moja nilikuwa nipo pale watumishi wakaambiya kuwa ni marufuku kuanzia kesho au kesho kutwa watumishi kuwepo pale. Wale wananchi hawakukaidi wakakubali Sheria wakaambiya kaeni muda kidogo mtalipwa mafao yenu, lakini mpaka sasa ninapoongea, wale watumishi bado hawajalipwa mafao yao. Sasa nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri ni lini watumishi wale watapata mafao yao ambayo kila siku wanasumbuka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bandari ile inalindwa na watu ambao ni wageni. Vijana waliopo pale wamejaribu kuomba ajira lakini hawakuweza kufanikiwa. Kwa hiyo, bandari ile inalindwa na watu ambao ni wageni, vijana wa Kigoma wamenyimwa nafasi ya kuilinda bandari ile. Vijana wanaolinda pale wanatoka Burundi. Hiyo ajira kwa vijana wa Kigoma wataipata lini? Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya ni lini itafanikiwa kama wageni ndiyo watakuja kulinda Bandari ya Kigoma na vijana wa Kigoma waachwe nje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri na uchukuzi ambao ni reli; kwa kweli mimi nataka niseme jinsi nilivyopata adha wakati nasafiri kwenye treni. Ukitaka kusafiri kwenye treni uache kabisa umewaaga ndugu zako, uwaambie jamani nakwenda kufa. Ndivyo ilivyo. Ukipandia Kigoma unaona nafuu kidogo, ukifika Nguruka treni itajaa mpaka inatapika. Utakuta *third class* ile nafasi wanayokaa watu watatu, wamekaa wengine katikati kwenye miguu, kwenye mabega na wengine wamekaa kwenye mstari ambao ni wa kwenda kwenye behewa lingine. Hata *TT* anashindwa kufika *third class* kwa ajili ya wingi, ina maana wale waliopandia njiani wanafika mpaka Dar es Salaam bila kulipa. Ukifika *second class* na *third class* unasema naam, labda unaenda pale kunyoosha miguu. Pale kwenye *corridor* unakuta abiria wamejaa na wengine wamelala.

Sasa unajiuliza; wakati wa kwenda chooni utakwendaje? Ina maana unapita kwa kuwakanyaga mmoja mmoja unaruka mpaka unafika chooni. Ukipika chooni hakuna nafasi ya kupita, ukigonga mlango haufunguliwi watu saba wamekaa chooni. Unaamua kurudi, kama una sahani, bakuli au mfuko wa rambo unajisaidia humo humo unatupa dirishani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wasafiri wa Kigoma tunapata adha sana. Kama ni mama ana watoto watatu au wanenye, akifika anakokwenda ajue watoto wawili wanazikwa kwa sababu ya kusukumwa na kufinyangwa. Kwa kweli kwenye treni kuna adha kubwa, *first class* ukienda mle magodoro yale yamechanika, shuka linanuka, panya wanakudokoa kwenye miguu, vitanda vina kunguni! Jamani hiyo kweli ni *first class?* *Second Class* ni hivyo hivyo. Nilipofika kwenye ule mlango wa choo nikawaomba jamani naombeni kupita niende chooni; wakasema hakuna nafasi, sasa nikataka nijitambulische kwamba jamani nipisheni mimi Mbunge nikaogopa wangeniambia tuambie kwa nini unaenda Bungeni; ni kitu gani kinachokupeleka kule wakati treni inajaa hivi! (*Kicheko*)

Nikaogopa kupigwa makofi, ikabidi nimezee kujieleza na kama ningejieleza ningepata matatizo, wangenipiga. Maana wangeniuliza ni kitu gani kinakupeleka kule Bungeni wakati unaona treni inajaa hivi? Kwa kweli tunapata adha. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, adha ni kali mno. Sasa hivi ukitoka Dar es Salaam kwenda mpaka Tabora kuna *buffet* ukifika Tabora *buffet* inatolewa inakwenda Mwanza; Kigoma tunasafiri hivyo hivyo bila kula. Chakula ambacho tunakipata baada ya hapo, ukipewa maandazi, supu, soda au maji, ina maana yale maji na zile soda na yale maandazi yamewekwa karibu na choo. Kuna mlango pale ambapo huwa wanafunua wanaweka. Jamani hivi sisi wasafiri wa Kigoma Serikali imeshatuona kama ni watu wa Burundi au wa wapi, sio Watanzania? Wameshatuona sisi ni wanyama? Tunasikitika sana, hiyo ndiyo adha niliyoipata niliposafiri na treni. Unakuta abiria wengine wanakaa kwenye injini wakati hata dereva anakuwa hajawaruhusu lakini wanarukia kwa nguvu.

Siku moja tulikuwa na Mheshimiwa Switi kwenye chumba kimoja tunaangalia dirishani, tulimwona mtu mmoja akianguka kutoka kwenye injini na nilipojaribu kufuatilia wakaniambia yule mtu kafa. Sasa hapa Serikali imesema kuwa abiria waliosafiri ni 572,000 haikusema ni wangapi waliokufa na wangapi walioachwa na treni kule kwenye stasheni za njiani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wajawazito, walemvu na wazee sasa hivi hawapandi treni. Tunaomba Serikali itusaidie. Sasa hivi Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba, safari ya treni iwe mara nne kwa wiki. Tunaomba safari hizo ziwe za kweli. Safari mbili jamani zinatumiza na tunaomba mtuambie ni lini hizo safari nne zitaanza; msituambie zitaanza tu tunataka tujue zitaanza lini na wananchi wasikie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie nyumba ambazo ziliwekwa alama ya X. Nyumba hizi zimebekwa alama hiyo mara ya kwanza mwaka 2004, mara ya pili mwaka 2007 mwezi wa Novemba na Desemba. Nikamuuliza Waziri Mkuu kwenye maswali ya

ana kwa ana; akaniambia niliandikie, nikaliandikia. Kwenye swali na jibu la msingi la mwaka 2007 ambalo niliuliza Bungeni, Mheshimiwa Naibu Waziri aliyejamishiwa Wizara nyingine alisema kuwa, kwa kuwa nyumba zimeshawekwa X hicho ni kielelezo tosha kabisa cha kuvunja nyumba zao na wananchi hao walikuwa wameshavunja nyumba zao kuanzia mwaka 2005. Nimeambiwa kuwa Tamko la Serikali lilitamkwa tarehe 25 Aprili, 2006. Sasa wale waliovunja nyumba zao tangu mwaka 2005, Serikali inasemaje? Mheshimiwa Waziri naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wa Nkungwe katika Jimbo la Mheshimiwa Zitto, wanapata shida sana wakati wa masika. Lazima watu watano wafe kutokana na Mto Lwiche, wakitoka shambani mto ukifurika wakijaribu kuvuka wanakufa. Wakati mwingine wakitumia mitumbwi inapinduka watu wanakufa na ni lazima kila mwaka watu wafe. Sasa naiomba Serikali iwajengee daraja ili na wao wasaidiwe. Siku za nyuma walitengenezewa mtumbwi na Halmashauri na ule mtumbwi ukapasuka wakafa watu watano. Sasa kwa nini Serikali haiwajengee daraja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja asilimia mia kwa mia. (*Makofî/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Nkayamba, kwa kuuliza maswali yako, ingawa hukuuliza majibu hayo yatapatikana tarehe ngapi, mwezi upi na mwaka upi, lakini Mheshimiwa Waziri ujumbe huo umekufikia. Sasa namwita Mheshimiwa Damas Nakei, halafu Mheshimiwa Dr. Luka Siyame ajiandae.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii nami niweze kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Miundombinu. Labda nianze kwa kumpongeza Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara hii ambayo ni nzito. Nampongeza sana na naamini Mheshimiwa Rais, aliona atamfanya kazi vizuri. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri iliyoandalisha vizuri, yeye akiwa pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Chibulunje. Nianze kwa kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi katika hotuba yangu, nitakuwa nafanya kazi ya kuishukuru Serikali kwa sababu ya yale ambayo nilikuwa nimetarajia jinsi yanavyoenda vizuri. Katika hotuba ya bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Hotuba ya Waziri Mkuu, suala la Miundombinu ya Uchumi liliwekwa katika nafasi ya juu kabisa kwamba ni muhimu katika kujenga uchumi wetu na kuondoa umaskini. Mindombinu hiyo ni kama reli, barabara, bandari na usafiri wa anga. Dira ya Maendeleo 2000 – 2025, nayo pia imezungumzia habari ya umuhimu wa miundombinu katika kujenga uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusemea hotuba zote hizo na vile vile baada ya kupitia au kujikumbusha juu ya *Vision 2025*, kama inavyozungumza zaidi juu ya kuweka lami katika kuunganisha barabara zote za Mikoa, Barabara Kuu zinazouanganisha Makao Makuu ya Mikoa, bado sijasikia kama kuna mpango wa kuunganisha au wa kuwa

na *Railway System*, ile *network* ya kuunganisha Mikoa na Miji Mikuu ya Mikoa. Kwa hiyo, inaonekana *Railway System* katika nchi yetu bado hatujaiona kama ni miundombinu muhimu sana. Katika nchi zozote duniani ambazo zimeendelea, Miundombinu ya *Railway* ni ya muhimu sana. Sisi tumebakia tu kuzungumza habari ya Reli ya Kati, habari ya Reli ya kwenda Tanga na Musoma basi. Hatuzungumzii habari ya *connections* za *Regional Headquarters*. Kwa hiyo, nilifikiri japo kwa miaka 50 ijayo hata 100 ijayo, tuwe na mpango huo kwa sababu lazima tuzoee mipango ya muda mrefu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwhali kubahatika kuona au kupita juu ya daraja refu kuliko yote duniani, ambalo lilikamilika mwaka 1997, lakini walituambia kwamba, ujenzi wa daraja hilo ulipangwa au ulikuwa *conceived* miaka zaidi ya 70 iliyokuwa imetangulia. Kwa hiyo, unaona wenzetu wana mipango ya muda mrefu, sisi hatuna mipango ya namna hiyo. Nadhani ni vizuri kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, vilevile niongezee kwamba, mara nyingi tumezungumza matatizo ya fedha na namna ya kujenga miundombinu hiyo. Nijikumbushe, mwaka 2001 wakati nachangia katika Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, akizindua Bunge Jipyä wakati ule, nilikuwa na ndoto kwamba kwa sababu kuna *potential* ya madini hasa dhahabu, tutakuwa na barabara za lami nchi nzima. Nasema tu kwamba, leo naendelea na ndoto hiyo, kwa sababu leo ile dhahabu sasa imekuwa *reality*, inachimbwa na inauzwa. Kwa hiyo, ni hakika kwamba, tuna kila sababu kwa nini tusiwe na barabara za lami katika nchi yetu kutokana na utajiri wa dhahabu na madini mengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa siku ya siku tuwe na *equation* hii ni hesabu ya kujumlisha tu kwamba, miundombinu ya reli jumlisha na barabara zote nchini ni sawa sawa na idadi ya mashimo ya dhahabu yatakayokuwa yameachwa. Dhahabu itaisha, lakini tuone *something material left behind*. Kwa hiyo, nilifikiri viongozi wetu walione hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naishukuru Serikali kuhusu ujenzi wa barabara kutoka Minjingu – Babati – Singida. Naishukuru sana Serikali kwa sababu hatua iliyofikiwa sasa ni ya kuwekwa lami katika barabara hiyo na kuelekea mwisho wa mwaka huu, kitu wanachoita *physical works* zitaanza katika barabara hiyo. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kuishukuru Serikali kwa kuondoa kero hiyo iliyokuwepo muda mrefu. Nakumbuka barabara ilikuwa *the busiest in the country* na ilikuwa na magari makubwa zaidi ya 400 kwa siku, tungeweza kuiita *Motor Way* kwa sababu ni barabara iliyokuwa inafanya shughuli nzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru vilevile Serikali kwa barabara ambazo zipo katika Jimbo langu la Babati Vijijini, ambazo zitaangaliwa. Napenda tu niwaambie wananchi wa Babati Vijijini kwamba, wawe na furaha tele kwa sababu mwaka unaokuja, hali ya barabara itakuwa nzuri. Barabara hizo ni Mbuyu wa Mjerumanî – Magara – Mbulu, Babati – Dareda – Dongobeshi na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea katika barabara hii ya Minjingu – Babati – Singida, ninashauri kwamba, barabara hii inapita katika maeneo kame kabisa, ambayo wananchi pale tumekuwa na ahadi nao kwamba ifikapo mwaka 2010 tutakuwa tumewaunganishia huduma ya maji, kwa jinsi ipi? Nilifikiri ujenzi wa barabara hii uwe kwa namna fulani msaada kwamba, wakati wanafanya kazi hizi wanaita *earthworks* wale wenzetu kwamba, kuna mashimo makubwa yanachimbwa kutokana na suala zima la kuchukua changarawe pale. Sasa nilifikiri hiyo kazi ifanyike *strategically* ili mashimo hayo yaweze kuwa *modified* baadae na kuwa mabwawa ili kuweza kuvuna maji ya mvua. Sasa hii inahitaji maelewano au mahusiano kati ya Wizara ya Maji na Wizara ya Miundombinu ili suala linaloitwa *economies of scale* liweze kuwa *realized* katika hatua hiyo kwamba, huku una shimo la changarawe, baada ya hapo unatumia shimo hilo kuwa ndiyo bwawa la maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la matengenezo ya barabara. Katika nchi yetu kuna suala hili la kutumia kandarasi zaidi kuliko zamani tulizoea kitu wanachokiita *Force Account*. Sasa hizi ni *reforms* ambazo zinajaribu kuonyesha matumizi ya *value for money* yaweze kuwa *realized*. Ninakerwa na tatizo la kukaa na shimo dogo tu barabarani, linakuwa kero kwa magari yanayopita kwa mwaka mzima kwa sababu huwezi ku-*mobilize contractor* kwa ajili ya hilo shimo moja barabarani pale au kikwazo kidogo tu ambacho ungeweza kutumia kitu wanaichokiita labda *maintenance unit* katika Idara au katika Wizara. Sasa kwa nini wataalam wasi-*brainstorm*, wakatuambia *the way out* ili kuondokana na tatizo la kukaa na *maintenance need*, eneo dogo tu kwa mwaka mzima kwa sababu eti hatuna fedha za ku-*mobilize contractor*. Kwa hiyo, nafikiri turejee; siyo vibaya kurejea kule tulikotoka pale inaposaidia. Nilifikiri hili ni vyema likaangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa nafikiri haipendezi kama nilivyosema, wataalam wetu watusaidie; kuna tatizo la magari makubwa kupaki kando kando ya barabara na imekuwa ni *source* ya ajali nyangi katika nchi yetu. Ukienda mahali pengine duniani kwa mfano, nchi kama zetu tu, Namibia huwezi kukuta gari au lori limepaki barabarani kwa sababu yoyote ile. Kama ni matatizo, linawekwa pembeni ili kuepusha au kutoa *free access* kwa magari yote yanayopita. Kwa hiyo, nilifikiri Serikali na Wataalam wetu katika Wizara hii watusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala zima la maendeleo ya watumishi. Naipongeza sana Wizara kwa sababu imeweka *strategies* inasomesha watumishi, inawapa *training*, inawapa *promotions* na kadhalika na pia inatarajia kuajiri watumishi 176 mwaka huu. Hii itasaidia sana katika suala zima la *succession plan* katika utumishi kwamba, kila wanapostaa fu, basi kuna watu wanao-*step into their shoes*. Kwa hiyo nadhani huu ni utaratibu mzuri. Nilidhani ni vizuri nirejee kwa sababu katika hotuba hiyo sijaona mambo ambayo tunayasikia sikia; kuna matatizo ndani ya Wizara hii hasa katika eneo linalohusika na matengenezo ya barabara, *TANROADS*. *TANROADS* ni eneo ambalo tunalitegemea sana. Watumishi wake wasipokuwa *motivated*, wasipokuwa na moyo wa kufanya kazi, basi kuna tatizo kubwa katika kuona *realization* ya *maintenance plans* katika nchi zetu.

Kwa hiyo, watumishi hawa tunasikia wakilalamika, wakiwa na wasi wasi mkubwa kuhusu ajira zao, utaratibu unaobadilika badilika. Tunasikia kwamba, *there are forthcoming changes* kwamba, kutakuwa na kuajiriwa kwa mkataba wa mwaka mmoja mmoja. Hii mara nyingi italeta wasiwasi katika *job security*. Kwa hiyo, nilifiki Serikali ituambie, *what is a problem* kuhusu ajira ya hawa watumishi ambao wana wasiwasi kwamba, kuna mambo yanafanyika kunakuwa wasiwasi. Ina maana hawajashirikishwa na kwa kweli *management isiposhirikiana na employees, you will end somewhere* ambako siyo kuzuri.

Kuna wakati pia tulisikia kwamba, wakurugenzi kadhaa walismamishwa kazi, nadhani hata wao hawajui kwa nini walismamishwa na sisi vilevile hatujui na Bunge vilevile kwa maana nyingine au wananchi hawajui. *They are still being paid.* Sasa, je, hiyo siyo hasara na kwa nini watu wanasmamishwa halafu hakuna maelezo? Mimi nilidhani ni vizuri tukafahamishwa ili tuweze kuelewa nini kinaendelea katika *TANROADS* ambayo kwa kweli tunaitegemea sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watumishi; kumekuwa na *a lot of exits* katika *TANROADS*, watumishi wanaondoka kwa sababu ya wasiwasi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kuna haja ya kuweka mazingira vizuri kwa sababu *we expect a lot from TANROADS* kwamba, itutekelezee ile mipango ambayo tunaitarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie hapo, lakini nirudie shukrani zangu kwa Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea kufanya na namtia moyo zaidi Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa inayomkabili katika Wizara hii. Nasema tutakuwa pamoja nawe tukishirikiana vizuri. *We need each other.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. DR. LUKE J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba awali ya yote, nichukue fursa hii kwanza kabisa, kumpongeza Mheshimiwa Dr. Kawambwa, Waziri wa Miundombinu, kwa hotuba yake iliyotolewa kwa umahiri kabisa na ikiwa inaelezea kwa upana ile Ilani ya utekelezaji wa Wizara yake kuanzia mwaka 2005 – 2010. Pia, napenda niwapongeze Naibu wake, Mheshimiwa Chibulunje, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutayarisha hotuba ya bajeti hii na utekelezaji wake. Napenda katika hatua hiyo, niseme kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa sababu kama nilivyokwisha kusema, imejikita katika kuhakikisha kwamba, inafikisha huduma za miundombinu kwa uwiano mzuri kwa nchi nzima hususan zile huduma za miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbozi Magharibi, napenda niseme kwa kuanza kabisa ni Jimbo ambalo lipo pembezoni na lichukuliwe hivyo na ni Jimbo changa,

lenye umri wa miaka isiyozidi 12. Katika hali hiyo, Jimbo hili lenye eneo la kilomita za mraba 6275 kati ya eneo la mraba wa kilomita 9679 la Wilaya ya Mbozi nzima, lina barabara kuanzia hizo za Mkoa hadi zile za Wilaya zisizozidi urefu wa kilomita 260. Kwa hali hiyo, zaidi ya asilimia 85 ya Vijihi vya Mbozi Magharibi havifikiki kwa njia ya barabara au kwa njia nyingine yoyote. Hii ina maana kwamba, kama barabara haifikiki, sitegemei kama itafikika kwa ndege, kwa zaidi ya miezi minane kwa mwaka kati ya Novemba na Juni. Sasa hilo tu ni kiashiria cha hali duni ya kiuchumi, kielimu na maendeleo yote kwa ujumla kwa Jimbo hili. Hivyo basi, napenda niiombe Serikali itoe kipaumbele au upendeleo maalum kwa Jimbo hili la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote niliyokwisha kusema, napenda niseme naishukuru sana Serikali, kwani kwa mwaka huu imeweza kulifikiria Jimbo hili la Mbozi Magharibi katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, imeweza kukubali ombi letu la kupandisha barabara mbili kutoka hadhi ya Wilaya kuwa Barabara za Mkoa. Barabara hii ni ile ambayo siku za awali niliwhahi kuiongelea inayotoka Chapwa – Chiwezi – Chindi – Msangano – Chitete – Chilulumo – Mkulwe hadi Kamsamba. Barabara hii inapita kwenye Bonde la Ufa la Rukwa, ambalo ni nusu ya eneo la Jimbo zima na inaunganisha kata saba za Jimbo hili. Kwa hali hii, tunategemea utengenezwaji wake utaweza kuinua uchumi na maendeleo ya wananchi wa Jimbo hili kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya pili ni ile inayoambaa na mpaka wa Zambia, ambayo inaanzia Kakoozi – Chisitu – Kapele – Kasinde hadi Ilonga na kuunganisha barabara hii na ile ya Ilonga – Matai - Kasanga ambayo inafika bandarini Kasanga, Ziwa Tanganyika. Matumaini yangu ni kwamba, utekelezwaji wa utengenezaji wa barabara hizi utakuwa umefungua njia ya maendeleo kwa Wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hii, napenda niishukuru sana Serikali kwa kuweza kukubali kufanya matengenezo pia kwa barabara mbili ambazo hapo awali ndizo zilikuwa barabara pekee za Mkoa katika Jimbo hili. Barabara ile ya kutoka Mlowo hadi Kamsamba, ambayo kwa taarifa tuliyokuwa tumepewa hapo awali na Wizara ya Miundombinu, itaunganisha barabara ile kwa upande wa Rukwa kutoka Kijiji cha Chiliamatundu hadi Ntendo na kuendelea hadi Mpanda na hivyo itarahisisha usafiri wa kutoka Mbeya badala ya kuzunguka Tunduma – Sumbawanga, basi wananchi watakatisha moja kwa moja pale Mlowo kuititia Kamsamba hadi Mpanda na hivyo kupunguza umbali wa safari. Pia ipo barabara nyingine ya Igamba – Msangano – Utambalila.

Barabara hii ni muhimu kwani inapita kwenye ukanda ambao ni wa kahawa na kwenye msitu asilia wa miombo, mininga na miti ambayo nafikiri mtu ukipita pale hutaamini kwamba, misitu hii ni ya asili kwa sababu inafanana na ile ambayo imepandwa. Ni mandhari ya kipekee ambayo ukiiiona utapenda uweze kupita kila wakati. Hivyo, nalo hili limewezesha kusaidia katika kusukuma maendeleo kama litatekelezwa vilivyo.

Kwa bahati mbaya sana, barabara hii ya Igamba – Msangano – Utambalila ilikuwa ikilimwa kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita tokea Igamba – Msangano tu japo ilikuwa inaripotiwa kwamba, barabara nzima inalimwa. Naamini sasa hivi maadam imekwishaeweka wazi kwamba hailimwi, basi *TANROADS* watailima na kuikamilisha yote ili wananchi waweze kupunguziwa adha ya usafiri katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niseme kwa kipekee kabisa, napenda kuishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kuitengeneza Barabara ya Tunduma – Sumbawanga kwa kiwango cha lami kwa sababu nayo itakuwa imerahisisha usafiri na usafirishaji kati ya Mkoa wa Mbeya, Rukwa, Kigoma na hata Mikoa mingine. Zaidi ya hapo, itakuwa imefungua njia kwa wale wananchi wa Kata zangu nne za Tunduma, Nkangamo, Ndalambo na Munga, kuweza kusafiri na kusafirisha mali zao bila matatizo kwa mwaka mzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo langu inapita Reli ya *TAZARA* ambayo ni muhimu sana kwa usafiri na usafirishaji wa wananchi wengi wa Tanzania, hususan wale wa Mikoa ya Pwani, Morogoro, Iringa na Mbeya. Reli ya *TAZARA* ilivyuoanza kwa hakika ilikuwa imeanza vizuri, lakini jinsi muda ulivyopita, tumeona ikizorota katika utendaji wake. Hivyo basi, pamoja na Reli hii, naomba pia Reli nyingine za nchi hii ambazo sisi tulipokuwa tunakua tulizitumia kama njia kuu za usafiri, ziweze kuwekwa katika hali nzuri ili hawa wananchi wote niliokwisha kuwasema wa Kigoma na sehemu nyingine, waweze kufika sehemu hizo kwa urahisi na kwa furaha kabisa ama kwa raha mustarehe, kama ilivyokuwa zamani. Isiwe kama alivyokwisha kusema mwenzangu kwamba, sasa hivi hata kule kwenye *first class* kuna panya na kunguni, ambayo kwa kweli ni aibu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba tena niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nakushukuru wewe Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja hii ya Wizara ya Miundombinu. Napenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu. Pili, ningependa kuwapongeza sana Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa na Naibu wake, Mheshimiwa Hezekia Chibulunje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naingia hapa, Mheshimiwa Makwetta aliwaita ninyi mna *angel faces*, yaani mna sura za malaika. Hii ni sifa kubwa sana kwenu. Mimi niliwahi kufanya kazi Wizara ya Ujenzi, nafahamu sana Makandarasi wanavyofanya kazi zao. Kwa hiyo, pamoja na sifa hizi, ningependa kuwatuhadharisha kwamba, kuweni makini, kwa sababu pamoja na kuitwa kwamba mna sura za malaika, kama mtafanya vinginevyo, mtaitwa mna sura za kitu kingine na haitapendeza hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza, niwapongeze wananchi wangu wa Jimbo la Mufindi Kusini, kwa namna wanavyoshirikiana na mimi Mbunge wao katika

kujiletea maendeleo yao. Namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Halmashauri, Ndugu yetu Nyaganilwa na namshukuru sana Diwani Kaguo, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeanza na barabara za Jimbo langu la Mufindi Kusini. Nianze na Barabara ya Nyololo – Igowole – Kibao – Mtwango. Awali barabara hii ilikuwa nzuri sana, magari yalikuwa yanakwenda kwa kasi. Jambo la kushangaza, sasa hivi barabara imepata mashimo yasiyo ya kawaida, sababu mimi sielewi, tena katika kipindi kifupi tu kilichopita. Kwa hili ningependa Mheshimiwa Waziri alichukue. Sisi katika Bodi ya Barabara ya Mkoa, tulimwagiza *Regional Manager* wa *TANROADS*, kwanza, barabara hii ni nyembamba mno. Ukumbuke Mufindi tunalima chai, asilimia 67 ya chai Tanzania tunalima Mufindi. Sisi tunazalisha mbao, asilimia 60 ya *softwood* yote ya Tanzania inatoka Mufindi. Kwa hiyo, Bodi ya Barabara ya Mkoa ilipendekeza kwamba, barabara hii iwekewe lami kuanzia Mafinga – Sawala – Kibao – Nyololo. Tunastahili kuwekewa lami kwa sababu maeneo haya yanazalisha, yana *economical return* kwa Taifa hili la Tanzania.

Kabla haijawekwa lami, basi angalau ipanuliwe ili yale malori makubwa yanayosomba magogo, chai na nguzo, maana tuna viwanda vyta kutengeneza nguzo kule, yaweze angalau kupishana. Kwa hali ya bararabara ilivyo sasa, inakuwa vigumu sana malori yale kupishana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ambayo ningependa kuizungumzia ni ya Mbalamaziwa – Mwilavila – Kwatwanga. Barabara hii imechoka kabisa, mimi sielewi kwa nini, yaani nyasi zimeota mpaka kwenye kingo za barabara? Barabara hii inakwenda Shule ya Sekondari ya Malangali na Shule ya Sekondari ya Itengule. Mimi nilikuwa *Headmaster* Itengule kwa miaka mitano, niliondoka pale mwaka 1994. Miaka ile barabara ilikuwa na nafuu kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali itilie maanani sana hizi barabara mbili ambazo nimezizungumzia; Barabara ya Nyololo – Igowole – Kibao – Mtwango na Barabara ya Kwatwanga – Malangali Itengule – Ihowanza – Kwatwanga. Hii barabara ya Mbalamaziwa hadi Kwatwanga haihitaji kazi nyingi, *just light grading, una-grade* tu kwa greda basi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mimi ni Mhandisi pia, nimefanya kazi Sumbawanga kule na nimefurahi sana kwamba, Kijiji cha Kapele nacho kitapewa barabara nzuri. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ipo barabara ya Igowole – Kasanga – Udumka – Mtambula – Ihawaga hadi Nyingo ya *TANROADS*, lakini jambo la kusikitisha hata katika rekodi ya *TANROADS*, barabara hii haipo! Tulikuwa tunakaa katika Vikao vyta *Regional Road Board*, tunaulizana, kulikoni; mbona haitengewi pesa? Mimi ni Mbunge kwa zaidi ya miaka kumi, sijawahi kuiona hata Mheshimiwa Waziri ameiweka katika rekodi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Wizara imeisahau na *Regional Manager* ameisahau pia, nilisema naunga mkono hoja kwa asilimia 80, nina sababu kwa nini nafanya hivyo nitaitoa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni uvunjwaji wa nyumba, Serikali iliwaandikia wahusika barua kwamba vunjeni vyumba zenu, watu kwa kutii amri ya Serikali wakavunja nyumba ili kupisha ujenzi wa barabara. Agizo hili lilikuwa kwa nchi nzima, barua zikaandikwa na wananchi wakatii Agizo la Serikali, nyumba zao wakavunja lakini barabara hazikujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Sadani wananchi walivunja mpaka nyumba za shule, lakini mpaka leo hakuna barabara iliyokwishajengwa. Mimi naiuliza Serikali; Wananchi wa Sadani wamevunja nyumba, wananchi wa Malangali wamevunja nyumba, wananchi wa pale Mtwango kwa bahati nzuri hawajavunja lakini wanazo barua; hivi maana ya kuandika barua ili wananchi wavunje nyumba na Serikali haina pesa ya kujenga nyumba maana yake ni nini? Kama hii si kuwanyanyasa wananchi, kama hii haileti kero kwa wananchi maana yake mtu ukishaandikiwa barua kwamba vunja nyumba yako hata usingizi unashindwa kuupata. Kwa hiyo, wananchi kwa miaka mingi wamekuwa wakishindwa kupata usingizi wao kwa sababu wameandikiwa barua ya kuvunja nyumba zao na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iwaombe msamaha wananchi wale wote walioandikiwa kuvunja nyumba zao katika nchi nzima ya Tanzania, wakianza na Sadani, Malangali na Vijiji vyote vya Jimbo langu na Majimbo mengine yote katika nchi hii ili kuwatendea haki wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara nyingine inaitwa Changarawe – Matanana – Bunurainga - Kisada - Nyororo, zamani ilikuwa barabara kuu ya kwenda Zambia, baadaye Serikali ikajenga barabara ya lami inayopita katika Msitu wa Sao Hill. Serikali Kuu iliitelekeza barabara hii. Mimi nimezaliwa pale Kisada, ndiyo nyumbani kwangu, kuna siku nilikuwa nakwenda na gari langu ilibidi nitembee kilomita tano kwa mguu kwa sababu nilishindwa kwa jinsi barabara ilivyo mbaya, mashimo hata tembo hawezikupita. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Chifu Mwakyembe hapa anacheka...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa wewe endelea tu, wapo wachache wameshtuka uliposema tembo lakini endelea tu unaelewewka.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, atueleze ni nani mwenye barabara ile. Mimi ninavyotambua, barabara hii ni ya Serikali Kuu na ndiyo yenye wajibu wa kuitengeneza. Vilevile Wilaya yetu ya Mufindi, ipo hoi; haina uwezo mkubwa wa kutengeneza barabara zote. Kijiji cha Mbunga hakina barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende barabara nyingine inayoitwa Nyigo – Mgololo, kwa mujibu wa kumbukumbu zangu, zinanionyesha kwamba, Waziri wa Miundombinu mwaka jana wakati wa Kamati aliikubali barabara hii kuwa barabara ya Wizara ya Miundombinu. Lakini nashangaa, sijui kule kukubali kwake kumefia wapi, kwa sababu katika Bodi ya Barabara ya Mikoa jambo hili bado tunaendelea kuliomba, sasa tutaiomba Serikali mpaka lini wakati Waziri wa Miundombinu mwaka jana alikubali? Kwa hiyo, kama Waziri wa Miundombinu anataka nimpe asilimia mia moja, basi aikubali barabara hiyo ya Nyigo – Mgololo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgololo kuna kiwanda kikubwa cha karatasi. Sote tunakifahamu ndani ya Bunge hili na Watanzania wote wanajua kwamba ni kiwanda muhimu sana kwa uchumi wa Taifa hili la Tanzania. Kwa zaidi ya mika 12 huwa nazungumzia umuhimu wa barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimechoka, nampa asilimia 80 Mheshimiwa Waziri, kama hataichukua barabara hii wakati wa Kamati nitatoa shilingi kwa hakika, kwa sababu sisi Halmashauri hatuna uwezo wa kuitengeneza barabara hii. Halmashauri yetu inapewa shilingi milioni 30 – 40, barabara kilomita 60 inabeba magogo makubwa kabisa kutoka kule Njombe kwenda kuzalisha umeme pale, *after all* inapita Njombe – Mufindi sasa Mufindi ndiyo watengeneze wakati inapita katika Wialaya mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika rekodi zetu kuna madaraja yapo Njombe, ili haki iweze kutendeka barabara hii namkabidhi Mheshimiwa Dr. Kawambwa leo aichukue, kuanzia dakika hii ninapomalizia maneno na sentensi zangu hizi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makofi haya maana yake nimekubalika hoja yangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ningependa nizungumzie juu ya Barabara ya Dodoma – Babati - Mijingu, kama nilivyosema hapo awali, nilifanya kazi Wizara ya Ujenzi. Ramani ya barabara hii ilichorwa mwaka 1964, mimi niliiona mwaka 1981 nilikuwa *Technician* wakati huo. Sasa leo wanaposema wanafanya upembuzi yakinifu, toka mwaka 1964 mpaka leo, huu upembuzi yakinifu utaisha mwaka gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili haki itendeke kwa Wananchi wa Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Arusha mpaka Cairo kuanzia Johannesburg, barabara hii ianze kutengenezwa ikipendeza kuanzia mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Dodoma hii tunasema tunataka yawe Makao Makuu ya Nchi, lakini kwa hakika haitawezekana kama Barabara ya Iringa – Dodoma – Babati - Arusha haijafunguliwa. Tutakuwa tunazunguka zunguka tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia na Uwanja wa Ndege wa Iringa – Ndui. Uwanja ule ndiyo ulirusha ua la kwanza alilovishwa Malkia Elizabeth mwaka 1952. Ua lilizalishwa pale Mufindi, sasa sisi Mufindi hatuzalishi maua kwa sababu tukizalisha tutayauzia wapi? Arusha wanazalisha maua sasa hivi kwa sababu wana *Kilimanjaro International Airport (KIA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule Uwanja wa Ndege wa Iringa wala hauhitaji gharama kubwa. Kwa sababu najua muda wangu umeisha, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti na vilevile napenda kuwashukuru sana Waziri wa Miundombinu, Naibu wake na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa asilimia 80 mpaka hapo barabara yangu ya Nyigo - Mgololo itakapothibitishwa kwamba, inachukuliwa na Wizara ya Miundombinu, kwa sababu ndiyo wenye barabara. Kwanza, waliipasua wao wala haikupasuliwa na Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliipasua wao ili kusaidia Reli ya *TAZARA*. *I want to put this in records, iingie katika kumbukumbu za Taifa hili la Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiyo Mheshimiwa Malangalila, naomba nikubali kwamba, mchango wako umekuwa mzuri na umetoa changamoto jioni hii ya leo. Kabla hatujamaliza shughuli zetu, Mheshimiwa Waziri umeambiwa ukitoka hapa leo uondoke na hiyo barabara, sasa sijui utaiweka kwenye *briefcase* yako ama wapi hilo shauri yako.

Waheshimiwa Wabunge, muda tuliobakwa nao hauwezi kututosha kwa msemajji ye yeyote na nilipofanya mawasiliano na wasemaji waliobakia kila mtu amesema muda huu uliobakia hauwezi kumtosha.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli zetu za leo, ninayo matangazo mawili, matatu hapa mezani. Tangazo la kwanza nimelipokea kutoka kwa Mkurugenzi wa Shughuli za Maswali Bungeni, Mama Masaga, ameniambia niwaarifu kwamba, kesho kutakuwepo na Kipindi kile Maalumu cha Maswali kwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote ambao wana nia ya kushiriki katika kumuuliza Waziri Mkuu maswali basi wajiandae.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea tena taarifa nyininge kutoka Ofisi ya Spika, nayo inaniambia niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote walioalikwa na Mheshimiwa Spika kwenda *African Dream* kwa chakula cha jioni kwamba, badala ya shughuli hiyo kuanza saa moja jioni itaanza saa mbili kamili usiku huu. Kwa hiyo, wote mliaoalikwa mnaombwa mhudhurie.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea hapa meseji nyangi zikiniuliza jana Mheshimiwa Spika alitangaza timu inayoongozwa na Captain Said Nkumba, lakini

hakueleza timu hiyo ya nini na inatakiwa ifanye nini. Sasa naomba tu niwape taarifa kwamba, Siku ya Jumamosi, wenzetu wa *TBL* wame-organise function kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge wote hapa Dodoma na shughuli hiyo itaanza mchana kwa mashindano kadhaa; kutakuwa na mechii ya *football* baina ya Wabunge na Timu ya *TBL*, mshindi wa kwanza atazawadiwa shilingi milioni moja.

Waheshimiwa Wabunge, kutakuwa na mechii ya kuvuta kamba na ile timu ya Mheshimiwa Said Nkumba ndiyo wachezaji maalum kwa ajili ya kuvuta kamba. Timu itakayoshinda katika kuvuta kamba itapewa zawadi ya shilingi laki tano. Kwa hiyo, Mheshimiwa Said Nkumba, anawaomba sana wale wachezaji wake kesho waende mazoezini; leo alikuwa peke yake. Taarifa niliyoletewa hapa alisahaulika jana Mheshimiwa Captain Komba atakayeshirikiana na ile timu ya akina Mheshimiwa Missanga, Mheshimiwa Sumry, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mama Hewa, Mheshimiwa Mama Kyendesya, Mchungaji Rwakatare msomi na wengine wote. Kwa hiyo, timu ijiandae na tunaamini tunachukua ushindi mkubwa tu. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nimalizie kwa kusema kwamba, *TBL* jioni watakamilisha shughuli yao kwa kuwa na *entertainment* ya muziki na wenzetu wa *Diamond Musical International* ndiyo watakaokuwepo na Khadija Kopa pia atakuwepo kwenye *entertainment* hiyo ya jioni.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ni matangazo ambayo niliona niyatolee taarifa na baada ya kutangaza matangazo hayo, nawashukuru sana kwa michango yenu ya leo. Naomba nikubali kwamba, mmetoa uwakilishi muhimu kwa wapiga kura na kwa Taifa letu zima la Tanzania. Sasa naomba niahirishe shughuli zetu na tutakutana tena kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.48 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 03 Julai, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)